

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 4 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali la kwanza kwa siku ya leo kama ilivyoada linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde. Kwa niaba yake.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Nipo.

**MWENYEKITI:** Leo uko upande gani?

**MBUNGE FULANI:** Amebadili chama. (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naingia.

**MWENYEKITI:** Ubaki huko huko. (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Haya ahsante. (*Kicheko*)

Na.140

**Umuhimu wa Mwenge wa Uhuru**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

(a) Je, bado kuna faida kwa Watanzania kuendelea kukimbiza Mwenge wa Uhuru kila mwaka, kama zipo ni faida gani?

(b) Kama hakuna faida, je, ni lini Mwenge huo wa Uhuru utasitishwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze muuliza swalil leo kwa kukaa upande ule alioulizia swalil. (*Makofii/Kicheko*)

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Hajji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Kimataifa ni pamoja na kuendelea kuhamasisha ari ya wananchi kujitegemea na kuwekeza katika maeneo mbalimbali katika Taifa letu; kuwa ni chombo pekee cha kujenga umoja, mshikamano na kudumisha amani pale ambapo Mwenge unapita bila kujihusisha na itikadi za kisiasa; kuendelea kuhamasisha na kuimarissha umuhimu wa Muungano kwa Watanzania wa pande mbili za nchi yetu; na kila mwaka hufungua na kuweka mawe ya msingi kwenye miradi mbalimbali ya wananchi na kuhamasisha uzalendo wa kuendelea kujitolea. Mfano mzuri ni kutokana na takwimu zilizopo ambazo zinaonyesha miradi ya maendeleo iliyozinduliwa pamoja na kuwekwa mawe ya msingi kuitia Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na miradi 1,342 yenye thamani ya shilingi 463,519,966,467.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kimataifa Mwenge wa Uhuru umeendelea kusimamia dhana na maudhui yake ya kumulika hata nje ya mipaka yetu kwa kuwa msuluhishi wa amani katika Bara la Afrika na mfano wa kuigwa kwa mataifa mengine ya Afrika duniani kote. Umoja, mshikamano, upendo na ukarimu wa Watanzania ni matunda pia ya Mwenge wa Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na faida na mafanikio makubwa yanayopatikana kuitia mbio za Mwenge wa Uhuru, Serikali inaamini kuwa zipo faida za kuendelea kukimbiza Mwenge huo wa Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali haina mpango wowote wa kusitisha mbio za Mwenge wa Uhuru. Dhana hii itakuwa ni endelevu na tungependa kuiendeleza kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kusitiza misingi hii bila kuchoka. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hajji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Swali la kwanza, malengo, dhamira ya kuanzishwa Mwenge wa Uhuru yameonekana kutotimizwa ikiwemo badala ya kueneza upendo Mwenge wa Uhuru umekuwa unaeneza chuki. Mfano, katika Mkao wa Rukwa hivi karibuni Wenyeviti na Watendaji waliwekwa ndani kwa kosa la kutochangisha wananchi kuhudumia Mwenge wa Uhuru.

Je, kama ni mfano wa kuigwa na katika Afrika na Dunia hakuna nchi iliyotuigiza wakakimbiza Mwenge huu hamuoni kwamba kukimbiza Mwenge sio kuleta maendeleo katika nchi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali pili, nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mwenge wa Uhuru historia yake ni kuupamba Uhuru wa Tanganyika na Zanzibar ina historia yake ya kupata Uhuru kutoptaka na Mapinduzi. Kwa sababu Mwenge sio jambo la Muungano, hamuoni sasa iko haja ya kuacha kuuleta Mwenge huu kule Zanzibar ambapo hatuoni maana yake yoyote? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango, uratibu na utekelezaji wa kimfumo na wa kifalsafa wa ukimbizaji wa mbio za Mwenge, huratibiwa kwa kufuata kanuni na utaratibu wa maandalizi uliowekwa kwa nchi nzima ya Tanzania. Hivyo basi, kama ziko dosari ambazo zimekuwa zikijitokeza eneo moja hadi lingine hazitaki kumaanisha kwamba historia ya falsafa ya Mwenge ile ambayo imejengwa katika misingi ya uhuru wa nchi yetu, eti sasa ndiyo iondolewe kwa sababu ya dosari hizo ndogo zinazojitokeza. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali kwenye dosari ndogo tutaendelea kuzipitia na kuziondoa ili falsafa ya Mwenge wa Uhuru iendelee kubaki kama ilivyo. (*Makof*)

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Mheshimiwa Mbunge anasema Zanzibar si sehemu ya Mwenge huu wa Uhuru. Nataka kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba kati ya matunda mema ambayo yalizaliwa kwa sababu ya falsafa ya Mwenge wa Uhuru ni pamoja na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Azimo la Arusha na ukombozi wa Bara la Afrika. Hivyo, kwa sababu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni matunda ya Mwenge wa Uhuru, Mwenge huu utaendelea kukimbizwa Bara na Visiwani na utaendelea kuenziwa na Watanzania wote Bara na Visiwani ukiwemo wewe Mheshimiwa Mbunge Haji kutoka Visiwani kama Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linaenzi falsafa ya Mwenge wa Uhuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Hebu tuone Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka kuuliza kwa mtu ambaye ni Mtanzania aliyezaliwa katika nchi yetu, anayehojoji juu ya Mwenge...

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Badala ya kuhoji juu ya mambo mabaya yanayotokea kwenye Mwenge, anayehojoji juu ya Mwenge unafanya nini huyu unaweza kumkabidhi hii nchi akaendelea kukaa nayo? Nataka tu kupata ufanuzi huo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Anataka ufanuzi. Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo linaonyesha jinsi alivyokomaa katika kujua historia ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niwaambie Watanzania, falsafa ya Uhuru wa nchi yetu ya Tanzania haiwezi kutenganishwa na Mwenge wa Uhuru. Naomba

niwakumbushe, wakati wa Uhuru tarehe 9 Desemba 1961, Marehemu Baba wa Taifa alisema, sisi tutawasha Mwenge na kuuweka juu ya Milima Kilimanjaro umulike ndani na nje ya mipaka yetu ulete amani, tumaini, upendo, uondoe chuki na dhuluma, sasa jambo hili si dogo. Kwa Mtanzania anayemuenzi Marehemu Baba wa Taifa itashangaza sana kama hatataka kuenzi falsafa ya Mwenge wa Uhuru. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tu kuwaomba Watanzania kwa kweli hatuna haja ya kuchukuliana hatua ya namna moja au nyingine lakini wote tutambue Mwenge wa Uhuru ni tunu kubwa ya Uhuru wa nchi yetu na unapaswa kuenziwa na Watanzania wote. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kama ziko dosari katika kukimbiza Mwenge basi zitarekebishwa. Mimi nachotaka kumwambia hakuna dosari, dosari ni huu Mwenge wenyewe. Kwa sababu kwanza unapoteza fedha nyingi kupita kiasi na wakati na kwa kule kwetu tunaamini kukimbiza Mwenge ni ibada. Kwa nini tuendelee tulazimishwa kuabudu moto?

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Swali langu ni hilo kwa nini tulazimishwe kuabudu moto? Sisi tunaamini ni ibada ya moto hiyo. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimia Mwenyekiti, labda tu nianze kwa kumnungu mwanafalsafa mmoja ambaye nilimsoma anasema, viro vitu vingine vinahesabika lakini huwezi kuvihesabu. Unaweza ukawa na

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

vitu vinavyohesabika lakini ukashindwa kuvihesabu na nataka nikuambie hata wewe unaweza kuwa na mtazamo ambao ni hasi kuhusu Mwenge wa Uhuru lakini utashindwa kutekeleza mtizamo huo wa kuufuta Mwenge wa Uhuru katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nakuambia hivi Mheshimiwa Mbunge, mwaka jana wakati tunahitimisha mbio za Mwenge Mkoani Simiyu, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Simiyu, kwa kutumia Mwenge wa Uhuru Mkoa wa Simiyu umeweza kuzindua viwanda vitatu ambavyo vimeongeza maendeleo ya kiuchumi na vimeongeza ajira kwa Watanzania. Kwa hiyo, ukiangalia faida za Mwenge huu ni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumezindua mbio za Mwenge wa Uhuru Mkoani Katavi. Mkoa wa Katavi haukuwa na uwanja mkubwa wa michezo wa Mkoa. Nje ya bajeti ya maendeleo ya mkoa, Mkoa wa Katavi umeweza kuanza ujenzi mkubwa wa kiwanja cha mpira katika mkoa huo. Nimeeleza hapa miradi ya kujitegemea ambayo imebuniwa na wananchi ambayo imeongeza chachu ya maendeleo na uchumi wa wananchi katika Tanzania nzima. Mwenge wa Uhuru utadumu, utaendelea kusimama kama tunu ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwaka jana Mwenge ulizimwa Simiyu, Mtukufu Rais John Pombe Magufuli alizuia misafara ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na baadhi ya Wakurugenzi na kuokoa kiasi cha pesa sijui zaidi ya shilingi bilioni sita.

Nataka kujua kwa mwaka mzima kukimbiza Mwenge wa Uhuru kunagharimu Taifa hili shilingi ngapi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Keissy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimwa Keissy kwa kutambua namna ambavyo Mwenge huu wa Uhuru kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais ultiweza kuokoa fedha nyingisana ambazo zilikuwa zikitumiwa na Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine kuhudhuria katika mbio hizo za Mwenge. Tumekubaliana kwamba ni lazima tuendelee kuthamini namna nzuri ya matumizi ya fedha katika kukimbiza Mwenge wa Uhuru. Kwa hiyo, hilo halina shaka Mheshimiwa Keissy na sisi tunalisimamia vizuri kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Mwenge wa Uhuru ambayo Mheshimiwa Keissy anataka kujua ni kiasi gani zimekuwa zikiandaliwa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine. Hivyo kama anataka kujua ni kiasi gani bajeti zinatumika katika kila Halmashauri moja kwenda nyingine nitamuomba aonane na mimi na tutawasiliana na hizo Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea. Mwenge utadumu na utaendelea kutembezwaa nchi nzima. (*Makofii*)

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe na linaulizwa kwa Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Na.141

### **Kuongeza Bajeti ya Ujenzi na Vifaa Tiba**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Waathirika wa UKIMWI katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wamekuwa wakipoteza maisha haraka zaidi

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

kutokana na kutembea umbali mrefu kwenda kupata huduma za matibabu.

Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya ujenzi, vifaa tiba na dawa katika kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Njombe ilitengewa bajeti ya shilingi 295,000,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo mpaka Machi, 2017 tayari shilingi 87,000,000 zilipelekwa na kuelekezwa katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya afya. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri hiyo imetengewa bajeti ya shilingi 433,000,000 sawa na ongezeko la asilimia 47. Vilevile Serikali imeongeza fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kutoka shilingi milioni 259.4 zilizotengwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi milioni 306.2 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 18. Fedha hizo zinatumika kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri inatakiwa kutumia makusanyo ya Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) ili kuhakikisha vifaa tiba vinapatiwana pamoja na dawa katika vituo vinavyotoa huduma ya afya. Serikali itaendelea kuongeza fedha kila mwaka na kushirikiana na wananchi ili kuimarisha huduma za afya Wilayani Njombe na Tanzania kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joram Hongoli swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa dawa za kurefusha maisha kwa waathirika hawa wa UKIMWI zimekuwa zikitolewa kwenye vituo vy'a afya na kwenye zahanati chache. Kwa nini sasa Serikali isitoe huduma hizi kwenye zahanati zote ili kuwapunguzia wananchi hawa ambaao wameathirika kutembea umbali mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, waathirika hawa au hawa watu wanaoishi na Virusi vy'a UKIMWI wanaoishi vijijini sehemu kubwa ndio waathirika pia kwa maana ya umaskini. Kwa nini sasa Serikali isiweke utaratibu wa kuwakopesha waathirika hawa kwenye vikundi mikopo midogo midogo ili waweze kupata fedha waweze kufanya shughuli ndogo ndogo kama vile kilimo, kufuga na bustani ili kuwainua kiuchumi au kuweza kupata fedha za kuweza kujikimu kwa maana ya kuwasaidia kuishi vizuri kwa kupata mahitaji madogo madogo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ikiwezekana hizi dawa zitolewa katika zahanati zote, naomba niseme sasa hivi tumeanzisha zile *center* maalum na tutambue kwanza zoezi hili lilipoanza tulikuwa tunafanya katika Hospitali za Wilaya lakini tuka-scale up hii programu sasa imeenda katika vituo vy'a afya mpaka zahanati.

Kwa hiyo, tunachukua hoja hii ya msingi lengo kubwa ikiwa ni jinsi gani tutafanya tuwasaidie wananchi wetu waweze kupata huduma kwa karibu.

Kwa hiyo, tutashirikiana na wenzetu Wizara ya Afya, kuangalia tufanyeje mambo yetu ya kisera ili wananchi wetu

wa Tanzania ambao wameathirika na janga la UKIMWI waweze kupata tiba kwa maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili amesema kwamba hawa waathirika wengi wao ni maskini, ni kweli na ndiyo maana ukiangalia mipango ya Serikali hivi sasa hata ule mpango wa *TASAF*, lengo kubwa ni zile kaya maskini ambazo upatikanaji wa fedha inakuwa ni tatizo tunaziingiza katika mpango wa *TASAF* ziweze kupata fedha kuweza kujikumu katika maisha yao.

Hata hivyo, nizielekeze Halmashauri zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa vile tunakuwa na mpango maalum wa kuziwezesha familia zetu hasa za wanawake na vijana ambapo asilimia tano ni kwa vijana na asilimia tano ni kwa wanawake, tuangalie kama tuna watu ambao wameathirika basi familia hizi tuzipe kipaumbele katika suala zima la mikopo ili waweze kushiriki katika suala la uchumi ili kujikomboa na umaskini. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika swali la msingi muuliza swali Mheshimiwa Joram Hongoli alisema kwamba wamekuwa wakipoteza maisha kule Njombe kutokana na kutembea umbali mrefu bila kupata matibabu.

Pia kule Njombe na maeneo mengine ya karibu kuna tatizo au tabia ya kurithiana wajane na wagane pale ambapo mmoja amefariki bila kupimwa vizuri afya zao. Wengine wamekwenda mbali zaidi, kumekuwa na tabia ya kwenda katika mapango jambo ambalo linaongeza matatizo ya VVU na UKIMWI na viongozi ndani ya Halmashauri wamekuwa wakilifahamu suala hili.

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada ili kuhakikisha kwamba tabia ya kurithiana wajane na wagane na matambiko katika mapango unakomeshwa katika maeneo hayo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, suala analozungumzia Mheshimiwa Masoud ni kweli ni jambo halisia na lipo. Miiongoni mwa sababu kubwa zinazosababisha hili janga la UKIMWI liweze kuongezeka ni ile tabia ya kwamba mtu amefariki halafu mtu mwingine anamrithi, lakini kuna visababishi mbalimbali. Jukumu letu kubwa hapa sisi kama Serikali ni kutoa elimu kwa wananchi ni vitu gani ambavyo vinasababisha ongezeko la UKIMWI katika maisha yetu. Katika suala hili zima la kurithiana, Serikali imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kwamba utaratibu ule wa zamani wa kimila kwamba mtu amefariki bila kujua afya zao zikoje basi shemeji au mtu mwingine anamrithi si utaratibu mwema.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa hiyo, tunaelekeza maeneo mbalimbali hasa katika Halmashauri zetu kwa sababu Serikali za Mitaa ziko kwenye maeneo yote kuendelea kutoa elimu hii. Ni vyema wananchi wote sasa wajue kwamba programu ya upimaji wa afya zetu ni jambo la msingi kwa sababu sio wagane peke yake hata katika hali ya kawaida katika suala zima la ndoa ajenda ya kupima afya zetu ni jambo la msingi ili kuzilinda familia zetu na watoto watakaozaliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, Hospitali ya Kibena katika Jimbo la Njombe Mjini ndiyo inayotumika kama Hospitali ya Mkoa wa Njombe lakini haina kipimo cha *x-ray*.

Je, Serikali ipo tayari kutuwezesha wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini mashine ya *x-ray* ili iweze kusaidia wananchi wote wa Mkoa wa Njombe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza niseme kwamba amehamisha goli, goli limehama kutoka katika swalii la msingi, hii ni kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anaguswa na wananchi wa Njombe. Ni kweli pale hakuna *x-ray* na tulivyofika pale ilibainika kweli changamoto kubwa pale ni *x-ray*. Hata hivyo, tulitoa maelekezo kwa Halmashauri katika mipango yao ya bajeti kuhakikisha wanapata *x-ray*, aidha, kwa kupata mikopo kutoka NHIF au kutumia mikakati yoyote kupata *funds*.

Napenda nimtaarifu Mbunge kwamba suala hili tumelichukua na tutakaa pamoja naye kuangalia tufanye nini ili tuwaokoe wananchi wa pale Njombe wanaohudumiwa na Hospitali ya Kibena kupata *x-ray* kwa sababu mtu akiumia inakuwa shida. Tunatambua eneo hilo imepita barabara kubwa ya magari yanayotoka Songea, kwa hiyo, ajali zikitokea pale lazima waweze kupimwa na vipimo hivyo vya *x-ray*. Kwa hiyo, nitaomba tukae pamoja kuona ni jinsi gani tutakuwa na mpango mkakati, Halmashauri na Serikali tubadilishane mawazo ya jinsi ya kupata *x-ray* katika Hospitali ya Njombe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kilema inahudumia zahanati zaidi ya 13; lakini zahanati hizo zina upungufu mkubwa wa vifaa tiba pamoja na watumishi ambapo zahanati ya Miwaleni imefungwa kabisa kwa kukosa watumishi. Ni nini tamko la Serikali kuhusu watumishi hawa kwenye zahanati zote 13? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Mbatia ali-raise concern hii nadhani wki iliyopita kuhusu hospitali hii. Mimi nafahamu wazi hata katika zoezi letu hili la uhakiki wa watu walioghushi vyeti, katika sekta ya afya tutakuwa na changamoto kubwa sana ya kukosa wataalam. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais juzi alitoa maelekezo kwamba tutakuwa na ajira takribani 52,000 lakini mionganoni mwao watakuwa ni wa kada ya madaktari, wahudumu wa afya pamoja na wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira mpya tutaipa kipaumbele zahanati yake kwa sababu tunajua kuna vifaa vingi vimewekezwa ni lazima tupate wataalam wa kufanya ile. Kwa hiyo, tutalichukulia kwa umakini mkubwa ili kuwasaidia wananchi wa Vunjo waweze kupata huduma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa suala la umbali linalowakabili wagonjwa wa UKIMWI kule Njombe ndilo hilo hilo ambalo linawakabili akina mama wajawazito wa Jimbo la Mwibara. Kutoka katika Kituo cha Afya cha Kasiguti pamoja na Kisorya kwenda Hospitali ya Misheni ni takribani kilometra 40. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili la bajeti kuambatana na mimi ili twenda kwenye Kituo cha Afya cha Kisorya na Kasuguti ajionee namna ambavyo wananchi wametumia nguvu zao kujenga wodi ili Serikali iweze kutusaidia kukabiliana na changamoto ya umbali mrefu inayowakumba akina mama wajawazito?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na Waziri wangu Mheshimiwa Boniface Simbachawene tumekuwa na mkakati mkubwa sana wa kuyafikia maeneo

mbalimbali. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hapa tutaangalia tufanye utaratibu gani ili tuweze kufika katika maeneo yake, lakini siyo hapo peke yake tutafika mpaka Rorya pamoja na Tarime kule kwa sababu kuna changamoto mahsusii katika Mkoa wa Mara ambazo lazima twende tukazifanyie kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali letu namba 142 na linaulizwa na Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 142

**Malipo kwa Watumishi Waliohamishiwa  
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa**

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ni mionganii mwa Halmashauri mpya zilizoanzishwa mwaka 2015 na watumishi 98 waliohamishiwa kutoka Halmashauri za Sengerema, Misungwi, Ilemela, Jiji la Mwanza, Kwimba na Magu lakini watumishi hawa hadi sasa hawajalipwa fedha za uhamisho:-

Je, ni lini Serikali itawalipa stahiki zao watumishi hawa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ni mionganii mwa Halmashauri zilizoanzishwa Julai,

2015 baada ya kugawanywa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Watumishi 98 waliohamishwa Buchosa kutoka Halmashauri za Sengerema, Illemela, Jiji la Mwanza, Kwimba na Magu wanadai jumla ya shilingi 354,075,500 na tayari madai ya shilingi 44,531,000 yamelipwa kwa watumishi 16. Hadi Disemba, 2016 Halmashauri imebakiwa na madeni ya uhamisho kwa watumishi 88 wenyewe jumla ya shilingi 292,531,000. Madeni hayo yaliyobaki yamewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uhakiki ili yalipwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kemilembe.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ila nina swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili na siku ya Mei Mosi ametoa tamko watumishi wote watakaohamishwa vituo vyao walipwe fedha zao kabla ya uhamisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini kuna baadhi ya watumishi wengi tu ambao wamehamishwa kwenye vituo vyao vya kazi, wameenda kwingine na hawajalipwa fedha zao za uhamisho mpaka leo. Kuna baadhi ya taasisi hata waliohamishiwa hapa Dodoma Makao Makuu hawajalipwa fedha zao mpaka leo.

Sasa ni lini Serikali italipa fedha za watumishi hawa waliohamishwa na hawajalipwa fedha zao za uhamisho? Nashukuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa concern ya Mheshimiwa Mbunge na siku zote maswali yake yamekuwa yakigusa wananchi wake na hasa watumishi, nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu ilifanya zoezi la uhakiki wa madeni kwa sababu tuna Halmashauri mpya nyingi sana zimeanzishwa. Kwa mfano, siku nilivyofiga pale Busega au kwa mtani wangu Tabora Vijijini kwenye Halmashauri mpya ya Isikizya, nimekutana na watumishi wakilalamikia suala hili la madeni. Ndiyo maana ofisi yetu tukafanya uhakiki wa madeni na tumeyawasilisha Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazunguka maeneo mbalimbali tumekuta baadhi ya Halmashauri tayari madeni haya yameshaanza kulipwa. Kwa hiyo, kwa sababu uhakiki ulishafanyika na taarifa iko Hazina tufanye subira na wengine wameshaanza kulipwa na madeni yao yote yatalipwa kwa sababu Serikali haitaki kuona haki za watu zinadhulumiwa.

**MWENYEKITI:** Namuona Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Selemani Jafo kwa majibu mazuri, lakini pia Mheshimiwa Kemilembe kwa swali zuri ambalo kusema ukweli linawagusa watumishi wengi na hasa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia za Wakurugenzi wa Halmashauri kuwahamisha na hasa walimu kwa kuwakopa garama ambazo wangepaswa kuwalipa kwa ajili ya usumbufu na garama za uhamisho.

Nilisema hapa Bungeni hadi tarehe 30/04/2017 wanapaswa kuwa wamewalipa walimu waliowahamisha. Hili nililisema si kwa madeni ya nyuma sana ya uhamisho maana yale yote tulishayapeleka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kulipwa, lakini kuna uhamisho uliofanyika kati ya mwezi Januari hadi Machi wa kupanga ikama za walimu. *Deadline* imefika na kuanzia sasa Wizara yangu itachukua hatua kwa wale wote ambao hawajawalipa walimu waliowahamisha. Haiwezekani Serikali tunapambana kupunguza madeni lakini

wako watu wengine ni viwanda vya kuzalisha madeni yasiyokuwa na sababu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kusema ukweli suala hili tumelitilia msisitizo mkubwa lakini pia Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa fedha kwa ajili ya kupanga hizi ikama kwa nchi nzima kwa Halmashauri zote. Zoezi hili litaenda sambamba na malipo ya moja kwa moja kwa watumishi watakaohamishwa kwa sababu ni haki yao ya msingi ya kiutumishi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyoko huko Buchosa yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko Itigi katika Halmashauri mpya ya Itigi. Wakati Halmashauri hii inaanizishwa ilipata watumishi kutoka Halmashauri mama ya Manyoni ambayo hata nayo ilikuwa na watumishi wachache na hivi tunavyozungumza Halmashauri ya Itigi pia imekutana na janga hili la vyeti *fake*, kuna baadhi ya watumishi ambao wameondoka, je, Serikali iko tayari sasa itakapotoa ajira kutuletea watumishi wa kutosheleza katika Halmashauri mpya ya Itigi? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massare kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua upo upungufu na kama ambavyo tumekuwa tukieleza humu

ndani, mwaka kesho tunatarajia kuajiri zaidi ya watumishi wapya 52,436. Jana tu pia tayari Mheshimiwa Rais alishaagiza, tumetoa kibali cha watumishi wapya 15,000 kwa ajili ya kwenda kuziba pengo la watumishi ambao wamekutwa na vyeti vya kughushi, lakini vilevile kuweza kuziba ikama na tutaendelea kufanya hivyo kila mara itakapobidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ambayo yametolewa kuhusiana na suala la kuhamisha watumishi katika Halmashauri zetu lakini suala hili limekuwa sugu sana. Ukiacha hao walimu ambao wamewazungumzia lakini wapo pia wauguzi, watendaji wa kata na vijiji. Mimi kama Mbunge au Diwani naweza kwenda kwa Mkurugenzi nikamuambia Mtendaji huyu simtaki mpeleke katika kijiji au kata nyingine bila kujali stahiki zake. Ni nini sasa kauli ya Serikali kuhusu watumishi hawa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Mheshimiwa Sikudhani ni kweli na hili sisii viongozi tunatakiwa tujitathmini kwamba wakati mwingine una *interest* zako binafsi unasababisha mtu fulani ahame kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine bila kujua kwamba unalimbikiza madeni katika maeneo hayo. Bahati mbaya sana wakati mwingine Mkurugenzi akikataa ndiyo unaanza bifur (kutokuelewana) naye kuanzia hapo kwamba Mkurugenzi huyu hatufai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba utaratibu wa kuhamisha kama alivyozungumza Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Boniface Simbachawene ni lazima uendane na bajeti iliyokuwepo. Vilevile si vyema kwa viongozi wowote kuwaweka katika mazingira magumu

watumishi hawa na kuwa *frustrate* kwa kuwahamisha bila sababu yoyote. Tunasema jambo hilo likome na lisiendelee katika Halmashauri zetu kwa sababu haliletii afya kwa watumishi wetu ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mawaziri na Naibu Waziri, kwa Wilaya ambazo ni mpya na Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia suala la Busega kwamba alikuta pale matatizo ya watumishi, je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Wilaya hizi mpya ambazo zimeanzishwa zenyehu haba wa ikama ya watumishi? Vilevile pili baadhi ya watumishi walio wengi hawajalipwa mafao yao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu pale awali ni kwamba tutajitahidi Halmashauri hizi mpya ambazo zimeanzishwa na bahati nzuri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) amezungumza wazi kwamba tuna hizi ajira mpya ambazo zinakuja lengo kubwa ni kuziba mapengo yote yaliyokuwepo katika maeneo yetu. Ofisi yetu imeshaanza kufanya tathmini ya kujua ni watumishi wangapi wanahitajika katika Halmashauri gani ili kuziba haya mapengo yaliyopo. Kwa hiyo, mtani wangu Mheshimiwa Dkt. Chegeni ondoa hofu zoezi hili litaweza kujibu matatizo ya watumishi katika Jimbo na Halmashauri yako ya Busega.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Kibaigwa unakua kwa kasi sana na kwa sasa mji ule ni Mji Mdogo. Hata hivyo, kwa kuwa hatuna watumishi wa kutosha na mji ule haujafanywa kuwa mamlaka, naiomba Serikali sasa ituambie ni lini Mji wa Kibaigwa utapewa mamlaka ili waweze kupanga shughuli za mji wao na kupewa watumishi wa kutosha kuendeleza Mji ule Mdogo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, toka asubuhi nimesema leo kuna utaratibu wa kuhamisha goli katika uwanja. Naomba nikuambie Mheshimiwa Felister Bura kwamba hoja yako imesikika na lengo letu ni kupanga miji hili yetu yote vizuri, kuna Kibaigwa, Kibakwe na maeneo mengine katika Mkoa wako wa Dodoma najua inakua kwa kasi sana. Hata hivyo, wakati tunajielekeza katika mipango ya Mamlaka ya Miji Midogo tutajielekeza jinsi gani tupate watumishi kuweza kuziba nafasi hizo ili wananchi wetu wapate huduma vizuri. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo naona Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tena kwa sababu jambo hili limekuwa likiwigusa Waheshimiwa Wabunge wengi na katika maeneo mengi na hasa pale inapoanzishwa Mamlaka za Miji Midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutaratibu mwenye dhamana ya kuendeleza miji hii kuweza kuanza kufanya

shughuli zake inapokuwa imeanzishwa Mji hii Midogo ni Halmashauri Mama. Kwa hiyo, inapokuwa Serikali tumekubali kwamba mji huo uanze mipango yote na utaratibu wa uanzishwaji unaanzia kwenye Halmashauri Mama kujengea uwezo Halmashauri hiyo ya Mji Midogo ili iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwasihii Waheshimiwa Wabunge kwamba mipango yote itapaswa iingie kwenye mipango ya Halmashauri Mama na ndipo sasa kwa yale maeneo ya upungufu wa watumishi Serikali inaweza kuwaleta. Hata hivyo, kama hakuna bajeti au mpango kutoka kwenye Halmashauri Mama sio rahisi kwa Halmashauri hizo za Mji Midogo kuweza kuanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ryoba, Mbunge wa Serengeti.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye Jimbo langu la Serengeti katika process za kuongeza vijiji, vitongoji na kata, kuna baadhi ya maeneo ambayo utaratibu haukuuatwa, baada uchaguzi kuna Serikali za Vijiji walijiuuzuru. Kwa hiyo, kimsingi kuna migogoro ya mipaka kati ya vijiji na vijiji na mpaka ninavyoongea hakuna uongozi kwenye vijiji hivyo. Nini tamko la Wizara kuhusu maeneo ambayo yana migogoro ya mipaka kati ya vijiji na vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba iko migogoro mbalimbali lakini migogoro inatofautiana, iko mipaka ya kijiji kwa kijiji, kata kwa kata, iko ya aina nyingi na kwenye orodha tumeorodhesha zaidi ya 250 kwa nchi nzima.

Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mazingira ya migogoro hii inatofautiana kutoka mgogoro mmoja hadi mwingine hatuwezi kuwa na tamko la pamoja

kwa hiyo atuletee ili tuweze kuona hiyo *scenario* ikoje ili tuweze kutatua mgogoro husika ikiwa ni pamoja na mamlaka za uongozi wa maeneo husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa, nimewapeni muda wa kutosha, tunaenda swali namba 143, linaulizwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti.

Na. 143

### **Mamlaka ya Mji Mdogo-Kibiti**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Wananchi wa wa Kibiti wanaishukuru Serikali kwa kupata Mji Mdogo Kibiti na kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti na viongozi.

(a) Je, kuna tatizo gani hadi leo Mamlaka ya Mji haijaanza kazi na kumpata Meya?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka Mkurugenzi wa Mji Mdogo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Jafo majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ni mpya na ilianzishwa rasmi Julai, 2016. Halmashauri hiyo ilipatikana baada ya kugawanywa kwa Halmashauri Mama ya Rufiji ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Sababu kubwa iliyochelewesha uundwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibiti ni ufinyu wa bajeti. Hali hiyo imechangia Halmashauri kushindwa kuitisha uchaguzi mdogo kujaza nafasi zilizo wazi za Wenyeviti wa Vitongoji ili kuunda Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo pamoja na Mwenyekiti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Halmashauri hiyo inajidesha kwa kutumia mapato ya ndani ambayo yalianza kukusanya Oktoba, 2016. Hivyo, hali ya kifedha itakapokuwa nzuri, Halmashauri itafanya uteuzi wa Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo pamoja na kukamilisha uchaguzi wa Mwenyekiti ili Wenyeviti hao waweze kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo anayetakiwa kuchaguliwa mionganoni mwa Wenyeviti hao wa vitongoji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ungando swalii la nyongeza.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kutokana na vitendo vya uhalifu vinavyoendelea ambavyo vinasababisha Kibiti kushindwa kukusanya makusanyo yake ya ndani, je, Wizara italiangaliaje kwa jicho la huruma ili kuhakikisha wanapata Mwenyekiti wao wa Mamlaka ya Mji Mdogo Kibiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu la pili, kutokana na ukweli kwamba Kibiti ni Halmashauri mpya Mkurugenzi na *DC* hawana vifaa vya kutenda kazi kama magari. Je, Serikali inaliangaliaje hilo kwa jicho la huruma? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba

nitoe pole kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Kibiti na Rufiji kwa tatizo kubwa linaloendelea pale kwa sababu mpaka hivi sasa tumpoteza Wenyeviti wengi sana na hali hiyo inaogopesha.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko na wananchi wa Kibiti na Rufiji na tutaangalia nini cha kufanya kwa sababu sasa hivi ukiitisha uchaguzi pale hata Wenyejekiti wenyeewe kujitokeza kugombea nafasi yenyeewe wanaogopa.

Kwa hiyo, Serikali inafanya kazi ya kurudisha hali ya utulivu na amani ili hali ya usalama iweze kukaa vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge amini kwamba Serikali yako itashirikiana na wewe kama inavyofanya hivi sasa ndiyo maana timu ya Mkoa wa Pwani iko kule *site* kuhakikisha mambo yanakaa sawa. Kwa hiyo, hili jambo tumelichukua kwa moyo wa dhati kabisa na tutashirikiana kupata ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyejekiti, swali la pili la changamoto ya magari, ni kweli na Mheshimiwa Ungando nikushukuru sana, tulipotembelea vile visiwa 40 vya delta kule tulifanya kazi kubwa sana, tokea asubuhi mpaka tulivyomaliza saa mbili usiku, nimebaini changamoto hizo. Ndiyo maana kipindi kile nilivyorudi haraka tukafanya utaratibu kuwaaletea gari moja pale la *Road Fund*. Hata hivyo, Serikali imeona hili tatizo kwa DC na Mkurugenzi tutajitahidi nini tufanye kwa pamjua kuisaidia Halmashauri hii mpya ambayo ina changamoto kubwa sana katika suala zima la vitendea kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyejekiti, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyejekiti, kwa kuwa Mamlaka ya Mji wa Lushoto sasa hivi ina zaidi ya miaka nane. Je, Serikali haioni sasa imefikia wakati wa kuipandisha hadhi kuwa Halmashauri

ya Mji wa Lushoto ukizingatia Mheshimiwa Jafo alitembelea kule na kuona Mji wetu wa Lushoto jinsi unavyopendeza na ulivyokuwa mkubwa? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jafo Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani *concern* hii Mheshimiwa Mbunge aliileta ofisini kwetu na ndiyo maana Waziri wangu aliniagiza niweze kufika Lushoto kule na nimeweza kufika. Kimsingi wana mambo mengi, kuanzisha hii Mamlaka ya Mji wa Lushoto, suala zima la Halmashauri ya Mlalo, kuna mambo mengi sana yamejitokeza kule. Kwa hiyo, kama Serikali Waziri wangu alituma timu kule ikaenda kufanya *assessment* na taarifa zile ziko Ofisi ya TAMISEMI katika uchambuzi pale itakapoonekana kwamba vigezo vyote vimekidhi basi hakutakuwa na tatizo. Mheshimiwa Shekilindi naomba vuta subira tu wakati maamuzi yanaenda kufanyika kwa kuangalia kama imekidhi vigezo mbalimbali basi mtapata jibu halisi. Na mimi nimefika pale nimeona ile hali halisi basi tuache michakato iweze kuendelea baadaye tufanye maamuzi sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sitakuwa mbali sana na wanaohitaji miji ipandishwe hadhi. Kwa kuwa kata ya Majimoto sasa imekuwa kubwa kiasi ambacho inatakiwa kupandishwa hadhi na tumekwishaleta maombi katika Wizara inayohusika. Je, ni lini sasa maombi hayo yatashughulikiwa ili kata ya Majimoto iwe Mji Mdogo?

**MWENYEKITI:** Kata ya Maji Moto kuwa Mji Mdogo ni lini, Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupandisha hadhi na naomba nijibu na Wabunge wengine

kwa sababu nimeona wengi wamesimama humu ndani na *concern* yao wote inafanana na ndiyo maana tuliunda kikosi kazi kwenda kupitia maeneo mbalimbali ikiwemo kwako Majimoto Mheshimiwa Mbunge. Jambo lile sasa liko ofisini kwetu linafanyiwa uchambuzi wa kina, naomba nikutoe hofu kwamba uchambuzi ule wa kina ukishafanyika basi maamuzi sahihi yatafanyika kwa mujibu wa sheria ambapo Waziri mwenye dhamana amepewa mamlaka hayo. Naomba vuta subira tu wakati kazi hii inawekwa vizuri lakini siyo Majimoto peke yake nikifahamu Dongobesh kule na maeneo mengine wote *concern* yao ni hiyo hiyo, kwa hiyo kama Serikali inafanya kazi kwa upana wake suala hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi naomba nifahamu, Jimbo la Kilombero lina Halmashauri mbili, Halmashauri ya Mji wa Ifakara wenye kata tisa na Halmashauri ya Kilombero yenye kata kumi. Kama ambavyo Jimbo la Bariadi ambalo lina Halmashauri mbili, Bariadi Vijijini kuna kata ishirini na moja na Bariadi Mjini kuna kata kumi. Hata hivyo, Mbunge wa Kilombero amezuiliwa na alizuiliwa kushiriki vikao vya Halmashauri ya Kilombero. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Uliza swali tu sasa.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotaka kushiriki nimefungwa miezi sita. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwenzangu anashiriki mwanzo mwisho sehemu zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nifahamu, ni kwa nini mimi wa Kilombero siyo tu kwamba nimezuiliwa kushiriki vikao hata kufanya maamuzi kwenye hizi kata zangu kumi sishiriki, lakini mwenzangu wa CCM anashiriki? Sasa

naomba Waziri aniambie ni kwa nini ubaguzi huu unafanyika dhidi yangu halafu mwenzangu wa CCM anaachiwa afanye kazi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu inawezekana vipi Mbunge wa Kilombero nazuiliwa kushiriki vikao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mimi sikukuruhusu kutoa hotuba humu, nimekuruhusu kuuliza swali. Haya majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Lijualikali ni Mbunge ambaye ana Halmashauri mbili. Kama zilizovyo haki za Wabunge wengine katika majimbo yao na katika Halmashauri zao wanapaswa kuwa wajumbe wa vikao mbalimbali ikiwepo Kamati ya Mipango na Fedha lakini pia na Baraza la Madiwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa vigumu sana kulisema jambo hili kwa sababu mhusika angepaswa tu *ku-balance interest* za maeneo yote na akaweza kufanya Ubunge wake. Kinachotokea ni pale ambapo mhusika pia ni Diwani na Diwani wa upande mmoja wa Jimbo. Kwa hiyo, *scenario* yake haiwezi ika-fall in all four angles kama ilivyo *scenario* ya Bariadi. Kwa sababu hiyo Mheshimiwa Mbunge anayo maelekezo yangu ambapo mimi na yeye tulizungumza sana jambo hili tukiwa pamoja na Mheshimiwa Kiwanga ambayo hayo hayatekelezi. Hivyo, kwa sababu ameleta jambo hili hapa Mheshimiwa Lijualikali ofisi yangu ipo, njoo tuzungumze tuone huo ugumu unaoupata na kwa nini haitokei hivyo, tutalimaliza jambo hili, nakukaribisha sana ofisini.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeshapata majibu mazuri tu. Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize swali kwamba

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

mwaka 2013 Mji Mdogo wa Igunga ulianzishwa na tumekuwa na tatizo hili ambalo wanalisema wote kwamba umeanzishwa lakini haufanyi kazi. Namshukuru Waziri ameeleza kwenye swali namba 142 kwamba ni Halmashauri inatakiwa isimamie, lakini sisi tumejaribu kuishauri Halmashauri isimamie jambo hilo na nimeweza kufika ofisini kwake mara moja na akaahidi kwamba angeweza kuandika Waraka wa kumwambia Mkurugenzi au kuiambia Halmashauri ifanye jambo hilo na halijafanyika.

Namuomba Mheshimiwa Waziri hebu utusaidie kwa sababu *DED* sasa hivi hataki kabisa kuisikiliza hiyo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Igunga na hawana bajeti, hawana gari, wana mtendaji tu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie kama ikiwezekana njoo Igunga ili mamlaka hii iweze kuanza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia swali la Mheshimiwa Mbunge na tutawasiliana tuone namna bora ya kulifanya jambo hili kwa sababu ni kweli tumekwishazungumza na ni kweli nilikwishatoa maagizo lakini halitekelezeki. Kama nilivyosema, mamlaka hizi zinapoanzishwa zinalelewa na Halmashauri Mama. Kwa hiyo, kama hakuna mipango madhubuti inayopanga mchakato wa namna ya kutafuta rasilimali fedha na rasilimali watu basi tatizo linakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, tutajaribu kuliona namna liliyo na halina tofauti sana na *scenario* za Miji mingine Midogo iliyoanzishwa ili tuone namna bora ya kuweza kulifanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana katika Halmashauri mbalimbali nchini baada ya kauli

ya Mheshimiwa Rais katika sherehe za Mei Mosi juzi kule Kilimanjaro alivyosema kwamba Halmashauri yoyote au Baraza lolote la Madiwani litakalojiteza na kutaka kumuondoa Mkurugenzi kazini au kumfukuza, Baraza hilo litavunjwa mara moja na ye ye ndiye mwenye mamlaka ya kumteua Mkurugenzi kwa hiyo atahakikisha anaifuta Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Madiwani ndiyo wasimamizi wa shughuli na miradi ya maendeleo na mapato na matumizi ya fedha za Halmashauri.

Je, Mkurugenzi akiwa ametumia fedha vibaya na akatumia madaraka yake vibaya, ni utaratibu gani ambao Waheshimiwa Madiwani watautumia kama siyo kumuondoa Mkurugenzi wakati Rais tayari ameshawaonya na amewaambia kwamba ataivunja Halmashauri hiyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu ya kisheria tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba kauli ya Mheshimiwa Rais imeleta mkanganyiko. Kauli ya Mheshimiwa Rais imemaanisha pale ambapo mkakati unafanywa na Waheshimiwa Madiwani kumuondoa Mkurugenzi kwa maslahi binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wa mwaka wangu mmoja na miezi kadhaa yote mawili yanatokea, wakati mwingine kunakuwa na mkakati wa upande wa watumishi kumuondoa Mwenyekiti na wakati mwingine kuna mkakati kwa upande wa Madiwani kumuondoa Mkurugenzi kwa sababu tu maslahi yamegongana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anapolizungumzia hili hazungumzii kwa scenario unayoisema ya kwamba kumetokea ubadhirifu na wala Mheshimiwa Rais halindi wabadhirifu, anazungumzia pale ambapo kuna utaratibu unapangwa wa Madiwani

kumuondoa Mkurugenzi anayesimamia watu wasifanye wizi, ndicho anachokizungumzia.

Kwa hiyo, huo mfano mwagine baki nao lakini wa Rais ni huu aliokuwa anausema kwamba pale kunapokuwa kuna mkakati wa kumuondoa Mkurugenzi ambaye anasimamia fedha za Halmashauri hapo yuko tayari kuivunja Halmashauri na mimi mwenyewe nasema wala haitafika hata kwake mimi mwenyewe nitavunja hiyo Halmashauri. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii namba 144 linaelekezwa kwa Waziri wa Nishati na Madini na linaulizwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 144

**Kukosekana kwa Umeme katika  
Vijiji vinavyozunguka Tagamenda Substation**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

*Tagamenda Substation* ni kituo kikubwa kati ya vituo vinavyosafisha umeme wa Gridi ya Taifa kwani kinapokea umeme kutoka Mtera, Kidatu na Kihansi, lakini vijiji vya Tagamenda, Ikuvilo na Wangama vinavyozunguka kituo hicho havina huduma ya umeme ingawa ndivyo vinalinda kituo hicho.

(a) Je, ni kwa nini Serikali inashindwa kutoa huduma ya umeme katika vijiji vinavyozunguka kituo hicho?

(b) Je, ni sababu gani zinazofanya vijiji hivyo kukosa kupatiwa huduma hata ya umeme wa *REA*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitongoji cha Malulumo Kijiji cha Tegamenda kiliwekwa katika Mpango wa kupatiwa umeme kuitia Shirika la Umeme *TANESCO* katika mwaka 2015/2016. Kazi hiyo ilianza Mei, 2016 na inakamilika Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za kupeleka umeme katika Kitongoji hicho zimejumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa umeme wa kilovoti 33 yenyе urefu wa kilometa moja; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenyе urefu wa kilometa 1.4; ufungaji wa transfoma moja pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 70. Kazi hii imekamilika kwa asilimia 90 na inagharimu shilingi billioni 93.1.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijiji Awamu ya Tatu umeanza nchi nzima tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele-mradi vitatu vya *densification, grid extension* pamoja na *off-grid renewable* vinavyolenga kuongeza wigo wa umeme katika vijiji vyote nchini, vitongoji vyote vilivybaki, taasisi za umma na maeneo ya pembezoni ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na visiwa. Vijiji vya Irukilo, Wangama pamoja na maeneo mengine ya kijiji cha Tagamenda vimewekwa katika utekelezaji wa Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu wa *Densification* na *Grid Extension* utakaokamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenyе urefu wa kilometa 10.3; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenyе urefu wa kilometa 9.7; ufungaji wa transfoma tatu pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 300. Gharama ya kazi hii ni shilingi billioni 14.45.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega. Waheshimiwa Wabunge, itabidi msubiri Wizara yenyewe, naona nyumba nzima imesimama, haya.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kuwa *REA III* meanza Machi, 2017. Kwa kuwa wananchi katika vijiji hivyo vya Wangama, Ikuvilo, Tagamenda, Lupembelwasenga pamoja na Lyamzungwe ni wakulima na wanajihuisha na kilimo cha umwagiliaji na kuna wawekezaji ambao wameonesha nia ya kujenga viwanda na tunasema tunahitaji Tanzania ya viwanda lakini umeme haupo. Naomba *commitment* ya Serikali ni lini watapata umeme kwa sababu imekuwa ni muda mrefu kutopatiwa umeme katika maeneo hayo ili wanufaikie na viwanda? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika kipengele cha kwanza majibu ya Waziri ni tofauti kabisa na hali halisi ya eneo hilo la Malulumo kwa sababu mimi natokea eneo hilo na wanasema utekelezaji umefanyika kwa 90%. Je, Waziri yuko tayari kuongozana na mimi akaone huo utekelezaji wa 90% uliopo maeneo yale? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na swali la pili, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Grace kwenda kwenye eneo lake ili kuangalia utekelezaji wa Mradi wa *REA Awamu* ya Tatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Grace tukimaliza Bunge tu mguu mmoja mimi na wewe Iringa tukamalize kazi hiyo, lakini kwa ruhusa yako Mwenyekiti. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Grace na Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa kwa jinsi ambavyo wanafuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme. Niwahakikishie kwamba tarehe 21 Machi, 2017

tulizindua rasmi utekelezaji wa Mradi wa Umeme Awamu ya  
Tatu katika Mkoa wa Iringa na eneo la Iliwa kwa Mheshimiwa  
Mwamoto ndipo tulipofanya uzinduzi kwa niaba ya mkoa.  
(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwahakikishie  
kabisa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Iringa pamoja  
na Mufindi, Kilolo, Njombe, tumeshawakabidhi wakandarasi  
wawili, *NACROI* na *NAMIS* na wameshaanza utekelezaji wa  
kazi hiyo. Kwa hiyo, kuanzia Machi tumeshaanza kutekeleza  
mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo amevitaja  
Mheshimiwa Grace vya Wangama, Lupembelwasenga,  
Tagamenda na Mseke pamoja na vijiji vingine ambavyo  
amevitaja na kwa Mheshimiwa Mwamoto vitapatiwa umeme  
katika awamu hii ya mradi. Nimeenda kwa Mheshimiwa  
Mwamoto na Waheshimiwa Wabunge wengine, nimeenda  
Nang'uruwe, Kihesa Mgagao na huko tumeshawapelekea  
umeme. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge  
kwamba utekelezaji wa mradi huu umeanza na utakamilika  
mwaka 2020/2021.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo,  
atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na wa mwisho  
Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, ahsante sana. Mji wa Maswa umekosa maji kwa  
mara nyingine tena kwa muda zaidi ya wiki moja baada ya  
operesheni kata umeme. Kata umeme imeathiri hadi  
mamlaka ambazo ziko daraja la tatu ambapo kama  
Mamlaka ya Maji ya Mji wa Maswa iko daraja la tatu kwa  
hiyo bili zake zinalipwa na Wizara, hawajilipi bili wao  
wenyewe. Kwa hiyo Wizara hajjalipa *TANESCO* ...

**MWENYEKITI:** Swali sasa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** *TANESCO* wanakata.  
Swali langu, napenda kupata *commitment* ya Serikali ni lini

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Maswa watarudishiwa umeme katika Mamlaka ya Maji ili wananchi wa Maswa waweze kupata maji katika Mji wa Maswa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuona Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Injinia Isack Kamwelwe majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo nakiri kweli lipo lakini Serikali tumeekaa kikao Wizara ya Maji na Hazina pamoja na TAMISEMI tumekubaliana. Vilevile tarehe 8 Mei Makatibu Wakuu wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji watakan kukamilisha suala hili ili kuhakikisha tatizo la malipo lililokuwepo tukishakaa na Hazina tutalimaliza ili maeneo yote umeme uweze kurejeshwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka nimueleze Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa wa Mtwara ndiko inakozalishwa gesi inayozalisha umeme wa Dar es Salaam ambako haukatiki kila mara, kiasi tumeanza kuamini gesi yetu haitunufaishi ni bora tungerudishiwa yale majenereta yaliyokuwa yanazalisha umeme Mtwara wakati huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme la Mtwara linasababishwa na kuharibika kwa transfoma ya jenereta moja yake ambayo nafahamu mpaka sasa kuna mvutano mkubwa kati ya *TANESCO* pamoja na *MANTRAC Tanzania Limited* kwa ajili ya *ku-supply* ile transfoma kwa sababu ya madeni sugu ambayo *TANESCO* hawajalipa.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Waziri, naomba utueleze kinagaubaga ni lini matatizo ya *TANESCO* na

*MANTRAC*yatakwisha ili kuwarejeshea wananchi wa Mtwara umeme wa uhakika? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwoneyekiti, ni kweli kabisa liko tatizo la kuharibika kwa mashine moja Mtwara kiasi cha kushindwa kupeleka *megawatt* 18 kwa ujumla wake. Kwa sasa hivi ni kweli kabisa Mtwara wanapata *megawatt* chini ya 18, wanapata 16 na 15.6.

Mheshimiwa Mwenyekeki, pamoja na Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Mtwara na Lindi lakini hatua zilizochukuliwa ni kwamba hivi sasa ukarabati umeshaanza. Mgogoro uliokuwepo kati ya *TANESCO* na *MANTRAC* umekwisha na jenereta inatengenezwa, ni hatua ya kwanza. Hatua ya pili, Mtwara tunawaongezea mashine nyingine sita ambapo kila mashine itakuwa na *megawatt* mbili. Kwa hiyo, mtakuwa na *megawatt* nyingine za ziada 12 na jumla kuwa na *megawatt* 30. Kwa hiyo, sasa umeme wa Mtwara pamoja na Lindi maeneo ya jirani utakuwa ni wa uhakiki zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekeki, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili linashughulikiwa na baada ya Bunge hili Mheshimiwa Mbunge tutakwenda wote kukagua mashine hii ikiwa imeshakamilika na umeme unapatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje. Sasa naambiwa *gender* sijafanya haki, basi Mheshimiwa Martha Mlata atakuwa wa mwisho.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekeki, naomba niulize swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekeki, kwa kuwa vijiji vya Makutupa, Mlembule, Tambi, Bolisazima na Mgoma tayari nyaya na nguzo zimeshawekwa bado transfoma. Sasa

namuuliza Naibu Waziri, vijiji hivi vitapata lini transfoma ili waweze kuanza kupata huduma ya umeme?

**MWENYEKITI:** Tatizo ni transfoma tu, Naibu Waziri Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge Mkongwe katika Bunge hili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kulikuwa na transfoma mbili mbovu katika Jimbo lake na jana tulikuwa tunawasiliana na Meneja na amenihakikishia kwamba mwisho wa wiki hii transfoma mbili zitapatikana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje kwa niaba ya wananchi wake na nimwambie kwamba transfoma hizi mbili zitapatikana Ijumaa (kesho kutwa) mwezi huu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie, kwanza napongeza kasi ya usambazaji wa umeme lakini kuna tatizo la nguzo kwenda chache.

Naomba aniambie katika kata ya Bumanga kwenye kiwanda cha akina mama cha kusindika mbogamboga, msitiki, kanisa na shule walikosa nguzo hivyo hamna umeme, ni lini mtapeleka nguzo hizo ili waweze kupata umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mheshimiwa Mlata ameniambia kwamba kuna tatizo la nguzo, nitawasiliana na wataalam leo hii ikiwezekana mwisho wa wiki hii au wiki ijayo ziweze kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba kwa sasa nguzo, mashine na transfoma zinapatikana hapa nchini hatuagizi kutoka nje. Kwa hiyo, uhakika wa upatikanaji wa nguzo pamoja na vifaa vingine utakuwa ni rahisi zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mlata tutafuatana lakini mwisho wa wiki hii au wiki ijayo nguzo zitapatikana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, najua tuna maswali mengi ya nyongeza hasa kwenye Wizara hii, lakini muda ndiyo huo umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, yupo mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan. Huyu amewahi kuwa Mbunge wa Bunge hili kutoka Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar kuanzia mwaka 2000 - 2010. Karibu sana Mheshimiwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wanafunzi wamekuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo.

Waheshimiwa Wabunge, naambiwa pia kuna mdada mmoja mwana mitindo (*model*) yuko Marekani kule New York anaitwa Flaviana Matata. Karibu sana. Hawa ndiyo wanaitangaza nchi yetu huko nje kwa *fashion* na mtamuona hata vaa yake alivyovaa ni nadhifu kweli kweli lakini muishie hapo tu. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 4 Mei, 2017 saa 7.30 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ukumbi wa *Utawala Annex* kule *dispensary*.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine la kazi linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu,

anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 4 Mei, 2017, saa 7.000 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa Msekwa B. Wajumbe wote mnaombwa mhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo niliyonayo hapa Mezani kwa sasa, kama nitakuwa nimeghafilika basi tutaona mbele ya safari.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 46(1) juu ya maswali kujibiwa kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hii wakati Ofisi ya Waziri Mkuu ikijibu swalii la Mheshimiwa Khatib Said Haji kuhusu swalii dogo la nyongeza la muuliza swalii la msingi juu ya gharama za Mwenge, imeonekana gharama za kukimbiza Mwenge nchi nzima hazijulikani kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu bali gharama hizo zinajulikana kwa kila Halmashauri moja moja. Hivyo inaonesha bajeti ya Mwenge inayopitishwa humu huwa haiendi kwenye Halmashauri hizo na Halmashauri zinabebeshwa mzigo mkubwa sana wa kuendesha gharama za ukimbizaji wa Mwenge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Halmashauri hazina fedha ya kukimbiza Mwenge gharama zile zinahamia kwa wananchi wetu maskini kwa kubeba msalaba huo. Nataka kupata Mwongozo wa Kiti chako, huu Mwenge ni wa Serikali Kuu au ni wa Serikali za Mitaa au ni wa wananchi binafsi kama mali yao binafsi? (*Makof!*)

Naomba Mwongozo wako. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nonapotoa fursa wote mnaotaka kuomba mwongozo msimame, haya Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68, sina haja ya kuendelea kuielezea vyote lakini naomba Mwongozo wako kuhusu swali hilo hilo la Mheshimiwa Khatib kuhusu masuala ya Mwenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anaelezea, ameleezea faida kubwa sana za Mwenge hasa unapopita katika maeneo yetu lakini bado imeonekana Waheshimiwa Wabunge kutokuziona au kutozitambua faida hizo. Pia uzoefu unaonesha Mwenge karibu miaka yote unakimbizwa na vijana. Hii inaonesha sasa hivi vijana wanajua sana manufaa ya Mwenge kuliko watu wazima na hasa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mwongozo wako kwamba Serikali ione umuhimu katika wakimbiza Mwenge wale na Waheshimiwa Wabunge wachache washiriki hasa wale ambao hawajui manufaa ya Mwenge ili wakati wakimbiza waweze kuyaona yale manufaa yanayopatikana katika kukimbiza Mwenge. Naomba Mwongozo wako katika hili. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na nianze na hili la Mheshimiwa Hawa Ghasia ingawa yote yanafanana. Mheshimiwa Hawa Ghasia nadhani alikuwa anaomba kuchangia tu kwa sababu hakupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, ninapounganisha sasa na hili, Mheshimiwa Mwalimu Bilago, maana kama wewe unaamini swali la nyongeza au swali la msingi hasa halikujibiwa kikamilifu kwa mujibu wa Kanuni zetu kwanza tusaidiane tu kuelewana na Kanuni ndiyo tunajifunza.

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Waheshimiwa Wabunge, kama mwenye swalii la msingi ameridhika na majibu ya Serikali wewe uliyeuliza swalii la nyongeza na ukajisikia vibaya huwezi ukaliombea Mwongozo. Uamuzi huu umeshatolewa siku za nyuma, tufahamu hilo, ambaye ana haki ya kusema kwamba swalii langu la msingi au la nyongeza sikujibowi kikamilifu ni yule aliyeuliza. Kwa vile suala hili la Mwenge limejibowi vizuri sana sana na Serikali na Mheshimiwa Haji ambaye ndiye ameuliza swalii la msingi kajibowi vizuri na akaridhika na majibu ya Serikali. Nadhani suala hili mwongozo wangu ni kwamba limekaa vizuri, hatuhitaji kuliendeleza. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa ombi la Mheshimiwa Hawa Ghasia, nadhani Serikali itaona nafasi ya kuweza kusaidia uzalendo huu hasa kwa sisi. Waheshimiwa Wabunge niwaambieni kabisa nilitegemea sisi kama viongozi ndiyo tungekuwa mstari wa mbele wa kusemea faida za mwenge huu ili sasa watoto wetu hawa ndiyo tunawapatia kama *legacy* (urithi) wa Taifa hili, maana ya mwenge huu kutuunganisha kama Taifa lakini kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. Tutaona Serikali itaweza kusaidia vipi katika kudumisha uzalendo wa nchi yetu. Huo ndio mwongozo wangu kwa suala hilo la mwenge na sasa tunaendelea na shughuli kubwa iliyo mbele yetu. Katibu. (*Makofii*)

### **NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa leo na kama nilivyo sema jana hoja hii lazima leo ihitimishwe, orodha ni ndefu lakini tutafanyaje. Nianze na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na

Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga Tisekwa na Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae. Mheshimiwa Munde.

**MBUNGE FULANI:** Ni dakika tano tu?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, watakaochangia kwa orodha niliyopewa na Chama cha Mapinduzi wanachangia kwa dakika tano-tano wamekubaliana hivyo. Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia. Dakika tano ni chache yaani leo nitaacha hata kukisifia chama changu na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichangle moja kwa moja matatizo yangu ya Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora tuna Chuo cha Waaguzi pamoja na Madaktari, nimeongea hapa Bungeni mara kadhaa. Mheshimiwa Naibu Waziri amekwenda Tabora kufuatilia, akatoa maagizo kwamba Katibu Mkuu atakuja, Katibu Mkuu hakwenda Tabora, wakaenda Maafisa watatu tarehe 27 Januari, wakasema watarudi lakini mpaka leo hii hawajarudi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za walipa kodi zimefanya kazi kubwa, mpaka napoongea hapa chuo kimefikia *stage* ya magodoro na vitanda, *theatre* imekamilika kwa mashine zote, kasoro mitungi ya hewa tu lakini mkandarasi amefunga, ufunguo anao yeye, hata Naibu Waziri alivyokwenda amechungulia dirishani hakuweza kuingia. Ni asilimia kumi tu zimebaki, kwenye chuo ni *tape* za mabomba na kwenye *theatre* ni mitungi ya hewa lakini hela ya walipa kodi inapotea bure, jengo lile limegeuka kuwa gofu, linaharibika, *value for money* imepotea.

Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa uje uniambie kuhusu *status* ya Chuo cha Manesi na Madaktari wa Tabora. Kwa kweli hizi hela za walipa kodi zinapotea hivi hivi huku mkiziangalia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba niongelee Hospitali ya Wilaya ya Tabora Manispaa. Tabora Manispaa tumeanzisha jengo la Hospitali ya Wilaya miaka mitatu sasa, tulitenga shilingi milioni 150, tukatenga shilingi milioni 120 lakini Serikali Kuu haijatuunga mkono. Tunamuomba sana Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Ummy, najua hizi Wizara zinaingiliana mtusaidie kuhusu Hospitali ya Wilaya ya Tabora Manispaa. Msongamano katika Hospitali ya Mkoa ni mkubwa sana, Wilaya ya Tabora Manispaa ina *population* ya watu zaidi ya 400,000 bila kuwa na Hospitali ya Wilaya hatutaweza kabisa kumudu hali hii. Tutabaki tunailaumu Serikali kila siku lazima tuwe na Hospitali ya Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya Uyui pia wameanza kujenga jengo lao la ghorofa lakini wameshindwa kumalizia tu. Tunaomba muwa-*support* nao wapate Hospitali ya Wilaya ili kuondoa msongamano mkubwa kwenye Hospitali ya Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy bajeti iliyopita alituahidi mikoa yote ya pembezoni atapeleka Madaktari Bingwa. Ninavyoongea hapa Hospitali ya Mkoa wa Tabora kuna Madaktari Bingwa wawili tu badala ya 34. Kuna daktari wa mifupa na daktari wa wanawake alioazimwa kwenye Manispaa. Tunaomba mtupelekee Madaktari Bingwa sisi tulioko pembezoni kwani nako pia kuna Watanzania wanaohitaji huduma za hospitali. Muhimbili madaktari wamejaa tele, lakini huku kwenye hospitali zetu hakuna. Mheshimiwa Waziri alituahidi naomba anapokuja kutujibu atuambie kuhusu suala hili la upatikanaji wa Madaktari Bingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Nursing Officer* tunahitaji 37 lakini tunao watatu tu, tunahitaji *Assistant Nurse* 131 tunao 82, wauguzi wenyе *certificate* tunahitaji 147 tunao 44, hatimaye wodi kubwa wenyе watu 80 analala *nurse* mmoja atahudumiae watu, tutakuwa tunalaumu ma-*nurse* lakini tatizo kwa kweli lipo. Haiwezekani *nurse* mmoja akahudumia watu 80, mmoja *drip* imeisha, mwingine

anataka kujisaidia, mwagine muda wa sindano umefika, matokeo yake wanaona kama ma-nurse hawawasaidii watu, lakini kwa kweli ma-nurse ni wachache wagonjwa ni wengi sana. Mheshimiwa Ummy tunakuamini naomba na sisi uendelee kutunza imani yako kwetu, hili jambo ni kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena suala la *x-rayya Nzega*, Wabunge wote wa Nzega wameongea. Mimi niseme tu Phillips anadai hela zake Mheshimiwa Ummy tuambie unamlipa lini hela zake atengeneze *x-rayya Nzega*, tusipindishe maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Benki ya Wanawake. Mheshimiwa Ummy uliahidi utakuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda ndio huo.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Dakika tano-tano tu, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga.

**MHE. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii. Pamoja na kwamba dakika ni tano lakini mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii sitaacha kuipongeza Serikali yangu pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa juhudi kubwa walizofanya kwa muda mfupi katika kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumejionea, ukiangalia pale *Ocean Road* akina mama wengi wanafariki kwa sababu ya *cancer* lakini kumeboreshwa kwa hali ya juu. Sasa hivi kusubiri mionzi sio miezi mitatu ni wiki sita na tunaelekea wiki mbili, huduma ya dawa kutoka asilimia nne

mpaka asilimia 60 bado vifaa vya kupima pamoja na *PET Scan* ambayo itapunguzia gharama Serikali lakini pia kuokoa maisha ya Watanzania hususan wanawake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atusaidie Mkao wetu wa Morogoro, ni mkubwa sana tuna Wilaya nane, lakini Hospitali za Wilaya ni chache sana. Kwa hiyo, ili kupunguza vifo vya akina mama inabidi kwa kweli uliangalie suala hili ingawa kwako inakupa shida sasa inabidi uende TAMISEMI ndiyo maana tulisema kama inawezekana Waziri wa Afya ashuke mpaka chini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijikite kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hii inachukuliwa kama kitu ambacho hakina umuhimu na mpaka kuna viongozi wa kitaifa wakisimama wanassema hawa walioajiriwa hawaoni kazi yao, lakini wanashahau kwamba Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii ndio *engine* ya maendeleo katika nchi yetu. (*Makof*)

Sasa hivi Tanzania wananchi hawaelewi, hamna mtu wa kuwaunganisha wananchi na Serikali yao, utakuta wanaunganishwa na wanaharakati. Mwanaharakati hata siku moja haisaidii Serikali, kazi yake ni kukosoa lakini hawa *Community Development Officer* na *Social Workers* ndio kiini na ndio hasa *engine* ya maendeleo. Kwa hiyo, tunaomba hii fedha sasa iliyotolewa itolewe yote muende kufufua sekta hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, watu wanafikiri kwamba uchumi unaletwa na wanauchumi na sayansi asilia, siyo kweli. Baada ya *industrial revolution* watu walipata *social problem* nydingi, wana-commit suicide, wanatumia dawa za kulevyta, *family breakdown*, watoto wa mitaani, maadili, sisitunabaki kupiga makelele lakini kazi kubwa ni hii ya Idara ya Maendeleo ya Jamii. Tukiweza kuiboresha wao ndio wanaotafuta *solutions* kwamba wafanye nini katika jamii yao. Utakuta sasa hivi hata barabara ikiharibika wanasubiri Serikali, kujenga vyoo wanasubiri Serikali kwa sababu hakuna mtu wa kuwaongoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, sana Idara hii ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii ipewe kipaumbele. Ikiwezekana sasa tuboreshe vyuo vyetu kama cha Tengeru, kule kumechakaa, hakuna *training*, watu hawana *new skills*, tunategemea maendeleo yatatoka wapi? Tusione kwamba maendeleo ni kitu kingine hapana, tuanzie hapa chini. Kwa hiyo, naomba sana Serikali yangu Tukufu iweze kuangalia suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba sasa niongelee suala la UKIMWI. Wale watu wanaoishi na VVU tunaomba halmashauri iwasaidie wapate CHFili waweze kupata *septrin* wanaumia sana kule, hakuna dawa na vitu vingine. Kwa hiyo, ombi lao kubwa dawa hizi za *septrin* ziweze kupatikana ingawa ni sehemu ya Halmashauri, lakini sasa ndiyo bado tunarudi kwenye changamoto ileile kwamba Wizara ya Afya kama italchia kwenye sera haiwezi kuangalia utekelezaji wa sera zake mpaka huku chini bado tutaendelea kupata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante na kwa kulinda muda pia. Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Mwitwa Getere ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kutujalia uzima na uhai. Kabla sijaanza naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Kwa kweli Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imefanya mambo mengi na makubwa katika nyanja mbalimbali. Kila eneo kwa kweli imefanya kazi kubwa na ni kazi ambayo kwa kipindi kifupi imeweza kuonekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongozi za pekee vilevile zimfikie Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa ambaye ye ye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Shukrani nyingine za pekee ziwafikie Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wako kwenye Serikali hii ya Awamu ya Tano, hongereni sana kwa kazi nzuri na kubwa ambazo mnazifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nizungumzie maeneo makubwa mawili; kwanza nizungumzie afya ya mama na mtoto pamoja na eneo la UKIMWI kwa ujumla wake. Kabla sijaenda kwenye maeneo hayo, niseme kwamba Serikali hii ina dhamira ya makusudi kabisa ya ku hakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanaishi kwa kuwa na afya bora na nzuri zaidi na ndiyo maana kwa misingi hiyo hata ukiiangalia bajeti ya mwaka 2016/2017 inatofautiana sana na bajeti ya mwaka 2017/2018. Hii ni kuuthibitishia umma kwamba Rais, Mheshimiwa Magufuli ana dhamira ya dhati kuwaweka Watanzania kwenye afya nzuri na afya bora zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie afya ya mama na mtoto. Takwimu zinaonesha kwamba katika vizazi hai 100,000 wanawake 556 hufariki dunia. Wanawake hawa 556 ambao wanafariki dunia hii takwimu ni kubwa zaidi. Hatutaki mwanamke hata mmoja afariki wakati analeta kiumbe kingine. Kwa kweli kwa misingi hiyo hili jambo ni lazima litazamwe kwa jicho la pekee kabisa ndani ya Wizara hii. Nasema haya kwa sababu kubwa za msingi. Sababu ya kwanza, takwimu hizi kwa mara ya mwisho zilikuwa 446 hivi lakini sasa zimetoka kwenye 446 zimefika kwenye 556, hapa ni lazima tupaangalie kwa namna ya pekee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na vizazi hai, tunaingia kwenye eneo la watoto, watoto 25 kati ya 1,000 wanapoteza maisha. Watoto hawa wanaopoteza maisha lengo letu ndiyo waje kuwa watu wazima hatimaye washike mamlaka ndani ya Taifa lao. Sasa kama hivi leo tunawapoteza watoto hawa nini matokeo ya baadaye? Hili

jambo ni lazima liwe kwa mapana yake kama ambavyo tumeangalia katika maeneo mengine tusiruhusu mtoto afe wakati akija duniani. Naiomba Serikali/Wizara ihakikishe kwamba wanaboresha maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine, akina mama waliambiwa waende na vifungashio hospitalini. Leo hii akina mama wanabebe vifungashio vyao na akina mama hawa ni maskini, tunafanya juu ya jambo hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, narudia tena kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete kwa mchango wako mzuri na kwa ushauri mzuri uliotoa kwa Serikali. Mheshimiwa Oscar Mukasa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Maria Kangoye ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Itabidi twende mwendo kasi maana dakika tano hizi hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada na inavyostahili nawapongeza sana Mheshimiwa Ummy na Naibu wake, Katibu Mkuu naye anafanya kazi nzuri sana, inaoneka watu tunamsahau na timu yake pia, kwa kweli kazi inaoneka. Mimi ni mmoja wa watu ambao binafsi nikijaribu kufuatilia unaona kabisa kwamba sasa kuna mahali tunakwenda kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna mwanafalsafa mmoja anasema dunia yetu siyo mbinguni na kufanya vizuri haitoshi ni lazima tufanye vizuri zaidi. Kwa hiyo, mnafanya vizuri lakini lazima tufanye vizuri zaidi. Sasa nasema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Waziri, ukurasa 127, kiambatanisho namba tatu, anapoongelea upatikanaji wa dawa, kuna majedwali pale yanazungumzia

kila Wilaya asilimia 80, 90 na mambo kama hayo lakini kwa wastani kitaifa anasema upatikanaji ni asilimia 87, ni jambo zuri. Hata hivyo, hii maana yake ni kwamba katika kila watu 10 unaokutana nao wametoka hospitalini pale, tisa watakuambia tumepata dawa tulivoandikiwa, kitu ambacho uhalisia kule chini sio kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wasiwasi wangu ni kwamba inawezekana Bohari ya Dawa kusukuma madawa kule wilayani ndio asilimia 87 lakini upatikanaji wa dawa kwa maana ya kutoka pale ilipo kumfikia mgonjwa sio tunachokiona kinachofanana na hii 87. Biharamulo pale ukizungumza na watu kumi wanaotoka Hospitali ya Wilaya pale, ukasimama tu nje, watu watano mpaka sita wana malalamiko ya dawa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ujumbe wangu ni kwamba umefanikiwa sasa kusukuma dawa kwenda kwenye hospitali zetu lakini ukashughulike na kituo cha tiba na mgonjwa ili upatikanaji wa dawa uwe kwa mgonjwa. Kuna habari ya *committed supply* na *actual supply*. Kwa hiyo, tuone namna gani mgonjwa anapata dawa hiyo hatua inayofuata. Naomba hata *CAG* aende mbele zaidi afike hapo na kwenda hatua ya pili kwa sababu lazima twende kasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anasema kuna shilingi kama bilioni mbili za Mfuko wa *CHF* henzieleweki zimefanya nini huko kwenye maeneo yetu, sio maneno yangu ni *CAG*. Kwa hiyo, naomba tutazame kwenye ukurasa fulani hapa kwenye hotuba unazungumzia *CHF*iliyoboreshwa inakwenda kutatua habari ya mipaka ya tiba kwa kutumia *CHF*kuondoka nje ya Halmashauri lakini hiyo haijibu matumizi ambayo hayaeleweki ya pesa ambayo tayari watu wamechanga. Wananchi wakisikia habari sisi inatuwia ngumu kuwahamasisha waendelee kujiunga na *CHF*. Tunaomba muende hatua ya ziada zaidi ya kuongelea *CHF*iliyoboreshwa kuwaondolea mipaka ya matumizi ya ile bima yao lakini ukatazame ni kwa nini pesa hizo hazitumiki kama zilivyopangiwa, anasema *CAG* sio maneno yangu hayo twende kinachofuata kwa sababu tunakwenda kasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biharamulo tuna vituo vya afya vitano lakini katika vituo hivyo ni kimoja tu ambacho kina mtaalamu wa maabara tena ambaye sio wa kiwango cha *Laboratory Technician* ni *Laboratory Assistant*. Maana yake kwenye vituo vya afya vyetu vyote pale hawa madaktari wetu waganga wasaidizi wanapiga ramli yaani hata mtu akisema nina dalili za malaria hawezি kwenda kupima, inabidi mganga apige ramli ndio ajue hii ni malaria ama ni nini. Tunaomba tuangalie ni namna gani tutakwenda chini hasa kwenye zile huduma ambazo ni lazima na zinamsaidia yule mganga kufanya tabibu zake kama anavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 57 mpaka 58 kwenye hotuba ya Waziri anaongelea makundi ambayo yanahitaji msamaha na anataja walemvu, familia zenye migogoro, wakimbizi, waathirika wa pombe kwamba hao ndio wanafikirwa pale.

Mimi nikafikiria tuna 10% ile ya akina mama na vijana kwenye halmashauri na tumewapa wale kwa sababu ni makundi maalum lakini yako makundi maalum zaidi, walemvu na watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI hawa wana mahitaji zaidi, ni makundi maalum, maalum ndani ya maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute namna ambavyo na wenye kwenye tuwajumuisho kwenye ile 10% waangaliwe kwa upekee waweze kufanya shughuli za uzalishaji, waweze kununua bima na waweze kupata tiba lakini ukimfikiria kwenye msamaha mpaka mtu aliyeathirika na pombe, mpaka mkimbizi, wakati mlemavu hujamfikiria, nadhani vipaumbele vyetu vinakuwa sio sawa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Getere, Mbunge wa Bunda atafuatiwa na Mheshimiwa Kongoye.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Niendelee kutoa pongozi kwa Jemedari wetu, Rais wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya, sina mashaka na yeye. Wasiwasи wangu ni kwamba akimaliza miaka yake kumi atakuja mtu mzuri kama yeye au vipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Hospitali ya Mkoa wa Mara. Sijajua kwa Mkoa wetu wa Mara ni kitu gani kinatokea kwa sababu vitu vingi haviendi vizuri. Hospitali hii imechangiwa karibu miaka 32 na hajjaisha. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ya Kongwa, imekuwa ikitengewa fedha kidogo kila mwaka na mpaka leo hajjulikani itaisha lini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atueleza kwa mwaka huu wa fedha imetengewa kiasi gani na ni lini hospitali inaweza kwisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, nadhani ukurasa wa 149, anazungumzia habari ya kupeleka fedha za vijana na akina mama katika vikundi. Katika Wilaya ya Bunda wameandika kwamba imepeleka shilingi milioni 106, nikashangaa! Sasa nataka kujuliza haya maandishi humu ni ya kweli au mtu ameyabandika tu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nimempigia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kumuuliza hii hela mmepeleka ninyi? Anasema sisi tumepeleka shilingi milioni 20 tu. Maana Bunda yenyewe kukusanya shilingi milioni 100 ni kesi. Sasa nataka kujuliza hizi fedha zimetoka Wizarani za muda mrefu au za namna gani? Kwa hiyo, kama ni za Wizarani ni sawa lakini kama ni za kutoka kwenye Halmashauri

na ni *own source*, hizi fedha hazijatoka. Kwa hiyo, nataka kuuliza suala hili limekaaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nizungumzie habari ya watumishi katika Jimbo langu la Bunda. Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ametembelea katika Jimbo langu la Bunda ameona katika kila kituo *nurse* ni mmoja-mmoja tena wale wa daraja la chini na akaahidi mtakapopata nafasi mtatuletea watumishi katika Jimbo la Bunda. Zahanati zote zina *nurse* mmoja-mmoja na Naibu Waziri ameshuhudia mwenyewe. Kwa hiyo, naomba katika nafasi zitakazopatikana mnisaidie kupata watumishi wa maeneo hayo. (*Makofi*)

Lakini pia mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Tumetembelea Muhimbili, *Ocean Road* na maeneo mengine mengi, fedha haziendi kwenye vituo vyote vikuu. Tunaiomba Serikali katika bajeti inazotenga fedha ziende kwenye maeneo muhimu ambayo imezitengea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona Mloganzila, tumeambiwa kile Kituo cha Ufundishaji cha Tiba kimeisha lakini hakina watumishi. Kinahitaji fedha kiasi cha shilingi bilioni nne ili kianze kazi. Tunaomba Serikali ipeleke pale madaktari na kituo kile kiweze kuanza kazi mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa iko hapa, tunaomba watumishi waende maeneo hayo ili waweze kusaidia wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna Hospitali ya Nyamuswa, ni kituo ambacho tumekijenga kiko kwenye hali nzuri. Tunaomba pale mtakapopata *x-ray*na nimesikia Waziri anasema mtapata *x-ray* basi mtupelekee kwenye Kituo cya Nyamuswa ili watu waweze kupata huduma katika maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika haya mambo ya vijana mimi nadhani sasa kuwepo na mkakati

maalum kupitia hii Wizara na Wizara ya Kazi tujuje sasa hizi fedha za taasisi za kijamii zinazoenda kwa ajili ya kuwakopesha akina mama na vijana zina mfumo mzuri ambao unaeleweka. Maana inaonekana kwamba kuna maeneo mengine yanapata fedha kutoka makao makuu na wengine wanapata kutoka *own source* sasa haijulikani ni wapi wanapata manufaa. Nashauri tuweke mfuko mmoja wa hizi fedha zijulikane kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kongoye atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kwa kuunga mkono hoja na sina mashaka na Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nianze na suala zima la udhibiti wa UKIMWI. Napenda kuipongeza Wizara kwa juhudzi nzuri inazofanya kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo kubwa la watoto wanaozaliwa na maambukizi ya VVU. Kwa mujibu wa Kanuni ya Maadili, watoto hawa hawapaswi kupimwa bila idhini ya wazazi. Mara nyingi wazazi hawa wamekuwa hawawapi taarifa ya *status zao* watoto hawa na tatizo linakuja pale ambapo watoto hawa wanaingia katika mahusiano katika umri mdogo wakiwa shulenii ama mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba lipo ongezeko kubwa la watoto kujihusisha na

ngono katika umri mdogo. Napenda kutumia fursa hii kuiomba Serikali ije na programu nzuri ambayo itawawezesha watoto hawa kuweza kujitambua na kufahamu ni namna gani ya kuweza kujilinda wao pamoja na wengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu tatizo la hedhi isiyo salama. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la hedhi zisizo salama ambalo limekuwa likiwaandama sana wasichana na wanawake ambaao wako vijijini lakini na wale ambaao hawana uwezo wa kupata taulo salama. Changamoto hii imesababisha matatizo mengi yakiwemo magonjwa mbalimbali yanayotokana na kutumia zana ambaao sio salama kipindi hicho cha hedhi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mdau mmojawapo wa hedhi salama na napenda *ku-declare interest* kwamba ni mzalishaji wa taulo ambazo zinatumika zaidi ya mara moja na mara nyingi nimekuwa nikijitolea kutoa bure sehemu mbalimbali ikiwemo mashulenii na magereza. Napenda kuiomba Serikali yangu kuungana na sisi wadau ili pale inapowezekana iweze kutoa pedi hizi kwa makundi mbalimbali yakiwemo ya wafungwa wanawake, wanawake wasio na uwezo lakini pia kwa watoto wa kike ili kuweza kupunguza tatizo la utoro wa shulenii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja nijielekeze katika Mkoa wangu wa Mwanza. Kwanza napenda nianze kwa kumkumbusha Waziri ahadi ambazo ametuahidi, ipo ile ahadi ya kutuongezea *OC* katika Hospitali ya Sengerema ambapo *OC* inayokuja kwa ajili ya vitanda ni ndgo mno kulingana na hali halisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkumbusha pia Mheshimiwa Waziri ahadi yake ya vitanda katika Kituo cha Afya cha Malya. Alimuahidi Mbunge wangu wa Sumve na sisi tunasubiri ahadi hiyo itimie kwa sababu akina mama wanahangaika sana, wanajifungulia chini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Magu nitaongelea Kituo cha Afya cha Kisesa, ni kituo ambacho

kinahudumia takribani kata tano na tarafa nzima ya Sanjo. Kituo hiki kina uhitaji mkubwa wa *x-ray* na chumba tayari kimeshaandaliwa vizuri kwa ajili ya mashine hiyo. Hivyo basi, tunaiomba Wizara itushike mkono tuweze kupata mashine hiyo ili wananchi wa Tarafa ya Sanjo wasipate tabu kwenda maeneo ya mbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Illemela haina Hospitali ya Wilaya. Kwa juhudhi ya Halmashauri imeweza kuanza kujenga jengo la *OPD*. Tunaishukuru Wizara kwa kuweza kuchangia shilingi milioni 300 kwa ajili ya jengo hilo ambalo lina thamani ya zaidi ya shilingi milioni 600. Hata hivyo, bado safari ni ndefu, hospitali nzima gharama yake ni shilingi bilioni 25, hiyo ni kwa ajili ya majengo pamoja na vifaa. Tunaomba sana Wizara ituangalie ili wananchi wa Illemela wapungukiwe na matatizo ya kwenda katika misongamano ya wagonjwa katika Hospitali ya Bugando pamoja na Sekou Toure. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa James Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Afya na nguvu ni bora kuliko dhahabu; mwili wenye nguvu ni bora kuliko utajiri mwingi. Joshua Bin Sira 30:13. Hakuna utajiri ulio bora kuliko afya ya mwili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hayo kwa sababu hatuvezi tukazungumzia maendeleo ya aina yoyote kama hatuvekezi ipasavyo kwenye afya ya binadamu. Lengo la Tatu la Maendeleo Endelevu ya Dunia yanazungumzia afya bora kwa rika zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya afya ya Tanzania ikoje? Hali ya afya ya hapa kwetu Tanzania kwa kiasi kikubwa ambapo tuko zaidi ya watu milioni 50 inatisha. Takwimu za Shirika la Afya Duniani zinaonesha ifikapo mwaka 2030 zaidi ya Watanzania 85,000 watafariki kwa magonjwa ya moyo; Watanzania 42,000 watafariki kwa magonjwa ya saratani; na Watanzania 68,000 watafariki kwa magonjwa haya ya ajali. Sasa tujiulize tunashindaje changamoto zote hizi? Tufikiri *globally* na *tu-act locally* tutaweza namna gani kupambana na changamoto hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, magonjwa ya moyo, magonjwa ya kansa, magonjwa ya figo, mashine kwa mfano ya kusafisha damu kwa kiasi kikubwa mashine hizi ziko Dar es Salaam zaidi na ni ghali sana. Kwa mfano sindano moja wakichomwa ni shillingi 67,000 unaandikiwa sindano 12, huyu Mtanzania hata wa kipato cha kati atawezu kumudu kiasi gani? Tujiulize ile *linear accelerator* kwa ajili ya magonjwa ya kansa ambayo tumeimba kwa zaidi ya miaka kumi ifungwe pale *Ocean Road* ni lini itafungwa? Tumekuwa tukizungumzia uwekezaji kwenye sekta ya afya kwamba Hospitali za Apollo kutoka India watakuja kuwekeza hapa Tanzania ili kusaidia *foreign* kuwekeza kwenye sekta ya afya ili kuwe na ushindani hali ikoje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiri hivi karibuni nilikuwa natibiwa Hospitali ya Zydus kule India. Ni hospitali ya watu binafsi ina vitanda zaidi ya 550, ina vitanda vya *ICU* 162 na ina mashine za kisasa ukililinganisha na sisi kama Taifa la Tanzania. Hospitali za namna hii namna gani tunafanya mazungumzo nao kwa sababu penda tusipende dunia leo imekuwa ni kijiji, kama hapa kwetu Tanzania hatujitoshelezi tunaweza tuka-source hata wenzetu wa nje wakawekeza kwetu hapa Tanzania. Kwa sababu leo hii sekta ya afya ina upungufu wa wataalam zaidi ya 58% na Afrika Mashariki hapa Kenya, Uganda na Tanzania, Tanzania tunashika nafasi ya chini sana katika kuwa na watalaam wa kutosha katika sekta ya afya. Sasa changamoto zote hizi tunashiriki namna

#### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

gani kuziondoa? Ndiyo maana nimesema afya ya mwili ni bora kuliko utajiri mwingine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa kawaida kabisa wakati iliyotokea kikombe cha babu, ni Watanzania wangapi waliokimbia kwa babu, ni Watanzania wangapi waliopoteza maisha kwenda kwa babu na namna gani Serikali ilijitoa kwenye sera yake ikaenda ikawekeza miundombinu kwa babu na Serikali karibu yote ikahamia kwa babu kwa ajili ya matibabu kwa babu? Sasa unaweza kuona tu kwamba Watanzania wengi ni kwamba afya, afya, afya ziko katika hali ambayo siyo nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano watalaaam mabingwa kutoka nje wanaokuja hapa nchini, kupata vibali tu vya kufanya kazi (*working permit*), inachukua miezi sita mpaka minane lakini unawapa kwa muda wa miaka mwili tu! Sasa wale mabingwa hawawezi wakasubiri muda wote huo. Badala ya kuwapa miaka miili wape basi hata miaka mitano au zaidi ili kuwapa *confidence* ya kuwekeza katika sekta ya afya. Hata tukijiiliza miaka 10 iliyopita ni mabingwa au ni taasisi ngapi za kidunia zimewekeza vizuri katika sekta ya afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikienda Vunjo, Hospitali ya Kilema nimeizungumzia na hata leo asubuhi nimeizungumzia. Tukiangalia Hospitali ya Kilema ina zahanati zaidi ya 13 za Maua, Makomu, Womboni, Mboni, Mbabe, Rauya, Arumeli, Uparo, Mawanjeni, Uchira, Miwaleni, Iwa na Yamu lakini Zahanati ya Miwaleni imefungwa moja kwa moja haina hata wataalam.

Mheshimiwa Mwentekiti, sasa ni namna gani tunawekeza akili na fikra zetu ili bajeti ya Wizara hii iweze kutosheleza mahitaji. Nikiri bajeti ya Wizara hii ni kidogo mno katika kutekeleza majukumu yote katika sekta ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya mwanadamu na utu wa mwanadamu ni afya kwanza. Mwanadamu aliyeshiba vizuri na mwenye afya nzuri, na nikupongeze Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu na Naibu wako kwa kazi kubwa mnayofanya lakini bajeti yenu kidogo mno. Katibu Mkuu atadaiwa huku na kule, Dkt. Mpoki, anafanya kazi nzuri tu lakini sasa afanyeje wakati bajeti ni kidogo kiasi hiki? Kwa hiyo, tujifikirie. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge, tumepewaa mamlaka na Katiba ya kuismamia na kuishauri Serikali. Tukiacha tofauti ya itikadi zetu hapa tukaamua kuismamia Serikali vizuri, tunaweza tukapangua hata bajeti hii tukaiongezea Wizara ya Afya bajeti zaidi ili binadamu aweze kushiba vizuri, binadamu aweze kuwa na uelewa vizuri na aweze kuondokana na haya matatizo ambayo ni makubwa katika Taifa letu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya miundombinu katika Hospitali ya Kilema pamoja na Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi. Tuna changamoto ya uzio kwa mfano pale Mawenzi na miundombinu yote ile ni chakavu. Pale Kilema hatuna Kitengo cha *ICU*, ujenzi wa jengo la utawala ni matatizo, uzio wa hospitali ni matatizo, nyumba za watumishi ni matatizo, marupurupu kwa watumishi kwa ujumla wake ni matatizo wanafanya kazi katika hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde chonde tuangalie ni namna gani Wizara inashirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuwa na mawazo mapana zaidi na kuangalia wenzetu duniani wanafanya nini ili tuweze kuondokana na changamoto hizi tukawekeza vyta kutosha katika sekta hii ya afya ambayo ni duni kwa Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujifunze kwa wenzetu duniani na tuangalie wanafanya nini, kwa sababu kila mtu hapa atazungumzia Jimbo lake la uchaguzi, atazungumzia sehemu yake, bajeti ni kidogo, lakini Wabunge tunayo nafasi, tunayo nguvu, tunao uwezo wa Kikatiba wa kuweza hata kupangua bajeti hii, kwa sababu bajeti kubwa hajasomwa na wakati wa kukaa na Serikali ili Wizara hii ikaongezewe bajeti ili *performance* ya Watanzania katika Wizara ya Afya iweze kuonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde niombe tena, Serikali inaweza ikafanya maamuzi kwenye miundombinu, barabara, reli na mengineyo wakawekeza zaidi kwenye *private sector*, lakini fedha tunazopata ndani tukawekeza zaidi kwenye ile miundombinu inayokuza utu wa mwanadamu zaidi. Kwa mfano, afya, elimu ambayo ndiyo kipaumbele namna gani wataalam wetu wa humu ndani tunawapa haki zao, stahili zao, watumishi wetu. Madaktari wetu wa humu ndani wako kwenye hali gani, Wakunga wako kwenye hali gani, wauguzi wako kwenye hali gani, vituo vyetu vya afya viko kwenye hali gani. Kwa mfano, pale Vunjo Kituo cha Afya cha Kirua, Kituo cha Afya cha Mwika na Hospitali ya Marangu vile vituo vyote vya afya na zahanati zote zinazotoa huduma wanatoa huduma nzuri sana lakini katika mazingira magumu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali za Rufaa kwa mfano, *KCMC*, Bugando angalia Hospitali ya Muhimbili kweli tunazungumza kwamba hali ya Muhimbili bado ni tete sana angalia wagonjwa wanalala ndani wane, watano wajawazito hawa zaidi ya wawili watatu, wengine wako katika hali ambayo siyo nzuri sana tuwe wa kweli. Unaweza ukasema hapana, lakini ukienda Hospitali ya Mwananyamala, Temeke haziridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba chonde chonde Wizara hii naomba iongezewe bajeti ili iweze ikatoa huduma yake kwa kukuza utu wa mwanadamu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mtulia utafuatiwa na Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Balozi Kamala ajiandae.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyenzi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kunijalia uzima.

Pili, nikushukuru nawe kwa kunipa fursa hii adhimu nami kuchangia katika Wizara yetu hii muhimu sana. Nimpongeze kidogo Mheshimiwa dada yangu Ummy Mwalimu kwa kazi kubwa anayofanya, hasa kwa uwasilishaji mzuri alioufanya jana. Kwa kweli wakati anawasilisha Dada Ummy niliamini kabisa kwamba matatizo yetu yamekwisha. Vilevile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa katuonyesha wazi kwamba pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Dada Ummy lakini Wizara hii bado ina matatizo lukuki, hata bajeti waliyopewa haikufika zaidi ya asilimia 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kabisa kabisa hotuba ya Kambi ya Upinzani. Nimpongeze Dada yangu Mheshimiwa Ester kwa uwasilishaji mzuri na kuonesha matatizo yaliyopo kwenye Wizara yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina Sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambayo imetolewa mwaka 2007. Katika sera yetu hii ukienda ukurasa 10 ambaa unaeleza afya ya msingi ukienda kwenye ukurasa wa 11 nitayasoma madhumuni ya sera yetu hii. Madhumini ya sera yetu hii ni kupanua dhana ya afya ya msingi na kuwa na huduma bora za afya zinazoendana na wakati, endelevu na zinazowafikia wanachi wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye tamko la sera namba moja na namba mbili, tunaambiwa Serikali itahakikisha wananchi na sekta mbalimbali katika kuimarisha huduma za afya katika ngazi zote ili kuboresha afya.

Pili, Serikali itaimarisha uendeshaji na usimamizi wa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii imeingizwa kwenye utendaji kwa kutumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tumeambiwa mara nyingi hapa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema itajenga zahanati kila kijiji. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema itajenga kituo cha afya kila kata. Tumeambiwa mara nyingi hapa kwamba hii Ilani ndiyo imefanya wananchi kukiamini Chama cha Mapainduzi. Na mimi kwa kweli nitakuwa Wakili wa wananchi kuhakikisha Chama cha Mapinduzi wanatekeleza Ilani yao hii, Ilani ambayo ilikuwa ndiyo sababu wananchi kuwaamini. Wasipotekeleza tafsiri yake wamewarubuni wananchi, wamewalaghai wananchi, hawatekelezi yale ambayo ilikuwa ndiyo sababu ya kupewa madaraka ya kuongoza nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makubaliano ya Abuja ya mwaka 1989 Serikali zetu za Afrika walikubaliana Wizara ya Afya itengewe walau basi asilimia 15 ya bajeti, bajeti yetu hapa ni shilingi trilioni 31, asilimia 15 ni shilingi trilioni 4.5. Sisi tumetenga shilingi trilioni 1.1. Kwa utaratibu huu hivi kweli tuna malengo ya dhati ya kuhakikisha tunapunguza vifo vyta akina mama? Hivi kweli tuna malengo ya dhati ya kuhakikisha tunapeleka afya ya msingi kwa wananchi wote kama sera yetu ilivyosema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe wakweli, tuhakikishe basi walau niungane na *senior* kaka yangu Mheshimiwa Mbatia pale, bajeti hii basi walau tufanye asilimia tano ambayo itakuwa ni shilingi trilioni 1.5, na hii asilimia tano tukiweka tuongeze madaktari, tuna madaktari wanazungukazunguka tumewasomesha kwa gharama kubwa, kwa nini tusiwaajiri madaktari na wahudumu wa afya, wafanyakazi wote wa idara za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tushirikiane na Halmashauri kuhakikisha tunajenga hizo zahanati kila kijiji, tuhakikishe tunajenga vituo cha afya kila kata. Kama tuna nia ya dhati ya kumsaidia mama na mtoto, kuwasaidia watu wetu hawa, tuwe na zahanati kila kijiji kwa sababu kule ndiyo huduma itamfikia mwananchi. Vifo vyta akina mama

vinasababishwa na kutokwenda kliniki, hawapati huduma za kliniki, huduma ya kliniki zahanati isipokuwepo kijijini ataipatia wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hospitali yetu ya Mwananyamala, mimi ni Mbunge wa Jimbo Kinondoni, hospitali ya Mwananyamala imepandishwa hadhi, imekuwa ya rufaa, jambo la kusikitisha Serikali hawatoi fungu lolote la uendeshaji wa hospitali ile, badala yake imekuwa gharama kwa Halmashauri na Manispaa ya Kinondoni. Uendeshaji wa hospitali ya Mwananyamala inatugharimu karibu shilingi bilioni 6.9 kila wiki. Mbaya zaidi tumepewa tena jukumu, kwa kuwa hospitali yetu imekuwa ya rufaa tunatakiwa tujenge hospitali ya Wilaya. Serikali ipo kimya haitusaidii chochote kwenye ujenzi ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Kinondoni kwa maana ya Mwananyamala katika Jimbo letu na Wilaya yetu ina zaidi ya watu milioni moja. Msongamano umekuwa mkubwa na msongamano ukubwa wake unatokana na kwa sababu hatuna Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, naomba Wizara ije kutuambia ama wapeleke fedha za ruzuku kwenye Hospitali ya Mwananyamala au watusaidie kujenga hospitali ya Wilaya ambayo ipo Mabwepande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hali ngumu sana katika Hospitali yetu Mwananyamala. Dawa tunapata *MSD*, wakati mwingine dawa tunazozitaka wakati mwingine *MSD* hawana, Wanapokuwa hawana *MSD* hamna njia mbadala. Hakuna chombo kingine kinafanya ushindani na *MSD*. Ukitaka kununua dawa nje ya mfumo wa *MSD* unatakiwa ufuate mfumo wa manunuvi. Hivi leo dawa tunatumia kama tunataka kununua kipuli cha gari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Wizara ituletee njia mbadala ama *MSD*ipate mtu wa kufanya naye kazi mbadala wake au itupe kibali tunapokuwa tunahitaji dawa tusifuate utaratibu huu wa manunuvi ambao unatupa taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hatuna vifaa na

gharama za hivi vifaa vya upimaji ni gharama kubwa, Serikali ituambie ina mpango gani wa kutumia utaratibu wa *PPP* (*Public Private Partnership*) kwamba watu binafsi hasa hospitali zetu za Mjini, watu wana fedha wanataka kutibiwa matibabu mazuri, wako tayari kuchangia gharama na watu binafsi wanaweza wakatoa kununua mitambo kwa gharama zao, tukafanya *partnership*. Serikali inasemaje, imeshindwa hilo basi Serikali kutudhamini kwenye mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ukitaka kununua kitu kwa mkopo, ukitaka kukopa banki lazima upate dhamana kutoka Serikali, Serikali inasemaje katika hili, lazima Serikali itudhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni afya ya msingi. Elimu ya msingi Mheshimiwa Magufuli amesema bure namshukuru sana na nampongeza. Je, afya ya msingi kwa nini isiwe bure? Hivi wananchi hawa wanaoenda kutibiwa kwenye zahanati kuna shida gani hawa wakitibiwa bure? Ukiangalia kundi kubwa ambalo linakwenda hospitali mara kwa mara tayari linatibiwa bure, wanawake, watoto chini ya miaka mitano, wazee wanatibiwa bure, wagonjwa wa kifua kikuu, wagonjwa wa *HIV*, kisukari, wanatibiwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watu tunachangia huduma katika Mifuko ya Kijamii ya Afya. Sasa ukiangalia ukiondoa makundi hayo ambayo ndiyo yako mengi hospitali huyo anayelipia ni nani? Kwa nini Serikali sasa isikubali kwa afya ya msingi watu wetu wakapata huduma ya bure? Na kwa sababu tayari tunatoa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Hospitali yetu Mwananyamala tunataka tuongezewe wafanyakazi. Sisi kwa kutwa tunahudumia watu 2,500 ukiondoa watu 1,500 wa *methadone* jumla tunahudumia watu 4,000. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda ndiyo huo, ahsante sana. Leo

hujaongelea saluni za Kinondoni. Tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, atafutatiwa na Mheshimiwa Dkt. Balozi Diodorus Kamala.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wa Mkoa wa Kagera na hususan *Bukoba Town* amba majuzi usiku wa kuamkia tarehe 30 Aprili waliweza kupata tena mshutuko wa tetemeko ambalo tunamshukuru Mungu kwamba tetemeko hilo halikuweza kuleta athari kubwa zaidi ya kuongeza nyufa katika nyumba ambazo zilikwishapata nyufa pamoja na kuangusha kuta ambazo watu waliambiwa waanze kujenga wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichoweza kuwaombia ni kwamba nawaomba wawe watulivu na kuondoa hofu huku wakisubiri ripoti ya wataalam ambao tumeahidiwa kwamba watakwenda huko na hasa baada ya hoja yangu humu ndani ya Bunge na Mheshimiwa Waziri Muhongo kuweka kalenda kwamba timu hiyo itakwenda kule tarehe 17 kuweza kuwasilisha ripoti, pamoja na hayo amefanya uugwana ametanguliza *advance party* ya kufanya maandalizi na kuwaondoa watu hofu katika Mji wa Bukoba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tetemeko ambalo lilitupiga mnamo tarehe 9 Oktoba, 2016 liliacha athari kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake watambue kabisa kwamba zahanati nne pamoja na vituo vya afya viwili vilisambaratishwa kabisa. Baada ya Mheshimiwa Rais kutembelea Mkoa wetu na mji wetu na akavunja ile Kamati akitumia usemi kwamba hata kamati za harusi huwa zikakuwa na mwisho wake, jukumu la kuendelea kupokea michango na kuendeleza kazi zilizokuwa zinaendelea liliachwa kwenye kitengo cha maafa husika ambacho kiko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo shughuli nzima za Kamati ya Maafa zinasitishwa tayari vituo hivi kamati

ilikuwa imiteitengea shilingi milioni 380 kwa ajili ya ukarabati, tayari kwa zahanati za Buhembe pamoja na Rwanishenye tayari matofali yalishasombwa na kuwekwa pale, lakini tangu Rais alivyotoa maagizo yake na Kamati ile ikasitishwa kazi yake na shughuli zikarudishwa kwenye kitengo husika, ni kwamba zaidi ya matofali hakuna ambacho kimeendelea hadi hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati hizo pamoja na kituo cha afya bado viko katika hali ile ile, nitaomba Mheshimiwa Waziri aliangalile hili ili wananchi wa Bukoba Mjini waweze kutendewa haki na Serikali yao. Jamani hatujiombei maafa hili naomba litambulike, ni tatizo tu la kuwa katika mkondo wa majanga ya Kimataifa ndiyo kitu kinachotuletea matatizo. (*Makof*)

Kwa hiyo, tutaomba kabisa Mheshimiwa Waziri unapohitimisha ulijue hilo na kama unatenga mafungu yaende yakasaidie kwa kazi ambayo haikuweza kukamilika mtusaidie wananchi wa Bukoba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili natambua kabisa ni utaratibu na sera ya Serikali na hasa na mwenzangu alizungumza hii ni llani la Chama cha Mapinduzi kwamba kila Wilaya inapaswa kuwa na hospitali ambayo ni ya ngazi ya Wilaya.

Katika Mji wa Bukoba tayari hospitali hii ilishaanza kujengwa jengo kubwa la ghorofa moja, lakini jengo hilo limeendelea kutumika kama *OPD* kwa sababu hospitali hii ya Manispaa haina *theatre*, haina *pharmacy*, haina jengo la utawala wala haina majengo ya madaktari; yaani ni jengo hilo moja tu. Huko nyuma kipindi cha mwaka mmoja uliopita katika bajeti, tulielekezwa kuwasilisha maombi maalum ambayo tuliahidiwa kupewa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuendelea kuimarisha hospitali hii ya Wilaya. Nasikitika kuzungumza kwamba mpaka dakika hii fedha hizo hazijawahi kuletwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nimeona kabisa

katika mafungu ambayo yananuiwa kuelekezwa huko ni bilioni mbili tena. Naomba safari hii Serikali itutimizie haki hiyo ituletee fedha hizo na ikiwezekana iongeze fungu ili jamanii wananchi wa Bukoba Mjini muwaangalie kwa jicho la huruma kabisa. (*Makof*)

Mheshimwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Mkoa wa Kagera na Hospitali yetu ya Mkoa kwa utaratibu unaoleweka ndani ya Wizara ile ni Hospitali ya Rufaa. Nitaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie na Watanzania wote wajue kupitia hili, hivi hospitali inapoitwa Hospitali ya Rufaa tunaomba kujuu ipaswa kuwa na sifa zipi? Maneno tu ya kuita Hospitali ya Rufaa isiwe ni kigezo ya kuwa rufaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka huko nyuma hata Serikali iliwahi kungia kwenye mtego huo kila taasisi ikawa inageuzwa Chuo Kikuu, lakini baadaye Serikali ilikuja kujitafakari zaidi ikaondoa utaratibu huo.

Mheshimwa Mwenyekiti, nafikiri suala hili la Hospitali ya Rufaa inabidi tulitendee haki sawa na huduma inayopaswa kutolewa kama hospitali za rufaa. Sidhani kama suluhisho la timu kuifunga timu nyingine ni kupanua magoli, nafikiri suluhisho huwa ni kufundisha soko ndiyo unapata magoli kupanua magoli sidhani kama ndiyo *solution* ya kujuu kama timu inaweza kucheza mpira. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimwa Mwenyekiti, ninaomba wakati wa maafa ya tetemeko yalipotokea kupitia kwa Mkuu wa Mkoa kwa niaba ya kamati ya maafa na wananchi wa Mkoa wa Kagera, aliomba *at least CT-Scan* kwa sababu wakati wa athari za tetemeko wagonjwa wengi waliopata athari ilibidi wapelekwe Bugando, Mwanza, kwa sababu ya kukosa baadhi ya vipimo. Tunaomba hiyo ahadi tuliyaoahidiwa kwamba Hospitali ya Mkoa italetewa *CT-Scan* kwa njia ya dharura, nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha hotuba yako usingoje tuende kwenye mafungu kuzibiana mishahara, hii ahadi ya *CT-Scan* mnatuletea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi umeona tena tetemeko

lingine, hivi mnataka tuwe wageni wa nani kama Serikali inatuahidi, haitekelezi kile ambacho imetuahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wakati unahitimisha hotuba yako hili suala ulizungumzie ili wananchi wa Kagera na Mji wa Bukoba kwa ujumla waweze kupata *hope* na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lisemwalo lipo kama halipo linakuja. Mheshimiwa Waziri akina mama wanaojifungua wameanza kuwa na wasiwasi kwa baadhi ya matukio yanayotokea bila Wizara au Mamlaka husika kutoa taarifa za haraka au kutoa *statements*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Temeke inasemekana kuna mama mmoja alijifungua mapacha halafu pacha mmoja akayeyuka kinamna namna, mambo haya yamewahi kuwa *reported kwamba* kuna vitendo vya kuiba watoto. Kuna wafanyakzi wanafanya *deal* la kuiba watoto wanaozaliwa. Tutaomba kupitia kwako hebu waondoe akina mama wasiwasi wanaojifungua, warudishe imani na hospitali zetu, waache kujifungulia vichochoroni kwa sababu ya kukwepa kwamba wataibiwa watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kutunza muda. Narudi sasa kwenye mwendo wa kasi wa dakika tano-tano. Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kuongoza Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kama alivyoeleza kaka yangu Mheshimiwa Lwakatare, tetemeko

lililotukumba Mkoa wa Kagera, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri alipofika pale Jimboni kwangu Misenyi kuna eneo moja linaitwa Kabyaile akakuta zahanati imeenda chini yote kwa sababu ya tetemeko, akanipigia simu akaniuliza Mheshimiwa Kamala hapa zahanati yako imekwenda bado unahitaji zahanati au unahitaji kituo cha afya. Nikamwambia Mheshimiwa mimi ni nani kuombwa na Waziri nipewe kituo cha afya nikaendelea kung'ang'ania jambo dogo! Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu kituo cha afya hicho kimejengwa na kinafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ziko changamoto zinaendelea, lakini nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini kwa kuhakikisha umeme unafika pale kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, umeme umefika pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais alituahidi kutupa *access road* ya lami ya kwenda pale Kabyaire na lami hiyo sasa itajengwa kwenda pale Kabyaire ili wagonjwa waweze kufika pale bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kuwa tunayo na ahadi ya Makamu wa Rais ya kuhakikisha tunapata barabara nzuri ya kwenda Mgana basi tuunganishe hii *access road* ya Kabyaire na *access road* ya kwenda Hospitali Teule ya Mgana ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Pia nichukue nafasi hii kushukuru kwa kweli kwa mambo yote hayo ambayo yamefanyika ndani ya kipindi kifupi na wenzetu wa Bukoba Vijiji walipoona Kabyaire sasa inapata kituo cha afya na wao wakatuomba wakasema tunaomba nasi tupate huduma kutoka kwenye kituo hicho na hatuna sababu ya kuwabagua wenzetu, niombe basi Serikali ifanye utaratibu iunganishe barabaa ya Kabyaire pamoja na ile inayokwenda Bukoba Vijiji kwa kaka yangu Mheshimiwa Rweikiza ili wananchi wote waweze kupata huduma safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa siyo mkweli kama nitamaliza kuzungumza hapa bila kueleza ukweli kwamba

Hospitali Teule ya Mgana (*DDH*) pamoja na taarifa nzuri zilizopo ya fedha tunazooneshwa kwamba tumepokea kwa ajili ya kutoa huduma, lakini ukweli pale huduma ya mama na mtoto hakuna, hakuna huduma ya bure kama inavyotarajiwa itolewe, hili limekuwa tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Baraza la Madiwani walikuwa na kikao na wakazungumza, Mwenyekiti wa Halmashauri akaniambia wanakaa na mimi nikamwambia nilishamueleza Mwenyekiti wangu wa Halmashauri wakiona jambo lolote wakae na wakiona hawaoni siendi wajue bado naamini wanafanya kazi.

Kwa hiyo, wamekaa na wamezungumza walipomaliza akanipigia akasema Mheshimiwa mambo hayaendi, nikasema sasa kama mambo hayaendi, basi kabla mimi mwenyewe sijaja nitamuomba kwanza Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa sababu leo atawasilisha hoja yake basi nitamuomba atusaidie na yeye kuja hapo Mgana aweze kuangalia na kujifunza nini kimetokeea, Hospitali ya Mgana ambayo ilikuwa inatoa huduma nzuri kwa watoto sasa haitoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumuomba Mheshimiwa Waziri aungane nami tuende tutembelee hiyo hospitali ya Mgana tuweze kuondoa hii *pandora's box* inayojitokeza ya maajabu ambayo yameanza kujitokeza ya hospitali kushindwa kutoa huduma....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante Mheshimiwa.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdul-Aziz atafuatiwa na Mheshimiwa Bura na Mheshimiwa Mgimwa ajiandae.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri kuhusu matatizo ya hospitali ya Mkoa wa Morogoro, kuhusu *x-ray machine*, majokofu ya kuhifadhi maiti na upungufu wa madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo nisipomshukuru Waziri na Naibu Waziri. Walishughulikia tatizo ya *x-ray machine*, walitutumia Wataalam ambao *machine* yetu ilikuwa ni *analogue* wakaibadilisha kuwa *digital* na sasa inahudumia wagonjwa 50 mpaka 70 kwa siku. Pia tumeweza kuunganishwa katika mfumo wa *tele-medicine* ambao wanapata ushauri zaidi kwa Madaktari Bingwa.

Kuhusu majokofu tunamshukuru Mheshimiwa Waziri ametupatia na sasa katika wiki hii yanaanza kutolewa ya zamani na kuwekwa mapya katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Upungufu wa madaktari tunashukuru Mheshimiwa Waziri umetutimizia kiasi kikubwa ila tuna tatizo bado moja kubwa la *specialist* wa *ENT* ambaye hatuna hata mmoja.

Pili, tuna tatizo vilevile la wafamasia ambao walitakiwa wawe 14 lakini tunae mmoja tu msaidizi. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri katika hilo naamini kwa kazi unazozifanya na Naibu Waziri kwa *speed* ya Awamu ya Tano mtatumalizia kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nytingine ni wodi ya wazazi katika hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Hospitali ya Mkoa inapokea wazazi 40 kwa wastani kwa siku na wodi

inaweza kupokea wagonjwa 20 mpaka 25 tu kwa siku. Kwa hiyo, tungeomba Mheshimiwa Waziri atuongezee wodi nyingine katika bajeti yake ili tuweze kutimiza mahitaji ya wazazi katika wodi hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine tuliyonayo Morogoro ni *ambulance*. Tunayo *ambulance* moja tu na wagonjwa wanakuwa ni wengi mno kiasi ambacho wengine wanaandikiwa rufaa ya kwenda Muhimbili, *ambulance* moja inashindwa kufanya kazi yake. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo na nitakupa ushirikiano ili tuweze kupata *ambulance* mpya nyingine kwa ajili ya hospitali ya Mkoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine la gharama za wanaovunjika viungo kwa maana ya wanaovunjika mifupa kwenye ajali na matatizo mengine. Gharama zile katika Hospitali ya Mkoa ambao hawana bima ya afya ni kubwa mno kuanzia shilingi 500,000 mpaka shilingi 700,000, lakini ukiuliza unaambiwa kwa sababu ya gharama ya vyuma.

Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo kwa sababu gharama hizi kwa watu wa hali ya chini wanashindwa kumudu, tungeomba mtufikirie juu ya hili ili tuweze kupata vyuma na vifaa vingine kwa ajili ya kuweza kupunguza gharama hizo ili wananchi waweze kugharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kuokoa muda. Tunaendelea Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na pia nampongeza Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi ambazo tunaziona kwa macho pamoja na ukata wa fedha ambazo wanazipata kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kituo chetu cha afya kile kilichopo pale Chamwino - Ikulu, ni kituo ambacho kingeweza kuwa mfano kwa vituo vingi nya afya, lakini kile kituo hakina watendaji, hakina madaktari, hakina wauguzi, hakina vifaa tiba kituo ambacho kiko kwenye geti la Ikulu.

Mheshimiwa Waziri, ninaiomba Serikali sasa kwamba kituo kile kitazamwe kwa macho ya huruma ili wananchi wa Wilaya ya Chamwino waweze kupata huduma nzuri karibu na geti la Ikulu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kukamilisha majengo ya kituo cha afya Mima na Mbori. Vituo hivi nya afya vina zaidi ya miaka kumi havijakamilika. Kati ya wale wanawake 556 wanaokufa kwa mwaka, wanawake walio jirani na kituo cha afya Mima na Mbori ni kati ya hao wanawake 556.

Mheshimiwa Ummy nitafurahi sana ukiacha alama katika Wizara hii maana wewe ni mwanamke mwenzetu, wewe ni mwanamke kama wanawake wanaopata mimba na kupata matatizo makubwa. Nikusihhi, ninajua bajeti yako siyo kubwa, una bajeti kidogo sana na niwasihhi Waheshimiwa Wabunge tutakapokuja kujadili bajeti kubwa tuhakikishe kwamba Wizara hii inapata fedha za kutosha kwa sababu ndiyo Wizara inayoangalia afya za Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa mwenyekiti, hata wanawake ambao wanatamani kupata huduma ya ugonjwa wa *cancer*, kujua afya zao hawapati kwa sababu vituo vyetu havina wataalam. Sasa ukitaka kupunguza wagonjwa katika hospitali zetu za rufaa lazima uimarishe vituo nya afya, lazima uimarishe zahanati zetu na unaziimarisha kwa huduma, kwa kuwa na watendaji wa kutosha.

Nikusihhi na niisihi Serikali yangu sikivu, sasa kwamba sasa ifike wakati kwamba zahanati zetu zinaimarishwa, vituo nya afya vinakuwa na watendaji wa kutosha, vifaa tiba na wahudumu wa kutosha kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Taasisi ya Jakaya Kikwete imefanya kazi kubwa ya kukoa shilingi bilioni 3.75, lakini fedha walizopewa pamoja na kuomba shilingi bilioni nne wamepata shilingi milioni 500 tu. Hivi wanaweza wakafanya nini? Wamefanya kazi kubwa kwa Watanzania, wameokoa Watanzania walio wengi. Naomba Serikali yetu iiangalie taasisi hizi ambazo zinafanya kazi za kuwasaidia Watanzania katika kuimarisha afya zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuisiwavunje moyo Madaktari Bingwa wetu, wasomi hawa tuisiwavunje moyo, kama ni fedha wapelekewe ili ziwasaidie katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie dirisha la wazee. Hospitali zetu zina dirisha la wazee, lakini je, dirisha la wazee kuna dawa? Wazee ni asilimia sita tu ya Watanzania lakini je, wanapata dawa katika dirisha lao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliandika andiko maalum kwa ajili ya kituo cha afya Bahi, mpaka leo wanawake wanakufa kule Bahi kwa sababu ya kukosa huduma muhimu katika kituo cha afya Bahi tena kiko barabarani, kingesaidia na ajali zinazopatikana maeneo yale. Hawana *x-ray*, hawana huduma yoyote yaani ni kituo cha afya duni sana, lakini ni kituo cha afya cha Wilaya. Sasa hivi Wilaya ya Bahi ina zaidi ya mika kumi tangu ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia wodi ya wazazi Hospitali ya Mkoa. Tulikuomba shilingi bilioni moja tu mwaka jana ulipotembelea ile hospitali, tukakuamini Dada Ummy kwamba utatufikiria na utatuombea hizo hela...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Shally Raymond ajandae.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, vilevile kushukuru sana Serikali na Wizara kwa ujumla kuanzia Mheshimiwa Ummy, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo machache sana, jambo la kwanza ningependa kuanza na suala la mkanganyiko ambao upo katil ya *TBS* na *TFDA*. Tatizo tunaloliona hapa ni mkanganyiko au muingiliano wa kazi katil ya taasisi hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba katika maeneo mengi taasisi hizi mbili zinaingiliana katika utendaji wake wa kazi, na katika kutenda kazi unakuta kuna mambo ambayo yanaendelea katika taasisi hizi ambazo zipo kwa mujibu wa sharia, kwamba unakuta wakati kwa mfano, misaada inatolewa kutoka kwa wahisani mbalimbali nje ya nchi, misaada ile inapokuja nchini kunakuwa kuna mkanganyiko hapa, *TFDA* wataingia, *TBS* wataingia vilevile, *TFDA* kuna *charge* nyingine ambazo wanaziweka kwa ajili ya misaada hii ambayo tunapewa kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi yetu tuinajua, bajeti iliyoiezwa ni bajeti kubwa lakini ni lazima tuwe wazi kwamba bajeti iliyopita ilikuwa finyu sana vilevile haikutekelezeka kwa asilimia nyingi, sasa tunapopata fedha hizi au tunapopata misaada hii kutoka kwa wahisani halafu inavyofika bandarini inatozwa kodi kubwa, kwa mfano, magari ya wagonjwa, vifaa tiba na kadhalika, inapofika wakati Serikali inatoza kodi za namna hii, inarudisha nyuma maendeleo katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona kabisa kwamba hata wananchi wetu kule vijiji ni wanakosa huduma hizi kwa sababu ya urasimu ambaao upo katika taasisi mbalimbali za Serikali hasa pale *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye hata hivyo kipindi cha nyuma aliliongelea hili suala akatoa majibu kuhusu tatizo hili, ningependa sana kumsihi tena kwa mara nyine Waziri wa Fedha aweze kuliangalia suala hili ili tunapopata misaada kutoka kwa wahisani iweze kupita bure katika bandari zetu na huduma hizo ziweze kuwafikia wananchi moja kwa moja, kwa sababu tatizo la afya bado ni kubwa katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nigosie sasa suala kubwa ambalo lipo Jimboni kwangu Kalenga. Nimeongea sana na ninaomba nirudie tena kwamba Jimbo la Kalenga na Jimbo la Isimani katika Wilaya ya Iringa Vijiji ni tuna tatizo la gari la wagonjwa. Narudia tena kwa sababu tatizo hili ni kubwa. Wilaya ya Iringa Vijiji ina zaidi ya watu 300,000, tuna gari la wagonjwa ambalo ni *hiace*, kwa kweli kwa miundombini tuliyonayo halikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mwezi, akina mama ambaao wanajifungua ni zaidi ya 200 ambaao wanatoka maeneo mbalimbali lakini inahudumia majimbo mengine hata Jimbo la Mheshimiwa Mwamoto pia lipo katika huduma hii, hivyo ningependa sana Serikali iweze kuona uzito wa kutupatia *ambulance* katika Hospitali ya Ipamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea hili suala kwa muda mrefu na ninachokiomba zawadi pekee ambayo nitaiomba kutoka kwenye Wizara, Mheshimiwa Dada Ummy, Mheshimiwa Kigwangalla zawadi ambayo mtanipa mimi katika miaka hii mitano naombeni mnipe *ambulance* katika Hospitali ya Ipamba ili tuweze kuokoa maisha ya wananchi katika Jimbo letu, tuweze kuokoa maisha ya Watanzania katika Jimbo la Kalenga, tuweze kuokoa maisha ya

Watanzania ambao wapo katika Wilaya ya Iringa vijijini. Ni muda mrefu kwa kweli inasikitisha sana kama Serikali ambayo tumeona kwa namna moja au nyingine maeneo mbalimbali *ambulance* zimepelekwa, ninaamini kabisa Serikali itafanya namna tunaweza tukapa *ambulance* katika Jimbo la Kalenga, katika hospitali hii ya Ipamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuongea sana, nimshikuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Kigwangalla kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Kigwangalla ulikuja Jimboni, umefanya kazi nzuri na wananchi bado wanakukumbuka na wamenipa salamu kwamba wanaomba yale uliyowaahidi wawewe kutekelezewa. Na mimi nitaendelea kuongea haya na kuendelea kuwapongeza Serikali kwa sababu ninaamini Serikali hii ya Awamu ya Tano imejizatiti vizuri kabisa katika kuhakikisha sekta hii ya afya inakua na inaenda kuwafikia wananchi moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana niweze kukushikuru na ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Makilagi, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na hizi dakika za Mgimwa najua utanipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushikuru wewe na nimshikuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote aliyenipa nafasi ya kuweza kusimama na kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuunga mkono hoja na sababu zangu ni mbili zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hotuba imeandaliwa vizuri sana, pili, dhamira ya Serikali chini ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na watendaji wote wa Serikali hasa katika sekta hii ya afya na maendeleo ya jamii kwa kweli wamejipanga. Wanaonesha kabisa dhamira nzuri ya kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya bora. Kwa msingi huo naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe ushauri kwamba kwa kuwa Wizara imejipanga vizuri na kwa sababu changamoto za Wizara ya Afya na changamoto za Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni kubwa, nimefurahi leo nimemuona Waziri wa Fedha yupo hapa, ninaomba Serikali ipeleke fedha katika Wizara hii kwa sababu bila afya hakuna kilimo, uchumi wala chochote katika Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Fedha ijitahidi kupeleka fedha kwenye sekta ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nimejaribu kupitia kitabu hiki kila kitu inaonekana kama taasisi hii hakuna kitu. Taasisi hii ni mtambuka; bila Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kweli hakuna chochote. Ninafurahi Waziri wa Fedha ananisikiliza na katika mwaka wa fedha ujao tunataka kuona sasa *percentinaongezeka* katika sekta hii ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Serikali iboreshe maslahi ya wafanyakazi katika sekta hii. Wanafanya kazi ngumu sana ma-*nurse* wetu, madaktari na watumishi wetu katika huduma za maendeleo ya jamii, bibi na bwana maendeleo ya jamii, lakini kwa bahati mbaya ni kundi ambalo wakati mwingine linasahaulika.

Nimefurahishwa na hotuba ya Rais juzi wakati wa Mei Mosi kwamba anakwenda kuboreshwa maslahi ya wafanyakazi. Naomba sekta hii ya afya hebu angalieni ma-*nurse* wetu wanavyofanya kazi kwa tija, angalieni madaktari wetu wanafanya kazi usiku na mchana, wanafanya kazi saa za ziada, hawana kupumzika wala kuchoka lakini zile stahili na posho zao hawazipati kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali ipeleke vifaa tiba kama ambavyo imeanza kununua dawa, ipeleke vifaa tiba katika vituo nya afya na ipeleke wataalam wa kutosha na hasa kutokana na hili sekesekе lilitotokea juzi, watalaam sasa wamepungua katika taasisi zile. Naomba Serikali iwe makini ihakikishe hakuna kituo kinachopungukiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwenye ujenzi wa vituo nya afya. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia wanawake wanafariki kwa kukosa huduma, watoto chini ya miaka mitano wanafariki. Ni ukweli usiopingika kwamba vituo nya ya ni vichache, tunaomba Serikali sasa jje na mkakati maalum na hapa naomba nitoe ushauri kwamba sasa Serikali kila Halmashauri tujenge kila mwaka vituo viwili, ukipiga mahesabu kwa Halmashauri tulizonazo 183, kama tutajenga vituo viwili, viwili kila mwaka na inawezekana, tutaweza kufika mbali; mara baada ya miaka mitatu tunaweza kuwa tumejenga vituo zaidi ya 1,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vituo nya afya vipo ni maboma, vimejengwa hakuna mabaara, havijakamilika, nguvu za wananchi zimeishia pale. Ninaomba sana Wizara ya Fedha hebu tafuteni fedha zozote hata kama ni kwa mkopo, pelekeni ili hivi vituo vianze kwa sababu wananchi wamejikusanya wameishia pale kwa kushirikiana na Wabunge kupitia Mifuko ya Majimbo. Sasa Serikali ni jukumu lake kuhakikisha vituo hivi vinakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii pia iweke utaratibu wa kuhakikisha inaongeza fedha katika maeneo mbalimbali na hasa katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Mara. Ameongea Mheshimiwa Bonny Hospitali ya Rufaa ile ya Mkoa *Mwalimu Nyerere Memorial Centre* ni kituo ambacho kitakuwa ni ukombozi kwa watanzania na hasa wa Kanda ya Ziwa. Bugando sasa imeelemewa, tukipata kituo hiki na Serikali ikipeleka fedha za kutosha kila mwaka badala ya inavyofanya hivi sasa shilingi milioni 200 kila mwaka hakitakwisha leo.

Ninaomba Serikali ikiwezekana ipeleke hela kwa mkupuo shilingi bilioni 10 mwaka mwingine shilingi bilioni 10 ile hospitali ijengwe iwe ni ukombozi kwa hospitali za Kanda ya Ziwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaofariki kabla ya kufikisha miaka mitano. Ninashukuru jitihada za Serikali vifo vimepungua. Kuna tatizo la watoto wanaozaliwa njiti. nimejaribu kupitia kwenye hotuba ya Waziri sikuona eneo hili. Katika vifo vya watoto wanaofariki chini ya umri wa miaka mitano mionganoni mwao ni watoto wanaofariki wakiwa njiti ni asilimia 40 na ni sehemu ya pili ya watoto wanaofariki. Ukiangalia takwimu kila siku watoto 100 wanafariki na kila mwaka watoto 9,000...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Tweve na Mheshimiwa Fredy Mwakibete ajiandae. Tunaendelea na Mheshimiwa Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. (*Makof*)

Awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dada yangu Ummy na Mheshimiwa Kigwangalla, mmekuwa mabalozi wazuri, kweli hilo jina linawafaa. Ni matarajio yangu Watanzania hasa wanawake na watoto wanatambua na wanajivunia mchango mkubwa ambao mnautoa kwenye Wizara yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 55 anasema: "Maendeleo endelevu ya Taifa lolote yanategemea uwekezaji katika

makuzi, malezi na maendeleo ya mtoto. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 idadi ya watoto ni asilimia 51.6 ya Watanzania wote.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambazo zimepiga hatua, zilifanya jitihada za makusudi kuhakikisha zinawekeza kwenye hii rasilimali watu. Kwa hiyo, kwa hotuba hii Mheshimiwa Waziri naungana na wewe kabisa kuwa ni jukumu letu kama Taifa kuhakikisha kuwa tunawatengenezea mazingira mazuri hii asilimia 51.6, kwa sababu tunasema tunataka Tanzania iweze kufika uchumi wa katika hii ndiyo nguvu kazi ambayo itatusaidia kuweza kufika hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti ambao umefanywa na *World Health Organization* wakishirikiana na *World Bank* wanasesma, Taifa kama tunataka kuhakikisha tunawekeza kwenye watoto umri ambao unafaa ni kuanzia mwaka sifuri mpaka miaka miwili. Sasa Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwa kuleta takwimu hizi, imetupa picha kamili kuwa sasa ni zaidi ya nusu ya Watanzania ni watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ningependa turudi nyuma kwa kutumia huu utafiti na ushauri ambao umetolewa na *World Health Organisation*. Turudi nyuma sasa tujue katika hii asilimia 51.2 ni watoto wangapi wako kwenye umri wa mwaka sifuri mpaka miaka miwili, kwa sababu hii ni *critical age* ndiyo maana wamesesma kama Taifa tunatakiwa kuanza kuwekeza hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema ni *critical?* Kama hotuba yako ambavyo inaonesha *mortality rate* ya watoto wa mwaka sifuri mpaka miwili ni kubwa sana, tunapoteza watoto 21 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa.

Pia umekiri kabisa kuwa udumavu ni tatizo kubwa sana kwa Taifa letu, tumekuwa na watoto ambao uelewa wao unakuwa ni mdogo sana. Tunajua kabisa tatizo la udumavu linafanya mtoto ashindwe kufikiri, kutunza kumbukumbu na hata kufanya maamuzi inawawia vigumu sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tuna kazi kubwa kama taifa kuhakikisha tunalinda hawa watoto wetu ili tuweze kuflikia malengo hayo ya uchumi wa kati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo kwa Serikali yatakuwa kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema hii *age* ya mwaka sifuri mpaka miwili ni *critical* na tunataka tuwe na watoto ambao wataweza ku-*grasp* hizi *concept*, sasa hivi kumekuwa na *frustration*. Mtoto anakwenda shulen, mwalimu ameandaliwa na tumetengeneza miundombinu mizuri lakini watoto hawa bado wanashindwa ku-*grasp* hizi *concept* zinazofundishwa shulen. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali na kama wizara naomba tupitie hizi sheria, tuzilite hapa ili tuweze kufanya mabadiliko na tunaweza tukaanza kidogo tu, hizi *maternity leaves* tunazipuuzia, tunasema zipo vizuri, hazipo vizuri, ukiangalia nchi ambazo zimeendelea kwa mfano, *Scandinavian countries* wanatoa kipaumbele kikubwa sana kwa wamama wajawazito, si ndiyo. Wengine wanapewa hadi siku 480 sisi hapa bado ni siku 120, siku hizi haitoshi kwa sababu tunatakiwa kumlinda huyu mama ili aweze kumlea mtoto wake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze juhudzi za Serikali za kuhakikisha tunatoa elimu kwa mama mjamzito juu ya lishe ya motto, lakini hii haitoshi tunatakiwa kwenda mbali zaidi. Tumesema kuna viwanda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja nitaleta mapendekezo yangu kwa maandishi. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ambao watagawana dakika tano na Mheshimiwa Lathifah Chande.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya.

Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu tupo hapa kwa sababu ya afya na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameitendea haki Wizara hii ya Afya. Tumeona na tumeshuhudia ajira zikitolewa, tumeona jinsi ambavyo magodoro pamoja na vitanda vikipelekwa kwenye Halmashauri zote nchini, pia tumeona jinsi ujenzi wa chuo pamoja na hospitali ya Mloganzila kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, zote hizi tunasema ahsante sana Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wakuu ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nikija katika Jimbo langu la Busokelo kuna changamoto ambazo mara nyingi nimekuwa nikiongea nawe Mheshimiwa Waziri kwa bahati mbaya sana hazijaweza kutekelezeka. Tuliomba mashine ya usingizi na kwa bahati mbaya pia tuna kituo kimoja tu katika Jimbo zima la Busokelo na mashine hii haipo, maana yake inawalazimu wananchi wangu kusafiri umbali wa zaidi ya kilometra 60 kufuata huduma mijini. Kwa hiyo, nitashukuru sana kama ambavyo uliniahidi kwamba unaweza kufuatilia na kutupatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, pia tunaomba sana katika hospitali hii ya Kandete tunasema kuna changamoto ya *ultra sound* na *x-ray machine* hatuna. Kwa hiyo, tunaomba kama mtawezza kutusaidia katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana kwa jinsi ambavyo mmejitahidi kupeleka dawa, lakini hizi dawa kwa bahati mbaya wakati mwingine ama yanachelewa kununuliwa katika Halmashauri zetu ama kunakuwa kuna *technical delay* hapo katikati. Kwa hiyo, tunaomba Wizara kama mtafuatilia vizuri na hii inakuwa ni nchi nzima. Wizara inatoa fedha lakini Halmashauri haziwajibiki ipasavyo. Kwa hiyo, katika hili nafikiri ingekuwa jambo jema kama tungefuatilia pia kama Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niwashukuru kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Hospitali ya Rufaa ya Mbeya tumeona jinsi ambavyo mmeipa kipaumbele kwa maana ya majengo pamoja na vitanda. Bado haitoshi hospitali hii kuna *specialist* ambao wapo pale kwa zaidi ya miaka mine, *categorization* zao za mishahara bado ni zilezile za zamani. Kwa hiyo, tungeomba hata hospitali nyingine katika nchi hii ambapo wamepandishwa ngazi kwa kusoma ama kwa taaluma yao waweze kulipwa kufuatana na jinsi ambavyo wanafanya kazi pale kazini kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala hili la TEHAMA kwenye afya. TEHAMA kwenye afya ni muhimu sana katika ulimwengu wa sasa, ukizingatia kwamba kwa sasa bajeti iliyopita Wizara mlipendekeza kwamba mtaanza kutumia *tele-medicine*. *Tele-medicine* ni mfumo ambao unatumika kutibu wagonjwa ama kufanya *consultation* na wagonjwa kwa daktari alie mbali na eneo husika. Anaweza akawa Dar es Salaam akamtibu ama akampa ushauri mtu ambaye yupo nje kabisa na Dar es Salaam labda mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba hii *tele-medicine* iweze kuwezeshwa zaidi ili daktari aweze kupata nafasi ya kuhudumia wagonjwa wengi zaidi kuliko hivi sasa mpaka mganjwa ama *client* aende hospitalini kutibiwa. Ni muhimu sana hili lizingatiwe kama Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningefurahi zaidi kuona *database* ambazo zinatumika hospitalini hasa hizi za *CTC II* ambayo ni *Care and Treatment Clinic* pamoja na *DHIS II*

ambayo ni *District Health Information Systems* kama zinakuwa *developed au programmed* na wazawa kuliko hivi sasa wazawa wanashiriki kwa sehemu ndogo, asilimia kubwa sana tunapewa misaada kutoka nje kwa maana kwamba hata wale *specialist* wa kusimamia hizi. Lengo lake ni kufanya *sustainability* yake iweze kuwepo kwa sababu hii misaada kuna wakati itakwisha na ikiisha hatutakuwa tena na *support* nyingine yoyote. Kwa hiyo, tukiwashirikisha wazawa itaturahisishia zaidi kufanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikija katika suala la *HIV* (UKIMWI) tumeona mmetenga shilingi bilioni 251.5; ninaiomba Wizara na Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi, hivi karibuni tulikuwa na semina ya kutoka *National Council of People Living With HIV* humu ndani. Tuliona kwamba kuna changamoto kubwa sana kwa dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi. Kwa bahati mbaya sana hizi *opportunistic infections* wafadhili hawatoi wala Serikali hainunui. Maana yake inaishia kuwa gharama kwa wagonjwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na Mheshimiwa Lathifah Chande na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae. Hawa wawili wa kwanza ni dakika tano tu.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya napenda kuzungumzia Hospitali ya Rufaa ya Mkao ya Ligula. Hospitali ile imepandishwa kuwa ya Rufaa ya Mkao lakini jambo la

kusikitisha sana tena naomba mnisikilize na Mheshimiwa Kigwangalla nilikuufuata nikakuuliza lakini haukunipa majibu. Hatuna mtaalam wa *x-ray* wa uhakika, vijana wetu wanapopata matatizo ya kuvunjika miguu na kadhalika, ni kama sawa mtu anaendelezwa kwenda kutiwa kilema, kwa sababu karibu watu wengi wanaofungwa mikopa (*P.O.P*) pale wanaopata tiba za mifupa hakika tiba zile siyo za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi inabidi watoke kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa waende Ndanda ama Nyangao bila Rufaa kwa sababu zile ki-rank ni ndogo kuliko hii ya Rufaa ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtuangalie, mmeipandisha hadhi sawa tunashukuru, lakini tukienda kwenye wodi ya wazazi vitanda ni vichache mno, mtu ametoka kwenye uchungu wa kujifungua anaambiwa alale kitandani watu watatu. Nina uhakika ninachokizungumza, nilikaa pale wiki mbili namuuguza wifi yangu hali iko hivyo, haijalishi huyu mtu kajifungua kwa *operation*, ama kajifungua kawaida. Kwa hiyo, tunaposema hali ni mbaya ninamaanisha hali ni mbaya kwa sababu ni kitu ambacho nakijua nanime-*experience*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu duka la *MSD*la Kanda ya Kusini linaenda kujengwa Ruangwa kwenye Jimbo la Waziri Mkuu, sina shida na hilo. Shida yangu kubwa iko wapi, kama kweli mnakujuwa Ruangwa, Ruangwa ni ndani barabara ile ya kilometra 45 kutoka Nanganga kwenda Ruangwa ni ya vumbi na kipindi cha masika hakufikiki. Barabara ile na Jimbo la Ruangwa lipo ndani haliunganiki zaidi na Wilaya zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini duka hili lisikae Masasi ambako ni *centre* mtu wa Tunduru analikuta, mtu wa Mtwara analikuta, mtu wa Lindi na anayetoka Newala analikuta, kwa nini lisikae pale mkaamua kwenda kulipeleka kule? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama

mnaona kabisa ni lazima liende likakae Jimboni kwa Waziri Mkuu, mtengeneze zile kilometra 45 za barabara ili kusudi watu wanapoenda kuchukua madawa wasihangaike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa za watu wenye ulemavu wa ngozi. Siku ya maadhimisho ya wanawake nilienda shule ya msingi Masasi ambayo inatoa elimu jumuishi. Nimewakuta watoto pale takribani 39 wenye ulemavu wa ngozi, wana ari ya kujifunza lakini yale mafuta hawapati.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba muwafikirie watoto wale ili nao wapate haki yao ya elimu. Pia kuna watoto wenye uoni haffiu na ambao hawaoni kabisa lakini vifaa vya kujifunzia vya kutosha hakuna, hivyo wanashindwa kupata haki yao ya elimu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya nafikiri mna jukumu la kuhakikisha watoto wale wanapata haki yao ya elimu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mangaka ambayo inahudumia Nanyumbu. Hospitali ile imepandishwa hadhi kuwa ya Wilaya lakini haina *x-ray*. Kwa hiyo, naomba katika mpango wako Mheshimiwa Waziri, basi ufanye kila linalowezekana ili *x-ray* ile ipatikane iweze ku wahudumia watu wa Nanyumbu na majirani zao. Tunasema afya kwanza ili twende kwenye mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 76 amezungumzia suala la kuhakikisha wodi za watoto wachanga zinaanzishwa katika hospitali zote za rufaa. Namuomba Mheshimiwa Waziri suala hili lisiwe kwenye makaratsi na maneno... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lathifah Chande.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea juu ya sera ya Serikali ya kuhakikisha kila kata nchini inapata kituo cha afya. Mpaka sasa hivi imeonesha hii sera imeshindikana na kupelekeea katika kata za nchi nzima 3,959, kata 448 tu ndio zimepata vituo vya afya. Sasa tukienda kwenye Mkoa wa Lindi, tuna kata 138 lakini cha kusikitisha sana ni kata 19 tu ambazo zina vituo vya afya. Kibaya zaidi ni kata moja tu yenye kituo cha afya ambacho kinatoa huduma ya dharura ya upasuaji ya mama mjamzito, hii kata iko Kilimalondo - Nachingwea. Hii imepelekeea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi kuwa tegemezi kubwa kwa ajili ya kutoa huduma ya afya *especially* kwa akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kibaya zaidi na kutegemewa kote kwa hii hospitali ukiangalia majengo yake tangu mwaka 1954 hayajawahi kufanyiwa ukarabati wowote. Vilevile hakuna nafasi ya kutosha, hata tukisema pawe *expanded palepale* kibaya zaidi *labour ward* ina uwezo wa kuhudumia akina mama wajawazito 30 tu kwa wakati mmoja wakati wa kujifungua, hii ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vifaa muhimu kama *x-ray* hakuna, sasa hivi ni miezi mitatu ilikuwepo *x-ray* moja tu ambayo mpaka sasa hivi haifanyi kazi, kwa hiyo hilo pia liangaliwe. Pia watumishi hawatoshelezi mahitaji ya hospitali ile ya Mkoa. Wauguzi wengi wamestaafu, hakuna *specialists* wa kutosha na hii tumbua tumbua yenu hii kwa maana hiyo hata hao wachache waliopo tumbua tumbua kwa sababu ya kutuaminisha kwa ajili ya kuwa na vyeti *fake*, matokeo yake hawa wachache pia wataendelea kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali ihakikishe inatekeleza sera yake ya kuhakikisha kila kata inafikiwa na kupatikana vituo vya afya katika hizo kata, pia kutokana na kwamba tayari kuna eneo limetengwa kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Mkoa wa Lindi, basi kwa nini Serikali

isifikirie angalau *unit* ya *labour* iweze kuwepo pale, ambayo itakuwa na *facilities* zote zinazohitajika kwa ajili ya mama anapokuwa anajifungua, hii itasaidia kupunguza hata *maternal mortality rate*. Pia kuweza kuajiri watumishi zaidi watakaoweza kukidhi mahitaji yaliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bima ya afya, takwimu zinaonesha kwamba ni asilimia nane tu ya Watanzania ambao wako kwenye mfumo wa bima ya afya, ni dhahiri mnafahamu ni mzigo kiasi gani wa gharama uliyopo kwa wananchi juu ya huduma hii ya afya. Napenda kuishauri Serikali iweze kupunguza tozo zisizokuwa za msingi ili hata *private sectors* waweze kutoa huduma hii ya afya kwa gharama zilizo nafuu ili wananchi waweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa tiba na dawa; Serikali imekuja na mfumo ambao uko *centralized*, ambapo dawa zote zinasambazwa na *Medical Stores Departments*, ni dhahiri kwamba usambazwaji wa dawa kikamilifu umeshindikana, maeneo yote yanashindikana kufikiwa...(*Makofii*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda dakika tano na jirani yako Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba dakika tano.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijachangia ninaunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani, nafikiri ripoti yetu iko sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoendelea nataka nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, nafahamu

amefanya kazi kwenye *NGO'S*, hiyo peke yake inamsaidia kum-*shape* na kumfanya akafanya kazi vizuri ikaweza kumsaidia kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia na Wabunge wenzangu wengi wamezungumzia matatizo ya mimba za utotoni. Tumepiga kelele tukijua kwamba mimba za utotoni janga la Taifa hili, kila Bunge linalopita tunazungumzia habari hii. Ndugu yetu amepeleka kesi Mahakamani ameshinda lakini Serikali imekata rufaa. Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kuweka alama katika Wizara yako tusikubali sisi kama wanawake, kwa namna yoyote, iwe ya dini, iwe ya mila, itakayopelekea watoto wakapata shida katika umri mdogo na kupewa mimba. Ninaomba tupambane na tukubaliane kabisa, hatutakubali watoto wetu wakirolewa, sasa hivi inafika mpaka miaka tisa watoto wameingizwa kwenye ndoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza pia kwa kuanzisha kanzidata katika Wizara yako kwa upande wa mambo ya kijinsia, nafikiri hilo ni suala la kukupongeza. Bado kuna shida, tunapofanya udahili, kwenye hotuba yako ukurasa wa 81 umeelezea jinsi tutakavyofanya udahili wa wanafunzi katika Vyuo vya Uduktari, watoto wa kike ambao tumewashawishi wasome sayansi wanapokuwa vyuoni hawana pesa za kulipia mikopo japokuwa wanafanya vizuri darasani na tunajua kabisa tuna uhitaji mkubwa sana wa madaktari katika Taifa letu. Ukienda Chuo cha Kairuki kuna wasichana wameacha shule mwaka wa pili kwa kushindwa kulipa ada za masomo yao. Tunawezaje kusaidia wanawake hawa na Wizara hii kama ni Wizara husika ikawasaki wasichana wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kukumbusha, Wizara ikahamasisha uanzishwaji wa nyumba salama (*safe home*), hizi nyumba salama zitasaidia wasichana wadogo, wanawake ambao wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wakati wakishughulikiwa masuala yao, wapate sehemu sahihi ya kusubiri, wakati mambo yao yakishughulikiwa. Ninafikiri Wizara hii ni wakati muafaka sasa wa kuhamasisha. Kuna

wadau binafsi wamejitokeza na wameanza, nachukua nafasi hii kumpongeza huyu Dada Janeth Mawinza wa Mwananyamala, ye ye amejaribu kuwa na *safe home* kwa ajili ya wale akina mama wanaopigwa au wale wasichana ambao wanafanyiwa ukatili na baadaye wakaenda wakawahifadhi. Wizara lazima mtambue watu kama hawa, lakini ni wajibu wenu wa kuanzisha vituo kama hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la wanawake na uchumi. Hii Wizara inazungumza mambo ya wanawake na kuwatetea. Leo hii tunazungumzia Benki ya Wanawake binafsi nimefanya kazi na Benki ya Wanawake. Mwaka jana Mheshimiwa Ummy ulimwambia Meneja atoe maelezo jinsi gani anafanya kazi, sasa sikujua kama ni siasa au alikupa maelezo na wananchi haujatupa mrejesho ulifikia wapi. Benki hii ina-charge kama benki za kawaida. Inatoa riba kubwa kama benki za kawaida, jina lake ni tofauti na matumizi ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Mbeya benki hii ina mawakala, lakini Mikoa kama Mbeya, Mwanza, Mikoa mikubwa lazima ingekuwa na matawi makubwa na kuweza kusaidia wanawake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamezungumza vijijini ambako kuna asilimia kubwa ya wanawake benki hii haijafika, tutaendelea kufanya siasa au tutaendelea kusaidia wanawake.

Ninaomba Mheshimiwa Ummy pamoja na Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake fanyeni hima...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuunga mkono hoja ya hotuba ya Kambi ya Upinzani. Ninaamini yapo mazuri mengi ambayo Serikali ikiamua kuyafuatilia na kuyatekeleza tunaweza tukafikia lengo la Tanzania yenye Watanzania wenyе afya bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuzungumzia vifaa tiba. Kumekuwa na tatizo kubwa sana, Dada yangu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu unafahamu, wewe ni wa Mkoa wa Tanga, unafahamu hali ya Hospitali ya Bombo, unafahamu kwamba kuna changamoto kubwa sana ya vifaa, kuna changamoto kubwa sana ya mashine za *x-ray*, kuna changamoto kubwa sana ya vifaa. Lakini pia mmeweka duka la *MSD* pale, lakini mara nydingi na lenyewe pia linakosa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pana duka la *MSD* ambalo mmeliweka pale lakini inafikia hatua mgonjwa anatibiwa Bombo anaambiwa atoke akanunue dawa nje ya Bombo, kwa hiyo niwaombe sana na pia tumesikia tunaomba Waziri utakapokuja kuhitimisha utuambie, tumesikia jamii ya Mabohora wametoa msaada wa *CT Scan*, we are not sure utakuja kutuaminisha, lakini inasemekana kwamba hakuna eneo la kufunga zile mashine. Kwa hiyo, mashine zimetolewa zimewekwa pending, wananchi wanahitaji huduma hakuna pa kuweka mashine. Tunakuomba Waziri utakapokuja hapa utuambie kama kweli hakuna eneo, ni lini na mkakati gani mmepanga kwa ajili ya kujenga jengo kwa ajili ya kufunga hizo mashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni bima ya afya. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa watumiaji wa bima ya afya, pamoja na kuwa bado idadi ya watumiaji ni ndogo, ni asilimia nane tu ya Watanzania. Bima ya afya ukichukulia Wilaya ya Muheza wananchi wanachangia shilingi 10,000 ambapo wanatumia kwenye zahanati na kwenye Hospitali ya Wilaya, lakini katika ile bima ya afya tunaomba Serikali kupitia Wizara iandae utaratibu wa kuwa na maduka katika kila Hospitali ya Wilaya ambayo yatasaidia wale

ambao wanakosa dawa kwenye hospitali kwenda kupata dawa kwenye maduka ambayo yanaweza kupokea bima. Kwa sababu ukikosa dawa kwenye hospitali kwa kutumia bima hakuna namna unaweza kupata dawa nje ya pale na wananchi wanapotumia bima wanaamini hakuna namna wanaweza kutumia hela zaidi ya kupata ile huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna magonjwa ambayo siyo ambukizi yanazidi kuongezeka kwenye nchi yetu kama kisukari, *pressure*, magonjwa ya wanawake yanayoambatana na uzazi, shingo ya kizazi na mambo mengine. Ninaomba Wizara ije ituambie ina mkakati gani wa dhati kwa ajili ya kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee hapa kuhusu watoto wa kike, masuala yanayoambatana na uzazi. Kumekuwa na hilo tatizo kubwa tunaita *fibroid* kama sikosei, imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wanawake, kwa watoto wa kike kuanzia miaka 18 mpaka 25 wengi wanapata hilo tatizo, inavyosemekana kwenye jamii yetu kwa sababu hakuna elimu ya kujua hasa chanzo cha hilo tatizo, wengine wanasema ukiwa na hilo tatizo wewe ulikuwa unajihusisha na ngono na watu wengi, wengine wanasema wewe ulitoa mimba sana kwenye usichana wako. Kwa hiyo, hata wale wanaougua huu ugonjwa wanajificha kwa kuogopa jamii inavyochukulia huo ugonjwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuititia Wizara mtoe elimu kwa Watanzania wajue kwamba ugonjwa huu sababu zake ni hizi ili yule anayeugua ule ugonjwa awe huru kutoa na kusema kwamba mimi naugua hiki. Wengine tunaogopa, wale wasichana ambao hawajaolewa wanaogopa kusema hilo kwa sababu inaweza ikapelekeea kukosa watoto kwenye ndoa, kwa hiyo anakaa kimya, anaolewa, anaendelea na matatizo yake. Ninaomba Wizara itoe elimu katika haya masuala, pia watoe elimu ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wananchi, wafanyakazi wa Serikali, mashirika binafsi wanakuwa na mazingira magumu ya kufanya mazoezi, pia wanakuwa na

mazingira magumu ya kuwa na *diet* nzuri. Niombe kupitia Wizara yako, tengenezeni vipeperushi, tengenezeni utaratibu wowote ambao utasaidia kutoa elimu kwa wafanyakazi hasa wa Serikali, katika masuala ya mazoezi na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu afya ukila vizuri, ukifanya mazoezi magonjwa mengi yatakuwa mbali na wewe. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara itumie fursa hiyo, itoe elimu kwa wananchi, itoe elimu kwa viongozi, tuwe na tabia ya kufanya mazoezi, tuwe na tabia ya kujali afya katika chakula. Itasaidia kupunguza gharama nydingi ambazo tunazitumia...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ummy kwa kuwa na Wizara ambayo ni ya muhimu sana kwa maisha yetu na pia kwa afya zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee katika ule ukurasa wa 16, ibara ya 43 katika hotuba yake, hapa anazungumzia uzazi wa mpango. Ukitungumzia uzazi wa mpango watu wanakimbilia labda kufikiria ni vidonge, ni njiti, ni sindano, sio lazima, kuna uzazi wa mpango wa kuhesabu. Naomba watu waandaliwe katika kuhesabu namna ya kutenganisha watoto miaka mitatu, mitatu ili wawe na watoto ambao wana afya bora toka utotoni wawe watu wazima ambao wana afya bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu kasi ya kuongezeka Watanzania ni kubwa, ni kubwa zaidi ya maendeleo yetu. Tunapozungumzia watu na

maendeleo watu ndio wanaotawala na kuendeleza maendeleo. Unakuta kwamba idadi ile inaongezeka kwa kasi kuliko maendeleo yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo sahihi, ninaomba Wizara hii sasa iangalie jinsi gani itaelimisha watu ili tuende tukiongezeka taratibu na hapo nina maana, familia ikiwa na mtoto mmoja, wawili au sana wale waliotangulia kama sisi watatu, inatosha. Yale mambo ya familia kuwa na watoto sita, kumi yamepitwa na wakati. Najua maandiko yanasema zaeni mkaongezeke, lakini tukiongezeka holela pia tunakufa kiholela, ifikapo mwaka 2025 ongezeko hili litakuwa limepitwa kabisa na maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde, nimuombe Mheshimiwa Ummy atakapopita mashulenii aende akatoe elimu na pia wale wanaohusika watoe elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda watoto na sasa hivi natarajia wajukuu, nawapenda sana wawe wengi, lakini siyo hovyo hovyo tu, nataka vitoto vyenye afya, vitoto vitakavyoweza kukidhi nchi yetu hapo tunapoenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani hao ninaotrajia waelimishwe, ni ile ofisi ya maendeleo ya jamii. Ile ofisi imekaa choka mbaya, ina wasomi wazuri wana *degree*, wana *masters*, wengine wana *postgraduate*, wengine nilikutana nao mashulenii, lakini hawana vitendea kazi kabisa. Ofisi ya maendeleo ya jamii popote ilipo labda kwingine huko miji mikubwa lakini kule kwenye miji midogo midogo hata gari lenyewe la kuwafuata ile jamii wakatoe elimu halipo. Naomba sana Mheshimiwa Ummy, imezungumzwa jana na mimi nasisitiza, ofisi hiyo ipatiwe vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taasisi zetu, likiwemo Kanisa Katoliki, lina Vyuo vya *Nursing* lakini vyuo hivyo vimekosa walimu wa kutosha na hivyo naomba atakapokuwa anazungumza Mheshimiwa atauangalie ni jinsi gani atatoa pia walimu katika Chuo cha *Nursing* kule Kibosh, chuo ni kizuri katika Hospitali ya Kibosh, ni chuo

ambacho najua nae ana ndoto ya kwenda kukiona, lakini viko vyuo vingi tu na hospitali nyingi tu ambazo hazina Madaktari wa kutosha ikiwemo Bambo kule Same na vituo vingi vya afya. Hata kile kituo cha afya ambacho alikijenga Lucy Lameck, Moshi Vijijini miaka hiyo kiko Shimbwe, kiko mbali sana hakuna hata usafiri wa kufika mjini, bado watu wanabebwa na chekecheke kuletwa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kukumbushia Hospitali ya KCMC, hospitali hii sasa inataka kusaidiana na *Ocean Road*, hospitali hii sasa inakwenda kutoa huduma Kaskazini na Mikoa yote inayozunguka katika kutibu kansa. Hili ni eneo ambalo linahitaji gharama kubwa, wadau wamechangia vya kutosha, tunaiomba Serikali iweze kuangalia eneo hilo ili tupunguze ule msongamano pale *Ocean Road* ili huduma hii ya kansa ya mionzi na nyiningeyo ya *chemotherapy* itolewe vizuri pale KCMC. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kila mmoja wetu anapojifirkiria anafirkiria afya yake...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ummy kwa uwasilishaji wa taarifa yake, iliyosheheni afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa jitihada kubwa inayofanya katika kuimarishe na kuboresha afya zetu Watanzania. Lakini niendelee kuipongeza Serikali kwa kutuunganisha Watanzania katika mfumo rasmi wa bima ya afya. Nimpongeze kwa dhati kabisa Mkeshimiwa Waziri Ummy na Naibu wake kwa jitihada kubwa sana waliyoifanya katika kampeni ya kuhamasisha mfuko huu wa bima ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwetu Lindi tunashukuru kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Waziri Ummy aliandaan utaratibu wa kampeni rasmi, japokuwa yeze hakufika lakini wawakilishi wake walifanya kazi na jitihada kubwa ilioneekana na tuliweza kuongeza idadi ya watu wanaotumia bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi kubwa zinazooneekana za kuimarisha na kuboresha afya za Watanzania, bado tuna changamoto kubwa sana. Katika upande huu wa bima ya afya inaoneekana watumiaji wa bima ya afya ni wengi lakini upatikanaji wa dawa umekuwa ni duni kabisa. Kwa hiyo, naiomba Wizara kuimarisha katika eneo hili la upatikanaji wa dawa ili wananchi waweze kupata tiba vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali yetu ya Mkoa wa Lindi tuna changamoto mbalimbali. Tuna changamoto kubwa sana ya Madaktari Bingwa, kwa sababu Hospitali ya Sokoine Mkoa wa Lindi ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, wateja wake wakubwa ni wananchi kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Lindi, hivyo tunahitaji Madaktari Bingwa katika Hospitali yetu ya Sokoine.

Mheshimiwa Waziri Ummy alituahidi kutupatia madaktari wanne, ningependa kujua madaktari hawa watakuja lini katika hospitali ya Mkoa wa Lindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Lindi ni hospitali kongwe iliyojengwa mwaka 1954, naishukuru sana Serikali kwa kuifanyia ukarabati wa kutosha na majengo yanaoneekana ni mazuri, majengo nadhifu, yanapendeza lakini bado tuna changamoto kubwa ya miundombinu ya maji taka. Ninaiomba sana Serikali kusimamia katika eneo hili ili hospitali hii iweze kuwa na miundombinu ya maji machafu katika mfumo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upatikanaji wa maji safi pale Sokoine ni mdogo kabisa, tunajua hali ya mji wa Lindi hakuna kabisa maji, wananchi wa Lindi bado tunaendelea

kupata shida, lakini bado tunaendelea kuiamini Serikali yetu na jitihada kubwa inayofanya ya kuimarisha upatikanaji wa maji katika Mji wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bado katika hospitali ya Sokoine kuna changamoto kubwa sana ya *x-ray*. *X-ray* iliyopo imeshapita muda wake wa matumizi, inashindwa kufanya kazi na wagonjwa wanashindwa kupata huduma hii ya *x-ray*. Ninamuomba kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Ummy kuitazama Lindi Sokoine ili tuweze kupata *x-ray* mpya iweze kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri Ummy, hospitali ya Wilaya ya Kilwa katika eneo la *mortuary* hakuna majokofu ya kutunza maiti pale, ninaomba kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Ummy tuitazame Wilaya ya Kilwa ili wahakikishe katika eneo lile la *mortuary* tunapatiwa majokofu ili tuweze kufanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hospitali ya Wilaya ya Liwale, tunayo *x-ray* pale katika hospitali ya Wilaya lakini mtaalam wa *ku-operate* mashine hizi za *x-ray* hakuna, Mheshimiwa Waziri Ummy tunaomba utuangalie...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuishakwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAMIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nichukue fursa hii kwanza kuwashukuru sana watumishi wa Wizara hii nikianza na Katibu Mkuu wa Wizara pia madaktari pamoja na wauguzi wote nchi nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mazingira magumu ambayo wanayo. Ninawapongeza sana kwa moyo wao na kwa kazi kubwa wanayoifanya na uzalendo wanaouchukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuhusu suala la wazee; nimesikitika sana kuona kwamba suala la wazee katika nchi hii inaonyesha kabisa ni suala ambalo siyo kipaumbele cha Taifa hili, ukijaribu kuangalia hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna mistari karibu mitano tu inayozungumzia suala la wazee na halieleweki ni namna gani Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha kwamba inatatua tatizo la wazee kukosa huduma muhimu kama za afya na huduma zingine zinazohitajika kwa wazee hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wazee ni suala muhimu sana. Humu ndani ya Bunge kuna wazee ambao sasa hivi siyo muda mrefu na wao watastaafu na watakwenda kuungana na wazee walioko mitaani. Pia na sisi vijana tunajua kabisa kwamba siyo muda mrefu tutakuwa wazee na baadae tutakwenda kuungana na wazee wengine walioko mitaani huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote ambalo halitawathamini wazee Taifa hilo ni lazima litakuwa na mapungufu makubwa na haliwezi kupata baraka za Mwenyezi Mungu. Ni lazima wazee hawa tuhakikishe kwamba tunawaheshimu na tunawatengenezea mazingira mazuri, ninaamini kabisa wazee hawa wamelitumikia Taifa hili kwa nguvu zao zote, kwa jasho na damu na mpaka sasa hivi wameishiwa nguvu zao wanahitaji msaada wa Serikali, lakini Serikali haijaweza kuonesha mpango thabiti kabisa wa namna gani wanaweza kuwahudumia wazee hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kuangalia kwenye takwimu za wazee, Serikali imetambua wazee karibuni 346,889, wazee hawa ni kati ya wazee asilimia 60 waliotambuliwa, lakini wazee waliopata vitambulisho, wanaopata matibabu na huduma zingine ni wazee 74,590 tu na wazee 272,299 bado hawajatambuliwa na hawapati huduma zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekaa inasema kwamba inataka kuwahudumia wazee, hatuhitaji huduma

za kwenye makaratasi, tunahitaji huduma ambazo wazee watakwenda kuzipata na wazee hawa waweze kupata vibali haraka iwezekanavyo ili waweze kupata huduma na waweze kunufaika na Taifa ambalo wamelipigania kwa muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na vifo vya mama na mtoto. Suala hili katika Taifa hili limeonekana ni jambo la kawaida tu. Tunakuja humu katika Bunge tunazungumza, bajeti zinatengwa na bajeti zinazotengwa ni kidogo sana, lakini fedha hizi haziendi kwa wakati na fedha hazipatikani kabisa. Akina mama wanaendelea kupoteza maisha, watoto wanaendelea kupoteza maisha, Taifa limetulia wanaona kama ni jambo la kawaida wanazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hili Taifa hili takwimu zinaonyesha kati ya vizazi 100,000 vifo ni 556 na hivi vifo ni kati ya akina mama wanaokwenda kwenye vituo vya afya na hospitali asilimia 64, asilimia 36 ambao hawajagusa kabisa katika vituo vya afya na hospitali hawa hawatambuliki kabisa ni wangapi wanaopoteza maisha. Kwa hiyo, tuna janga kubwa katika suala hili, tunaona Serikali haijaweka mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anakuja kujaribu kutoa ufanuzi wa mwisho atueleze Serikali ina mkakati gani, hatuoni vipaumbele muhimu ambavyo Seriakli inavichukua. Leo tunanunua ndege lakini watu wanapoteza maisha, Serikali haiangalii namna gani inaweza kuwahudumia wananchi hawa, Serikali inawakumbuka Watanzania hawa wakati wa uchaguzi, lakini baada ya kupata madaraka inawasahau na wananchi wanaendelea kufa, hakuna mkakati wowote ambao unaonekana kwamba ni wa kuwaokoa watoto pamoja na akina mama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kujua, kwa nini Serikali hii haitaki kuona kwamba ni muhimu hospitali zetu zote za mikoa zikapata *CT Scan*, nataka hospitali zote za mikoa ziweze kupatiwa *CT Scan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna *MRI*, hospitali zetu zote za Mikoa zinatakiwa kupata *MRI* pamoja na *CT Scan*, kinachoonekana sasa hivi ni kwamba huduma hizi zinapatikana baadhi ya maeneo tu na zimekuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo mgonjwa anakwenda kupima mgongo, anakwenda kupima kichwa kwenye *MRI* atatumia zaidi yashilingi 700,000 na kwenye *CT Scan* anatumia zaidi ya shilingi 200,000 mpaka 150,000 gharama ni kubwa, Serikali haijaonesha thabiti kuweka ruzuku katika matibabu haya, inaonyesha kabisa kwamba Serikali inafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itueleze ni namna gani inaweza ikahakikisha kwamba inapunguza gharama ya vipimo hivi ili Watanzania waweze kupata vipimo vizuri na waweze kutibiwa sawa sawa. Kwa hiyo, jambo hili tunataka wahakikishe kwamba linafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiri, pia kuna suala la kuhakikisha kwamba hospitali zote za Wilaya na hospitali zote za kanda ambazo zingeweza kujengwa katika nchi hii, ukichukua gharama za ndege moja ya *Bombadier* inaweza ikajenga hospitali ambazo zina hadhi ya *Ocean Road* karibu kanda zote katika nchi hii, leo hiki siyo kipaumbele cha Serikali, wananchi wanakufa kwa *cancer*, wananchi wanakufa kwa magonjwa haya na tunesikia takwimu hapa inaonesha kwamba miaka inayokuja kati ya miaka 2020 kutakuwa na vifo vingi sana vya watu ambao wanaweza wakapoteza maisha kwa ajili ya *cancer*.

Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani wanaweza wakapunguza matumizi kwenye maeneo ambayo hayastahili na wakapeleka kuokoa maisha na roho za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunajaribu kuendelea kushauri kuhakikisha kwamba mambo haya yanafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuokoa vifo vya akina mama na watoto, tumeangalia ni namna gani Serikali ilivyojipanga. Hiki ambacho kimeoneshwa hapa kwamba kinaweza kikasababisha upungufu wa vifo vya akina mama na watoto, tumeona siyo sababu sahihi. Sababu sahihi zilizopo ziko takwimu mbalimbali ambazo zinaonesha, ukiangalia katika nchi hii, hospitali za Wilaya zilihitajika 139, leo kuna hospitali 119, kuna upungufu wa hospitali 20 katika Wilaya zetu nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vituo vya afya vilihitajika 4,420 leo kuna vituo 507, kuna upungufu wa vituo 3,913. Kwa hiyo, vituo karibuni 3,913 havipo mpaka sasa hivi katika nchi hii. Ukiangalia zahanati zilizokuwa zinahitajika ni 13,545 leo kuna zahanati 4,470, kuna upungufu wa zahanati 8,075.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupunguza vifo vya mama na mtoto kama hatutasogea huduma hizi kwa wananchi katika vijiji vyote nchi nzima na Wilaya zote tuweze kujenga hospitali za Wilaya ziweze kukamilika. Hivyo, tunafikiri ni vizuri Serikali ikajaribu kuangalia vipaumbele hivi muhimu kwa ajili ya kupunguza vifo vya akina mama na watoto katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tunajiuliza sana kama Watanzania, sijui kama Tanzania imekuwa ninchi ya majoribio ya dawa za malaria. Kila zikifika ndani ya mwaka mmoja tunapata matangazo kwamba dawa hii haifai kwa matumizi ya binadamu inatakiwa iachwe na inaletwa dawa nyingine. Sasa tunataka wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuzungumza hapa atueleze ni kwanini Tanzania imekuwa kama ni nchi ya majoribio ya dawa ya malaria, atueleze wakati wanatangaza kwamba dawa hii haihitajiki na haifai kwa matumizi ya binadamu ni Watanzania wangapi wanakuwa wameathirika na nini ambacho kinaendelea ili kuokoa athari ambazo zimewapata Watanzania hawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na dawa moja ambayo ilikuwa inatumika hapo nyuma, dawa ya

*chloroquine*, dawa hii imefanya kazi kwa kipindi kirefu sana, ilikuwa inaokoa sana vifo vya akina mama kwa sababu pia walikuwa wanatoa kama chanjo kuhakikisha kwamba akina mama hawapati malaria kama kinga, leo dawa ile imefutika na hatuelewi ni utafiti gani ambao ulifanyika, Watanzania wanataka kujua utafiti uliosababisha dawa ya *chloroquine* ikaonekana kwamba haifai. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna jambo lingine la upungufu wa madaktari katika nchi hii. Imeonesha kwamba katika nchi hii kuna upungufu mkubwa sana wa madaktari, nataka kukuhakikishia kwamba nchi hii imesomesha madaktari wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika nchi za Kusini na Kati mwa Afrika, wanaofanya kazi karibuni asilimia 20 na 30 ni Watanzania wanafanya kazi katika hospitali zile. Ukienda katika nchi za Botswana, Congo, Mozambique na maeneo mengine, wanofanya kazi za kuwatibu wale watu ni Watanzania na hawa Watanzania wanaofanya kazi kule wametumia fedha kubwa kabisa ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweza kumfundisha daktari mmoja haipungui karibu shilingi milioni 10. Madaktari hawa wametumia *resources* za nchi, lakini leo wanafanya kazi katika nchi zile, juzi tumesikia Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara wameamua kuwachukua madaktari wetu kuwapeleka Kenya, jambo ambalo limekuwa ni jambo la kusikitisha na kushangaza wakati tuna upungufu mkubwa wa madaktari nchini. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida Nyimbo atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Mussa Sima ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake

Waziri Dkt. Kigwangalla, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya ndani ya Wizara hii. Pia nimpongeze Rais wangu aliyetokana na Chama cha Mapinduzi Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya katika Taifa hili la Tanzania. Wananchi wa Tanzania tuna furaha kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na kuwatendea haki Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ni kubwa, Dada yangu Ummy Wizara ni kubwa, kazi na majukumu uliyokuwa nayo ni makubwa, lakini haina budi ukiwa kama mwanamke mwenzangu nikupongeze kwa ufanisi mkubwa wa kazi na uwezo uliokuwa nao wa kazi, kuweza kumudu Wizara hii kubwa na Wizara ambayo imebeba watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumza watu wote, majigambo ya Wabunge, majigambo ya Makatibu Wakuu, majigambo ya waendesha boda boda yote yanategemea afya zao na umezibeba wewe dada yetu Ummy pamoja na kaka Kigwangalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache pia kuzungumza suala zima la afya kwa watoto. Mheshimiwa Waziri umelizungumza katika kitabu chako, umelizungumza na kuliongea kwa kina suala zima la afya ya watoto katika ukurasa wa tano, umelizungumza na umelitendea haki, ila dada yangu nikuombe ukiwa kama mwanamke kumbuka unapokwenda *labour* unapofikwa na uchungu. Unayoyafanya yote ni mazuri lakini wajibu wetu kukukumbusha kuna baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatupaswi kulaumu, tunapaswa kukuambia ili ukumbuke na kuangalia maeneo mengine. Unapokwenda *labour* mwanamke unaujua uchungu na dada yangu Ummy una watoto uchungu unauelewa. Watoto wamefikwa na janga kubwa linalowasumbua sasa la kubakwa, hatuna budi kama mwanamke angalia kwa jinsi ya pekee tatizo hili tunalitatuaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalizungumza Dada Ummy huwezi kulitatua peke yako, lazima kuna baadhi ya watu mshirikiane au Wizara mshirikiane. Lazima ushirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani, lazima ushirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria. Dada Ummy ni nafasi yako kama mwanamke kaa nazo Wizara hizi muone tatizo hili mnalitatuaje. Leo kilio cha kila mwanamke ndani ya Nchi hii, ubakaji wa watoto na unyanyasaji wa watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia nyingi za unyanyasaji wa watoto, lakini kwa sasa yenye sura ya pekee ndani ya Tanzania ni suala la ubakaji. Nimeambiwa jana Dada yangu Faida amesimama mpaka amefikia kulia, suala la ubakaji ni suala kubwa, Dada Ummy unafanya kazi kubwa lakini kaa na Wizara zingine hatalitatua peke yako na kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalizungumza hivi kwa sababu, Wizara hizi imefika wakati unapokwenda Mahakamani unaambiwa limekwama Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana polisi, lakini polisi ukifika ukifuatilia unaambiwa limekwama hatuna maelezo ya kutosha ndani ya Wizara ya Afya. Tuliione suala hili linakwendaje na suala hili Dada Ummy linahitaji pia elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wenzetu wengine hawafahamu kwamba mtoto unapompeleka ukamtia maji, tayari baadhi ya uthibitisho unaufuta kabisa. Inapaswa lazima kama mwanamke usimame na kutoa elimu ya kutosha ili tuone tatizo hili kama Serikali na kama viongozi tukiwa tuna nia moja na lengo moja ya kulitatua tatizo hili limalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 26, ulizungumza kwa makini na kwa kuitolea maelezo ya kutosha hospitali ya Muhimbili. Ndani ya mwezi mmoja uliokwisha nilikuwepo Muhimbili kwa muda wa siku tatu, ilinibidi nikae pale. Panapostahili sifa binadamu apewe sifa. Mmefanya kazi kubwa lakini naamini kazi hii anayewatia nguvu na kukuwezesheni ni Mheshimiwa Rais. Inapofika wakati kama

viongozi tusiwe wingi wa kulaumu tukakosa kushukuru. Unapoizungumzia hospitali ya Muhimbili uwe umekwenda umefika. Kuna tofauti kubwa ya nyuma tulipotoka na sasa hivi, lakini kwa sababu kuna baadhi ya watu nilipoenda, nilifanya kazi nikiwaona nisiache kuwataja kwa majina, lazima niwasifie. Kiongozi unapopata muda, posho tunayowalipa haitoshi kwa madaktari lakini basi... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja, ingawa nilmeambiwa nina dakika kumi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Sima ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dakika ni chache kwanza kabisa mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, hongera sana Dada yangu Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri Kigwangalla kwa kazi nzuri mnayoifanya, nina uhakika kabisa tunapoelekea vifo vya wanawake na watoto, lakini pia matatizo pamoja na ukatili wa kijinsia utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dakika ni tano, naomba nijikite katika suala moja ambalo limezungumzwa hapo jana kwa kirefu na aliweza kulizungumza Mheshimiwa Faida, na mimi pia naomba nijikite katika suala hilo. Suala la ukatili kwa watoto ni kubwa, kwa kiasi kikubwa sana na ukatili huu dhidi ya watoto katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia imeelezwa katika ukurasa wa 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite na kwa kutoa mifano katika suala hili. Utafiti uliofanywa na Jumuia ya Maimamu kule Zanzibar unaonyesha kwa kiasi kikubwa ukatili dhidi ya watoto, watoto wamekuwa wakilawitiwa, watoto wamekuwa wakinajisiwa kwa kiasi kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa mwaka 2014/2015 umebainisha kuwa suala hili ni janga. Watoto wameharibiwa kwa kiasi kikubwa, watoto wa miaka kuanzia minne na kuendelea. Kwa mujibu wa utafiti huu uliofanywa, unaonesha kwamba nchi za Magharibi kwa kiasi kikubwa zimetumia mbinu mbalimbali kuhakikisha kwamba nchi za Afrika zinaidhinisha mapenzi ya jinsia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya mila, tamaduni na desturi zetu imekuwa ni vigumu. Kwa maana hiyo, ipo nguvu kutoka nje ambayo kwa mujibu wa utafiti huu inawatumia baadhi ya walimu wa madrasa kule Zanzibar, lakini pia walimu wa shule za msingi inawatumia. Walimu hawa wanapewa pesa na kuhakikisha kwamba wanawalawiti watoto ili kuandaa kizazi ambacho itakuwa ni rahisi baadaye kuwa na kizazi cha watoto amba wanashiriki mapenzi ya jinsia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti huu nipo tayari kuuthibitishia Bunge hili na kukutanisha na wale amba tayari wamekwisha fanya utafiti huu na kubaini ni kwa jinsi gani watoto wetu wameharibiwa na watoto wengine wameshakuwa wazoefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti huu Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alishakabidhiwa ripoti, pia katika Siku ya Wanawake Duniani pia walizungumzia hawa maimamu kuonesha ni kwa jinsi gani wazazi, walezi, lakini pia walimu wa madrasa ambao ndio tunawategemea kuwalea na kuwakuza watoto wetu katika maadili ndio wanaoshiriki, lakini pia walimu wa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu angalizo kwamba sisi kama wazazi, hata wageni wanaokuja nyumbani kwetu tusijenge tamaduni za kuhakikisha kwamba wanalala na watoto wetu kwa sababu ndiyo hao wanaowaharibu watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia kwa undani zaidi ukazungumza na watu ambao wanashiriki mapenzi ya jinsia moja, atakuambia mjomba ndiye aliyeanzisha tatizo hilo, mwininge atakuambia ni ndugu wa baba ndiye aliyeanzisha tatizo hilo. Kwa hiyo, tujenge tamaduni watoto wetu tuisiweke karibu na ndugu wanaofika katika familia zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ni kubwa na ni janga, ni janga la kitaifa. Tunaandaa kizazi ambacho baadaye kitakuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Utaliendeleza baadae hilo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Sannda.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema, aliyetuwezesha leo tupo hapa, lakini nichukue fursa hii pia kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya, niwapongeze pia nimpongeze Waziri Mheshimiwa Ummy na Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache ya kuzungumza, jambo la kwanza ndani ya Singida Mjini leo tunajenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Mheshimiwa Ummy

alifika pale na alitoa maagizo na nimshukuru sana. Naomba nisisitize, tunayo changamoto kubwa ya Hospitali ya Wilaya ya Singida Mjini, eneo kubwa ambalo tunalitegemea ni ile hospitali ya Mkoa tuliyonayo iweze kuhamia iende Hospitali ya Rufaa ambayo ipo Mandewa na ile hospitali ya Mkoa iwe hospitali ya Wilaya. Ninamuomba sana Mheshimiwa Ummy wakati ana *wind up* atusaidie kutoa tamko hili ili tuweze kuharakisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mandewa na ile hospitali ya Mkoa iliyopo pale iwe Hospitali ya Wilaya. Tutakuwa tumetatuwa tatizo kubwa sana Singida Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nizungumzie zoezi la damu salama. Niipongeze Serikali inatumia gharama kubwa leo na katika mpango huu wa damu salama imetusaidia sana. Mkoa wa Singida, tangu Juni , 2016 mpaka Februari , 2017 wamekusanya *unit* takribani 2,300, bahati mbaya sana Singida Mjini zilizusanya *unit* 12 tu, changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira mengine inaonesha kabisa Singida Mjini tunawanyonya wenzetu wa Halmashauri zingine kwa ajili ya kutumia zile damu salama. Naiomba Serikali ifanye tathmini na iweze kusimamia zoezi hili kikamilifu kwa kila Halmashauri ili tujue tatizo lipo wapi. Kwa sababu kama unakusanya *unit* 12 maana yake watu waliochangia damu ni watu 12 tu. inawezekana mwamko ni mdogo au yawezekana watendaji wetu Serikalini wanashindwa kufanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifanyika tathmini itatusaidi kuweza kupata damu salama kwa wingi, zoezi hili litatusaidia sana. Niombe sana Serikali iweze kulisimamia jambo hili kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuishukuru Serikali, imetupatia fedha za dawa na mpaka sasa ni takribani milioni 200 tumeypata Singida Mjini fedha za dawa, nimpongeze sana Dada yangu Ummy. Karibu asilimia 93 ya fedha za dawa zilizokuja Singida Mjini, asilimia 93 siyo jambo dogo Serikali inafanya kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ninayoipata mwananchi anapokwenda kupata huduma na akaambwa dawa hamna, nami nasi mama kwenye majukwaa kuwaambia kwamba Serikali imeleta fedha za dawa asilimia 93, ninakosa ni mazingira gani ninaweza kuwaeleza, matokeo yake itanilazimu sasa na mimi nigeuke kuwa muuguzi au kuwa daktari au kuwa mhasibu ili niweze kusimamia fedha hizi namna zinavyoweza kutumika. Kwa hiyo, niiombe Serikali, tunapotoa fedha na mkatuachia tu tuendelee kuratibu jambo hili sisi wawakilishi wa wananchi mnatupa mtihani mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaona kwenye vitabu tumepata fedha na kweli fedha zimefika, lakini hakuna dawa. Mwananchi anapokwenda akakosa dawa huwezi kueleza, utaeleza kitu gani? Tuna kila sababu sasa ya kusaidiana ni namna gani tufanye kuweza kusimamia utekelezaji wa hizi fedha zinazoletwa. Kama dawa zimenunuliwa ni lazima tujue dawa zipo na wananchi wetu wasipate matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali Watumishi wetu wanapata wakati mgumu sana, leo tumefika mahali *call allowance* hamna, *extra duty* hamna, kazi ni kubwa. Daktari anamaliza shughuli zake, *nurse* anamaliza shughuli zake lakini ataitwa kwa sababu ni wito na atakuja, atakapokuja kufanya ile kazi halipwi, wanayo madeni makubwa sana watumishi wetu.

Ninaiomba sana Serikali iweze kulisimamia jambo hili, hatuna tatizo hilo, tuna tatizo tu la Menejimenti linalosababisha watumishi wasiweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaua morali ya watumishi. Sisi tunapokaa nao, unapozungumza nao, unafanya mikutano unaona kuna mahali wanajitoa wao kufanya kazi lakini sisi tumeshindwa kuweza kutimiza kile ambacho walistahili kupewa ni haki yao. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Baada ya Mheshimiwa Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa, kwanza kabisa niipongeze Waziri, Wizara na timu yake nzima kwa uwasilishaji mzuri. Napenda kusema machache kwa maana ya kuboresha na kurekebisha pale ambapo panahitaji marekebisco.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka niongelee kuhusiana na hospitali yetu ya Kondoa ambayo kabla ya kugawanywa Halmashauri kidogo tulikuwa tunakwenda vizuri, lakini sasa hivi kutokana na utaratibu bajeti yake imebaki kuwa kutokana na idadi ya watu wanaotokana na Halmashauri ya Mji Kondoa ni kidogo sana. Inapigiwa bajeti kwa ajili ya watu 68,000 wakati inahudumia watu 250,000 wa Kondoa Vijijiini, inahudumia watu wa Chemba karibu 250,000, kwa hiyo jumla inahudumia watu karibu 600,000 ingawa inatengewa bajeti kwa ajili ya watu 68,000. Kwa hiyo uwezekano wa kutoa huduma kwa ufanisi haupo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana jambo hili pamoja na kwamba tunaangalia kigezo cha *population*, hebu tuende mbele zaidi, hospitali hii inahudumia na akina nani wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, babaraba ya kutoka Dodoma - Kondoa kwenda Babati inaeelekea mwisho kumalizika kwa kiwango cha lami. Sasa hivi tena ndiyo tatizo linaongezeka kutakuwa na wasafiri pale watakaohitaji huduma, wako hata jirani zetu wa Wilaya zingine za pembezoni nao wanapata huduma pale. Ninakuomba suala hili la kuangalia kigezo hiki cha idadi ya watu peke yake kwa hospitali kama ya Kondoa najua na wengine wapo wanakumbana na matatizo kama haya, hebu tuliangalie tuweze kutoa huduma hii vizuri kuliko ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa hapo hapo niongelee kidogo kuhusiana na upungufu wa Miundombinu na vifaa muhimu. Kwanza kabisa ni *ambulance*, pongezi kwa kazi ambayo tayari imeshafanywa kwa Halmashauri nyingine kupata *ambulance*, ninakuomba Shemeji yangu Mheshimiwa Waziri Dada Ummy kwamba itakapofika awamu ya pili basi na mimi niwepo katika Halmashauri ambazo zitafuata awamu ya pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunachangamoto kubwa sana ya *mortuary*, *mortuary* ina uwezo wa kuchukua miili minne tu, kwa hospitali kubwa namna ile miili minne ni kitu kidogo sana. Tunahitaji kufanya utaratibu kuongeza *facility* hii. Hata maabara nayo ni changamoto. Upande wa madaktari pia tuna upungufu, ninakuomba katika utaratibu wako basi na kwenyewe utufanyie mpango.

Pia niongelee suala la dawa, tunazungumza hapa bajeti ipo vizuri fedha zimepelekwa, lakini Mheshimiwa Waziri hoja isiishie tu kwenye fedha zimepelekwa. Fedha zipo lakini ukitafuta mrejesho kwa wananchi huku dawa hazipatikani. Wananchi siyo kwamba wanaangalia fedha zimeingia au wanataka maelezo, wanataka dawa ziwepo, kuna tatizo pale. Kuna tatizo ambalo nahisi kwenye utaratibu wa manunuzi lakini pia na madaktari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri vitu viwili, namba moja tupate wataalamu *ma-expert* wa manunuzi ili *supply chain* ya madawa iweze kwenda vizuri isije ikafika wakati dawa zinakatika hela ziko kwenye hospitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili labda tutengeneze muundo wa *ki-digital* ambapo madaktari watakuwa wanajua *stock* gani ipo ndani kiasi kwamba hata anapo-*prescribe* dawa zile anajua dawa zilizopo, siyo daktari anatoa dawa kumbe kwenye *stock* hakuna. Sasa tutengeneze mfumo ambapo kila zinapotumika, zinapopungua anajua kiasi cha dawa zilizopo na ni dawa za aina gani. Hiyo itatusaidia sana kupunguza hii changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule *site* watu hawaangalii hela, wanaangalia dawa zipatikane. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili na mtuambie tu sasa hivi kuna *mechanism* gani ya kwenu kuhakikisha kweli dawa zinafika na mnapata mrejesho na mfumo gani unawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nataka kuzungumza kidogo kuhusiana na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sannda. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Mheshimiwa Waziri mwaka jana nilieleza hapa kwenye bajeti zipo zahanati tano jimboni kwangu zimejengwa, zimekamilika ila hazijafunguliwa kwa sababu hakuna wahudumu, lile tatizo limeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira mengine nimshukuru sana Waziri wa Ardhi, jana amefanya kazi kubwa, tena inahusu na Wizara yako Mheshimiwa Ummy.

Mheshimiwa Lukuvi namshukuru jana ameweza kumnyang'anya eneo mtu mmoja ambaye anapenda sana kuibaiba sana maeneo ya watu. Aliwahi kuiba eneo akamkabidhi Mkuu wa Mkoa Makonda pale Dar es Salaam, Mheshimiwa Lukuvi akamnyang'anya, jana tena kaenda kumnyang'anya hekari 4000, ambazo alitaka kuwaibia wananchi wa Jimbo la Mchinga katika kijiji cha Ruvu na kijiji cha Mchinga, kwa hiyo namshukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia aliyoitumia alijenga zahanati mbili, moja Mchinga na moja Ruvu. Kila alipokuwa anaambiwa azikabidhi akawa hataki kuzikabidhi,

akamtumia Afisa Mipango Miji wakaenda wakaghushi hati ya kumiliki ardhi, alipoona Mheshimiwa Lukuvi anakomaa naye wakaamua kusita, kwa hiyo zile zahanati mbili ambazo jana lile eneo amenyang' anywa, Mheshimiwa Ummy nafikiri sasa hivi muagize Mkuu wa Mkoo tuzichukue sisi. Tumemnyang'anya eneo lakini zile zahanati ziwe kwetu, kama hataki kabisa basi akavunje haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la upatikanaji wa dawa. Mheshimiwa Waziri siyo kila taarifa wanayokuletea watendaji wako uiandike na ui-copy kama ilivyo. Nimekisoma hiki kitabu, nimejiridhisha kwamba hii taarifa ulioisoma jana haukuipitia labda kabla haujaja Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uksoma hali ya upatikanaji wa dawa Mkoo wa Lindi ukurasa 126, wameeleza kwamba Mkoo wa Lindi umepata dawa kwa asilimia 70. Lindi ina Halmashauri sita, ukienda kwenye upatikanaji wa dawa kwa Halmashauri, Halmashauri ya Kilwa asilimia 77, *Lindi DC* asilimia 80, *Lindi MC* asilimia 84, Liwale asilimia 88, Nachingwea asilimia 81, Ruangwa asilimia 86, ukitafuta wastani ni wastani wa asilimia karibu 83. Lakini huku kwenye Mkoo umetuandikia kwamba tumepata dawa kwa asilimia 70, ukitazama kwenye mgao wa Halmashauri asilimia wastani wake ni asilimia 83. Mlifanya mahesabu? Ndiyo maana nikasema wakati umeletewa hii taarifa haukuipitia, kwa hiyo, najua kwamba asilimia ya dawa tuliyopata Mkoo wa Lindi ni asilimia ndogo kuliko Mikoa yote. Hii inasikitisha, mmetusahau kwenye walimu, mmetusahau kwenye madaktari, mnaendelea tena kutusahau kwenye dawa. Ninaomba sana hali ya upatikanaji wa dawa katika Mkoo wetu wa Lindi siyo mzuri, naomba muongeze hiyo kasi ya kutuletea dawa katika Mkoo wetu wa Lindi. (*Makofii*)

Suala lingine ni suala la vifo vya akina mama hususan wanaokwenda kujifungua. Mheshimiwa Waziri wewe ni mwanaamke, nilifikiri kwamba katika jambo ambalo utalipigania kwa dhati kabisa ya moyo wako, uache *legacy*,

kila siku kina mama 30 nchi hii wanafariki wakiwa wanajifungua. Umeikuta hali hiyo hivi sasa mwaka wa pili hali ipo hivyo hivyo, utaondoka miaka mitano, hali ikiwa hivyo utaacha historia gani! Akina mama watakukumbuka kwa lipi? Tunaomba sana na nimewasikia Wabunge hapa wanakusifia sana na mimi pia mwaka jana nilikusifia, lakini nimegundua haya maneno mazuri ni kwa ajili ya asili yako tu ya kutoka Tanga, watu wa Tanga mnajua vizuri Kiswahili, mnaongea vizuri, tunahitaji ufanisi na utendaji, tunataka tuone uache *legacy* kwenye hii Wizara. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umesemaje?

**MHE.HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa nimesema Tanga tu, maneno yale mazuri kwa sababu ya Tanga. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tunahitaji matendo, ninataka mtu ambaye ana-*perform* na ndiyo maana nilisema mara ya kwanza, nimemponegeza sana Mheshimiwa Lukuvi tumempelekea tatizo la ardh, mtu anataka kunyang'anya watu ekari 4000 katika mazingira ya wizi tu, watu wa Serikali mpo, huyu *Azimio Housing Estate* kwa nini hii kampuni na yenye msiifungie kabisa? Kila siku anafikiria kuiba maeneo tu ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tena kumshauri Mheshimiwa Waziri, hatuhitaji maneno mengi kwenye vitabu hivi, tunahitaji *action*, tunahitaji utekelezaji. Bajeti yako inapungua umechukua *mechanism* gani kuishauri Serikali ikuongezee bajeti, usiwe unakubali tu unaletewa bajeti ndogo na wewe unakubali. Hii shilingi trilioni 1.1 haikutoshi, matatizo ya afya ya nchi hii ni makubwa kuliko kiwango cha pesa. Inawezekana hata hii shilingi trilioni moja usiipate yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu suala la magari ya wagonjwa niliona wakati fulani Mikoa ile ya Mwanza wapi kule, watu wanapewa magari ya kubeba wagonjwa, kwetu huku mbona hatuletewi? Mimi katika vituo vyangu vitatu, Kitomanga, Lutamba na pale Milola magari

yake yote yamechakaa na sasa hivi hayafanyi kazi, yamekufanya kabisa yote, lakini wenzetu tumeona mnawapatia magari, je mna mpango gani na sisi kutupatia magari ya wagonjwa? Hii *distribution of resources* uwe sawa, hii keki ya Taifa tuigawane sawa, tunaposhindwa kutenda haki katika mgawanyo wa hii keki ya Taifa tunasababisha matatizo na wengine tutakuwa tunajihisi wanyonge. Sasa binadamu anapojihisi mnyonge ni tatizo kubwa sana, nisingependa katika Taifa hili wengine tujione wanyonge na wengine wawe siyo wanyonge.

Kwa hiyo, naomba sana hakikisha katika bajeti hii unatupatia gari la wagonjwa japo moja katika Halmashauri yetu na *specifically* liende kwenye Jimbo la Mchinga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la vyeti *fake* limeathiri sana Halmashauri yetu. Ziko zahanati mbili zimefungwa hivi sasa ninavyokuambia kwa sababu watumishi wake wote wameonekana wana vyeti *fake*. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri uchukue *initiative* za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali umefikisha ujumbe. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, bado tunawachangiaji, nitatenda haki kwa uwiano wetu, kwa hiyo msiwe na wasiwasi. Wale wa mchana wakajiandae, Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Oliver Semuguruka nitakuja kuwaelezeni utaratibu, ni dakika tano-tano tu maana tuna saa moja tu ili tuweze kuhitimisha hoja hii vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na orodha yetu hapa mchana, nitaendelea nayo lakini kwa kutenda haki kwa sababu ile idadi ya 14, wawili tumeshatimiza. Tuna muda wa dakika arobaini tu, kwa hiyo nitachukua Waheshimiwa Wabunge watano kutoka upande wa Chama cha Mapinduzi, wawili CHADEMA na mmoja CUF. Naanza na Mheshimiwa Hawa Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke. (*Makofii*)

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia. Napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa sekta ya afya ambayo kwa kweli wanafanya kazi nzuri, ngumu na yenye changamoto kubwa lakini bado wanaonesha kuimudu, kwa hiyo napenda nimpongeze sana. Mheshimiwa Waziri amesoma hotuba yake vizuri ambayo inaonesha anajiamini lakini pia sekta hii anajua vizuri. Ameonesha malengo bayana ambayo anakusudia katika bajeti hii kutatua kero ambazo ziko ndani ya sekta ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunisaidia kunipatia gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kitele, kwa kweli namshukuru sana. Pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI kwa kutoa ufanuzi kuhusu suala la upanuzi wa Kituo cha Afya Nanguruwe na Nanyumbu kuwa hospitali ya Wilaya, kwa sababu ililetu mkanganyiko mkubwa sana, kwa hiyo nawashukuru sana kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maombi yafuatayo kwa Serikali. Ombi la kwanza ni kwamba bajeti hii iliyoengwa kwa kweli inatosha. Tunachoomba ni Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba pesa hizo zinakwenda kwa wakati ili yale tuliyoyapanga yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, namwomba Mheshimiwa Waziri wa UTUMISHI, kwa dhati kabisa, kama ambavyo wanatoa vibali nya kuajiri Walimu basi awamu hii wajitahidi na Sekta hii ya Afya itolewe vibali nya kuajiri. Kwa kweli hali ni mbaya sana kwenye vituo nya afya hasa kutokana na huu uhakiki wa vyeti uliofanyika, vijijiini kwetu huko kumeathirika zaidi kuliko hata mijini. Kwa hiyo tunaomba watoe vibali nya kuajiri Madaktari, Wauguzi pamoja na Matabibu. Kama wangesema sekta moja tu ipewe kibali, basi mimi ningesema ni sekta ya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika maombi ya mkoa wangu, Mkoa wa Lindi na Kanda ya Kusini kwa ujumla. Kila Kanda ina Hospitali ya Kanda ya Rufaa. Kanda ya Kusini ujenzi ulianza karibu miaka 10 iliyopita, lakini kwa miaka hii miwili mfululizo naona kama ujenzi umesimama inatengwa billioni mbili na hilo haitoki. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Ummy mdogo wangu afanye huruma kwa ndugu zake wa Kusini, atakapokuja basi atuambie ametuandalia nini cha matumaini ili kuhakikisha hospitali ile inakamilika kabla ya mwaka 2020 ili huduma ziweze kutolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Kamati ya Bajeti iliweka maombi na mapendeleko ya kuongeza tozo kwa ajili ya kupata pesa za kujenga vituo nya afya na zahanati katika kila Halmashauri. Lengo ikiwa ni kuboresha huduma za afya na pia kupunguza vifoo nya akinamama na watoto. Serikali iliomba ipewe muda ifanye tathmini ili katika bajeti hii, waje na mpango mahususi wa kujenga kituo cha afya angalau kimoja kwa kila Halmashauri na zahanati angalau nne kila Halmashauri. Sasa upande wa TAMISEMI bahati mbaya wakati wa bajeti yao sikuwepo, lakini pia nimesoma kwenye makabrasha yao sikuona na upande wa sekta ya afya sioni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile tathmini Mheshimiwa Ummy nina uhakika wamemaliza. Kwa hiyo, tutaomba atakapokuja kutoa ufanuzi au kutoa majibu atuambie, wametenga kiasi gani na baada ya kufanya tathmini wameona gharama ni kiasi gani na mwaka huu wanahisi ni

kiasi gani kitatosha ili kuweza kujenga hivyo vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo pia nataka nilizungumzie ni suala la udahili wa kada zote za afya, iwe Madaktari, Wauguzi, Wafamasia kwa kweli uongezwe na sio udahili tu, lakini waajiriwe na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Ishengoma

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nawapongeza Mawaziri wote kwa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naanza na Benki ya Wanawake Morogoro. Naomba kituo cha Benki ya Wanawake Morogoro kama tulivoongea na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hospitali ya Wilaya ya Morogoro ni muda mrefu mimi na Mbunge wa Jimbo tulikuwa tunaongelea hii hospitali ni lini itaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu hospitali ya Ifakara Kibaoni, hospitali ya Ifakara Kibaoni inatumika kama ya Wilaya, lakini kuna watoto njiti (*pre mature*) ambao hawana chumba cha watoto njiti, wanalazwa pamoja na watoto wengine ambao mama zao wametoka kujifungua, pamoja na wale wanaoumwa. Kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri aweze kuona kama tunaweza kupata chumba cha watoto hawa njiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Morogoro hatuna *X-ray*, *X-ray*iliyopo ni mbovu. Hili jambo lilishaongelewa tulikuwa tunaomba *X-ray*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuongelea Hospitali ya Ulanga. Hospitali ya Ulanga wodi zao ni mbovu, kwa hiyo naomba iweze kuangaliwa. Hospitali ya Ulanga tuna *X-ray* pamoja na *Utrasound* lakini hatuna wataalam. Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize, hatuna wataalam wa Hospitali ya Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lishe. Kwa upande wa lishe vyuo vikuu na vyuo vingine vinaendelea kutoa elimu ya akinamama lishe (*nutrition officers*). Naomba hawa nao muwatumie badala ya kutumia tu vidonge vyta *vitamin A*. Wataalam hawa wa lishe nao pia watumieni kwa kuwaajiri kwa kusaidiana pamoja na TAMISEMI mpaka huko wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jamii. Ni kweli maendeleo ya jamii yameachwa nyuma, Mheshimiwa Waziri amekazia sana kwenye mambo ya afya lakini Sekta ya Maendeleo ya Jamii ameisahau, naomba aiangalie. Vile vile na wataalam wa maendeleo ya jamii waajiriwe mpaka vijijini kwani wenyewe ndio wanaosukuma maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa; naomba sana hii Sheria ya Ndoa, kama wenzangu walivyosema, illetwe humu Bungeni na kufanyiwa kazi kwa sababu ya kumsaidia mtoto wa kike. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya. Hadi kufikia Marchi ni asilimia 28 tu ndio wanaotumia Bima za Afya kama Mheshimiwa Waziri alivyosoma hotuba yake. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati atafanyaje kusudi watu wote, wanawake, wanaume na vijana waweze kujunga na Bima ya Afya kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi kila kata ni lazima iwe na kituo cha afya na kila kijiji lazima kiwe na zahanati na kila Wilaya lazima iwe na Hospitali. Namwomba Mheshimiwa Waziri tutekeleze hii ahadi ambayo ipo kwenye llani ya Chama cha

Mapinduzi kusudi tuweze kutimiza na aanze kutuambia na ni vipi atafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote naomba kuongelea jukwaa la wanawake. Namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuanzisha Jukwaa la Wanawake. Jukwaa la Wanawake la kiuchumi ni jukwaa zuri, ambalo linaunganisha wanawake wote ambapo wanabadilishana mawazo na wanaweza kupata jinsi ya kukopa kutoka kwenye taasisi zote za kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mwenyezi Mungu akubariki. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ishengoma. Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo matatu tu, la kwanza upungufu wa watumishi; pilii, maboma ya zahanati pamoja na vituo vya afya ambayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na Serikali ambayo hayajakamilika, lakini la mwisho, itakuwa ni kuhusu maendeleo ya jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, mwaka wa jana Mheshimiwa Waziri alitembelea Mkoa wa Kigoma, alipitia karibu Wilaya zote na aliweza kujionea matatizo yaliyopo Kigoma. Mkoa wa Kigoma umekumbwa na wimbi kubwa la wakimbizi waliotoka Burundi, DRC kuja Kigoma, kwa hiyo watu ni wengi sana, wapo watu ambao wako makambini. Kama unavyojuua binadamu huwezi kumzuia, wapo wakimbizi wengine ambao wamezagaa katika Wilaya zetu. Kwa maana hiyo basi, katika hospitali zetu watu ni wengi sana,

kwa hiyo tuna kila sababu ya kuongezewa Madaktari na Manesi ili kuweza kukabiliana na tatizo kubwa la wagonjwa ambao ni wengi katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo tatizo la watumishi. Karibu nchi nzima kumekuwa na kilio kwamba watumishi hawatoshi, sasa kutokana na tatizo hili la vyeti lillijoitokeza tatizo la watumishi litakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo naomba Serikali ijipange haraka iwezekanavyo kuhakikisha inapeleka watumishi wa afya katika Wilaya zetu na hususani huko vijijini, la sivyo wananchi watapoteza maisha kwa wingi sana kwa sababu hakutakuwa na Wauguzi na Madaktari. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijipange kuhakikisha watumishi wanapelekwa katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ilani yetu ya CCM tulisema tutajenga zahanati pamoja na vituo vya afya na wananchi kwa kushirikiana na Serikali wameshajenga maboma ya zahanati na vituo vya afya. Hata hivyo kumekuwa na kilio cha muda mrefu kwa ajili ya maboma yale, kwamba, yanabomoka na hayana msaada wowote. Kwa hiyo, naomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI waweze kuliangalia hili ili yale maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi na Serikali kwa maaana ya zahanati na vituo vya afya yaweze kukamilika kusudi huduma...

**MHE. MARWA L. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Kuhusu utaratibu

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, hebu subiri sana Mheshimiwa keti tu, kifungu gani Mheshimiwa?

**MHE. MARWA L. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) (2) (3) na (4). Nimewasiliza Wabunge wengi toka asubuhi, akisimama anaomba zahanati anaomba kituo cha afya anaomba hospitali ya Wilaya, majengo. Sasa, hivi hii Wizara inahusika na vitu hivyo sio TAMISEMI? Kwa hiyo nataka kujua juu ya utaratibu, mambo

ya zahanati, mambo ya hospitali za Wilaya, mambo ya majengo hayo yako kwenye Wizara hii ya Afya au TAMISEMI? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyoba, Mbunge wetu wa Serengeti, Waheshimiwa Wabunge wanaochangia hawajakiuka Kanuni hiyo ya 64 kwamba hawajadili hoja iliyo mbele yetu. Wizara hii ya Afya ndiyo inayosimamia suala zima la sera kwenye nchi nzima, kwa maana wao wanatunga sera. Sera huwezi ukaitoa na kuiacha tu, lazima ufuatilie utekelezaji wake kwenye maeneo ya Wilaya, Mikoa na zahanati. TAMISEMI ni kweli tumepita lakini wao hizi zahanati, vituo vya afya ni vya wananchi; ndiyo, lakini Serikali ni moja na ndio maana Bunge kama wawakilishi wa wananchi, mnapokuja hapa hamuwezi tu kuishia kusema kuongea mpaka hapa usifike huko. Ninyi mnayachukua yote kwa sababu mnaisimamia na kuishauri Serikali katika ngazi zote. Kwa hiyo wako sahihi, lakini nakushukuru kwa umakini wako wa kutafuta Kanuni. Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa dakika zako zimelindwa. (*Makof*)

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kumwelisha huyu ni Mbunge mgeni mimi ni *senior*. Naomba niendelee na mchango wangu. Naamini Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya TAMISEMI wakikaa pamoja tutafanikiwa kuweza kupata majengo ya zahanati na vituo vya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu Maendeleo ya Jamii. Maendeleo ya Jamii yamesahaulilka, nakumbuka siku za nyuma, enzi za mwalimu Mabibi Afya walikuwa wanatembea katika vijiji kuhamasisha shughuli za maendeleo na wananchi walikuwa wanaelimika kwa kipitia mabibi maendeleo. Sasa naomba kwamba maendeleo ya jamii wapewe vitendea kazi, tofauti na sasa hivi wako chini ya Mkurugenzi, Mkurugenzi akipata makusanyo ndipo anawapatia pesa kidogo ndio wanakwenda kufanya uhamasishaji wa shughuli za maendeleo vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwa kutumia Bunge lako Tukufu niwapongeze wa Wakurugenzi wa Wilaya ya Kasulu, Kibondo na maeneo mengine ya Mkoa wa Kigoma kwa kuweza kutimiza kwa kupeleka asilimia tano kwa vijana na wanawake. Kwa sababu hiyo, naomba sasa juhudzi ziongezeke kusudi pesa hizo ziwe zinapelekwa kuweza kuwasaidia wanawake na vijana. Na watasaidiwa basi, ni kwa kuungana na watendaji pamoja na hawa watu wa Maendeleo ya Jamii kwenda kuhamasisha wanawake na vijana kuanzisha vikundi ili ile asilimia tano inayotolewa ya vijana na wanawake iweze kupelekwa kwenye vikundi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwamba tunafahamu kabisa viro vituo vipyaa afya ambayo vinajengwa ambavyo kwa sasa hivi kwa mfano kule Wilaya ya Kasulu viro vituo vipyaa vinavyojengwa... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bulaya dakika zako tano.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa nishukuru katika Jimbo langu la Bunda kituo cha afya cha Manyamanyama tumepeata gari la kubebwa wagonjwa, ahsante sana; lakini katika yote usisahau kinahitaji kupandishwa hadhi. Imemshinda mama Anna Abdallah, Mwakyusa na ni sasa ndugu yangu Kigwangalla na Mheshimiwa Ummy dada angu mbali na kazi zote anazozifanya Manyamanyama tunahitaji iwe hospitali ya Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukizungumza humu ndani tutamsulubu Ummy, tutamsulubu Kigwangalla, lakini wote tunatakiwa tuibane Serikali itimize, Azimio la Abuja la kutenga asilimia 15 ya bajeti

ya Serikali Kuu iende kwenye Sekta ya Afya. Hawa hata kama wawe na misuli ya kufanya kazi kiasi gani wasipopewa fedha, hawawezi kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Menyekiti, hilo ndilo jambo la ukweli lazima tuseme, asilimia 15 na hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha upo na wewe na mama unaliskia hilo, lazima uhakikishe Azimio la Abuja na Tanzania tumesaini linatekelezwa, kwa sababu zikitengwa asilimia 15 angala changamoto ya Sekta ya Afya nchini itapungua na imekuwa ni kubwa; kuna tatizo la madawa, kuna kansa ya uzazi, kuna matatizo ya ugonjwa wa akili ambayo yamesahaulika kabisa. Yote hayo hayawezi yakafanikiwa kama tusipotimiza lile Azimio la Abuja la kutenga asilimia 15 kwenye bajeti kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nchi za wenzetu South Africa, Zambia, kuna mambo ambayo wameyafanya, fedha za dawa na vifaa tiba zinatokana na matumizi ya kawaida, ambazo ni fedha ndani, ni Bunge hili sisi kuamua, taratibu siyo misaafu, tukihakikisha pesa za dawa tunaziweka katika fungu la matumizi ya kawaida, uhakika wa fedha zetu za ndani kwenda katika madawa na vifaa tiba utakuwa mkubwa. Hapa nimpongeze mdogo wangu Upendo Peneza, aliomba kuleta hoja binafsi katika Bunge hili Tukufu lakini hakupata nafasi. Kwa hiyo lazima tubadilishe utaratibu na sisi si wa kwanza, tukifanya hivyo, si tu tutakuwa tumetatua changamoto katika sekta ya afya, tutakuwa tumeokoa vifo vy'a akinamama na watoto na tutakuwa tumetatua matatizo mengi ambayo yapo katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine Mheshimiwa Waziri Vyuo vy'a Maendeleo ya Jamii. Kabla Wizara hii haijaunganishwa unakijua Chuo cha Kisangwa Bunda kina matatizo lukuki. Naomba chuo hicho mhakikishe kinapewa fedha za kutosha ili kutatua matatizo yaliyopo. Kingine gari ambalo limechukuliwa kinyume na taratibu, Wizara ilishaagiza gari lile lirudishwe, aliyekuwa Mkuu wa Chuo alijiuzia kinyume na utaratibu na barua ziko Wizarani, hakuna shangingi

linalouzwa kwa shilingi laki tano, niliwaambia, naomba wizi huo mimi Jimboni marufuku sitaki nimeshaanza kusafisha. Kama ulikuwa kipindi hicho cha nyuma nimeshaingia mimi, sitaki biashara ya wizi Jimbo la Bunda, ni maendeleo tu. Naomba mambo hayo yote yazingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na ndugu yangu Dkt. Kingwangalla, yeye ni Daktari na tulikuwa wote, *back benchers* huko. Suala la tatizo la afya ya akili pale Muhimbili, kila siku katika wagonjwa 150 mpaka 200 wanaenda pale, zile dawa ni ghali, sasa hivi wanachangia. Ukiangalia moja ya matatizo hayo yapo kwenye kurithi na yanachangia umaskini mkubwa, lakini kitengo hiki kimesahaulika kabisa. Mimi si daktari lakini wanasesma matatizo yale kuna *stage*, lakini *sometimes* mgonjwa anaruhusiwa kwenda kwa sababu tu hakuna vitanda, hakuna maeneo ya kutosha ya kuwahifadhi wale. Kwa hiyo naomba milifanyie kazi sana, tuwape...(*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Pauline Gekul. Hayupo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ambayo iko mbele yetu. Kwa sababu ya muda niende haraka; pamoja na juhudini ambazo zinafanya na Serikali na kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeiona ametusomea tumeona mengi yaliyofanyika, lakini kiukweli bado tatizo la afya katika nchi yetu halijafikia katika *standard* ambayo tunaweza tukajisifia, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika nchi yetu maeneo mengi sana wataalam, watumishi wa afya, maeneo yote kuanzia hospitali kwenda kwenye zahanati, vituo vyaa afya, bado ni wachache sana. Kwenye maeneo yetu, mfano tu ukienda Wilaya ya Kaliua vituo vyaa afya, kwanza tunavyo vichache, viko viwili tu, lakini kuna

wahudumu watatu mpaka wanne; hebu niambie kwa eneo ambalo lina watu karibu laki tatu, wanahudumiwaje? Vile vile zahanati zina Mganga mmoja au Nesi mmoja akiugua mmoja wapo au wote wakiugua, zahanati imefungwa na watu hawapati huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wajawazito wanakaa zahanati kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka jioni hospitali imefungwa, hakuna huduma. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na juhudzi zote lakini lazima kuhakikisha kuna watumishi wa kutosha kwenye maeneo yetu ya vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vingi vya afya kwanza havina Madaktari, lakini pia havina vifaa tiba vya kupimia malaria na magonjwa mengine. Leo Kaliua mtu akiwa na malaria, mpaka aende Urambo, vituo vya afya havina hata vipimo vya kupima magonjwa madogo tu mpaka aende Wilaya ya Urambo. Kwa hiyo naomba, kwa kuwa lengo ni kupunguza vifo vya Watanzania vituo vya afya vyote viwe na vipimo vile vya kawaida kama vile vya kupima malaria na *BP*viwepo; vinginevyo hatuwezi kupigana na suala la vifo vinavyotokea ambavyo ni vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Wilaya ya Kaliua hatuna Hospitali. Kwa nguvu za wananchi na fedha za ndani tumeanza kujenga jengo la *OPD*, lile ni jengo la ghorofa moja na lina vyumba vyote vya muhimu, tumejibana kwelikweli kwenye mapato ya ndani. Naiomba Serikali, sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho, tumeshapaua, bado kupiga rangi, kuweka milango na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali iweke mkono wake pale, itusaidie pale tulipofikia tuweze kuhakikisha kwamba tunakuwa na Hospitali ya Wilaya. Kutoka Kaliua kwenda Urambo ni zaidi ya kilomita 35, lakini pale hakuna huduma ya operesheni hakuna chochote kinachofanyika. Mtu ambaye hali yake ni mbaya na barabara hakuna kutoka Kaliua mpaka Urambo, wengi wanajifungulia njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, hospitali ile ambayo tumeshaanza *OPD* longezewe fedha za kutosha ili iweze angalau ndani ya muda mfupi tuweze kuhakikisha kwamba ndani ya Wilaya yetu ya Kaliua tunakuwa na Hospitali ya Wilaya tuweze kuokoa maisha ya akinamama na watoto ambayo yanapotea kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kuwepo na vituo vichache. Sera inasema na ni Sera ambayo tunatamani itekelezwe; kwamba kila Kijiji kiwe na zahanati, lakini mbona mpango huo hauzungumziwi? Kila kata iwe na kituo cha afya, mbona mpango huo hauzungumziwi? Leo tunasema tunaokoa akinamama wajawazito na watoto, tunawaokoaje wakati unakuta vijiji kati ya 100 labda zahanati ziko tano au kumi? Leo Kaliua ina vijiji 101, zahanati hazizidi 20. Si kila kitu wananchi wanaweza kukifanya; ni kweli wanafanya na tunawahamasisha wanafanya, lakini ni ngumu kwa wananchi kujenga kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunawaomba ile Sera ya Serikali itekelezwe ili tuweze kuwa na zahanati kila kijiji, tukaweza kuwa na kituo cha afya kila kata. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, mwaka jana tumeppata mwongozo kwenye vikao vyetu vya Halmashauri, Mheshimiwa Waziri alituma barua kwamba kila kata mbili ziandae maeneo kwa ajili ya kujenga vituo vya afya, tumeshaandaa yale maeneo, tukashauriana kila kata mbili zikaandaa eneo la kujenga Hospitali. Hebu atuambie, ni lini ujenzi au maandalizi ya kuanza kujenga vituo vya afya utaanza?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** ...Kwa sababu maeneo yametengwa yako pale na yako kwenye Wizara.  
*(Makofii)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa MwenyeKITI, ahsante sana. Naomba moja kwa moja niende katika Hospitali yangu ya Wilaya ya Ulanga. Hospitali ya Ulanga hali yake ni mbaya sana kiasi kwamba haiendani na hali ya Mbunge kama ilivyo, Mbunge mahiri na machachari. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa MwenyeKITI, moja, katika Hospitali ya Wilaya ya Ulanga, watumishi ni wachache, yaani wachache kupindukia. Madaktari ni wachache, wataalam kama wa *X-ray* yuko mzee mmoja ambaye alishastaafu miaka mingi iliyopita ndiye tunatumia huyo huyo kwa kumwajiri kwa mkataba. Pia *ultrasound* na yenyewe haina mtaalam, Serikali imejitahidi imenunua *ultrasound* mpya lakini hamna mtu wa kusoma. Hali hii imesababisha kumtafuta mtu kutoka Hospitali ya *Saint Francis* – Ifakara ambaye anapaswa kusafiri mpaka Ulanga kwa ajili ya kuja kusoma hivyo vipimo.

Mheshimiwa MwenyeKITI, Wodi zilizopo ni za tangu enzi za Mkoloni, na ni chache. Mheshimiwa Waziri naomba ujaribu kutembelea uone kwa kiasi gani Wilaya ya Ulanga tunavyopata tabu. Wagonjwa wanachanganywa, kwa mfano akinamama ambao wamefanyiwa *operation* wanaenda kulazwa wanachanganywa na wagonjwa wengine. Hali hii inapelekea hatari kwa magonjwa nyemelezi ambayo yanaweza yakasababishwa kutokana na vidonda vyao. (*Makof*)

Mheshimiwa MwenyeKITI, chumba cha upasuaji cha Hospitali ya Ulanga kina hali mbaya sana, kiasi cha kwamba kama ingekuwa Hospitali ya *Private* ingefungiwa. Chumba cha upasuaji hakina *monitor* matokeo yake Madaktari wanatumia uzoefu wao binafsi kama waganga wa kienyeji kwa ajili ya kuwafanya *operation*. (*Makof*)

Mheshimiwa MwenyeKITI, Hospitali ya Wilaya ya Ulanga mashuka ya wagonjwa yanafuliwa kwa mkono, kiasi

cha kwamba inapelekea hatari kwa hawa wafanyakazi. Hebu fikirieni mashuka ya wagonjwa yanafuliwa kwa mkono, Mheshimiwa Waziri akienda kweli machozi yatamtoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Ulanga haina gari ya wagonjwa, gari iliyokuwepo nilyonunua mimi ambayo haiendani sawa na ukubwa wa Jimbo. Gari yenyewe ni *haice*, nimejitahidi nimenunua basi Serikali iseme jamani kijana wetu umejitahidi hata mniunge mkono muongeze lingine. Liko lingine ambalo nimelichukua najikongoja kulitengeneza sasa hivi mwaka mzima lakini nimeshindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Hospitali ya Ulanga, *uniform* mwaka wa saba huu wanajinunulia wenyewe, hakuna *uniform allowance*, hebu fikirieni Maaskari wanajinunuliwa *uniform*, sehemu zingine wanajinunuliwa *uniform*, Ulanga pamoja na hali ngumu ya uchumi lakini wanajinunulia wenyewe, kwa hiyo naomba muwaunge mkono kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa; Wilaya ya Ulanga, ndio inaongoza kwa wagonjwa wa kifafa duniani, dawa za ugonjwa wa kifafa zinatolewa bure Tanzania lakini cha ajabu dawa hizi Ulanga zinauzwa. Ukienda Hospitalini hazipo, lakini kwenye maduka ya *private zipo*. Kwa hiyo naomba mliangalie hili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nipingane kwa nguvu zote kutokana na maoni ya Kamati wanasesma huduma za *NHIF* ziboreshweli mashirika ya umma yajunge. Wewe ni shahidi ili nyumba uimalizie vizuri inatakiwa uhamie ndani ndiyo utamalizia, ukisema nisubiri niimalize hutoweza kuhamia. Kwa hiyo tunataka, kwa sababu *NHIF* inaendeshwa kwa michango, haya Mashirika ya Umma yaingie, yakishaingia michango yao ndiyo itakayoboresha hizo huduma. Kwa sababu gani tunasema huduma bora, *NHIF* ndiyo yenye vituo vingi Tanzania, hakuna shirika lingine la bima ya afya ambalo linatoa huduma katika vituo vingi, *NHIF*

inatoa huduma bila kikomo. Shirika gani la bima ya afya ambalo linatoa huduma bila kikomo tuseme tusubiri huduma ziboreshw? *NHIF* ina wanufaika wengi kuliko bima za afya zingine, tunataka huduma zipe ndizo ziboreshw? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo yangu ni hayo machache kwa ajili ya kutunza muda. Ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kutunza muda. Mheshimiwa Selasini dakika zako tano atafuata Mheshimiwa Wanu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja hii ilio mbele yetu. Kwanza kabisa ningependa kuzungumzia ujenzi wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya ya Rombo. Wilaya ya Rombo ni Wilaya Kongwe lakini katika umri wake wote hajawahi kuwa na Hospitali ya Wilaya. Hospitali ambayo tunatumia ni Hospitali ya Huruma ambayo Meneja wake ni Askofu wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali inayojengwa sasa hivi katika Kituo cha Afya Karume tumejitalahidi, tayari tumekamilisha wodi zote tuna *Theater* tuna Mochwari lakini tunasumbuliwa na fedha za kumalizia jengo la *OPD*. Ujenzi umeshaanza, msingi umeshakamilika, lakini sasa hivi mkandarasi amesimama kwa sababu tumeshindwa kumlipa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alitembelea jengo hili na alitoa ahadi kutusaidia. Nataka tu ku-*register* maombi haya pia kwa Wizara ambayo ndiyo inasimamia sera, mtusaidie ili jengo hili liweze kumalizika tuweze kuwa na hospitali ambayo itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo ningepeda kuzungumzia hitaji la watumishi kama wenzangu walivoyozungumza. Tuna matatizo makubwa sana ya watumishi katika sekta ya afya kwenye Jimbo la Rombo, kuanzia Madaktari, Manesi na watumishi wengine. Wananchi

wa Rombo wamejitahidi sana kwa nguvu zao kujenga zahanati katika vijiji mbalimbali, lakini sasa ujenzi wa zahanati hizi ambazo nyingine zimekamilika na nyingine zinaendelea na ujenzi, tunapata shida kwa sababu tunawahamasisha wajenge, lakini hakuna wataalam. Kwa hiyo, ningewomba dada yangu Ummy atakapopata fursa pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kwa ajili ya kuwaajiri watumishi wa sekta ya afya atukumbuke Jimbo la Rombo kwa ajili ya Madaktari na Manesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mamtkuna, Mheshimiwa dada yangu Ummy alifika pale anakifahamu kile chuo, tunahitaji kubwa sana la watumishi Walimu na bajeti yake ni ndogo na kile Chuo kinasaidia sana. Tunaomba sana kama Wizara wanaweza wakaendelea kukitunza na kukiangalia kile chuo ili kuweza kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa kuzungumzia ujenzi wa jengo kwa ajili ya vifaa vyta kansa pale Hospitali ya *KCMC*. Jithada zimefanywa na wafadhili, jithada zimefanywa na Kanisa la Kinjilli la Kilutheri, kwa ajili ya kuhakikisha kumekuwa na kituo ambacho kitasaidia pia kupunguza msongamano katika Taasisi ya Kansa ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana fedha ambazo zinahitajika kwa ajili ya lile jengo ni kama bilioni sita hivi, ambazo kwa kweli kwa hapo tulipofikia *KCMC* ina mzigo mkubwa sana na vifaa vimeshapatikana. Kwa hiyo ningelomba Serikali, tusiache hivi vifaa mwishoni wafadhili wavitungie kwa namna nyingine, tungeomba sana muwasaidie jengo hili liweze kukamilika ili taasisi ile iweze kusaidia Taasisi ya Kansa ya *Ocean road* ili wananchi wenye matatizo ya kansa ambao sasa hivi ni wengi waweze kupata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ambayo yameendelea kuzungumzwa ya unyanyasaji wa watoto,

wazee na kadhalika, ningeomba sana Wizara iweke msisitizo kwa sababu hili na lenyewe ni tatizo ambalo ni *cross cutting*, liko karibu katika kila eneo. Ni kweli watoto wanadhalilishwa, ni ukweli kuna watu ambao wakishafanya mambo kama haya wanaachwa mitaani kiholela. Ningeomba sana Wizara iweke msisitizo katika jambo hili ili watoto wetu wawe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, hayo ndiyo nilikuwa nayo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Wanu atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege.

**MHE. WANU HAFIDH AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie katika Hotuba hii ya Waziri wa Afya. Kwa kuanzia kwanza nipongeze Serikali yangu ya Awamu wa Tano kwa kazi nzuri ambayo imekuwa inafanya na hili halitaki tochi kabisa mwenye macho anaona kabisa kwamba kazi inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa kazi yao nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Hongera za pekee nimpelekee Mheshimiwa Waziri, amekuwa akishirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Afya ya Zanzibar, pamoja na kwamba si Wizara ya Muungano lakini amekuwa akionesha ushirikiano kiasi kwamba kumekuwa na hamasa kidogo ya kazi katika Wizara ya Afya, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amekuwa akionesha mashirikiano, bado kuna changamoto kidogo katika mashirikiano haya. Tunashukuru sana kwamba anaonesha imani kwa upande wa Zanzibar, lakini bado kuna changamoto panapotokea mikutano ya Kimataifa kwa kweli upande mmoja unakuwa hauangaliwi vizuri. Kwa hiyo, tunaomba kuwe na mpango mahsus ambao utashirikisha upande mmoja wa Muungano kunapotokea mambo kama haya ili na wao wawe

wanafaidika katika fursa ambazo zinapatikana kutokana na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 69 amezungumzia kuhusu tafiti ambazo wamekuwa wakifanya. Naomba niishauri Serikali wanapofanya hizi tafiti basi na upande ule mwingine wa Zanzibar wawe wanawashirikisha. Kwa sababu huwezi ukawa unatibu upande mmoja au unafanya tafiti upande mmoja lakini upande ule mwingine unakuwa tatizo liko pale pale. Nitachukua mfano, kwa mfano Zanzibar tuko vizuri katika kutibu malaria, tuko chini asilimia moja lakini kwa upande wa bara kuna mikoa ambayo iko *even above 20 percent*, kama kungekuwa na ushirikiano naamini Zanzibar ingeisaidia Tanzania Bara katika kupunguza Malaria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pla katika maradhi mengine ya mlipuko kama kifua kikuu na UKIMWI huwezi ukaacha upande mmoja na kushughulikia upande mmoja kwa sababu kwa mfano kama kifua kikuu ni maradhi ambayo yanaambukizwa na hewa na sisi katika hii nchi yetu tuna pande mbili na kuna *free movement* za hizi pande mbili. Kwa hiyo, kama unatibu upande mmoja lakini upande mmoja hakuna matibabu yoyote na wana-*cross* kupita upande wa pili bado matatizo yanakuweko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi jioni ya leo kupata nafasi hii kuchangia. Naomba kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana. Naomba niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake. Baada ya kupongeza naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Serikali inayoongozwa na CCM kwa nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunaanza kujenga Hospitali ya Wilaya

ya Kalambo, naomba kasi hii ambayo imeoneshwa tusije tukasita hata kidogo, tuhakikishe kwamba tunaenda kuimalizia kabisa na itumike ili kuwasaidia Watanzania walio Mkoa wa Rukwa na hususani Wilaya ya Kalambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wenzangu wakiwa wanamshukuru Mheshimiwa Waziri, wamepata *ambulance* ni jambo jema, naamini zamu nyngine na sisi Kalambo tutakumbukwa, ili kuunga jitihada za Mbunge huyu ambaye anaongea, maana ameweza kusababisha zikapatikana *ambulance* tatu. Ni wakati muafaka Serikali ikaniunga mkono ili tuokoe wananchi walioko Wilaya ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matatizo ambayo tunayo makubwa wenzangu wamesema kuhusiana na suala zima la ukosefu wa watumishi pamoja na vifaa tiba na vitendanishi. Kama kuna maeneo ambayo yana tatizo kubwa ni pamoja na Wilaya ya Kalambo na ni kwa sababu kimsingi mikoa ya pembezoni imekuwa *disadvantaged* kwa kipindi kirefu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati wanapanga ikama ya safari hii naomba aitazame kwa jicho la huruma Wilaya ya Kalambo, tunahitaji kuziba pengo kubwa sana la upungufu wa watumishi katika kada hii ya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema wenzangu nami nilirudie. Ni matarajio yetu kwamba tunapoongea na Serikali tunaongea nayo kwa ujumla wake na mpango mzima wa kubadilisha utaratibu wa *circle* ya bajeti ni ili kama kuna jambo ambalo halikupita katika Wizara husika tunapokuja kuhitimisha bajeti basi tuhakikishe jambo hilo linakuwa *addressed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna hili suala zima la ujenzi wa vituo vya afya pamoja na kumalizia zahanati. Katika hali ya kawaida iko chini ya TAMISEMI lakini TAMISEMI na Wizara ya Afya ni Serikali moja na Serikali yenywewe inatokana na CCM, kwa hiyo tunaongea na Serikali ya CCM. Mlikuja kwenye Kamati ya Bajeti mkasema *last time* mnaenda kuleta bei halisia ili tukamalizie maboma na tuanze kujenga vituo

vya afya. Sasa mwenzenu katika Wilaya ya Kalambo yenne kata 23 na vijiji 112 kuna vituo vya afya vitatu tu; mnaweza mkaona jinsi gani uhitaji ulivyokuwa mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejitolea wamejenga kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali hii kwamba wajenge kufika usawa wa lenta na baadaye Serikali *i-take over* na hakuna hata siku moja ambayo Serikali imekuja ikasema utaratibu ule umefutwa. Kwa hiyo, bado ni jukumu letu ni jukumu la Serikali kuhakikisha Wananchi ambao wamejitoa kwa moyo wao kazi nzuri hii iweze kumaliziwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mapendekezo, kwa namna iliyo nzuri tulipendekeza shilingi hamsini iwe kwenye tozo ili iende ku-*address* tatizo hili la ujenzi wa vituo vya afya pamoja na kumallizia zahanati ambazo wananchi wamejitoa kwa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wasikie na watie uzito katika haya ambayo nnayasema naomba niishie hapo nashukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kandege.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niombe kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia 100. Pili nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii hususan Mheshimiwa Waziri Ummu Mwalimu na Naibu wake kwa msaada mkubwa walioutoa kwenye vituo vya afya viwili; kituo cha Bulungu kupewa *ambulance* na kituo cha afya cha Nguruka nacho kilipatiwa *ambulance*. Tunaishukuru sana Wizara kwa msaada huo na tuiombe Wizara pale ambapo *ambulance* zinapatikana basi nitaomba kukiombea kituo cha afya cha Kalya ambacho

kiko kilometra 270 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Lugufu. Wakina mama wajawazito wanapata taabu sana tena sana pindi wapatapo shida ya kujifungua kwa kupasuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe pia Wizara itupitishie ombi letu maalum la shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, tayari tumetenga eneo la hekari 30 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Uvinza ina jumla ya zahanati 33, kati ya vijiji 61 tunavyo vituo vya afya vitano katika ya kata 16 hivyo tuna upungufu wa vituo vya afya 11. Kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa vituo vya kata za Kazura Mimba, Basanza pamoja na Mwakizega. Hivyo Mheshimiwa Waziri utaona ni jinsi gani hali ya afya bado haijaimarika ndani ya Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na ujenzi wa zahanati zifuatazo; katika kijiji cha Mazugwe ujenzi umekamilika. Kuna jitihada ya uanzishwaji kupitia Mfuko wa Jimbo na Halmashauri na kumalizia; zahanati za Lufubu, Ikubuvu, Kalilani, Msiezi, Kajije, Katenta, Malagarasi, Humule. Zahanati zote hizi tisa zinajengwa kwa nguvu ya Mfuko wa Jimbo na nguvu za wananchi. Tunaiomba Wizara kutuletea pesa kwa wakati ili tuweze kuunga mkono jitihada hizi za mimi Mbunge wao pamoja na nguvu za wananchi. Sambamba na jitihada za ujenzi wa zahanati tuiombe Serikali kutupa upendeleo kituo cha afya cha Nguruka kwani kinahudumia wakazi wapatao 80,000 ndani ya kata nne na kata moja ya jirani, kata ya Usinge Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vifaa tiba si nzuri kabisa. Kuna zahanati hazina vitanda wala magodoro, tunaiomba Wizara itusaidie vitanda, magodoro pamoja na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya kwa asilimia 70. Tunaiomba Wizara itakapoanza kuajiri basi Wilaya ya Uvinza

iangaliwe kwa jicho la huruma, hali inatisha. Tuna mtumishi wa zahanati ya Mwakizega anaitwa Zainabu Hassan Salim, hivi karibuni nchi nzima ilishuhudia jinsi wananchi walivyoandamana kupinga *nurse* huyo kuhamishwa. Hebu Wizara iwe na utaratibu wa kutoa motisha kwa watumishi kama huyo; na kwa kuanzia si vibaya wakaanza na *nurse* Zainabu Hassan Salim wa zahanati ya Mwakizega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia haya naomba kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwa Mheshimiwa Waziri Ummy kwenye maeneo kama ya Jimbo langu, si vibaya kuwa na *ambulance za speed boat ili* kuokoa vifo vya mama na mtoto kwenye Ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mara nyingine niunge mkono. hoja.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu usimamizi wa masuala ya hedhi mashulenii. Mashulenii hakuna wataalam wanaotoa elimu ya masuala ya hedhi wala elimu ya afya ya uzazi ili wanafunzi waweze kupata elimu ambayo itawasaidia kuweza kuepukana na mimba za utotoni kwa kuwa miili yao bado ni midogo kuhimili kubeba mzigo (mimba) ambazo huweza kuleta madhara yakiwemo upungufu wa damu, shinikizo la damu, ugonjwa wa fistula na hata vifo vitokanavyo na uzazi. Nashauri wataalam wa idara ya afya wanaoshughulika na masuala ya *outreach services* watoe elimu ya masuala ya afya mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa uimarishaji wa afya ya msingi kwa kuzingatia matokeo (*result based financing*); Mkoa wa Simiyu ni moja ya mikoa ambayo mradi huu unatekelezwa kulingana na vigezo vya *star rating* na tayari kuna baadhi ya zahanati zimepatiwa kiasi cha shilingi 10,000,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya upungufu wa watumishi, naomba Mkoa huu upewe kipaumbele mara ajira za afya zitakapotoka, pia wapo wahitimu ambao wapo tayari kuajiriwa Mkoa wa Simiyu kulingana na changamoto ya watumishi kuhama mara baada ya kuajiriwa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia kwa maandishi. Natumia fursa hii ya kufanya wajibu wangu wa Kibunge kwa kuishauri Serikali katika bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana katika michango yangu Bungeni kwa Wizara hii nilitoa ushauri kwa Serikali kwamba Serikali iliangularie suala la hedhi na upatikanaji wa *sanitary pads*. Natumla fursa hii kuikumbusha Serikali haja ya kulishughulikia suala la hedhi ili kusaidia kupunguza mimba za utotoni na *school drop-outs* kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iunde chombo ndani ya *TFDA* kitakachofanya kazi ya kusimamia bei ya bidhaa ambazo zimeondolewa *VAT*kama vile dawa na *sanitary pads* ili lengo la kuondoa *VAT* liweze kutimia kwa kuwasaidia wananchi kupata bidhaa hizo kwa bei rafiki tofauti na ilivyo sasa ambapo wafanyabiashara hujipatia faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa *sanitary pads* kunamfanya mtoto wa kike kukosa siku nne mpaka saba suala ambalo linajenga utoro shulenii. Watoto wakike hukosa ujasiri kwenda darasani kwa kuwa hawana vifaa bora vya kujihifadhi kipindi cha hedhi. Utoro huo wa siku nne hadi saba humfanya mtoto wa kike kupoteza muendelezo wa kimasomo na hivyo mtoto wa kike anakuwa katika hatari ya kufanya vibaya katika masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoro pia unachangia katika ongezeko la *school drop-outs*, yaani kuacha shule kwa watoto wa kike ambapo baadaye huleteleza (husababisha) mimba za utotoni. Ni vyema Serikali ikalitazama suala hili

kama suala muhimu na kuweza kulifanyia kazi ili kuwaokoa watoto wetu. Serikali ikisaidia kupatikana kwa *sanitary pads* kwa bei rafiki au bure itasaidia kuongeza kiasi cha ufaulu cha watoto wa kike kwa kuwa utoro utakoma na upatikanaji wa *sanitary pads* utapunguza idadi ya watoto wa kike wanaoacha shule na hivyo kupunguza mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptitia Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu iratibu suala la upatikanaji wa pesa ili kugharamia *sanitary towels*. Serikali iongeze pesa kwenye *capitation funds* ili watoto wa kike wapate *sanitary pads/towels* mashulenii. Katika kusimamia hilo, Serikali ihakikishe anapatikana mwalimu wa kike (*matron*) atakayeshirikiana na Mwalimu Mkuu wa Shule katika kusimamia pesa za *capitation* ambazo zitakuwa zimepangwa kwa ajili ya upatikanaji wa *sanitary pads*. *Matron* atawajibika kuunda *girls club* mashulenii ili kujuu namna ya kutumia na kupata *sanitary pads* lakini pia *girls clubs* hizi zitasaidia kutoa elimu ya afya ya uzazi. Wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu wapatiwe ongezeko kwenye mkopo ili waweze kugharamia *sanitary pads*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeandaa hoja binafsi ingawa kutokana na ufinyu wa nafasi sijaweza kuiwasilisha; pamoja na kwamba imewasilishwa kwa Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge. Hoja hiyo nilijenga katika kuliomba Bunge liazimie kuitaka Serikali katika kubadilisha kifungu cha dawa kuwa katika fungu la matumizi ya kawaida ya Wizara. Kwa sasa kifungu cha dawa kiko kwenye fungu la bajeti ya maendeleo ya Wizara ambapo pesa hizo hazipatikani au kutolewa kwa kila mwezi na hivyo kuathiri upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu la bajeti ya maendeleo la Wizara katika magonjwa kama UKIMWI na *TB* hutegemea wahisani ambao huchelewa kutoa pesa hivyo huathiri upatikanaji wa dawa. Ni vyema sasa Serikali ikaweka pesa za dawa na vifaa tiba katika fungu la matumizi ya kawaida na ifuate vipaumbele kama ifuatavyo; kwanza, mshahara;

pili, dawa za binadamu na vifaa tiba na tatu matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia dawa za binadamu kuwa na pesa za uhakika ambazo ni pesa za ndani na hivyo kuondoa tatizo la upatikanaji wa dawa. Kwa kusema pesa za dawa za binadamu na vifaa tiba namaanisha dawa pamoja na vifaa tiba wezeshi kama vile pamba, sindano, *gloves* na si vifaa kama *x-ray machines* ambazo zibaki kwenye fungu la maendeleo ya bajeti, ahsante.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara hii, ninaomba vitu viwili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilolo ni kati ya Wilaya kubwa Tanzania, illanzishwa mwaka 2002 lakini hatuna Hospitali ya Wilaya na kituo cha afya ni kimoja tu. Ili mwananchi apate matibabu inabidi asafiri kilometra 100 hadi llula. Changamoto kubwa ni gari la wagonjwa, yaani gari langu sasa limekuwa gari la wagonjwa; Mheshimiwa Naibu Waziri anajua sana tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninaomba sana nipate gari Wilaya ya Kilolo. Bado tuna ikama kubwa ya watumishi wa afya. Tunaomba sana uwasiliane na Wizara ya Utumishi ili tuongezewe watumishi.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya malengo ya milenia ilikuwa ni kupunguza vifo vyta wanawake wajawazito, watoto wachanga pamoja na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Pamoja na kuwepo lengo hili, Tanzania bado tuna changamoto kubwa ya vifo vyta wanawake na wajawazito pamoja na watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 16 ameeleza na kuthibitisha kuwa vifo hivi bado ni changamoto kubwa, ambapo kwa mwaka 2015 idadi ya vifo ilikuwa 556 kwa kila vizazi hai

100,000. Hili ni tatizo kubwa ambalo linahitaji nguvu ya pamoja kati ya wanawake na wanaume. Wanaume wakielimishwa na wakawa karibu na wake zao kuna uwezekano mkubwa wa kupunguza vifo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mila potofu katika jamii zetu ni tatizo. Kwa mfano katika baadhi ya makabila mwanamke mjamzito hawezi kwenda kujifungulia hospitali mpaka apate ruhusa ya mama mkwe au wifi ndipo aende hospitali au kwa waganga wa kienyeji. Hili ni tatizo na elimu ni muhimu kutolewa kwa jamii hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Arusha takwimu zinaonesha kuwa vifo vya wajawazito vimeongezeka kwa asilimia 31 kutoka vifo 49 kwa mwaka 2015 na kufikia vifo 72 kwa mwaka 2016. Kwa upande wa vifo vya watoto kwa mwaka wa jana kulikuwa na vifo 978 wallipoteza maisha sawa na kifo kimoja kwa kila vizazi hai 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya vifo hivi ni kutokana na upungufu wa vituo vya afya katika Halmashauri za Mkoa wa Arusha ambapo kwa jamii za wafugaji kama inavyoileweka wanaishi mbali na mijii, hivyo naomba Wizara isaidie kwa kutimiza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *WHO* duniani kote hasa nchi zinazoendelea wanawake 300,000 hufa wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua, na zaidi ya watoto milioni mbili hufa katika siku 28 za mwanzo na wengine zaidi ya milioni mbili wakiwa si riziki. Kwa upande wa watoto takwimu za *WHO* zinasema kuwa watoto wachanga na wale wanaozaliwa wanakufa. Vifo hivi vinaweza kuzuilika kwa kuwa na huduma bora za afya wakati wa ujauzito na kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana vifo vinavyorekodiwa ni kwa wale tu wanaofika hospitali na wengi hujifungua majumbani kutokana na umbali pamoja na mila na desturi.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata muda huu wa kuchangia humu ndani ya Bunge lako Tukufu. Napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi kwa Serikali napenda kuongelea Benki ya Wanawake. Mheshimiwa Waziri uliniahidi kituo cha mikopo na mafunzo ya ujasiriamali, je, Mheshimiwa Waziri ni lini wanawake wa Mkoa wangu wa Morogoro watapata kituo hiki? Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, wanawake hawa hawapatiwe kituo hiki ili waweze kufaidika na mikopo inayotolewa kwa riba nafuu. Naomba tamko lako kwa hili Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya Morogoro, Wilaya hii haina hospitali, je, ni lini hospitali hii itaanza kujengwa kwa ukamilifu? Mheshimiwa Waziri naomba jibu lako wakati utakapokuwa unatoa majibu. Hospitali hii ya Wilaya itaweza kupunguza vifo vyta akina mama na watoto na hasa kina mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hospitali ya Ifakara au Kibaoni namuomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Waziri wa TAMISEMI kusudi matakwa ya Hospitali za Wilaya, zahanati na vituo vyta afya yatimizwe. Hospitali hii ya Ifakara Kibaoni kuna tatizo ambalo linawahusu watoto ambao wanazaliwa kabla ya wakati yaani watoto njiti, (*pre-mature*). Hospitali hii haina chumba maalum kwa ajili ya watoto njiti. Watoto hawa njiti wanalazwa wodini pamoja na wale watoto wanaozaliwa kwa wakati (miezi tisa) na wale watoto waliozaliwa kwa ajili ya kuumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si nzuri kwani watoto hawa njiti wanatakiwa uangalizi wa hali ya juu. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana chumba cha watoto hawa njiti (*pre-mature*) kingejengwa haraka iwekanavyo. Pia ingawa hospitali inatumiwa kama hospitali ya Wilaya lakini ina uhaba wa wataalam, dawa na vitendea kazi pia vitendanishi.

Mheshimiwa Waziri, naomba uiangalie hospitali hii ya Ifakara Kibaoni kwa sababu hasa ya watoto hawa njiti ambao hawana chumba maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro tunaomba jengo la *mortuary* na *theatre*, *x-ray* iliyopo haifanyi kazi vizuri na ni ya muda mrefu. *Mortuary* ni ndogo pia *theatre* ni ndogo kufuatana na mahitaji, Mheshimiwa Waziri maombi haya ni ya muda mrefu kama hospitali ya rufaa inapaswa kuwa na *x-ray* inayofanya kazi vizuri, *mortuary* na *theatre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya lishe, miaka ya nyuma elimu ya lishe ilikuwa inatolewa kwenye kliniki na hasa wajawazito na akina mama wanaonyonyesha. Elimu hii illhusu vyakula vya mtoto na hasa vyakula vya kulikiza na jinsi ya kunyonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo bado vinatoa watu waliochukua *nutrition*, naomba tuwatumie kikamilifu licha ya matone ya vitamini A, kuweka virutubisho kwenye unga (*fertilization*), kutoa *folic acid etc*. Pia Mheshimiwa Waziri tuzidi kuwatumia wataalam hawa kwa upande wa vyakula, kwa namna hii tutapunguza utapiamlo kwa ujumla na vifo vya watoto wachanga na wajawazito. Kwa kusaidiana na Wizara husika waajiriwe kila wilaya/kata mpaka vijijini wapewe vitendea kazi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya jamii, idara hii imesahauliwa, Mheshimiwa Waziri nakuomba jitahidi kuiona na hasa Maafisa Maendeleo ni watu muhimu katika kusukuma maendeleo ya nchi na kwenye makazi yetu. Waajiriwe kimko/a/kiwilaya/kata mpaka Afisa Maendeleo wa Kijiji, namuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bima ya Afya, mpaka Machi 2017 ni asilimia 28 tu ya Watanzania ndio wanaotuma bima ya afya. Mheshimiwa Waziri ni mkakati gani utumike

hasa ili watu wote, wanawake, wanaume na vijana waweze kutumia bima ya afya kikamilifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kijiji kuwe na zahanati, kila kata kuwe na kituo cha afya na kila wilaya kuwe na hospitali kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri naomba useme ni mkakati gani unatumika/utatumia kukamilisha matakwa haya? Naomba na ninashauri jitahidi za kusaidia Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itimize jambo hili litapunguza vifo vyta watoto na kina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Ndoa, naumuomba Mheshimiwa Waziri afanye awezavyo iletwe Bungeni. Nimuhimu sana kwa maisha ya watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja .

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendoe ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata huduma hiyo stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wake imara kwa nchi yetu hasa katika kuimarisha huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mzuri na kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya CCM na hasa katika masuala ya afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote tunatambua umuhimu mkubwa na wa mwanzo kabisa wa afya ya wananchi wetu. Afya ni suala la msingi katika ustawi na hata uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa afya kwa kila Mtanzania inabidi Serikali kuangalia namna mbadala za kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora ya afya. Katika ukurasa wa 65 na 66 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya ameeleza kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) una wanachama 792,987 hadi kufikia Machi 2017; vilevile idadi ya wanufaika ni 3,880,088 hadi kufikia Machi 2017. Kwa upande wa Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) ulikuwa na kaya 1,595,651 na wanufaika wa *CHF* walikuwa 9,573,906

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Machi 2017, Mifuko ya Bima ya Afya ya *NHIF* ilikuwa na wanachama (kaya) 2,388,638 zenye wanachama 13,453,994 tu. Hii ni sawa na asilimia 38 ya Watanzania wengi hasa wa vijijini wanaoendelea kukosa huduma ya afya kwa ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya uzinduzi wa bodi mpya mwaka 2016 ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*), Waziri wa Afya alisema mkakati wa Serikali ni kufikisha huduma ya bima ya afya zaidi ya asilimia 50 kwa Watanzania wote ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza muswada huo wa bima ya afya uwasilishwe mapema iwezekanavyo ili Watanzania wengi zaidi wajunge na bima ya afya na mazingira ya muswada yepelekee ulazima wa kila kaya kuwa na bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutafikia kaya 15,000,000 kwa malipo ya shilingi 30,000 kwa mwaka kwa kila kaya, mfuko utakusanya shilingi bilioni 450 kwa mwaka. Makusanyo hayo kwa mwaka yatawezesha mfuko kutoa huduma bora zaidi kwa Watanzania wengi na wanaweza

hata kukopesha Halmashauri kujenga zahanati na vituo vya afya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa vituo vya afya na zahanati kutachochea ongezeko kubwa la wanachama na pia mapato makubwa kwa mfuko. Kwa mkakati huu wa kuboresha bima ya afya si tu itaboresha huduma za afya, lakini itapunguza kwa kiasi kikubwa bajeti ya Wizara ya Afya na hata TAMISEMI kutegemea mfuko wa Hazina unaotokana na kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Tabora watumishi wa sekta ya afya ni wachache kwenye maeneo yote na hili ni tatizo la muda mrefu, wanaopoteza maisha kwa kukosa huduma ni wengi. Vituo vya afya vina wahudumu watatu mpaka wanne tu na wanafanya kazi usiku na mchana. Zahanati nyingi zina *nurse* mmoja na mganga mmoja tu. Ikitokea akapata dharura hakuna huduma na maeneo mengine wanatoa huduma wasio na taaluma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe kipaumbele kwa Mkoa wa Tabora kupelekewa watumishi wa afya kwani uhaba huo, hata takwimu za kitaifa zinaonyesha miaka zaidi ya minne iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua hakuna Hospitali ya Wilaya; tumeanza kujenga *OPD* kwa kutumia fedha za ndani na nguvu za wananchi. Tumejenga jengo la ghorofa moja kubwa lenye vyumba muhimu vyote na sasa tuko kwenye hatua za mwisho. Serikali iko tayari kutoa fedha kusaidia kuongeza nguvu kwenye jengo hili ili likamilike na Hospitali ya Wilaya ianze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kaliua lenye kata 13 lina vituo vya afya viwili tu. Serikali mwaka wa jana ililetä barua Wilayani ya kutaka kila kata mbili ziandae maeneo ya kujenga vituo vya afya, maeneo hayo yameshaandaliwa. Ni

lini ujenzi wa vituo hivyo utaanza maana bajeti hii Waziri hajasoma lolote kuhusu mpango huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bima ya afya limehamasishwa na wananchi wengi wamejunga, tatizo kubwa ni pale wanapokwenda hospitali, vituo vyatya zahanati wanakosa dawa. Kwa nini Mfuko wa Bima ya Afya hauboreshwi sambamba na uwepo wa dawa zakutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sekta ya afya kutaka kuwa watoto *under five years*, wajawazito na wazee zaidi ya miaka 60 kupata huduma bure halijatekelezwa katika maeneo mengi sana. Wazee wakienda vituoni bila pesa hawapati huduma. Pamoja na Waziri/Serikali kutoa kauli hapa Bungeni mara ngapi mbona bado ni tatizo? Leo Mheshimiwa Waziri atoe kauli ambayo itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wanawake wengi na watoto wanapoteza maisha kwa kukosa huduma ya mama na mtoto. Kuwepo kwa zahanati chache, vituo vichache na kukosekana kwa *mobile clinic* ni chanzo cha kupoteza wanawake wengi na watoto bila hatia. Wilaya yangu ya Kaliua hakuna kabisa *mobile clinic* na hakuna gari la kupeleka chanjo kwenye maeneo ambayo hakuna vituo. Serikali inaokoaje maisha ya akina mama wa Kaliua kwa kupeleka gari moja tu katika Wilaya ya Kaliua na kwa kuzingatia kwamba jiografia ya eneo la Kaliua ni kubwa na mapori mengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana kwa wananchi kununua dawa zinazotembezwa barabarani na makampuni mbalimbali na kutibu magonjwa bila kufanyiwa vipimo wala kujua vipimo sahihi na mbaya zaidi wanakuwa hawana ujuzi wowote ni kama njugu. Je, Serikali inaliona tatizo hili? Bahati mbaya kuna nyinyine ni za kunywa/kumeza. Kwa nini Serikali inaruhusu biashara huria ya dawa kwenye mabasi, vilabuni, njiani na barabarani? Afya ya wananchi inalindwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizi Hospitali za *Mission* kama vile *KCMC* ambazo Serikali inawekeza nguvu ili wananchi wapate huduma kama hospitali ya Serikali, je, sera ya afya kwa makundi yale muhimu kupata huduma bora inatekelezwa kwenye hospitali hizi? Wapo watoto walopewa rufaa kwenda *KCMC* kupata matibabu walipofika kule wakaambiya *KCMC* si hospitali ya Serikali hivyo huduma zote ni kulipia. Serikali itoe ufanuzi kwa hospitali zote za aina hiyo

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Pili, nakupongeza wewe binafsi kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Afya ni kwamba kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu dhidi ya Wizara hii kutoka kwa wananchi. Wizara ya Afya ndio Wizara mama inayoratibu ustawi wa afya za watu nchi nzima, na la kukumbuka ni kwamba afya ndio mambo yote, pasipo afya mionganoni mwa wananchi hapana Taifa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko yapo zaidi juu ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba kama mashine za *x-ray*, vitanda na mambo mengine. Kutokana na upungufu wa mambo haya jamii inawaangalia zaidi Waziri na watendaji wake kwamba ndio wanaohusika kukidhi mambo haya ikiwemo upatikanaji wa madaktari, wauguzi na hata magari ya wagonjwa. Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wana nia nzuri juu ya ufanisi wa mambo haya ila wamekuwa wakikwamishwa na ukomo wa bajeti na kutokupatikana kwa kile pia ambacho kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ili kuliweka Taifa katika hali nzuri kiafya, Serikali isilifumbie macho suala la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Serikali izishughulikie changamoto hizi kwa kuipa upendeleo Wizara ya Afya kwa kuitengetea fungu la kutosha litakalokidhi upatikanaji wa vifaa, dawa na madaktari ili kukidhi huduma za afya za Watanzania.

Naishauri sana Serikali kutumia vyema kodi za wananchi kwa kuziondoa changamoto za huduma za afya katika ngazi zote ili kuondoa malalamiko ya wananchi ambao ndio msingi wa Taifa. Ni imani yangu kwamba Serikali baada ya maombi mengi ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali itatenga pesa za kutosha na kuzipeleka zinakohusika kwa wakati na kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba haya yanatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la haki za watoto. Watoto wana haki zao za msingi kutoka kwa wazazi, ndugu, jamaa na Serikali kwa ujumla. Usimamizi huu ni jukumu la Serikali na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Jukumu hili limekuwa ni kikwazo hususan kwa wazazi kukosa elimu au uelewa juu ya haki za mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na idadi kubwa ya watoto wanaokoseshwa haki zao za msingi kwa kukoseshwa elimu na badala yake kufanyishwa kazi zisizowahusu, watu wanafikiri kwamba ajira ya watoto ni sehemu ya maisha yao. Kuna idadi kubwa ya watoto chini ya umri wa miaka 18 wanaofanyishwa kazi za ndani wakikoseshwa elimu ambayo ndiyo wajibu wao kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali izidi kukemea masuala ya ajira za watoto hasa za kuajiriwa majumbani kwa kazi za mapishi, usafi na uangalizi wa watoto. Pia Serikali iweze kufanya sensa nchi nzima kuwatambua watoto wote wanaotumikishwa kinyume cha sheria na haki za mtoto na kuweza kudhibitiwa kwa wale wote wenye tabia ya kuwatumikisha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha Tanzania ina waathirika wa *HIV* 1,538,382. Watanzania tuko zaidi ya milioni 50, haya ni makisio ya hivi karibuni, je, ni utaratibu gani utumikao kuwapima watu na kupata takwimu za uhakika? Ni dhahiri kwamba idadi kubwa hajafikiwa ili kupata takwimu inayowiana na idadi ya Watanzania, hivyo

naishauri Serikali kuzidi kutoa elimu juu ya watu kuweza kupima kwa hiari ili kupata takwimu halisi za watu wanaoishi na *HIV*.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wa Singida ni miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na changamoto nyingi za afya kuanzia vijijini hadi manispaa. Kwa sasa kuna vituo vya afya 17 tu wakati tunatakiwa kuwa na vituo vya afya 117 ili kuhudumia wananchi wa kata 134 za Mkao wote wa Singida. Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatuelekeza kuwa na kituo cha afya kwa kila kata na zahanati kwa kila kijiji, hivyo hilo ni tatizo kubwa katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi waishio vijijini ambako kuna changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua katika kukabiliana na hali hii kuna vituo vya huduma za afya 69 ambavyo ujenzi wake uko kwenye hatua mbalimbali. Ninaomba Serikali iongeze nguvu kuhakikisha vinakamilika haraka ili tuokoe afya za wananchi wetu na kuendelea kujenga Taifa lenye watu wenye afya njema. Lakini nisisitize kwa Serikali kwamba ujenzi wa vituo hivyo uendane sambamba na uboreshaji wa usambazaji wa vifaa tiba pamoja na dawa muhimu kulingana na mahitaji, miundombinu, watumishi na maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la uhaba wa watumishi kwenye mkoa wangu wakiwemo Madaktari Bingwa hasa wale wa magonjwa ya akina mama ambapo Hospitali ya Rufaa ya Mkao peke yake inatakiwa kuwa na Madaktari Bingwa 32 lakini walipo ni watano tu kwa mkoa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wa Singida una upungufu wa watumishi wa afya wa kada mbalimbali 305. Hii ni idadi kubwa sana wakati vyuo vyetu vinazalisha wataalam kila mwaka. Ni kwa nini hawa wataalam

tusiwasambaze kwenye vituo vyetu vyenye ukosefu wa wataalam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuiomba sana Serikali yangu kuendelea kusimamia kwa haki na kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa kada ya afya ambaeo ni watu muhimu sana na wanafanya kazi kubwa sana na kwenye mazingira magumu. Watumishi wa afya wote wanaostahili kupandishwa madaraja na nyongeza za mishahara wapewe stahiki hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwenye mkoa wangu kuna watumishi ambaeo hawajapandishwa madaraja kwa muda mrefu ikiwemo sababu ya Serikali kufanya uhakiki. Zoezi hilo limekwisha hivyo Serikali itimize wajibu wake. Zoezi hilo la kupandisha madaraja na maboresho ya mishahara yaende sambamba na mazingira bora ya kufanya kazi kwa watumishi wa afya ambaeo wengi wao wa vijiji hawana makazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi hayana nyumba za watumishi, ofisi hazina hadhi, hivyo nina imani kubwa Mheshimiwa Ummy atauangalia Mkoa wa Singida ambaeo unapokea na kuhudumia wagonjwa wengi wakiwemo wanaopatwa na majanga kama ajali. Mkoa wetu unahitaji nyumba bora 1,072 lakini zilizopo ni 345 kwa mkoa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali kuangalia kwa umakini afya za wanawake na kutoa kipaumbele katika kupambana na ugonjwa hatari wa saratani ya kizazi na matiti ambaeo umekuwa tishio kubwa. Nashauri vianzishwe vitengo vya saratani kwenye Hospitali zote za Rufaa za Mkoa badala ya wagonjwa kujazana pale Taasisi ya *Ocean Road* ambayo ni ukweli kuwa imezidiwa sana. Umefika wakati sasa kuanza mikakati kabambe ya kudhibiti ugonjwa huo kuanzia ngazi za vijiji kwa kufanya upimaji na kampeni za uchunguzi wa mara kwa mara hasa maeneo ya vijiji ambako wagonjwa wengi hufika hospitalini

wakati ugonjwa ukiwa umekithiri sehemu kubwa ya mwili wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazindua kampeni yangu ya Kijana jitambue, wakati ni sasa ambayo ilitoa stadi za maisha kwa vijana kujitambua utu wao na mbinu za kujikwamua kiuchumi, tuliendesha pia zoezi la upimaji saratani ambapo wanawake wengi walipata fursa hiyo na wengine kubainika kuwa na tatizo hilo na kuelekezwa namna ya kupata huduma. Kwa hiyo, jambo hilo limejidhihirisha wazi kuwa wanawake wengi waliopo vijijini wameathirika na saratani ya shingo ya kizazi na matiti lakini wanakuwa hajajitambui kama wameathirika kutokana na kukosa huduma za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya Mtanzania ndicho kitu muhimu cha kwanza kabisa kwani kama hatutakuwa na afya njema basi maendeleo ya nchi yetu yatazorota na kuwa nyuma, hivyo, Serikali inapaswa kuendelea kutoa kipaumbele kikubwa katika mapato yake katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ili kupunguza vifo vyta akina mama na watoto ifike wakati sasa zahanati zetu na vituo vyta afya viwe na wataalam wa kutosha, vifaa tiba vyta kutosha na dawa za kutosha. Iwapo tutaimarisha huduma katika vituo vyta afya na zahanati zilizopo zitasaidia sana kupunguza vifo vyta akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ndiyo utajiri mkubwa kuliko utajiri wowote na hospitali, vituo vyta afya, zahanati hizi zote ndizo ambazo tunaweza kuzisema *garages* za binadamu. Lazima pawepo na vifaa vyta aina zote (*apparatus*) ili ziweze kuwarahisishia utendaji kazi madaktari

na wahudumu wetu wa afya (*nurses*) ambao kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za vituo vya afya; katika maeneo ya vijiji kuna kero ya kufunga vituo vya afya na zahanati saa 8:30 mchana, hili ni tatizo. Mfano katika Jimbo langu la Tanga Mjini, vituo vifuatavyo ni miongoni mwao; Kituo cha Afya Pande (Kiromoni), Kirare, Manungu, Chongoleani, Mabokweni, Tongoni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri/ombi langu ni kuwa hivi vituo vikifanya kazi *24 hours* kuna tatizo gani? Naishauri Serikali yangu sikiu iwatumie madaktari 258 waliokuwa waende kufanya kazi inchini Kenya wakati wa mgomo na ambao Mheshimiwa Rais Magufuli ameshatangaza kuwaajiri, tupatiwe madaktari 70 kati yao waende katika vituo vya afya na zahanati zetu za Jiji la Tanga pamoja na vitongoji na viunga vilivypo maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Tanga lilianzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Tanga ili kuweza kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mkoa ya Bombo. Halmashauri ilishaanzisha ujenzi wa *Administration Block* (Jengo la Utawala) kwa gharama ya shillingi milioni 400 katika mwaka 2013/2014. Kwa sasa mpango wa Halmashauri ya Tanga 2017/2018 tumetenga shillingi 300,000,000.00 ili kujenga jengo la *OPD (Out Patient Department)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu naiomba Serikali iunge mkono juhudzi za Jiji la Tanga kwa kuipatia fedha takribani bilioni 1.2 ili iweze kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa, *theatre*, sehemu za tiba ya macho, moyo, mifupa na kadhalika; lakini pia gari la wagonjwa (*ambulance*). Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tukifanikiwa kuikamilisha *Tanga District Hospital/tutasaidia kuboresha* afya za wananchi wa Jiji la Tanga na Watanzania lakini pia tutaipunguzia *Bombo Regional Hospital* msongamano wa wagonjwa wanaotoka Wilaya zote nane na Halmashauri tisa za Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za madaktari/wahudumu, naomba pia wahudumu (*nurses*) wengi wanaosoma katika Vituo vya Hospitali Teule za Tanga, Matc na Eckenforde *Nursing Training* waajiriwe katika hospitali yetu ya Wilaya tunayoitaraja pamoja na vituo vyetu vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la dawa *MSD, medicine supply chain* iwekwe wazi. Naomba kwa kuwa Jiji la Tanga tayari tunao mpango na utekelezaji wa Hospitali ya Wilaya, mgao wa dawa za *MSD* ungepelekwa katika zahanati na vituo vya afya vilivypopo (ama msaada au kwa kununua ili kupunguza upungufu wa dawa katika Jiji la Tanga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hospitali ya Mkoa ya *Bombo Hospital*, naiomba Serikali (Wizara) kuingilia Hospitali ya Mkoa wa Tanga (*Bombo Regional Hospital*) ambayo imepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa lakini haina hadhi hiyo kwa kuwa haina:-

- (i) Madaktari Bingwa wa kutosha;
- (ii) Vifaa tiba vya kutosha (*oxygen machine, x-ray, ultra sound, CT Scan*);
- (iii) *Intensive Care Unit* ina mapungufu mengi;
- (iv) Barabara za ndani za hospitali mbovu kupita kiasi;
- (v) *Lift* ya Bombo imekufa zaidi ya miezi 36 iliyopita (paundi 126,000 zinahitajika); na
- (vi) Gari za wagonjwa mbovu inayofanya kazi ni moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maombi yangu kwa Serikali (Wizara) ni kwamba Serikali iangalie kwa jicho la huruma Hospitali hii ya Mkoa ya Bombo kwa mapungufu yote kuanzia (i) – (vi) na namkumbusha Mheshimiwa Ummey (Waziri) kwamba *charity begins at home*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za ustawi wa jamii, ukurasa wa 57; nawazungumzia wale mavu wa akili. Serikali itenye fedha kila Halmashauri ili kuwepo kitengo cha

kuwatunza walemvu wa akili (vichaa) ili kuwapatia nguo, kuwakata nywele, kucha na kuwatibu kwa kufuatilia chanzo cha maradhi yao, kama ni matumizi ya dawa za kulevyta, mtindio wa akili na kadhalika, watibiwe kwa kuwa nao ni Watanzania wenzetu. Inatia aibu kuwaona vichaa watu wazima wanatembea uchi mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za watoto, wajawazito na wazee; naiomba Serikali iangalile katika eneo hili kwa sababu kuna maneno kuliko vitendo. Akina mama, wazee na watoto wanalipa, naomba Wizara itoe vifaa vya kujifungulia na dawa za wazee bure.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Mb), Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla (Mb), Naibu Waziri na ndugu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo ni pamoja na vituo vya wazee katika makambi; ni muhimu majengo yao yakarabatiwe, wazee wasiojeweza waingizwe kwenye mpango wa TASAFili kuipunguzia mzigo Serikali, kuwe na huduma ndogo za upatikanaji wa dawa kwenye maeneo ya makambi angalau duka dogo, kwani uwezo wa kufuata dawa kwenye zahanati ni mdogo, Wizara ishirikiane na TAMISEMI kuhakikisha wanajenga *x-reter* (kuhifadhi kondo la uzazi) kwenye zahanati na vituo vya afya ni tatizo kwani kwenye vituo hivyo wakazi wengi wanalamika kuwa mbwa wanachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyumba vya akina mama wanaokwenda kusubiria kujifungua vipewe kipaumbele kwa kutoa msisitizo, vifaa tiba kwa wazazi na watoto vipewe kipaumbele hasa *gloves*, dawa za kuzuia damu kutoka kwa wingi, kuwepo na wodi maalum ya kuwalaza wanawake wenye ugonjwa wa saratani mikoani na kupeleka dawa za kupunguza maumivu, elimu iendelee

kutolewa kwa ugonjwa wa fistula hususan zahanati na vituo vya afya, ugonjwa wa tezi dume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa ukarabati wa ujenzi wa wodi ya wanawake ya upasuaji katia Hospitali ya Bombo – Tanga, iko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake, waandae utaratibu na kupelekwa mikoa yote kwani si Dar es Salaam peke yake au mikoa mikubwa yenyé Majiji, hata Tabora tunao uwezo. Kwa kuwa mimi ni mwakilishi ambaye nilitoa shilingi 2,000,000 mpaka sasa sijaona faida yoyote, niombe maelezo ya hisa zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU D. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali yangu chini ya Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufulikwa jinsi anavyoismamia Serikali yake, nasema ahsante. Pia nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Ummy na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kusimamia vyema Wizara yao kikamilifu, nawapongeza sana, Mwenyezi Mungu awasadie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu huduma ya afya ya uzazi na watoto. Vifo vitokanavyo na uzazi bado vinaendelea japokuwa vimepungua lakini wajawazito wengine hawana elimu kutokana na umbali kutoka wanakoishi mpaka kwenye vituo vya afya. Kwa hiyo, naishauri Serikali wapatiwe huduma elekezi, japo wauguzi wa vituo mbalimbali wasogee vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wajawazito wengi wanapata operesheni, kwa nini iwe hivi? Watoto wengi sasa wanaozaliwa afya zao zinakuwa si nzuri. Aidha, wamekuwa wadogo sana au wamelegea. Mzazi anahangaika mpaka anachoka. Huduma wodini madaktari wanajitahidi sana, lakini wodi ndogo hazina ukarabati, vitanda vidogo, inafikia hatua kitanda kimoja wazazi watatu au wawili, hivi na magonjwa kila mtu na yake ukizingatia maambukizi ni mengi.

Kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye juhudhi zake ili ipanue wodi au ukarabati kwenye hospitali zetu zilizokwu zimechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Mwanza ambavyo ni asilimia 21 kitaifa. Idadi hii ni kubwa sana. Vifo vya uzazi kwa asilimia 37 hutokana na kutokwa damu nyingi wakati wa kujifungua, hivyo kama mama asipowahishwa hospitali hupoteza maisha, na hii husababishwa na vituo vya afya kuwa mbali. Vilevile asilimia 21 ya vifo vya wajawazito hutokana na kuchelewa kufanya maamuzi ya njia ya kujifungua hususan upasuaji wa kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza pia una upungufu wa vituo vya afya vinavyotoa huduma ya upasuaji. Hivyo, tunaiomba Serikali ituongezee vituo vya afya vyenye huduma za upasuaji hususan Wilaya za Ukerewe, Sengerema na Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Mfuko huu utengewe fedha ili kusaidia Halmashauri kuwakopesha akina mama kwa kujumuisha na asilimia tano ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa kufanya hivyo, akina mama watakuwa wamewezeshwa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri za Mkoa wa Mwanza ambazo zimefanikiwa kutenga na kupeleka fedha kwenye vikundi vya akina mama zikiwemo Halmashauri za Ilemela, Sengerema, Mwanza Jiji, Kwimba, Misungwi na Buchosa. Niiombe Wizara

husika kufuutilia Halmashauri ambazo hazikutoa fedha hizo kama vile Halmashauri za Ukerewe na Magu na kuzitaka Halmashauri hizo kupeleka fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la Benki ya Wanawake. Benki hii ilianzishwa ili kusaidia akina mama kukopesheka kwa riba nafuu, lakini benki hii haitengewi fedha za kutosha kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Ummy wakati akihutubia kwenye maadhimisho ya sita ya wanawake duniani 2016, kwamba Wizara itatenga shilingi bilioni mbili kila mwaka lakini katika mwaka huu imetengwa shilingi milioni 69 tu. Naiomba Serikali itenye fedha ya kutosha ili benki hii iweze kukopesha kwa riba ndogo ya asilimia 10 mpaka 12 na pia kuongeza matawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali iangalie suala la *CT scan* katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando kwani inategemewa na mikoa ya jirani kama Kagera na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mimba za utotoni; hizi pia zinachangia vifo vyta mama na mtoto. Niiombe Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Ndoa ili kusaidia watoto wanaolewa na umri mdogo na hivyo kupelekea mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa yote yaliyotekelezwa ndani ya kipindi hiki cha mwaka mmoja kupitia Wizara hii. Pili niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa utendaji wenu mahiri na jinsi mnavyojituma kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee *Mental Health Act 2008* sheria namba 28. Sheria hii ipo toka mwaka 2008 lakini mpaka leo ni miaka tisa kanuni hazijatungwa ama kuandaliwa. Kutokuwepo kwa kanuni kumesababisha sheria hii kutoanza kutumika na hivyo kupelekea wagonjwa wa akili

na walemavu wa akili kukosa haki zao za msingi. Naomba kufahamu, ni lini kanuni hizi zitaandalishi na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana? Pia kuna upungufu wa madakatari (kuna madaktari 15 tu nchi nzima).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee msamaha wa matibabu kwa wenyewe ulemavu. Wakati linajibiwa swali langu Bungeni, Serikali ilikiri kutokuwa na utaratibu wa kuwabaini watu wenyewe ulemavu wenyewe vipato duni hivyo kupelekeea Watanzania kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali ikubali kuwaingiza watu wenyewe ulemavu ambao wana vipato duni kwenye huu msamaha wa matibabu. Kwanza iwabaini kwa kuwapatia vitambulisho ili wanapofika hospitali pasiwe na usumbufu kwao. Nafahamu kuna mpango wa Serikali wa kuwapatia Watanzania wote bima ya afya. Naipongeza Serikali kwa mpango huu. Mpango huu ni *long term*, hivyo ninaiomba Serikali wakati tunasubiri ione ni jinsi gani itawaangalia watu wenyewe ulemavu kwa masuala mazima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee watoto wenyewe vichwa vikubwa. Kadi Toto Afya haiwakubali watoto wenyewe vichwa vikubwa, wanaambiwa wao ni wagonjwa, kadi hii kwa nini inawabagua watoto hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee upungufu wa dawa za walemavu wa akili. Ninaiomba Serikali iongeze bajeti ama itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa za akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watu wenyewe ualbino, limekuwa ni ombi la muda mrefu kuwa *sunscreen lotion* zinunuliwe ama ziagizwe na Serikali kama dawa zingine zinavyoagizwa ama kununuliwa. Ninaiomba Serikali yangu sikivu ilizingatie ombi kwani mafuta haya ni muhimu na ni kama chakula kwa wenzetu wenyewe ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna uhitaji mkubwa wa vifaa vya ku-*detect*kansa kwa hatua za awali (*Kliogan*). Vifaa hivi vitakuwa msaada mkubwa si tu kwa watu wenyewe ualbino bali kwa Watanzania wote maana kansa imekuwa tishio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa zoezi la ugawaji wa vifaa mbalimbali kwenye hospitali zetu vikiwemo vitanda. Katika vitanda hivi, je Serikali ilizingatia ombi letu la vitanda vya kujifungulia wanawake wenyewe ulemavu? Kama haikuzingatia kwa kweli wanawake wenyewe ulemavu tuna uhitaji mkubwa wa vitanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye hospitali zetu kuna uhitaji mkubwa wa wakalimali wa lugha ya alama kwa wagonjwa ambao ni viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kodi kwenye taulo za kike (*pads*), ninaiomba Serikali iondoe kodi kwenye taulo hizi kutokana na umuhimu wake na kulinganisha na vipato vya wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba ufanuzi wa hoja zangu wakati mtoa hoja anamalizia.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali yangu kwa jitihada inazoendelea kuzifanya katika kuboresha sekta ya afya nchini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utendaji wake mzuri uliotukuka kwa kuisimamia vizuri llani ya CCM. Nampongeza pia Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pamoja na Mawaziri wote wakishirikiana na watendaji, wanafanya na kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake Dkt. Hamisi Kigwangalla nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao katika Wizara hii, hongereni sana.

Hata hivyo Watanzania wengi zaidi ya nusu ya wakazi wote nchini wanaishi vijiji. Hivyo basi tunapoimarisha huduma za afya katika maeneo vijiji tutawanusuru maisha ya watu wengi ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuangali ikama ya watumishi wa sekta ya afya kwa lengo la kuondoa mlundikano wa madaktari na wahudumu wengine wa afya katika miji mikubwa na kuwapeleka maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zahanati ambazo zikijengewa uwezo kama vile wa vifaa, majengo na wataalam zitapunguza mlundikano katika hospitali za Wilaya na Mikoa. Moja ya zahanati hizo ni zahanati ya Ulanga iliyoko Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri binti yangu mchapakazi, mbunifu na msikivu, uje kuitembelea zahanati hii iliyoko Kalenga ambayo ipo katika hali mbaya sana. Uchakavu wa majengo, miundombinu kama nyumba za watumishi, hata chumba cha wazazi, inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwa kuipongeza tena Wizara kwa kazi kubwa ikiwemo kuikarabati Hospitali ya Mkoa wa Iringa na kuipandisha hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa, ila nashauri tena Wizara ikae na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kurahisisha upanuzi wa hospitali hiyo kwa kuondoa Gereza la Iringa Mjini katika eneo lilipo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara/Serikali kuangalia uwezekano wa kuziongezea fedha programu za *NACP/NBTS/NTLP* kwa kuwa ufadhili wa *PEPFAR/CDC*

umepungua sana. Serikali iangalie uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ofisi ijulikanayo kama mradi wa *NACP/NTLP Joint Office Project* iliyopo nyuma ya ofisi za *WHO*. Mradi huu ulisimama miaka mingi iliyopita kufuatia *Global Fund* kuacha kutoa fedha kwa ajili ya jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Mbinga tunaomba kuboreshewa huduma za upasuaji. Vilevile kwa kadri hali itakavyowezekana tunaomba hospitali hii ipatiwe chumba cha kuhifadhi maiti (*mortuary*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara iangalie uwezekano wa kukipandisha Kituo cha Afya cha Mapera ili kiweze kuhudumia kama Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga baada ya kuipandisha hadhi ili kuipunguzia mzigo Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kugawa vifaa tiba kwa kila Halmashauri. Ushauri wangu ni kwamba vifaa hivyo vigawiwe kupitia Mbunge kama ilivyofanyika kwenye mgao wa madawati ya chenji ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANGELINA S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha niwapongeze sana kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara hii kwa kushirikiana na Naibu Waziri na timu nzima ya wataalam. Mwenyezi Mungu aendeleee kuwabariki muendeleee kuwatumikia Watanzania. Vilevile nichukue fursa hii kutoa shukrani kwa mara nyingine kwa mgao wa gari la wagonjwa, hakika mlitusaidia kwa kiasi kikubwa sana kusaidia huduma ya mama na mtoto katika jimbo langu hususan Kituo cha Afya Sangabuya ambako gari lilipelekwa na Kituo cha Afya Karume linakotumika pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Manispaa ya ilemela haina Hospitali ya Wilaya mpaka sasa, kwa juhudhi za Halmashauri na kwa msaada wa Serikali Kuu jengo la wagonjwa wa nje tayari limepanuliwa. Tunaomba Wizara isaidie ukamilishaji wa hospitali hiyo ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando na Hospitali ya Mkao ya Sekou Toure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ina vituo vya afya vitatu tu kati ya 19 vinavyotakiwa. Pamoja na mapungufu hayo, vituo tulivyonavyo bado vina mapungufu mengi sana. Naomba Wizara yako katika majengo ya *theatre* yatakayo jengwa nchini walau kituo kimoja kipate, hasa kituo cha Buzuruga ambacho kina mapungufu mengi. Kwa kuainisha Kituo cha Afya Buzuruga, kinahudumia wagonjwa takribani 25,877 lakini hakina jengo la upasuaji, wodi ya wanaume wala wodi ya akina mama waliojifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Karume kinahudumia wagonjwa 25,654 lakini hakuna nyumba za watumishi pamoja na jengo la wagonjwa wa nje. Kituo cha Afya cha Sangabuye hakina nyumba za watumishi, hakuna wodi ya watoto, hakuna wodi ya wanaume. Tunaomba walau tupate jengo la wodi kwa wanaume na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika kada ya wateknolojia maabara, wateknolojia dawa, wahudumu wa afya pamoja na watunza kumbukumbu za afya.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Rombo hatuna Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo Kituo cha Afya cha Karume Usseri kinaandalishi kwa ajili hiyo. Hivi sasa majengo yote muhimu yapo tayari kasoro jengo la *OPD* ambalo ujenzi wake uko ngazi ya msingi. Ujenzi umesimama kwa sababu ya deni tunalodaiwa na mkandarasi. Tunaiomba Serikali kutusaidia kumalizia deni hilo na kutoa pesa ili kuharakisha ujenzi wa jengo hilo ili hospitali ipate kufunguliwa na hatimaye kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika wananchi wamejitahidi sana kujenga kwa kujitolea zahanati na vituo vya afya. Hata hivyo tunakabiliwa na matatizo mawili ambayo ni wataalamu, madaktari, wahudumu wengine wa afya pamoja na vitendea kazi. Tunaiomba Serikali katika mgao wa wahudumu na vitendea kazi itufikirie ili nguvu za wananchi walizojitolea katika kujenga ziwe na manufaa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Kituo cha Maendeleo ya Wananchi Mamtukuna. Chuo hiki ni muhimu sana lakini kunakwamishwa na matatizo ya uhaba wa wataalamu (wakufunzi), uchakavu wa majengo, maji pamoja na bajeti ndogo. Tunaiomba Serikali isikiache chuo hiki ikitengue fedha za kutosha walau kutatua kwa awamu matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumezuka mtindo wa kuwadhalilisha sana watoto wa kike na wa kiume. Baadhi wanaingiliwa, wanaolewa wakiwa na umri mdogo na kufanyishwa kazi ambazo haziendani na umri wao. Imefikia wakati Serikali ichukue hatua thabiti kuzuia mateso haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni ujenzi wa jengo kwa ajili ya *installation* ya mashine za kansa katika Hopitali ya *KCMC*. Hospitali pamoja na wafadhili wameshafanya kazi kubwa sana, gharama ya ujenzi wa jengo hilo ni karibu billioni sita. Kutokana na kuzidiwa kwa taasisi ya kansa *Ocean Road* na kutokana na wingi wa wagonjwa na mahitaji ya upimaji kwa wananchi, tunaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kusaidia ujenzi wa jengo hili.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ushetu lina vituo vya tiba 27 na linahudumia wananchi zaidi ya 300,000 kulingana na sensa ya mwaka 2012 na lina ukubwa kilometa za mraba 5,311. Kati ya vituo hivyo vya tiba kuna vituo vya afya vitatu vya Mbika, Ukune na Bulungwa. Kati ya vituo hivyo

vituo viwili vya Mbika-Ushetu na Bulungwa vina huduma ya upasuaji, vituo hivi vinahudumia watu wengi sana kwa kuwa watu wa Jimbo la Ushetu wanahudumiwa na Hospitali ya Wilaya ya Kahama ambayo imezidiwa sana kwani inahudumia Halmashauri nyingi ikiwemo Halmashauri za Ushetu, Ulyankulu, Kaliva, Uyui, Bukene, Mbogwe, Msalala na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niiombe Serikali ifikirie kupandisha Kituo cha Afya cha Mbika-Ushetu kuwa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ili kusaidia mzigoto mkubwa unaobebwa na Hospitali ya Wilaya ya Kahama. Hivyo kuanzishwa au kupandishwa hadhi kituo cha afya kutasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kupunguza vifo kutokana na wananchi kusafiri umbali mrefu kwenda Hospitali ya Wilaya kwa kata za Ushetu, Uyogo, Nyamilagano, Ulowa, Ubagwe pamoja na wananchi wa majimbo ya Kaliua, Ulyankulu, Uyui ambao hutibiwa Kahama Mjini kuititia maeneo ya Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaondoa dhana kwa wananchi kuona kwamba wametengwa. Vilevile itaboresha huduma za afya Jimboni Ushetu pamoja na kupunguza mrundikano katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itsaidie kupata *ambulance* ili kuokoa maisha ya wananchi wa Jimbo la Ushetu. Sisi kama Jimbo au Halmashauri tunajitahidi kujenga ili kupata zahanati nyingi katika harakati za kutekeleza sera ya kuwa na zahanati kila kijiji. Kwa sasa tunayo majengo 48 yanayoendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi na Halmashauri yao. Majengo hayo ni zahanati 44 na nyumba za watumishi nne. Tunaomba tusaidiwe gari ya kubeba wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gari ya chanjo, Halmashauri ya Ushetu haina gari ya chanjo, tunaiomba Serikali itsaidie gari ya chanjo katika Halmashauri ya Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mko hoja.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa maabara kwenye vituo vya afya iwe kipaumbele. Kwa Biharamulo *DMO* anatoa pesa mfukoni mwake kulipa watu watatu wenye vyeti vya taaluma ya maabara ambao wanafanya kazi kwa kujitolea. Watu hawa hawalipwi mshahara, wanalipwa posho na *DMO* kutoka kwenye mshahara wake. Naomba waingizwe kwenye ajira na wabakizwe pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *CHF* kwa wajawazito wa Wilaya ya Biharamulo, tutafikiwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PLH/V* na walemavu wajumuishwe kwenye asilimia kumi ya Halmashauri inayokwenda kwa vijana na wanawake. Haya ni makundi maalum zaidi, wakipata pesa hizi zitawasaidia kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kuweza kulipia *CHF*.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea. Katika sera ya zahanati kila kijiji/mtaa na kituo cha afya kila kata, pia hospitali ya wilaya na mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Mjini kwa asili ya mji ulivyo karibu kata nane za mjini zinategemea Hospitali ya Mkoa. Hivyo ninaiomba Serikali kuharakisha kuanza kazi kwa Hospitali ya Rufaa ili Hospitali ya Mkoa ihamie kwenye Hospitali inayojengwa sasa hivi na eneo/majengo ya Hospitali ya Mkoa yatumike kama Hospitali ya Wilaya, tutakuwa tumemaliza tatizo la Singida Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu damu salama, mpango huu ni mzuri sana na unasaidia sana wananchi hususan Singida Mjini. Changamoto inayojitokeza hapo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwamko mdogo kwa wananchi kuchangia damu; na

(ii) Halmashauri hazitengi bajeti kwa ajili ya zoezi hilo hususan Singida Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwezi Juni, 2016 hadi Februari, 2017 Halmashauri ya Manispaa ya Singida imekusanya *unit 12 tu out of 2300* za mkoa mzima. Hivyo tunaishi kwa kutegemea Wilaya nyingine au tunatumia damu isiyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye tathmini kwenye jambo hili. Pia Mganga Mkuu wa Mkoa awe na mamlaka ya kuisimamia Halmashauri katika kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za dawa, ninaishukuru sana Serikali kwa kutoa fedha Singida Mjini takribani shilingi 203,100,000 ambayo ni sawa na asilimia 93. Tatizo tunalolipata dawa hazionekani, nakosa majibu ya kuwaambia. Naiomba Serikali itusaidie kusimamia upatikanaji wa dawa.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda nichukue fursa hii niweze kuchangia mawazo yangu katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kabla sijakwenda moja kwa moja kwenye mada zangu naomba kwa heshima na dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa juhudzi zake mahsusni katika usimamizi na uendeshaji wa masuala ya afya ya Mtanzania, afya ya akina mama na watoto pamoja na afya ya ustawi wa jamii yetu hususani kwa rika la vijana na wazee pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya ya mzazi, Mheshimiwa Waziri pamoja na juhudzi zako za dhati katika kunusuru akina mama wanaojifungua lakini pia na watoto wachanga bado tunayo changamoto kubwa sana kwenye vifo vya akina mama wanapojifungua. Takwimu zinaonesha kwenye kila vizazi hai 100,000 tuna vifo 556 vya kina mama wanopoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu, sambamba na changamoto hii ya vifo vya akina mama wanaopoteza maisha pindi wanapojifungua lakini tunayo

changamoto kubwa ya vifaa tiba na miundombinu ya kitabibu kwa upande wa tiba za watoto wachanga. Ni kweli tuna vifo vingi nya kina mama pindi wanapojifungua lakini pia tuna vifo vingi nya watoto wadogo/wachanga kutokana na changamoto ya uwepo wa *PRE NATAL ICU (P)* kwa watoto under five years.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitendo kinachokatisha tamaa na *morale* ya matabibu walio wengi nchini Tanzania hususan katika Hospitali ya Muhimbili ambayo kimsingi wamekuwa na historia ya kazi nzuri ya kitabibu ya kuokoa maisha ya vichanga especially pale inapotokea *emergence* ya upasuaji kwa watoto wachanga. Wengi wa madaktari wamewahi kusema tumekuwa na kazi nzuri *theatres* lakini kazi zetu nyingi zinaharibikia kwenye vyumba tunapowalaza watoto wagonjwa ambao wamewahikufanyiwa upasuaji kwa kuwa vyumba nya *ICU* kama *PRE NATAL ICU* zimekuwa na msongamano mkubwa wa watoto kwa kuwa katika Hospitali za Mikoa, Wilaya na Halmashauri hatuna huduma za vyumba nya watoto za *PRE NATAL ICU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wangu kwa Serikali yangu kuwa Wizara hii iweze kuongezewa fungu la uboreshaji wa miundombinu ili hospitali zetu ngazi za Mikoa na Wilaya ziweze kupata wodi za *PRE NATAL ICU* ili kunusuru vifo nya watoto wachanga. Sambamba na hili pia niombe Serikali yangu iangalie kwa jicho la kipekee kabisa vifo nya kina mama wanaopoteza maisha pindi wanapojifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa ya afya ya akina mama especially case ya *cancerya shingo* ya kizazi. Ni rai yangu kwa Serikali kuititia taasisi za tafiti za afya ya binadamu tuweze kufanya utafiti wa kina ili kubaini nini changamoto tulizonazo kwenye mfumo mzima wa afya ya mama na msichana ambayo inasabisha ongezeko la ugonjwa wa *cancerya shingo* ya kizazi. *Sanitary towels* zote zinazosambazwa kwa umma wa Watanzania zifanyiwe utafiti wa kina, jamii zenye mila za kutotahiri wanaume nazo zifanyiwe tafiti za kina ili kubaini kwa nini ongezeko kubwa la *cancer* ya kizazi. Ikiwa *HPV Vaccine* ndiyo jawabu la kinga

ya maambukizi basi Serikali yangu ije na majibu kwa umma wa Watanzania ili tupate suluhihisho la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasichana waliopo kwenye umri mdogo wanapoteza maisha kwa kasi isiyokubalika, tuiombe Wizara itusaidie kuja na suluhihisho la kudumu kwenye suala zima la ongezeko la *cervical cancer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *HIV & AIDS*, ni kweli tunayo changamoto kubwa ya tiba na vifaa tiba pamoja na mifumo ya uendeshaji tiba kwa watu wenye maambukizi ya *VVU*. Kupitia *data* ya *USAID* Novemba, 2016 Serikali ya Tanzania imekuwa ikichangia kwenye tiba ya *HIV & AIDS* kwa asilimia tatu tu ikilinganishwa na michango ya nchi wahisani kama mathalani USA ambayo imekuwa ikichangia takribani asilimia 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto ya utegemezi mkubwa kwenye dawa za *ARV* kutokana na kwamba mifumo ya TEHAMA ambapo asilimia 100 ya mifumo ya kitabibu imetengenezwa na kufadhiliwa na Wamarekani. Naona shida kuona hata masuala ya mifumo ya uendeshaji wa tiba ya wagonjwa walioathirika *CTC2(Care & Treatment Clinic)* ambayo mfumo huu unatumika katika kuhifadhi kumbukumbu za wagonjwa wote walio na maambukizi ya *VVU*, *DI+IS* 2. Mfumo huu nao unatumika kuhifadhi kumbukumbu za wagonjwa; kwa kitaalam mfumo huu unatambulika kama *District Health Information System* ambao nao unafadhiliwa na Wamarekani kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata taabu sana kuona tunashindwa kuendana na *principle ethics* za namna ya kuhifadhi ama kutunza usiri wa wagonjwa hawa ikiwa mifumo hii itaachiwa mashirika ya nje waitengeneze na kuifadhili. Je, nini nafasi yetu kama nchi katika kulinda *privacy* za wananchi wetu wenye maambukizi ya *VVU*? Ni dhahiri kabisa kwa utendaji huu hatuna *assurance* ya *sustainability* ya mifumo hii na hata tiba za dawa ikiwa Tanzania itakubali kusimama kama mtizamaji. *Three percent of contribution as a country is too peanut for us to stay safe.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba ione sababu za msingi katika kutumia rasilimali ya Tanzania kwa ajili ya kuunda mifumo ya kitabibu. Ndani ya DIT (*Dar es Salaam Institute of Technology*) tunao vijana wazuri wenye umahiri mkubwa katika kuunda *software* kama *software developers* na vijana hawa wana utaalam na uzoefu wa kutosha kwenye masuala ya *programming*, tuwape nafasi vijana wetu wa Kitanzania kwenye ushiriki mzima wa masuala ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono juhudzi za Serikali kuitia wasilisho la hotuba hii muhimu kwa ustawi mzima na afya ya kina mama na watoto. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa hongera sana kwa kazi nzuri sana wanayoifanya chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri Ummy naomba kukumbushia vitanda vitano na magodoro yake, ahadi uliyoniahidi na mimi nikaenda kutoa ahadi ya vitanda vitano, magodoro na mashuka yake katika Kituo cha Afya cha Malya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi hiyo imekuwa ya siku nyingi, naonekana muongo kwa sababu ya kutotekeleza ahadi iliyopitia kwangu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Mimi naheshimika kwa kutosema uongo kwa wananchi wangu ambao nawaamini na wao wananiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba utekelezwaji wa ahadi hiyo ya vitanda vitano katika Kituo cha Afya cha Malya, Jimbo la Sumve. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yaliyo mbele yenu.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mweleyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuongeza watendaji kazi wa maendeleo ya jamii ili kutoa ushauri kwa

jamii kuacha tabia za wanandoa kutengana na kusababisha malezi ya watoto kuwa shida, hali inayosababisha kuwepo watoto wengi wa mtaani. Tatizo la watoto hawa linapelekea kuwepo kwa watoto wanaozaa kabla ya wakati jambo ambalo linaendelea kuzalisha watoto wa mtaani. Nashauri Serikali ili kupunguza ongezeko la kasi la watu wanaolitegemea taifa moja kwa moja lioneze watoa elimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuzungumzia juu ya uhaba wa dawa za kutibu na kuzuia magonjwa nyemelezi ya watu walioathirika na UKIMWI ambayo yanababisha vifo vingi. Nishauri hospitali kugawa dawa za kufubaa na ziambatane na dawa za magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kushauri kwamba vitendea kazi viongezwe katika hospitali, katika maeneo mengine hawana vifaa vya kuhifadhiwa watoto njiti. Niishauri Serikali kuweka zahanati kila kata ili kurahisisha ufikaji wa wagonjwa kwenye huduma. Pia niishauri Serikali kuhakikisha inaongeza dawa ya kuwezesha kupima UKIMWI kwani mara nyangi zimekuwa adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba matengenezo katika Chuo cha Maendeleo Kibaha na Shirika la Elimu *FDC* ili kuweza kutekeleza malengo ya kuanzhishwa kwake. Majengo yamechakaa sana na hakuna majiko, wanapika kwenye majiko yaliyochakaa na finyu, pia yanahatarisha afya za wapishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kukiangalia kwani kilikuwa kinatoa wahitimu ambao wanasaadia sana kuleta mabadiliko kwa jamii. Niombe *mortuary* ya Kibaha iongezwe kwani ajali zote zinapotokea Morogoro majeruhi na maiti huletwa Tumbi Kibaha pia tuongezewe na dawa.

**MHE. LUCIA M. MLLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja hii ya afya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na maendeleo ya jinsia. Kwa kuwa Benki ya Wanawake iko katika maeneo machache, naiomba Wizara kuhakikisha kuwa Benki ya Wanawake inakwenda katika mikoa yote na kwa namna ya pekee naomba benki hii ianzishwe katika Mkoa wa Njombe kwenye Wilaya hata tatu za Makete, Njombe na Ludewa kwa kuwa benki hii itawanufaisha wanawake wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia, kumekuwa na matendo yaliyokithiri ya unyanyasaji wa wanawake kwa kupigwa na waume zao katika familia nyangi. Naiomba Serikali isimamie sheria hiyo. Pia kumekuwa na ukatili dhidi ya watoto na hasa watoto wa kike ambapo wamekuwa wakibakwa na hasa katika Mkoa wa Njombe. Naomba Wizara ishughulikie suala hili na kuhakikisha ukatili huo unatokomezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za ustawii wa jamii, kwa kuwa kumeendelea kuwa na wimbi kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi Serikali isaidiane na wadau mbalimbali wanaojitolea kuwahudumia watoto hao kwa kuwawekea mazingira wezeshi ya kutoa huduma bila kuwakatisha tamaa kwa kuwatoza kodi wakati wanatoa huduma kwa watoto hao. Kwa mfano vituo vya watoto yatima visitozwe kodi yoyote. Pia wanapokuwa na vyombo vya usafiri wasitozwe mapato, pia vituo hivyo vimekuwa vikiomba leseni pamoja na kuwa vigezo vyote lakini wamekuwa hawapewi leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba Serikali ikague vituo vyote nchini ambavyo vinakidhi vigezo wapewe leseni. Pia vituo vinavyofanya kazi vizuri basi wapewe motisha kwa kupata ruzuku. Hivyo naomba bajeti ya Wizara iongezwe ili kitengo hiki cha ustawii wa jamii kifanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya ya mama na mtoto; vifo vya akina mama wanaojifungua 556 kwa kila vizazi 100,000 ni idadi kubwa sana. Naiomba Wizara kufuatilia kwa ukaribu tatizo hilo na kuendelea kubaini vyanzo vya vifo hivyo na kutatua changamoto zinazogundulika kuwa ndivyo

visababishi. Mfano katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, Hospitali ya Kibena ambayo ni Hospitali ya Mkao ya muda watoto wanaozaliwa njiti ni wengi lakini kutokana na kutokuwa na vifaa vya kuwatunzia watoto hao, wanapoteza maisha. Pia hawana *x-ray*. Naiomba Serikali itusaidie Wanajombe kuboresha Hospitali ya Kibena ili kuwaokoa wanawake wanaojifungua watoto na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la UKIMWI; watu wanaoishi na VVU wana changamoto kubwa za kupata *septrin* ambazo zingewasaidia sana kutopata magonjwa nyemelezi na watu hawana fedha za kununua dawa hizo. Naiomba Serikali kuwakatia bima za afya ili kunusuru maisha yao. Maana wakiwa na bima ya afya wanaweza kutibiwa bila matatizo na hivyo itasaidia kurefusha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali kufuatilia suala la mila potofu zinazosababisha UKIMWI uendelee kwa kasi katika Mkao wa Njombe. Tatizo ni kurithi wajane na mikutano ya mapangoni ambako wanajamiiiana bila kujali kama ni ngono salama au laa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iboreshe maslahi ya wafanyakazi kama *call allowance* na posho nytingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii muhimu na adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima. Nikushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuniruhusu na mimi nichangie ingawa kwa ufupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano ya UKIMWI pamoja na kuendelea ndani ya nchi yetu lakini inaonekana bado UKIMWI unaongezeka pamoja na maambukizi mapya. Kama juhudzi za makusudi hazitochukuliwa basi Taifa letu litafika pabaya sana. Kwa hivi sasa UKIMWI umekuwa uko sirini sana kiasi ambacho watu wengi wamekuwa na

matumaini makubwa kwamba UKIMWI umepungua kwa style za watu zilivyo. Watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI si rahisi kuwatambua kama hajajieleza mwenyewe. Hii inatokana na kuitikia wito wa kujunga na vituo vya dawa za ARV, kwa hiyo watu wengi kwa kupungua athari za kuonekana moja kwa moja wanadhani kuwa UKIMWI umepungua.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba mkakati na juhudzi endelee kuelimisha Watanzania kwamba UKIMWI upo na bado unaua. Wataalam wa UKIMWI wametoa taarifa kwamba Mkoa wa Njombe unaongoza kwa UKIMWI ambao una asilimia 14.8, hii ni asilimia kubwa na ya kutisha. Naomba Serikali ifanye utafiti ni jambo gani linalosababisha maambukizi makubwa kiasi hiki katika mkoa huu. Tatizo lijulikane na itolewe elimu ya uhakika ili kuondoa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia suala la wazee. Tunafahamu fika kwamba wazee wa sasa ndio vijana wa juzi na wa jana ambao walijituma kwa utumishi uliotukuka na mafanikio ya utumishi wao mwema ndio uliolifikisha Taifa letu hapa lilipo. Hivyo nashauri Serikali kutowasahau na kuwadharau wazee ambao ndio waliokuwa dira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba wazee hawapati huduma inavyopaswa na badala yake wazee wanaonekana kama hawakuwa na mchango wowote katika Taifa hili. Kwa mfano katika huduma za matibabu wazee wamekuwa wakisumbuka kana kwamba hawastahili kupatiwa huduma hii, wamekuwa wakitozwa malipo makubwa ambayo hawamudu lakini ni haki ambayo imeidhinishwa na Serikali kupatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuliwekea kipaumbele suala la kuwajali wazee kwa kufuatilia huduma zinazostahiki kwao Serikali ina nia na dhamira thabiti juu ya wazee inaonekana changamoto hii inayowakumba ni utendaji mbovu usiojali mchango wa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia hoja yangu napenda kugusia angalau kidogo suala la mazoezi ya viungo kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazoezi ni jambo muhimu sana kwa afya ya mwanadamu na michezo ni sehemu ya mazoezi. Kwa hiyo, michezo ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi na hasa katika kuimarisha miili yetu kiafya na kuwa wakakamavu. Sasa hivi nchi yetu imekumbwa na magonjwa mengi sana ambayo kama tungkuwa makini tusingeathiriwa sana na magonjwa haya, mfano wa magonjwa hayo ni kama vile kisukari, moyo na kadhalika. Magonjwa haya kwa ujumla wake yanaitwa magonjwa sugu na yanayogharimu fedha nyingi za wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali na Wizara ya Afya kuhamasisha jamii na suala zima la kufanya mazoezi na kutoa misaada pale inapobidi ili kuendeleza mazoezi.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Ili mtu aweze kuendelea ni lazima kwanza awe na afya bora. Hivyo basi, sekta ya afya ni muhimu sana kuhakikisha Serikali inatenga bajeti ya kutosha. Je, ni lini Serikali itatimiza Azimio la Abuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa *None Communicable Diseases(NCD)*: magonjwa haya kama sukari ya kupanda na kushuka, shinikizo la damu ya kupanda na kushuka, magonjwa ya moyo na kadhalika, mengi ya magonjwa hapa yanayoweza kuepukika tu kama elimu ya kutosha inaweza kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, siku hizi imekuwa ni kawaida watu kununua vyakula vya barabaran kama chips, mihogo, sambusa na *juice* zenye sukari nyingi, unywaji wa pombe na ulaji wa nyama nyekundu kupita kiasi, vitu vyote hivi vinachangia kuongezeka kwa magonjwa haya, hata watoto wadogo mpaka wenye miaka 10 wanapata magonjwa haya. Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza au kutokomeza magonjwa haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano nchi za Ulaya sasa hivi wanahimiza watu kufanya mazoezi, wanashauri wafanyakazi kutembea kwenda kazini, lakini hapa kwetu ni vigumu sababu barabara zetu siyo rafiki kwa matembezi ya miguu. Ni kwa nini Wizara ya Afya isishirikiane na Wizara ya Miundombinu ili wakijenga barabara wahakikishe wanajenga barabara za wapita kwa miguu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ndoa za utotoni na mimba za utotoni. Ni wakati muafaka sasa kuhakikisha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inarekebishwe ili isiruhusu watoto wa kike kuolewa wakiwa na miaka 14, tukumbuke wasichana hawa wakipata mimba utotoni mara nydingi wakati wa kujifungua huchukua muda mrefu sababu uchungu huchukua muda mrefu na hali hii huweza kusababisha kifo cha mama au mtoto au wote wawili kama matibabu ya dharura ya upasuaji kwa ajili ya uzazi hayatafanyika na ukizingatia vijijini huduma hizi sehemu nydingi hazipo na umbali wa kutoka kijijini mpaka Wilayani miundombinu ni mibovu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa pia hukosa fursa ya elimu kwa kuwa wengi wao hufukuzwa shule, wazazi husita kuwaendeleza na hii hupelekea baadhi ya watoto hawa wa kike kufungua mlango wa kuingia katika umaskini na kuzaa ovyo bila mpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa zaidi wengi hupata fistula (*vescovaginal fistula (VVF)* au *rectovagina fistula (RUF)*), hii husababisha msichana kutokwa na haja ndogo au kubwa bila kujizuia. Haja kubwa pia inaweza kumtoka msichana kwa kuititia tupu ya mbele na hii kuharibu sana afya ya mwili na hisia za msichana. Hayo ni machache tu katika ya matatizo ya mimba za utotoni, ni imani yangu Serikali itayaona haya na kuleta marekebisho ya sheria mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vifaa tiba na madawa. Hospitali nydingi hazina vifaa vya akina mama vya kujifungulia, hata baadhi ya hospitali hazina madawa. Mfano, tarehe 28 Februari, 2017 kulikuwa na mashindano ya

*Kilimanjaro Marathon* na pale uwanjani kulikuwa na kitengo cha huduma ya kwanza, jambo la kusikitisha pale kwenye huduma ya kwanza hawakuwa na mtungi wa kuongeza hewa (*oxygen*). alikuwa na kijana aliyekimbia na alikuwa mahututi na alihitaji *oxygen* lakini wahudumu wale hawakuwa na mtungi wa *oxygenna* kibaya zaidi *ambulance* ilivyofika na wao pia hawakuwa na *oxygen cylinder* na kupelekea kijana yule kufariki pale uwanjani. Mungu alilaze roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama magari yote ya kuokoa yangekuwepo na vifaa vyote, pengine kijana yule angeweza kupona. Je, katika bajeti hii ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya vifaa hivi hata *MRI* kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya *KCMC*? Kipimo hiki ni muhimu sana kwa Hospitali ya Rufaa kutokuwa nacho unakuta wagonjwa wanaagiziwa kwenda kwenye hospitali za binafsi kufanya vipimo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Hospitali ya *KCMC* kwa kuanzisha kitengo cha saratani kama ilivyo *Ocean Road*, ni vizuri kitengo hiki kianzishwe Mwanza na Mbeya. Serikali iwasaidie kwa kupeleka wataalam, vifaa tiba na ruzuku kwa ajili ya kitengo cha kansa kule *KCMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 500 hazitoshi zinahitajika shilingi bilioni saba za kujenga jengo la kuweka vifaa walivyovipata vyta msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na ongezeko kubwa sana la kansa ya shingo ya kizazi, tumelepoteza akina mama wengi lakini ugonjwa huu unaweza kuepukika kama ukigundulika mapema, lakini huduma ya kansa ya kizazi sio hospitali zote zinatoa huduma hapa nchini na kupelekea vifo vingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hizi hata mpaka kwenye ngazi ya vituo vyta afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maambukizi ya *UKIMWI* yapo juu sana, lakini kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa

kondomu za kike, je, Serikali ina mpango gani ili tuokoe watoto wa kike?

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kipekee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo mahali hapa. Vilevile ninamshukuru Mungu kwa kunipa nguvu na nafasi hii na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo inagusa moja kwa moja maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mawaziri pamoja na wataalam wao kwa kuandaa bajeti nzuri yenye kukidhi mahitaji na kutatua kero zilizopo katika sekta nzima ya afya. Bajeti hii inatekeleza llani ya chama tawala, Chama cha Mapinduzi. Katika misingi hiyo llani yetu imezungumzia utekelezaji wa sekta ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa juhudzi zake za dhati kabisa katika kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kila eneo la nchi yetu, pia kuhakikisha maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto yanazingatiwa kwa mujibu wa sheria zetu na taratibu zilizopo. Kwenye kila jambo lolote la kimaendeleo halikosi changamoto na changamoto hizo yatupasa Serikali kuzichukua kama fursa katika kuhakikisha zinatatuliwa na kuboresha huduma kwa manufaa ya wananchi wetu. Bado tumekuwa na matatizo ya upungufu wa wahudumu wa afya katika zahanati zetu hasa maeneo ya vijijini. Mapungufu haya yamekuwa yakileta kero kwa wananchi wetu kwa kukosa huduma kwa wakati. Kumekuwa pia na upungufu wa madaktari ilhalil tunao madaktari wengi waliomaliza vyuo na kufaulu vizuri lakini hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iajiri watumishi hawa kwa wingi ili waende katika maeneo mbalimbali kuhudumia wananchi. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwapa ajira madaktari takribani 250 ingawa Wizara hii imesema haina fedha za kuwalipa mishahara, lakini Rais kafanya uthubutu ili wataalam hawa waende kuwashudumia

wananchi. Naishauri Wizara kuchukua hatua madhubuti na kutafuta vyanzo vya fedha ili iweze kuajiri wataalam wa afya wengine. Kufanya hivyo kutasaidia sana kumaliza tatiozo hili la muda mrefu la upungufu wa wataalam hawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa na hilo, Wizara iweke mkakati wa kujenga nyumba za wataalam wa afya hasa vijjini, mfano katika Jimbo langu la Kibaha Vijjini tuna changamoto kubwa sana ya uhaba wa nyumba za watumishi wa afya na imekuwa kawaida kwa watumishi hawa wakipangiwa kuja katika maeneo ya kwetu, hufika kuripoti na punde wakigundua mazingira siyo rafiki, kwa maana hakuna nyumba basi huondoka kwa kusema wanaenda kuhamisha vitu watarudi, lakini hawatokei tena. Hali hii inarudisha nyuma juhudhi tunazochukua kama viongozi katika kujitolea huku Serikali ikilalamika kila siku haina fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya vijjini ndiyo kumeonekana kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa nyumba, nafikiri watumishi hawa wanastahili kabisa kukaa sehemu nzuri, Wizara lazima iwe na mkakati wa kujenga nyumba za watumishi hawa wa afya ili kwao iwe motisha na kutoa huduma kwa mazingira yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninaishauri Serikali ihakikishe inaongeza kujenga vituo vya afya ili kuepusha wananchi kutembea umbali mrefu kufuata vituo hivyo vya afya, kwani vimeduwa vikisababisha vifo vya watoto wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Jimboni kwangu Kibaha Vijjini tumetenga kabisa maeneo ya kujenga vituo hivi, hivyo katika bajeti hii naomba Wizara kuititia Serikali kumaliza changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto kuzagaa mitaani nimelisema sana humu Bungeni katika nyakati tofauti na changamoto hii bado ipo. Wizara hii ndiyo wahusika wakuu wa kuchukua hatua na kuhakikisha watoto wote wanakuwa katika vituo maalum siyo kuzagaa mitaani

kuomba omba. Hata hivyo naishauri Serikali kuwachukulia hatua baadhi ya wazazi wa watoto hawa ambao wao ndio wamekuwa wakiyatuma kwenda kuomba na wao wazazi kukaa pembedi. Ni jambo la aibu sana kwa nchi yetu kwani mambo haya yameshapitwa na wakati katika dunia ya leo.

Napenda kugusia pia suala la wazee, natambua uwepo wa vituo vya wazee maeneo mbalimbali hapa nchini, vituo hivi vimeduwa havitengewi bajeti ya kutosha na Serikali na zaidi vituo hivi vimeduwa vikitegemea misaada kutoka kwa jamii. Nafikiri ni wakati sasa Serikali ikachukua hatua kwa kutenga fedha mahsusini kwa ajili ya vituo vyote vya kulelea watoto na wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu zote nilizokuwepo humu Bungeni, nimekuwa nikilisemea hili la Kituo cha Afya Mlandizi kupandishwa hadhi, sifa na vigezo tunavyo, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Awamu hii ya Tano walitoa ahadi ya kukipandisha hadhi kituo hiki na kuwa hospitali, Iakini Awamu ya Nne imepita bila kituo hiki kupandishwa hadhi, sasa tuko Awamu ya Tano naombi ahadi hii itekelezwe, kwani Mheshimiwa Rais akitoa ahadi kinachofuata ni utekelezaji kwa mamlaka husika. Hivyo mimi na wananchi wangu tunashukuru sana katika bajeti hii maombi yetu ya muda mrefu na ahadi za Marais wawili zikitekelezwa.

Mimi kama Mbunge najitahidi sana kujitoa kwa hali na mali katika kuhakikisha majengo na vifaa mbalimbali vinapatikana katika vituo vyetu vya afya, kama sasa kuna ujenzi wa ukuta kwa maana uzio katika kituo cha afya Mlandizi na hizi ni juhudhi zangu kama Mbunge, hivyo Serikali ikituunga mkono katika mambo mazuri kama haya basi na sisi viongozi pamoja na wananchi tunafarijika sana na kupata moyo wa kuzidi kujitolea.

Hata hivyo nimeona bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 251 mwaka 2016/2017, ni jambo jema na la kupongezwa ila rai yangu kwa Serikali ni mamlaka husika

kumekuwa na changamoto za upungufu wa dawa katika vituo vyetu vya afya, zaidi dawa kuchelewa kufika kwa wakati. Naamini kwa ongezeko la bajeti basi changamoto hizo hazitakuwepo tena na kuleta nafuu kwa wananchi kupata dawa kwa wakati na kuwaondolea usumbufu wa kukosa dawa pindi wanapoandikiwa dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii, kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa uwajibikaji wao mzuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ukosefu wa magari ya wagonjwa katika Jimbo langu la Kwela na hasa kituo cha afya Mlepa, kituo ambacho kiko mbali na huduma na kiko katika mazingira magumu na kinaongoza kwa vifo vya akina mama wajawazito na watoto. Naomba kujua kwa nini Serikali haitaki kupeleka gari, kuna nini? Tunajua wazi yapo maeneo yanagawiwa magari karibu vituo vyote vya afya walivyonavyo. Mheshimiwa Waziri mnatumia vigezo gani? Nimesema tatizo la gari katika kituo hiki toka mwaka 2012 bado sijafanikiwa.

Naomba nijibiwe hii siyo haki, baadae natarajia, kutoa idadi ya vifo vya akina mama na watoto waliopoteza maisha yao kwa kungojelea gari la wagonjwa hadi kufa kwa kukosa msaada wa gari la wagonjwa.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimwa Mwenyekiti, llani ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wake 2010-2015 ilisema ujenzi wa zahanati katika vijiji na kata ili kuokoa vifo vya akina mama. Sera ya afya ni ya Wizara ingawa mtekelezaji ni TAMISEMI, lakini wananchi wanaitazama Wizara ndiyo inaona haitekelezi ili kumuokoa mama na watoto katika vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya zahanati hizo yapo katika vijiji na kata lakini yapo magofu bila ya Serikali

kuyamaliza. Je, Serikali hilo mmeliona maana tulitegemea mwaka 2015 -2020 yawe tayari yanafanyakazi ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Saratani inashindwa kufanya kazi zake kwani kipimo cha upimaji wa saratani ya matiti kimeharibika toka mwaka 2008 na akina mama wanapata taabu, inabidi kwenda vituo vya nje kwa matibabu. Hivi sasa Tanzania imekumbwa na kansa mbalimbali; kuna saratani ya matiti, ya shingo ya kizazi kwa wanawake. Pia kuna saratani ya tezi dume kwa wanaume limekuwa tatizo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Waziri ninaomba utoe elimu ya kinga badala ya tiba na pia elimu ya kutumia chakula gani ili kujinurusu na saratani, elimu ndiyo itamsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iendelee kuhamasisha kufanya mazoezi Watanzania kwani Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan anahimiza mazoezi kwa kila Mkoa katika wiki ya mwisho ya mwezi kwa siku ya Jumamosi, maana mazoezi ni afya. Ingawa Mheshimiwa Waziri Ummy anajitahidi kuhamasisha Watanzania lakini binadamu ni mzito. Hata sisi baadhi yetu Wabunge endeleeni kutuhamasisha kwa kufanya mazoezi kwa baadhi yetu tayari tunasumbuliwa na *pressure* pamoja na sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watoto njiti. *Nursing* ya watoto njiti ni mtihani kwani hakuna uangalifu na watoto wanafariki kwa kukosa matunzo. Vifo vya akina mama, vifo vya watoto hivi sasa katika akina mama 100,000 basi kuna akina mama 430 hadi 556 hufu kwa uzazi kwa kukosa huduma. Ninajua Waziri wa Afya ni mwanamke na ninajua atachukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kukosa *theatre* kwa ajili ya akina mama kujifungulia kwani mama anatakiwa kuwa karibu na sehemu ya kujifungulia. Ingawa Wizara yako ilitakiwa kutekeleza; je, suala hilo limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namkupongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi wa mambo mbalimbali ya sekta ya afya. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa vituo vya afya ni muhimu sana hasa katika maeneo ya vijiji ambako wananchi wengi wapo, vituo vya afya lazima viwe na wataalam wa kutosha na viwe na daktari msaidizi, wauguzi wa kutosha na wakunga wa kutosha. Madaktari wasaidizi wanasaidia sana kufanya *operation* hasa kwa akina mama wajawazito ambao hushindwa kujifungua, wakunga pia ni muhimu sana kwa ajili ya kuzalisha akina mama wajawazito. Akina mama wengi hupoteza maisha kwa kushindwa kujifungua kama vituo vya afya hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Bima ya Afya ya Taifa (*NHIF*) huduma za Bima ya Afya itakuwa na maana kila kituo cha kutolea huduma kama vile zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya na Mikoa kama vituo hivyo vitakuwa na dawa na vifaa tiba vya kutosha badala ya wanachama wa bima ya afya wataambiwa wanunue dawa katika maduka binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bohari ya Dawa (*MSD*); kwanza ninaipongeza sana Bohari ya Dawa (*MSD*) kwa kazi nzuri sana ya kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolewa huduma za afya, changamoto kubwa katika taasisi hii ni kutokopewa fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba ili kusambaza katika vituo vyote vya kutolewa huduma za afya. Ushauri wangu ni kwamba *MSD* watengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Afya ni muhimu sana hasa katika kusimamia afya ya mazingira na kuzuia

magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu (*cholera*), magonjwa ya kuharisha (*dysentery*), *typhoid fever* na kadhalika. Ipo haja ya kuimarisha Idara ya Afya Kinga (*Preventive Services*).

Maafisa wa Afya wakitekeleza majukumu yao vizuri hata magonjwa ya kuambukiza yatazungua. Naomba maelezo kwa nini Maafisa Afya wanahamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira? Maafisa wa Afya ni watumishi halali wa Wizara ya Afya na wamesomeshwa na Wizara ya Afya, kwa nini sasa wahamishiwe Ofisi ya Makamu wa Rais -Idara ya Mazingira? Nashauri Maafisa Afya wote warudishwe Wizara ya Afya - Idara ya Kinga na kusambazwa katika Wilaya zote hapa nchini.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri Mheshimiwa Ummey Mwalimu, Naibu Waziri Mheshimiwa Kigwangalla na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya ni moja ya sekta nyeti Tanzania inayosimamiwa na Wizara ya Afya pamoja na hospitali zote za rufaa, hospitali za wilaya pamoja na vituo vya afya na zahanati zilizopo chini ya Serikali za Mitaa, Manispaa na Wilaya hizi zipo chini ya Wizara ya TAMSEMI, pamoja na kwamba zote zinapatiwa miongozo ya kiutendaji kutoka Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa Idara ya Afya katika Mkoa wetu wa Iringa, inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Chumba cha uangalizi wa wagonjwa wa nje wa dharura (*OPD*) hivyo kusababisha msongamano mkubwa katika wodi kwa zile huduma zinazohitajika uangalizi wa muda mfupi.

(ii) Wastani mdogo wa daktari kwa wagonjwa. Hivyo kufanya kuwa na msongomano mkubwa katika vyumba vya

madaktari wachache wanapokuwa zamu, hivyo kuongeza *work load* kwa madaktari.

(iii) Kuna wodi nzuri za watoto zilizojengwa kwa ufadhili wa Hospitali ya Vicensa ya Italy na mzaledo mmoja familia ya ASAS lakini hakuna Daktari Bingwa wa Watoto (*Pediatrician*) pamoja na idadi kubwa ya watoto wanaolazwa hospitalini hapo.

(iv) Hakuna kitengo cha *ENT* (sikio, pua na koo) wala Daktari wa *ENT*. Hivyo *case* zote za *ENT* lazima zipewe rufaa au kusubiri *visiting doctor* ambayo inakuwa ni kero kwa wagonjwa wenye matatizo yanayohusiana na tatizo hilo.

(v) Vitendea kazi muhimu wodini ni vichache kama vile *oxygen cylinder* na *oxygen concentrators, pulsonetor* za kupima kiwango cha *oxygen* kwa mgonjwa, *BP machine* hazina uwiano inaostahili kwa ugonjwa (wodi nzima inakuwa na mashine moja tu), vipimo vyya sukari kwa wagonjwa wa sukari waliopo wodini wanaohitaji uangalizi wa kina.

(vi) Kitengo cha afya ya akili hakikidhi haja na mahitaji ya wagonjwa wa afya ya akili kwa sababu kina vyumba vinne yaani viwili kwa wanaume na viwili kwa wanawake, vyenye uwezo wa kukaa na wagonjwa wawili kila chumba, hivyo uwezo wa hospitali kuhudumia wagonjwa wa akili ni wagonjwa wanne tu, ambavyo ni hatari kwa hospitali yenye kiwango cha Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ukizingatia Mkoa.

(vii) Wagonjwa wanaostahili msamaha hawapati huduma za dawa kama inavyostahili kutokana dawa nyingi kutokuwepo hospitalini, hivyo kusababisha shida zaidi kwa wagonjwa wasio na uwezo, wazee na wenye magonjwa ya kudumu kama sukari, akili, *TB* na *HIV*.

(viii) Nyumba za madaktari zaidi ya asilimia 85 ya madaktari na wahudumu wengine wa afya wanakaa maeneo ya mbali na hospitali kutokana na kukosekana nyumba hasa nyakati za usiku kwa wagonjwa wetu.

(ix) Kukosekana kwa huduma zingine za msingi kama *CT Scan, MRI, ECG, ECHO* katika hospitali ya Mkoa hivyo kusababisha rufaa zingine zisizokuwa na lazima ambapo ni kero kwa wananchi wanaohitaji huduma hizo.

(x) Mifumo ya *ki-electronic* inayowezesha daktari kupata majibu ya mgonjwa kutoka maabara na taarifa nyingine za mgonjwa kwa haraka kama ilivyo hospitali nyingine za *private*.

(xi) Pia dawa muhimu hazipo hospitalini kila wakati, hivyo kusababisha wagonjwa kuhangainka kwenda kutafuta maduka binafsi na kero zaidi inakuwa wakati wa usiku ambapo hayo maduka binafsi yamefungwa, inaweza kuhatarisha maisha ya mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake; niipongeze Serikali kwa kuweka dirisha la kuweza kuhudumia wananchi wa Mkoa wa Iringa, lakini ili ile dhamira ya kuanzisha benki hii kwa ajili ya wanawake ipate kutimia. Pia kuwepo na *mobile agency* kwa ajili ya huduma hii kufikishwa vijiji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vituo vinavyolea watoto yatima; pamoja na wamiliki wa vituo hivi vyatoto yatima kuisaidia Serikali katika wimbi hili la watoto yatima na watoto wa mtaani, lakini kuna changamoto nyingi zilizopo katika vituo hivi. Kuna vituo havina hata uwezo wa kuwatibu watoto hawa wanapouqua au kupata ajali. Hivyo ni vema Serikali ikaweka utaratibu wa kusaidia vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu maradhi yasiyo ya kuambukiza. Kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaosumbuliwa na maradhi kama shinikizo la damu, kisukari na kadhalika ambayo hayakuwa ya kawaida siku za nyuma, lakini kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa huduma ama matibabu kwa maradhi haya hasa kwenye maeneo ya vijiji. Tofauti na

waathirika wa UKIMWI ambapo huduma zimesogezwa hadi katika zahanati na vituo vya afya, wagonjwa wa kisukari, shinikizo la damu na mengineyo yanayofanana na haya wanapata wakati mgumu kupata huduma. Naishauri Serikali isogeze huduma za maradhi haya kama ilivyofanya kwa huduma za waathirika wa UKIMWI.

Pili, ugumu wa huduma Visiwani Ukerewe. Kwa sababu za kijiografia wagonjwa wengi kisiwani Ukerewe wamekuwa wanapoteza maisha kwa kukosa huduma hasa panapohitajika kuwapeleka Hospitali ya Rufaa ya Bugando. Kwa mujibu wa ratiba ya meli, usafiri wa mwisho toka Ukerewe kwenda Mwanza unapatikana saa nane mchana, na njia ya kivuko (*ferry*) usafiri wa mwisho ni saa 11 jioni, baada ya hapo usafiri mwingine hadi siku inayofuata. Kwa hiyo, inapotokea dharura inapopelekea kutoa rufaa ili mgonjwa apelekwe Hospitali ya Mkoa au ya rufaa baada ya muda huo litakuwa ni kudra ya Mwenyezi Mungu ili awe hai hadi kesho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la ushauri wangu kwaSerikali ni kwamba itoe *ambulance boat* kwa Halmashauri ya Wilaya Ukerewe ili kusaidia kwenye matukio ya dharura kuwashisha wagonjwa kwa ajili ya matibabu zaidi.

Tatu, ni kuhusu Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*). Kuna tatizo la upatikanaji wa huduma kwa wanachama wa *CHF* hasa upungufu wa dawa na huduma kutotolewa kwenye maeneo mengine tofauti na pale ambapo mfaidika amejiunga. Jambo hili linakatisha tamaa. Nashauri Serikali iangalie upya na kuweka mfumo mzuri wa upatikanaji huduma kwa wanachama wa *CHF* ili kumwezesha mwanachama kupata huduma eneo lolote ama kituo chochote nchini ili mradi yeye ni mwanachama na ana kitambulisho.

Nne, ni kuhusu huduma kwa wazee. Halmashauri nydingi bado hazijatoa vitambulisho kwa wazee wala kutenga dirisha maalum la wazee, jambo hili linasababisha usumbufu mkubwa kwa wazee pale wanapohitaji kupata huduma za

afya. Nashauri Serikali itilie mkazo na ikiwezekana kuweka muda maalum ili kuzibana Halmashauri zote nchini kutekeleza jambo hili.

Tano, kuongeza vituo vya afya na zahanati. Kwa kuwa ni sera ya Serikali kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya na kila kijiji kinakuwa na zahanati, Serikali ihakikishe mahali ambapo vituo na zahanati vimejengwa basi maeneo hayo yasaidiwe na kupewa vifaa na watumishi ili kuwezesha zahanati hizo na vituo vya afya vifanyekazi ya kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Halmashauri ya Wilaya Ukerewe imeweza kujenga kituo cha afya Nakatunguru, lakini sasa ni zaidi ya miaka mitatu toka kimekamilika kimeshindwa kuanza kwa kukosa vifaa na majengo yanaanza kuchakaa. Lengo la kituo hiki illkuwa ni kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali ya Wilaya. Nashauri Wizara iwezeshe kituo hiki ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Sita ni uhaba wa watumishi. Kuna uhaba mkubwa wa watumishi wa afya kwenye maeneo ya pembezoni kama Ukerewe. Jambo hili linapelekea uhafifu wa utoaji wa huduma kwenye maeneo haya. Nashauri Serikali itoe motisha kama vile posho ya mazingira magumu kwa watumishi waliopo na kufanyakazi kwenye maeneo haya.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Pili, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nazidi kuwaombea mafanikio katika utekelzaji wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbusha Mheshimiwa Waziri Halmashauri ya Wilaya Songea imeleta muda mrefu sana maombi ya gari la chanjo. Tafadhalii sana Serikali itusaidie.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa

anayoifanya katika kuitumikia nchi yetu. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana ukiangalie kituo cha afya Kitomanga Kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, kituo hiki hivi sasa kinafanya kazi kubwa kama hospitali ya Wilaya lakini uwezo wake ni wa kituo cha afya. Changamoto kubwa iliyopo katika kituo kile ni uchache wa vitanda, kutokamiliika kwa jengo la *x-ray* pamoja na kuchakaa kwa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhalii sana nakuomba utuokoe kwa kutupatia gari la wagonjwa katika kituo cha afya Kitomanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu vyoo katika shule za msingi. Nakumbuka mwaka jana nilikueleza changamoto ya vyoo iliyopo katika shule nyngi za msingi zillizopo Jimboni kwangu. Changamoto hili zinawaathiri sana wasichana wawapo shulenii. Nakumbuka uliniahidi kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga vyoo kadhaa katika baadhi ya shule za msingi ukataja kuwa upo mradi Wizarani kwako ambao ungeweza kutusaidia katika baadhi ya shule. Ahadi yako ile bado hadi sasa hajalitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu fedha kidogo ya dawa zinazoletwa katika Mkao wetu wa Lindi. Mheshimiwa Waziri nakuomba uipitie taarifa yako uliyoisoma hapa Bungeni, utagundua kuwa Mkao wa Lindi umepata asilimia 70 tu ya fedha mliyoitenga mwaka wa fedha 2016/2017 tatizo ni nini? Lindi ni Mkao ambao wakazi wake wengi ni maskini wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kukosekana kwa Sheria ya Wazee ambayo inapaswa kwenda sambamba na Sera ya Wazee ya mwaka 2003. Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ili sera hii itungiwe sheria yake?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mufindi tunao mpango wa kujenga Hospitali

ya Halmashauri ili kupunguza tatizo kubwa la huduma ya hospitali, naiomba Serikali kusaidia katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kumalizia kujenga kituo cha afya cha kata ya Mtwango, kata ya Mnina, kata ya Makungu na kata ya Mtambula. Wananchi pamoja na Mbunge tumejitahidi kujenga majengo katika kituo cha afya cha kata ya Mnina na kata ya Mtwango bado kumalizia. Pamoja na vifaa kama vile vitanda, blanketi, shuka na vifaa vingine ambavyo viro kwa vituo vyaa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuleta watumishi katika zahanati za Jimbo la Mufindi Kusini hasa katika zahanati ya Mbalamaziwa, kata ya Itandula, zahanati ya Ihowanza zahanati ya Kibao na zahanati ya Makungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuleta gari la wagonjwa katika kituo cha afya cha kata ya Makungu, gari hii litahudumia kata ya Idete, kata ya Kiyowela na kata ya Makungu. Wananchi wa kata hizi wanapata shida sana hasa akina mama wakati wa kujifungua, wanashindwa kufika katika kituo cha afya sababu ya umbali, zaidi ya kilometra 60 mpaka 80 hadi kituo cha afya cha kampuni ya *MPM*. Naomba sana Serikali kutuletea *ambulance* kwa ajili ya wanachi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani kwa Serikali kwa kutenga fedha za ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Katavi. Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Katavi ni eneo linalokuwa siku hadi siku na una changamoto kubwa za afya. Ni vema Serikali ikaweka kipaumbele kikubwa kujenga Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanganyika haina Hospitali ya Wilaya, tunaomba Serikali kupitia Wizara ya Afya itupatiate fedha za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwani suala la huduma hiyo ni muhimu sana na ukizingatia jiografia ya

Wilaya yangu ni ngumu sana na ndiyo Wilaya pekee yenye eneo kubwa sana kuliko Wilaya zote ambazo zipo Mkao wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanganyika ina vituo vitatu tu japo ni Wilaya kubwa na ina idadi kubwa ya watu, bado ndiyo eneo ambalo lina vituo vichache sana. Naomba Serikali itupatие vituo vipyा vya afya ambavyo vitarahisisha kutoa huduma ndani ya Wilaya, na kupunguza mzigo mkubwa kwa Hospitali ya Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niiombe Wizara katika vituo tulivyonyavyo ndani ya Wilaya vituo hivyo bado huduma hizo ni duni sana. Naomba kituo cha Karema, Mwese na Mishamo vibreshwe na viwe na hadhi. Ni matumaini yangu Serikali italiano galia kwa jicho la huruma kwa kuboresha vituo hivyo kwa kuvifanya ukarabati na kupeleka dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ambulance*, tunaomba ombi maalum la kupatiwa gari la wagonjwa, katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ni Wilaya yangu ambayo ina taabu kubwa sana. Hivyo tunasisitiza ombi hili litiliwe mkazo mkubwa na muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama ifuatavyo:-

(i) Katika hospitali ya Wilaya ya Tunduru kuna tatizo la chumba cha kuhifadhi maiti cha kisasa na katika hospitali ile hamna wodi ya kulaza wagonjwa waliofanyiwa upasuaji, wagonjwa hao hulazwa katika wodi ya magojwa mchanganyiko kitu ambacho kina hatarisha afya ya wagonjwa hao.

(ii) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina kata 39 lakini kuna vituo ya afya vitano tu jambo ambalo

linasababisha wananchi wanapata shida kutembea kilometra ndefuata huduma za afya.

(iii) Katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna Hospitali ya *Mission* ya Mbesa ambayo inahudumia wananchi zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Tunduru na Wilaya jirani ya Namtumbo. Hospitali hii ina madaktari wanne tu, kati yao wawili ni wazungu ambao mkataba wao unaisha mwezi Juni, 2017. Hivyo naomba Serikali ipeleke madaktari kulingana na mkataba wa Serikali na hospitali hiyo.

(iv) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru tuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika sekta ya afya. Zaidi ya wafanyakazi 700 wanahitajika ili kukidhi mahitaji ya zahanati zilizopo. Tunaomba sana ajira zitakapotangazwa tuangaliwe kwa jicho la huruma ili kututengea wafanyakazi katika sekta hii ili kunusuru wananchi wa Wilaya ya Tunduru.

(v) Kuna upungufu mkubwa wa dawa katika zahanati, vituo vya afya kwa ajili ya kuhudumia wananchi wetu, sambamba na upungufu wa vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kukosekana kabisa kwa *ambulance* katika vituo vyetu vya afya ukizingatia Wilaya ya Tunduru ni eneo kubwa sana, wananchi wanatembea zaidi ya kilometra 100 kufuata Hospitali ya Wilaya, watu wanabebana kwenye matenga, akina mama wajawazito wanabebwa kwenye matenga kufuata huduma za afya.

(vi) Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi Hospitali ya *Mission* Mbesa kuwa Hospitali Teule kwa vile inahudumia wananchi wengi sana hasa wa hali ya chini wa Tunduru na Namtumbo. Ninaomba basi ahadi ile itekelezwe ili kupandisha hadhi hospitali ile kuwa Hospitali Teule kama ilivyoahidiwa na Rais Mstaifu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

(vii) Katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 tumeahidi kutoa posho kwa wazee wenye umri zaidi ya miaka 65, mpango huu utaanza lini ili kusaidia wazee hawa kupambana na hali ngumu ya maisha inayokabili wananchi?

(viii) Uboreshaji wa vituo vya afya katika kituo cha Mtina, Mchoteka, Nkade ili viweze kufanya upasuaji wa kawaida, mpaka leo vituo hivyo havina vyumba vya upasuaji, wananchi wanapata huduma hiyo Hospitali ya Mbesa au Hospitali ya Wilaya. Hivyo tunaomba tupatiwe vyumba vya upasuaji katika vituo vyetu vya afya na kuongeza vituo vingine vya afya kama tulivyoahidi kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Afya ni kigezo kimojawapo katika maisha ya mwanadamu. Hivyo basi, sekta ya afya ni muhimu sana katika mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa UKIMWI kwa akina mama ambao wamejifungua salama, kumekuwa na uhaba wa dawa kwa akina mama wajawazito na waliojifungua salama. Mfano, mama mjamzito anachukua dawa hospitali ya Vwawa na anaishi Usangu. Baada ya kupata mtoto na mtoto kufikisha miaka miwili mama anatakiwa kurudi kituo chake cha kwanza ili kuendelea na dawa. Ikifika wakati wa kurudi hospitali ya awali mama anaacha kwenda kuchukua dawa kwa sababu mbalimbali. Kwa mfano, umbali wa vituo vya afya vya kuchukulia dawa, ghamama za usafiri, majukumu ya malezi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi kwa Wizara ni kwa nini Wizara isiweke mpango wa kutoa dawa kwenye ngazi ya zahanati zilizoko karibu na wananchi ili kuendelea kuokoa nguvukazi hii ya Taifa letu. Mfano, mtu anatoka Ichesa kwenda Hospitali ya Wilaya ya Vwawa kilometra 45 hadi 50, barabara ya vumbi na usafiri wa bodaboda. Hii inasabishia watumiaji wa dawa kuacha dawa na kuendelea kuwa na madhara yatokanayo na magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto za vifaa tiba kwenye hospitali zetu, bado wajawazito wanatakiwa kuwa na vifaa vya kujifungulia. Mfano *gloves*,

code tie inayotumika kufunga kitovu cha mtoto anapozaliwa, pamba na *gauze*. Je, Waziri anatusaidiaje kwenye suala la vifaa hivi kwa wanawake wanaojifungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa aina ya *folic acid* kwa wajawazito bado zimekuwa adimu sana kwenye hospitali zetu, badala ya kutolewa bure mama mjamzito analazimika kununua kwenye maduka ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie kuhusiano na upungufu wa Madaktari Bingwa kwenye hospitali zetu za rufaa sambamba na wakalimani wanaotumia lugha za alama kwa walemavu wanaokwenda kutibiwa katika hospitali zetu.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Afya ni msingi wa maisha ya binadamu awaye yote kwa vile kuwa na afya mgogoro ni chanzo cha kufilisika kwa shughuli zote za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kabisa Wilaya yetu ya Mbogwe mwaka huu wa fedha Halmashauri yetu iliweka katika bajeti yake jumla ya shillingi bilioni 1.5, hata hivyo kutokana na ukomo wa bajeti fedha hizo zikaondolewa kwenye bajeti. Naishauri Serikali yetu ione umuhimu wa kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe. Tuna taabu Mbogwe, sikieni kilio chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutujengea *theatre* mbili katika vituo vya afya vya Masumbwe na Mbogwe ambapo Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNFPA* kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na kuvipatia vituo hivi vya afya *ambulance* mbili, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kituo cha afya cha Mbogwe bado hakijafunguliwa rasmi kwa vile vifaa havijakamilika katika *theater* licha ya kwamba kweli gari la wagonjwa la *UNFPA* lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbogwe tuna uhaba mkubwa wa watumishi katika Idara ya Afya kwenye vituo vya afya na zahanati, naiomba Serikali ilione jambo hili na itupatie watumishi wa kutosha Wilayani kwetu.

Mhesimiwa Mwenyekiti, aidha naiomba Serikali itusaidie kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vya Ilolangula Ikunguigazi, Ikobe, Nhomolwa, pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe ili kuboresha huduma za afya Wilayani Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Geita ni mpya tunahitaji hospitali ya rufaa yenye uwezo wa kuhudumia wananchi wilayani wanapopata rufaa. Ujenzi wa hospitali ya rufaa utakuwa ukombozi kwa wananchi wa Mkoa mpya wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JUMA ALI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake Mungu ampe nguvu ili aweze kutimiza majukumu yake katika kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nimpongeze Naibu Waziri, kwa msaada mkubwa anaompa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Wizara, Waziri Mheshimiwa Ummy pamoja na timu yake kwa taarifa iliyosheheni na kukidhi kiu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Wizara ningeomba kujenga au kuboresha vituo vyetu vya afya nchini. Kwa mfano, Jimbo la Lushoto lina kituo cha afya kimoja tu ambacho kipo katika kata ya Mlola. Kituo cha afya

hiki kilahidiwa kupata huduma ya upasuaji lakini mpaka leo huduma ile haipo. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ipeleke huduma hiyo mapema ili kuzuia vifo hasa vya akina mama na watoto.

Pia nniombe Serikali yangu tukufu ipandishe hadhi zahanati ya Makanya kuwa kituo cha afya, pamoja na kujenga kituo cha afya katika kata ya Ngwelo kwani maeneo yote haya yapo mbali sana na huduma za afya ukizingatia hata miundombinu ya barabara ni mtihani, hali hii inasababisha vifo vya wananchi walio wengi pamoja na vifo vya akina mama na watoto.

Sambamba na hayo wananchi wamehamasika kwa kujitolea nguvu zao kwa kushirikiana na Mbunge wao, wameanzisha ujenzi wa vituo vya afya viwili ambavyo vipo maeneo ya Ngwelo na Gare. Hiki cha Gare kina vyumba kumi bado wananchi wanaendelea kujenga. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu tukufu ichukue majengo yale ili iweze kuyamalizia na wananchi waweze kupata huduma kwa ukaribu zaidi kuliko hii adha wanayoipata sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sabamba na hayo pia kuna zahanati zaidi ya 13, zipo kwenye hatua tofauti, nyingine zimeisha lakini hazina vifaa wala watumishi, nyingine zipo kwenye hatua za kufanyiwa usafi. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali yangu ipeleke watumishi katika zahanati zilizoisha na zile ambazo hazijaisha Serikali izichukue ili imalizie ili wananchi tusiwavunje moyo kwa kazi yao kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Serikali inavyosema kila Jimbo itajenga kituo cha afya kimoja, mimi katika Jimbo langu kituo hicho kijengwe katika kata ya Ngwelo kwani wananchi hawa ndiyo wanaopata taabu zaidi hasa katika kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu Wilaya ya Lushoto ina Majimbo matatu na yote hayo yanaangalia hospitali moja ya Wilaya na Hospitali ile ni ndogo

inahitaji kupanuliwa hasa vyumba vyaa mama wajawazito, vyumba vyaa mama na watoto. Pamoja na hayo *x-ray* na *ultra sound* ni ndogo sana hazina uwezo, ndio maana inafanya kazi kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu sasa ipeleke vifaa hivi ili hospitali iweze kutoa huduma inayoendana na kazi ya hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hii ya afya ya uzazi na mtoto naiomba ifike vijijiini hasa katika Jimbo la Lushoto wananchi wengi wanaishi ndani sana yaani vijijiini mno. Kwa hiyo, naomba huduma hii ifike huko. Huko ndiko kuna wapiga kura wenye imani kubwa sana na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niishauri pia Serikali yangu haya mafungu yapelekwe vijijiini, mfano, hizi asilimia tano hazifiki kabisa vijijiini. Pamoja na hayo katika Mikoa ambayo itapelekewa mafungu, Mkoa wa Tanga sijaiona, naiomba Serikali yangu iangalie Mkoa wa Tanga nao uwe kwenye *list* ya kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu iweze kutoa ajira hasa kwa hawa maendeleo ya jamii, kwani hawa ni watu muhimu sana, wanahamasisha maendeleo vijijiini kuliko ilivyo kuwa sasa ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niongelee suala la magari katika vituo vyaa afya pamoja dawa, vitu hivi ni muhimu sana kuwa katika vituo vyetu vyaa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu ya UKIMWI ipelekwe zaidi vijijiini kwani bado mpaka sasa kuna maeneo ya vijijiini hawajapata elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ambariki Rais wetu wa Tanzania.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote, nianze kwa kuwapongeza kwa kazi nzuri ya kuwashudumia Watanzania. Binafsi ninawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri kwa ushirikiano mnaonipa kuwashudumia wananchi wa Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi mawili ambayo ni kwanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Hatua za awali kwenye Halmashauri na RCC zimekamilika tunakwamishwa na urasimu, ipo kwenye mchakato kwa upande wa Serikali Kuu. Wizara ya Ujenzi tayari imeridhia majengo ya *TANROADS* yaliyopo karibu na Makao Makuu ya Wilaya eneo la Kihanga yatumiwe kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Tunaishukuru sana Wizara ya Ujenzi.

Naiomba Wizara ya Afya uwapanguse machozi wananchi wa Karagwe kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kiasi cha fedha kitengwe kwenye bajeti mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali, hata kama ni kiasi kidogo cha fedha. Nitashika shilingi ya Waziri iwapo sitapata maelezo ya kuridhisha juu ya jambo hili. *TANROADS* itachukua majengo yake iwapo ujenzi wa hospitali hautaanza mwaka 2017/2018 kama tulivyoahidiwa kwenye maombi yetu na ombi namba mbili, *please refer to request number one.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Wizara hii ni nzuri na Waziri na Naibu Waziri wanafanyakazi vizuri kabisa. Tunawatia moyo muendelee kuwa wabunifu na kusimamia maadili ya wafanyakazi walio chini yenu. Pamoja na kuunga mkono hoja nina mambo yafuatayo kuishauri na kuiomba Wizara kwanza Nkasi tuna uhaba wa watumishi wa afya yaani madaktari, wauguzi na wataalam wa maabara. Kwa vile tuko pembezoni hali siyo nzuri, tusaidieni watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi huduma hutolewa kwenye zahanati chache kabisa, wananchi wamejenga

maboma zaidi ya 30 Wilaya nzima hayajamaliziwa yanahitaji kuezekwa, tunaomba bati ili wananchi waielewe Serikali iliyowahimiza wajenge na majengo yao yataezekwa.

Mheshimia Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya iliyopo inamiliikiwa na Wamisionari na usimamizi wa huduma siyo mzuri kabisa. Naomba mtusaidie tujenge hospitali yetu, huduma hazitolewi kwa msingi ya maadili hata mchango wa Serikali hauwanufaishi wananchi wa Nkasi ipasavyo.

Mheshimia Mwenyekiti, Nkasi bado kuna ukoma hasa maeneo ya mwambao mwa Ziwa Tanganyika. Naomba Wizara itambue jambo hilo na kuongeza huduma katika eneo hili. Pia dawa bado hazitoshelezi, nashauri fedha za dawa ziongezwe zaidi. Aidha, walemaru wawekewe utaratibu wa kutibiwa bure, hii ikiwa ni pamoja na walemaru wa ngozi (*allbino*), walemaru wa ngozi wanashida sana huko vijijini na hapajawa na ufuatiliaji toka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya nchini kote. Naomba ufuatiliaji uwe unafanyika, watambuliwe na wasimamiwe huduma za ushauri na matibabu yao.

Mheshimia Mwenyekiti, Nkasi kuwa pembezoni kuna vifo vingi vya akina mama na watoto. Hatuna vituo vingi vya afya hasa Jimbo la Nkasi Kusini. Naomba Serikali iweke miundombinu kwenye kituo cha afya cha kata ambacho kilijengwa na *Benjamin Mkapa Foundation* ili huduma ziweze kuanza kutolewa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimia Mwenyekiti, nina maombi maalum, naomba gari ya wagonjwa katika kata ya Kala lipatikane ili kupunguza vifo vingi vinavyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni watumishi wa afya walioonekana wana vyeti visivyokuwa halali wachunguzwe vizuri ili wale wenye weledi wasaidie kupunguza upungufu kwa masharti mapya, wale wasiofaa waachishwe kazi kabla ya kufukuzwa, haya ni maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kitengo cha *MOI* kinachotoa matibabu ya mifupa, kiangaliwe hakina huduma

nzuri na wauguzi na hata madaktari hawana maadili kabisa. Watu wanapoteza maisha wakati mwingine bila sababu za kutosha, nina shaka huenda kuna shida ya kuhitaji visenti ingawa sina ushahidi, hii ni kutokana na urasimu uliopitiliza wa kupata kitanda hata kwa mgonjwa ambaye hajiwezi kabisa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Afya na Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii pamoja na wataalam wao kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri kwa kukipatia gari kituo cha afya cha Kitere, suala ambalo nina imani litasaidia sana katika kuboresha huduma za rufaa kwa wagonjwa hasa akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri kuongeza watumishi wa afya katika vituo vya afya vya Nanguruwe, Kitere na Mahurunga ili viweze kutoa huduma bora kwani vituo hivyo vinavyo vifaa vya kisasa vya kutolea tiba, lakini baadhi yake vinashindwa kutumika kutokana na uchache wa wataalam wenye weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali pia kuongeza udahili wa wauguzi, maafisa tabibu, wafamasia na wataalamu wa maabara na kufadhili masomo yao ili tuweze kuwapa masharti ya kwenda kufanya kazi katika maeneo yenye upungufu kwa muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kuonesha nia ya dhati katika ujenzi wa hospitali ya Kanda ya Kusini. Kwa Kusini Mkoa wa Lindi na Mtwara ni kanda pekee isiyokuwa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda na kwa miaka miwili mfululizo kiasi kinachotengwa kwa hospitali hiyo kwanza ni kidogo na pili, fedha hizo hazitolewi. Kwa kifupi ni kama ujenzi umesimama, Mheshimiwa Waziri iwapo hutatoa mikakati inayotia moyo na yenye kuonesha nia ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hii nakusudia kuondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri na kwenye bajeti ya Wizara.

Mheshimi Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja na napongeza jitihada zako ikiwemo upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu. Niombe gari la wagojwa katika tarafa ya Matui ambayo ina *population* kubwa ya watu. Gari hilo likae kituo cha afya Engusero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba daktari wa *Anesthesia* katika kituo chetu Engusero ili *operations* ziweze kuendelea. Pia tunaomba madaktari na ma-nurse, Wilaya ina upungufu wa watumishi hao ikiwemo Daktari wa Kinywa na Meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ujenzi wa maabara ya Wilaya maana illyopo ni chumba kidogo *Prime Minister* alikiona akashangaa na akaniambia nikuambie.

Mheshimiwa Waziri, tunaomba upanuzi wa kituo cha afya cha Sunya maana kinabeba wagonjwa zaidi ya 30,000 tunaomba maabara na upanuzi wa majengo (wodi).

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa dawa nchini; kumekuwa na upungufu wa muda mrefu wa dawa hapa nchini, tatizo hili limekuwa la kudumu na kwa kuwa chanzo kikubwa cha fedha kwa ajili ya kununua dawa inategemewa na mapato ya makusanyo ya kodi mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, kumekuwa na mifuko ambayo inaanizishwa na chanzo cha mapato kwa ajili ya mfuko huo unakuwa wa uhakika na kuleta ufanisi unaokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ni Mfuko wa Barabara, Miradi ya *REA* ambayo chanzo cha mapato inatokana na fedha za mafuta na mfuko huo fedha zake haziguswi (*ring fenced*). Kwa kuwa dawa ni suala muhimu sana kwa ajili ya maisha ya Watanzania, hivyo ni wakati muafaka sasa Serikali ianzishe mfuko maalum wa dawa na

fedha zake zitokane na chanzo cha uhakika ili kupunguza na kuondoa kabisa tatizo la ukosefu wa dawa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Taifa ya *Mount Meru*; Hospitali hii ndio hospitali inayotegemewa katika Mkoa wa Arusha, hata hivyo kuna changamoto katika utoaji wa huduma kwa vifaa muhimu kama *x-ray machine* kuharibika mara kwa mara. Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha kwa kiasi kikubwa hospitali hii ambayo ni muhimu kwa Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni motisha kwa watumshi wa afya. Watumishi wa afya nchini ni kada muhimu sana ambayo wameamua kufanya kazi kubwa ya kutoa huduma kwa Watanzania wote. Hata hivyo, suala la afya ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu. Serikali lazima itazame kwa upya maslahi ya watumishi wa afya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazee; kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Serikali kuwa itaboresha makazi ya wazee, jambo hili limekuwa linaandikwa kwenye vitabu bila utekelezaji. Wazee ni hazina ya nchi, tunapaswa kuwaenzi na kuwashudumia. Serikali ijipange vizuri ili kuhakikisha makazi ya wazee yanaboreshwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kuanzia kwa Mheshimiwa Rais, Waziri na Naibu wake na watendaji wote.

Kwanza, kuongeza bajeti ya Wizara kwa zaidi ya mara kumi; kuendelea kutoa vifaa tiba vyta ya hospitali na vituo vyake yaani vitanda, magodoro na kadhalika; kutoa ajira ya madaktari wawili katika hospitali ya Wilaya ya Mbulu na kwagineko katika Wilaya za nchi yetu na kugawa pikipiki katika Halmashauri zetu nchini, naomba katika mgao ujao Halmashauri za Wilaya ya Mbulu wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iboreshe mfumo wa utoaji na upokeaji wa dawa katika hospitali za Wilaya vituo na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wajumbe wa Bodi ya Afya ya Wilaya na Bodi ya Vituo vya Afya na Kamati ya Afya ya Zahanati wapatiwe semina ya majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iondoe mpango wa kila Halmashauri za Wilaya kukamilisha kituo kimojawapo katika vituo vilivyoko kwa mwaka ili kuweka nguvu mahali pamoja hali itakayosaidia kuwa na vituo vitano kwa miaka mitano. Hivi sasa fedha za bajeti hugawanywa na Madiwani kiasi kwamba hakuna mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijitahidi kulipa madeni ya watoa huduma wa zabuni za chakula katika Halmashauri ya Mbulu, ni zaidi ya miaka saba sasa madeni hayo hayajalipwa. Japokuwa Serikali imesitisha watoa huduma ya chakula kwa wanafunzi wa chuo na huduma ya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ni taasisi kongwe kwa umri wake, kwa hiyo ninaomba Serikali yetu ione utaratibu wa kukarabati majengo ya hospitali hiyo. Naomba Serikali itusaidie kupata gari la *ambulance* kwani kwa sasa gari liilopo ni chakavu sana na wagonjwa wa rufaa ya kwenda Haydom ni kilometra 100, rufaa ya kwenda hospitali ya *KCMC* ni kilometra 360. Hivyo, naomba Serikali ituonee huruma kwa kutupa gari kwa ajili ya maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari 2017 nilifanya kikao cha watumishi wa afya hususan wale walioko katika Hospitali ya Wilaya, katika kikao hicho watumishi walitoa kilio cha kukosa kwa muda mrefu fedha zao za *on call allowance*(malipo ya posho ya masaa ya ziada), naomba Waziri wetu baada ya bajeti atoe kauli ili watumishi wawe na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusema kuna umuhimu mkubwa wa dawa za Serikali kuwekewa alama kwa ajili ya kupunguza uvujaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwaajiri watumishi wa afya, bado tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya katika Hospitali ya Wilaya, vituo na zahanati katika Halmashauri za Vijiji hali inayopelekea huduma za afya kuwa hafifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itazame upya mfumo wa *TFDA* ili kupunguza uharibifu wa rasimali za umma kwa ajili ya afya ya mlaji. Mfano, simu *fake*, viroba na kadhalika, hali inayosababisha kudhoofisha uchumi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu kuna chuo cha *PHN*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wetu wa Afya aweze kufanya ziara katika chuo hicho na hospitali hiyo. Hata hivyo, kuna jengo liliokuwa linajengwa na Serikali Kuu, jengo hilo liliojengwa chini ya kiwango, hivyo chuo chetu kinafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja .

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mafia inakabiliwa na changamoto nyingi, lakini kubwa ni ukosefu wa huduma ya *x-ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia ni kisiwa na kutokana na changamoto ya usafiri hospitali hii wananchi wanapata taabu sana kuwasafirisha kufuata huduma ya *x-ray* Wilayani Temeke, Dar es Salaam. Mimi binafsi kwa kushirikiana na

wahisani mbalimbali nimefanikiwa kupata *x-ray* mpya na ya kisasa na tayari ipo Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa *x-ray* imefika Mafia toka mwezi Aprili, 2016 mpaka leo hii bado ipo *store*, hajafungwa. Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja Katibu Mkuu wanafahamu suala hili, ukweli nashindwa kuelewa ni kwa nini hamtaki kutoa ruhusa *x-ray* ili ifungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga chumba kipywa kwa ajili ya *x-ray* mpya siyo wazo bayo ila ombi letu ni *x-ray* mpya ifungwe katika chumba cha *x-ray* zamani na ile ya zamani chumba kipywa kitakapokuwa tayari ifungwe. Hii itasaidia sana kwani kwa sasa wananchi wanapata usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hopitali ya Mafia pia haina jokofu la kuhifadhi maiti. Suala hili ni muhimu sana kutohana na kukua kwa sekta ya utalii na shughuli za kijamii kuongezeka, inapotokea dharura ya mtu au watu kufariki ambao siyo wenyeji kwa Mafia usumbufu mkubwa unajitokeza kama ilivyotokea kuanguka ndege ya Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuipandisha hadhi zahanati ya Kironywe kuwa kituo cha afya; Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mafia yenye jumla ya vijiji 23 na kata nane haina kituo cha afya hata kimoja. Tayari hatua za awali tumeshazikamilisha tunaomba Wizara sasa iharakishe mchakato huu ili Wilaya tuwe na kituo kimoja cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati za Bwejuu, Mlongo, Gonje na Jimbo zilitengewa fedha ili kumalizia mabomba, lakini mpaka sasa tumekapokea robo tu ya fedha hizo. Kwa namna ya kipekee zahanati ya Bwejuu ambayo ipo katika kisiwa kidogo cha Bwejuu ambapo hakuna huduma yoyote ile ya kitabibu, hakuna hata sanduku la msaada wa kwanza (*first aid kit*) tunaomba Serikali iharakishe upatikanaji wa fedha hizo ili wananchi wapatoa 1,000 wa kisiwa cha Bwejuu wapate huduma hii muhimu.

Kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya tunaomba Serikali iboreshe *CHFili* iweze kutumika mpaka ngazi ya Mkoa na pia huduma za upasuaji zijumuishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mgao wa vitanda na mashuka kipaumbele tupewe Wilaya za pembezoni kama Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri pamoja Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajieleza kama ifuatavyo:-

Kuhusu uzinduzi wa zahanati, wananchi wamefanyakazi nzuri za kujenga zahanati, tatizo kubwa lililopo ni uzinduzi wa zahanati hizo kwa sababu ya kukosa wataalam, vifaa pamoja na *allocation* ya dawa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wa Afya aje kwenye Majimbo yetu ili uzinduzi wa hizo zahanati ufanyike haraka iwezakanavyo ili kutovunja nguvu za wananchi waliojitelea katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni vituo vya afya, katika ilani ya chama chetu, tuliahidi kujenga kituo cha afya katika kila kata, naomba sana Serikali ituunge mkono kwenye maeneo haya ya kujenga vituo vya afya hii itakuwa suluhisho la kudumu na kwa namna ya kipekee niipongeze Serikali kwa kujenga vituo vya afya vya mfano kila Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la dawa katika zahanati zetu. Vituo vya afya pamoja na hospitali zetu naomba sana muongeze migao ili wananchi wasiendelee kusumbuka.

Kuhusu tiba kwa wazee ni vema sasa Serikali ikaweka mkakati wa kuhakikisha huduma zote muhimu zinapitika kwa wakati katika kitengo hicho cha wazee na kuwa wanapata dawa kwa wakati na madaktari wawepo wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, chapeni kazi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi katika hospitali zetu nchini suala hili limekuwa ni tatizo kubwa sana katika Wilaya zetu. Kwa mfano, Wilaya ya Kalambo, Nkasi, Sumbawanga Mjini na Sumbawanga Vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu saratani ya shingo ya kizazi, suala hili limekuwa ni tatizo kubwa kwa wanawake wa Kitanzania na kasi yake ni kubwa sana, lakini bado hatujaona Serikali ikiipa kipaumbele kulingana na tunavyopoteza wanawake wengi hasa walioko vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukosefu wa dawa kwenye hospitali zetu, hili limekuwa ni tatizo kubwa, Serikali ifanye utaratibu wa kufuatalia kama dawa zipo katika hospitali za vijijiini. Wizara ipeleke dawa ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Ndoa, kuna sababu ya kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ili kuokoa maisha ya watoto wetu wa kike kwa kukosa mambo ya msingi ikiwemo elimu, kwani wakiingia kwenye ndoa wakiwa na miaka 18 itapelekea kukosa elimu.

Kuhusu ukatili kwa wanawake, kwa kuwa ukatili huu umekuwa ukiendelea kwa kasi hasa kwa watoto wa kike wakiwa shuleni, mitaani na nyumbani, je, Serikali inaleta mkakati gani wa kumaliza tatizo hili la ukatili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vyta wanawake wajawazito hakuna mkakati wa dhati wa kumaliza tatizo hili

na kuona wanawake hasa waliopo pembezoni na wanawake wa vijijini, Serikali iweke kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzazi wa mpango, kuna kila sababu ya Serikali kutoa semina elekezi hasa kwa maeneo ambayo bado elimu hii haijawakomboa kwani kumekuwa na upotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kwa kupitia Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Afya ili kuboresha na kujenga vituo vya afya kwa kila kata na hospitali za Wilaya hasa katika Mkao wa Rukwa hakuna Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kuzingatia, kukosekana kwa hospitali hata moja ya Wilaya katika Mkao wa Rukwa kunapelekea mlundikano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Mkao ya Rufaa.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja ilioletwa na Serikali. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa utumishi uliotukuka katika kuwasaidia Watanzania, katika kuwa na afya na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii zilizopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari ya wagonjwa (*ambulance*); magari haya ni muhimu sana kama ilivyo muhimu kuwa na dawa za kutosha, vifaa tiba vya kutosha. Pia ni muhimu kila hospitali na baadhi ya vituo vya afya vilivypo maeneo ya vijijini ndiyo vinavyohudumia watu wengi sana ambao wanategemea kupata matibabu katika vituo hivi pekee tofauti na maeneo ya mjini ambako kuna hospitali na vituo vya afya visivyo vya Serikali. Mfano, katika Jimbo la Lupembe Hal mashauri ya Wilaya ya Njombe eneo hili lina takribani watu zaidi ya 100,000 lakini ina vituo vitatu tu vya afya na hakuna hospitali yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwa ajili ya kupata matibabu

kwenye kituo cha afya kilichopo Lupembe umbali wa kilometa 75 toka Hospitali ya Kibena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kituo kipywa cha Kichiwa kipo umbali wa kilometa 50 toka Hospitali ya Kibena na kituo cha Sovi ambacho kipo umbali wa kilometa 45 toka Hospitali ya Kibena. Katika Halmashauri yetu tumekuwa tukipoteza akina mama wengi kwa kucheleweshwa kupata upasuaji kutokana na kutokupata msaada wa usafiri kwa ajili ya kipelekwa Hospitali ya Kibena kwa ajili ya upasuaji. Hivyo tunaomba tupewe gari angalau moja kwenye vituo hivi vitatu kwa ajili ya kuwasaidia usafiri akina mama wajawazito na wagonjwa mahtuti ili kuwahi matibabu au huduma kwenye Hospitali ya Kibena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hospitali ya Wilaya, Jimbo letu na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe haina hospitali. Tumeanza jitihada za kujenga hospitali ya Wilaya. Wananchi kwa kutambua umuhimu wa kuwa na hospitali ya Wilaya, wamejitolea eneo lao lenye ukubwa wa ekari 52 ili eneo hili litumike kwa ajili ya ujenzi wa hospitali. Tunaomba Serikali itusaidie kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazee ambao ni wazazi wetu ambao sisi watoto wao tuna wajibu wa kuwasaidia kwa malazi, mavazi, chakula na kuwashudumia pale wanapokuwa na matatizo ya kiafya. Wazee wengi wanafariki kabla ya muda wao kutokana na ugumu wa maisha na msongamano wa mawazo unaotokana na watoto wengi hawatunzi wazazi wao, hata kama watakuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea wazee wanatunzwa vizuri na Serikali kwa kushirikiana na watoto wao. Hii inawafanya waishi miaka mingi tofauti na Tanzania na nchi nyigine za Afrika. Hivyo basi, napendekeza Serikali ije na sheria itakayotutaka Watanzania kuhakikisha kwamba wanawatunza wazazi wao hasa wanapokuwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mara nyingi watoto wakipata kipato huwa wanawasahau wazazi waliowalea, wazazi wanataabika vijijini bila chakula na makazi duni wakati wao wakiwa na maisha mazuri. Hivyo sheria ikitungwa itawabana watoto wao kuwa na wajibu wa kuwalea wazazi wao, angalau kwa kuwapa huduma za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hasa maeneo ya vijijini. Mara nyingi watumishi wa afya wakianzia kazi mjini huwa hawapo tayari kuhamia vijijini pale wanapopata uhamisho wa kwenda vijijini. Hivyo Serikali iangalie uwezekano wa kuwafanya watumishi wawe *flexible* kwenda popote atakapopangiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ipeleke watumishi wa afya katika maeneo ya vijijini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Pia pale penye upungufu wa watumishi au watumishi kutakiwa kufanyakazi masaa ya ziada tunaomba Halmashauri na Wizara kuwalipa malipo yao ya kazi za ziada au *on call allowances* wapewe na ikiwezekana Serikali iwaongezee, shilingi 25,000 ni ndogo sana. Serikali ione uwezekano wa kuongeza kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mimba za utotoni na ukatili wa watoto; pamoja na tatizo hili kuchangiwa na mila na desturi pamoja na imani za kishirikina, pia wazazi kutotimiza wajibu wao wa malezi inachangia watoto wengi kupata mimba wakiwa na umri mdogo. Kila mzazi anatakiwa na ana wajibu wa kumlea mtoto wake katika maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wengi wanaacha watoto wao walelewe na *house girls* na *television*, vitu hivi ndivyo vinavyochangia watoto wengi kukosa malezi bora. *House girls* na *television* ndio wamekuwa walimu wa watoto hususani kwenye upande wa ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalosababisha mimba za utotoni na ukatili kwa watoto ni

umbali wanaotembea watoto wetu kwenda shulenii. Mtoto anayetembea zaidi ya kilometra tano kwenda shule ya msingi au sekondari, ana hatari kubwa ya kukumbana na vishawishi vya ngono kuliko mtoto anayetembea chini ya kilometra tano. Shule nyingi zilizopo maeneo ya vijiji ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wapo hatarini kuijilingiza kwenye vitendo hivyo na hatimaye kupatikana na ukatili wa kijinsia au mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kutatua matatizo ya mimba za utotoni ambazo kwa sasa zinasababishwa na vijana wanaotoa msaada wa usafiri (*lift*) bodaboda na magari na kuwafanya ukatili watoto wetu, ni vizuri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI, tuje na mpango wa kujenga *hostels* kwenye shule zetu za msingi na sekondari ili kuwaepusha watoto wetu kuingia kwenye vishawishi vitakavyopelekeea kwenye matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za damu salama, bado kuna changamoto ya watu kujitolea kuchangia damu na maeneo mengine hasa vijiji wananchi wengi hawapo tayari kuchangia damu mpaka walipwe. Hivyo Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi waishio vijiji juu ya umuhimu wa kuchangia damu. Hii itaongeza mwamko wa wananchi waishio vijiji kuchangia damu bila malipo pale wanapoombwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Mawaziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Ummey Mwalimu na Mheshimiwa Dkt. Hamis

Kigwangalla kwa kazi nzuri ya kusimamia mapinduzi makubwa ya uboreshaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zinajieleza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la bajeti ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 mpaka shilingi bilioni 251.5 kwa mwaka huu 2016/2017. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 imetoa matumaini makubwa ambapo mpaka sasa kiasi cha shilingi bilioni 112.19 zilipokelewa *MSD*. Kati ya hizo, Mkoa wa Pwani Hospitali zetu na Vituo vya Afya tunategemea kiasi cha shilingi bilioni 1.6. Tunawapongeza sana kwa jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi na usambazaji wa vitanda vya kawaida 20, vitanda vya kujifungulia vitano, magodoro 25 na mashuka 50 kwa Halmashauri zetu zote vilivyogharimu shilingi bilioni 2.93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya ya Pamoja, napongeza hatua zilizochukuliwa na Wizara kuhakikisha kuwa fedha za dawa kuititia Mfuko wa Pamoja zitapelekwa moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma, hatua hii itachangia upatikanaji dawa kwa wakati kwa wananchi wetu. Pamoja na pongezi hizo, katika maeneo machache naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri yetu ya Chalinze, Wizara ilikubali ombi la kupandisha hadhi Kituo cha Afya Msoga kuwa Hospitali ya Halmashauri. Ombi langu, naomba Wizara ilete watumishi ili kukidhi haja ya kuipandisha hadhi. Kukosekana kwa watumishi wa Sekta ya Afya katika Hospitali hiyo tarajiwa ya Halmashauri, imepelekea pesa za *Basket Fund* takriban shilingi milioni 90 kati ya fedha zote zilizopokelewa kushindwa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kusimamia ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne ya kupandisha hadhi Kituo cha Afya Mlandizi kuwa Hospitali ya

Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijiji na Kituo cha Afya Kibiti kuwa Hospitali ya Wilaya mpya ya Kibiti. Maeneo haya yana wananchi wengi, hivyo vituo hivyo vinazidiwa na idadi ya wagonjwa, lakini kuwa na mgawo ule ule wa hadhi ya kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Ulanga ina hali mbaya sana. Watumishi ni wachache sana kiasi cha kukwamisha matibabu, mfano Madaktari ni wachache, wahudumu pia hakuna, wala mtaalam wa *X-Ray machine*; wodi ni chache, ndogo na zilizochakaa. Hii inapelekea wagonjwa kuchanganywa ambapo ni hatari; chumba cha upasuaji hakipo katika *standard*, hakina *monitor*; Madaktari wanatumia uzoefu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashuka na nguo za wagonjwa zinafuliwa kwa mkono (hakuna mashine ya kufulia). Hii ni hatari kwa afya za wafanyakazi. Pia gari la wagonjwa lipo moja ambalo nilinunua mimi Mbunge. Kutokana na jiografia ya Jimbo ilitakiwa kuwa na magari angalau matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wahudumu wa Afya wanajinunulia *uniform* mwaka wa saba huu (hakuna *uniform allowance*); kuna upungufu mkubwa wa dawa hasa za ugonjwa wa kifafa, ukizingatia Wilaya ya Ulanga ina wagonjwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni marupurupu ya wahudumu.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake, atolee maelezo mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari la wagonjwa ambalo Wizara iliahidi kuwa imetenga shilingi milioni 20 katika mwaka

wa fedha 2016/2017 katika Wilaya ya Muheza: Je, ni lini gari hilo la wagonjwa litafika Muheza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Waziri aliahidi kupeleka gari la wagonjwa katika Zahanati ya Mgambo, Amani itakapofika mwezi Januari, 2017 lakini sasa ni mwezi wa Tano hakuna utekelezaji. Wananchi wanapata usumbufu mkubwa katika upatikanaji wa dawa hasa wanaotumia bima kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa dawa katika hospitali zetu. Wizara imeandaa utaratibu gani kupitia *MSD* ili angalau kila penye Hospitali ya Wilaya kuwe na duka la dawa ambalo kadi ya bima inaweza kutumiwa na mgojwa kupata dawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ya mabohora Tanga wametoa mashine ya *CT-Scankwa* Hospitali yetu ya Bombo, lakini inasemekana hakuna jengo *special*. Kama ni kweli, Serikali ina mpango gani kuharakisha ujenzi wa hilo jengo ili mashine zifungwe na kutumika?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kakonko kwa muda mrefu imetumia Kituo cha Afya Kakonko kama Hospitali ya Wilaya. Naomba Wizara ya Afya isaidie kusukuma Halmashauri ya Wilaya na TAMISEMI kujenga Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Watumishi wa Afya Wilayani Kakonko ni mkubwa sana. Uhaba huo ni Madaktari wa kufanya kazi katika Vituo vitatu, yaani Kakonko, Nyanzige na Gwanumpu. Aidha, kuna uhaba wa kutoa huduma kama *AMO, Core Nurses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la akinamama kutozwa fedha wanapopeleka watoto *clinic* kupimwa. Hali hii inajitokeza kwa mama kuwalipa wahudumu wa afya (binafsi). Kwa nini kazi hiyo isifanywe zahanati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watendaji wa Ofisi ya Maendeleo ya Jamii watoe elimu ya ujasiriamali kwa wananchi ili waanzishe vikundi vya kujitafutia kipato. Aidha,

hamasa itolewe kwa wananchi kusajili vikundi kama *VICOBA*, *SACCO\$* na vikundi vinginevyo vya kijasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba matibabu bure ya wazee kutolewa kama Sera ya Wazee inavyoeleza. Wazee walipwe pensheni kila mwezi kama ilivyowahi kuamuriwa na Bunge. Vile vile Vitambulisho vya Wazee vitolewe kwa muda muafaka, kwani Mheshimiwa Waziri aliagiza viwe vinatolewa kabla ya tarehe 30/12/2016, lakini hadi sasa Wilaya ya Kakonko wazee hawajapata vitambulisho, sambamba na sensa ya kuwatambua wazee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ifanyiwe marekebisho ili kuepuka watoto (*underage*) kuolewa kwa kigezo cha umri wa kuolewa. Pia watoto wa kike wanaobeba mimba shulenii wapewe nafasi ya kuendelea na masomo. Wizara ishauriane na Wizara ya Elimu kuweka Sera (*re-entry policy*) ya wanaobeba mimba kuendelea na masomo mara baada ya kujifungua. Hii itasababisha watoto hawa kupata haki ya elimu.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya. Naishukuru sana Wizara kwa kutupatia gari la *Ambulance* kwa Kituo cha Lalago na Malampaka. Nashukuru sana kwa uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ninalotaka kuchangia ni kuhusu suala la waathirika wa madawa ya kulevyo. Kama tujuavyo, kuna madhara makubwa ya kiafya kwa waathirika wa madawa ya kulevyo (waraibu). Wizara ina jukumu la kupambana kuzuia baadhi ya madhara hayo ikiwemo maambukizi ya UKIMWI, homa ya ini (*hepatitis B*), TB na kadhalika. Moja ya shughuli ya kupunguza madhara haya ni pamoja na hatua za Serikali kuititia *Sober House*, lakini Wizara ina jukumu la kusambaza dawa ya *Methodone* na *Syringe* kwa waathirika (waraibu). Tatizo, Wizara haifanyi hivyo. Kuna upungufu mkubwa sana wa *Methodone* na

*Syringe. Syringe* zinagawanywa na Wilaya moja tu; na Wilaya hiyo ni Temeke tu, Wilaya nyingine hakuna mgawo wa *Syringe*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haioneshi juhudhi maalum kwa waathirika hawa. Matokeo yake kundi hili linaathirika zaidi na wengine wanarudi kwenye utumiaji wa madawa hayo na wanapoteza maisha kwa magonjwa mengine nyemelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni mojawapo ya Mkao wenye upungufu mkubwa wa Madaktari. Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkao, wanahitajika Madaktari (*MD*) 30; waliopo ni 12, pungufu ni 19. Madaktari Bingwa wanaohitajika ni 24 ila wapo watatu. Daktari Bingwa wa magojwa ya akinamama, Daktari Bingwa wa meno na Daktari Bingwa wa magonjwa ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia upungufu huo, Mkao uliamua kuajiri Madaktari (*MD*) na kuwalipa kwa kutumia fedha za uchangiaji wa huduma za afya (*cost sharing*). Hadi wiki iliyopita, walikuwepo Madaktari (*MD*) saba ambaao wanalipwa kwa fedha za *cost sharing*. Madaktari hao ni Dkt. Yunus H. Ibrahim; Dkt. Nathaniel Ngeta, ambaye kwa sasa amepelekwa kwa *DED Kyerwa*; Dkt. Paschal Peter; Dkt. Goodluck Chenga, kwa sasa amepangiwa Hospitali ya Mkao Bukoba; Dkt. Bartazar W. Benedicto, amepangiwa Wizara ya Afya; Dkt. Lunyonga R. Shija ambaye kwa sasa amepangiwa Hospitali ya Mkao Bukoba; na Dkt. Felix T. Otieno ambaye kwa sasa amepangiwa Hospitali ya Mkao Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Madaktari hao wawili waliobaki wapewe kipaumbele cha ajira na wapangiwe kufanya kazi kwa *RAS Kagera*. Pia tunaomba Madaktari Bingwa zaidi ili kupunguza upungufu uliopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya vifaa vya uchunguzi hasa *CT-Scan* na *MRI* pamoja na wataalam wa kuvitumia vifaa hivi vya uchunguzi ni muhimu kwa Hospitali ya Mkoa, kwa sababu huduma hii ya uchunguzi inapatikana Mwanza. Hivyo tunaomba sana muweze kutukumbuka Mkoa wa Kagera. Pamoja na maombi hayo, tunaomba pia Halmashauri zetu zipewe kipaumbele katika mgawo wa *Medical Doctors (MD)* hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya Halmashauri tayari zimeanza kutoa huduma ya upasuaji *CEMONC* katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vinavyotoa huduma ya upasuaji, licha ya upungufu wa Madaktari ni Nyakachura na Nyakanazi katika Halmashauri ya Wilaya Biharamulo; pia kwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa na Kayanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Vituo vinne vya afya vinavyotarajija kuanza kutoa huduma za upasuaji kuititia Mpango wa *Strengthening Primary Health Care for Results Programme* ni Mabame (Ngara), Kimaya (Muleba), Kishanje (Bukoba) na Morongo (Kyerwa). Vituo vingine vilivyokamilisha ujenzi wa *theatre* ili kuanza kutoa huduma za *CEMONC* ni Kaigara (Muleba), Bunazi (Missenyi), pamoja na Kabyaile (Missenyi) kilichojengwa na Kamati ya Maafa kufuatia tetemeko la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi anayoifanya kwa Taifa hili. Pili, nampongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kibiti hakuna budi kuishukuru Serikali yetu sikivu kuititia Wizara yake ya Afya kwa kutupatia gari la kubebea wagonjwa (*Ambulance*) aina ya *Toyota Land Cruiser* kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kibiti. Hii itatusaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia vifo vitokanavyo na

uzazi na pili, kupata vitanda 20 vya kulazia wagonjwa na vitanda vitano vya kujifungulia na magodoro pamoja na shuka zake. Sisi Wanakibiti kwa ujumla tunamwahidi tutavitunza vifaa hivi vyote pamoja na gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila penye mafanikio hapakosi changamoto. Changamoto kubwa ni Ikama ya Watumishi katika Wilaya yangu ya Kibiti. Pia tuna upungufu mkubwa wa watumishi. Vile vile posho zao za masaa ya ziada ya kufanya kazi, madai ya fedha za likizo na motisha kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibiti hadi sasa haina Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, inafanya Kituo cha Afya Kibiti kupokea wateja wengi kuliko uwezo wake. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara yako itupandishie kituo hiki kiwe Hospitali ya Wilaya. Katika kituo hiki hatuna Mochwari ya kuhifadhi maiti. Pia hakuna ukarabati wa kituo hiki kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kibiti kuna Kata tano, zipo maeneo ya *Delta*. Naomba Mheshimiwa Waziri atuangalie kwa jicho la huruma sana, kwani maeneo haya mtu akipata matatizo hakuna msaada wowote. Naomba tupatiwe ujenzi wa *theatre* ya upasuaji katika Kituo cha Afya Mbweri na kutupatia watumishi wa kutosha Ikama 149; waliopo ni tisa na pungufu ni 140. Naomba tusaidiwe. Kata hizo ni Maporini, Mbuchi, Msala, Kiongoroni na Salale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge katika Wizara hii, wameeleza tatizo kubwa la ukosefu wa *X-Ray* katika Hospitali zetu. Katika Jimbo langu ambalo lina Hospitali moja ya Shirika la Dini, hatuna huduma ya *X-Ray*. Jitihada nyingi zimefanyika zikiwemo pamoja na mchango wa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuchangia Shilingi milioni 40 mwaka 2010. Nasi Halmashauri kwa upande wetu katika

Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018, tumetenga Tanzania Shilingi milioni 20. Hivyo tunaomba Wizara itusaidie kuwasiliana na wenzetu wa Bima ya Afya ili waweze kutukopesha kifaa tiba hicho, kwani tayari tunazo shilingi milioni 60 mkononi ambazo zitawezwa kuwashawishi wenzetu kutukopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 127 inaonesha hali ya Halmashauri. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa hali yake ya upatikanaji ni asilimia 77. Ukilinganisha na Halmashauri nyiningine, Halmashauri hii ni mionganini mwa Halmashauri chache ambazo upatikanaji wake wa dawa bado uko chini. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha, atuambie ni kwa nini Kilwa? Je, kuna mikakati gani ya kutatua tatizo hili ili kuhakikisha tunapata dawa kama zinavyopata Halmashauri nyiningine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (*CAG*) inaonesha zaidi ya Tanzania Shilingi bilioni nne zimepotea kutokana na miradi iliyokamilika lakini haifanyi kazi. Katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini, kuna zahanati sita ambazo majengo yake yameshakamiliika, lakini bado hazijafunguliwa. Ni Zahanati ya Hongwe, Mpindimbi, Nambondo, Miyumbu, Marendego na Mwengei. Naomba kwa usimamizi wa Serikali izifungue zahanati hizi kwani nguvu za wananchi na Serikali zimepotea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika sakata la vyeti feki, uhakiki wa vyeti, Wilaya yangu imeathirika sana hasa katika Hospitali ya Wilaya ya Kinyonga na Hospitali ya Kipatimu. Madaktari tegemezi wamekumbwa na tatizo hilo. Naomba watakapopanga mgawanyo wa Madaktari kutokana na tatizo hili, Wilaya yangu iangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii ya Wizara husika. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemedari Mtukufu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na wasaidizi wake wote. Kubwa la msingi tuwaombbee mema kwa Mungu. Hata hivyo nina haya machache ya kutaka ufanuzi na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasomesha Madaktari wengi kwa gharama kubwa sana: Je, ina mkakati gani wa kuwa-*retain* angalau kuwa na mkataba wa *win win situation* kwani kuna uhaba sana wa Madaktari kutokana na wengine kukimbia nchi za nje *for green pastures?* Uzalendo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya mama na mtoto inaelekea mwaka huu vifo vimeongezeka. Kutokana na *data* ambazo zinaeleweka, nini chanzo na mkakati wa kuboresha? Tukumbuke mama ndiye familia. Elimu kwa umma iongezwe kuhusu umuhimu wa kujifungulia hospitali au zahanati. Pia akinamama wengi hawana uwezo, hivyo ni muhimu pia kuwapatia *tools* za wakati wa kujifungua endapo kutakuwa na dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ina-*extend* wodi ya watoto kwa juhudhi binafsi na ubunifu. Nampongeza sana Mkurugenzi wa Hospitali hiyo Dkt. Mbwanji. Hata hivyo, nahitaji kujua *contribution* ya Serikali katika ujenzi huo, kwani Hospitali hii ndiyo inayotoa huduma kwa Mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba na ndoa za utotonii ni tatizo sugu nchini kwetu, kwani licha ya kuwakatisha masomo watoto wa kike, pia inawaathiri kiafya na kisaikolojia. Hili suala kwa kiwango kikubwa linatokana na mila potofu na imani nyngine za dini ambapo sasa Serikali ichukue hatua na jitihada za ziada kwa kuzidi kutoa elimu kwa umma, kukutana na wadau husika, mfano makundi ya dini, Machifu na Serikali. Kwa Wizara husika, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara

ya Katiba na Sheria ilete Muswada wa kubadilisha Sheria hii ya Ndoa na Mimba za Utotoni. Nashauri umri uongezwe toka miaka 14 iwe 18 na hatua kali zichukuliwe kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji kujua *why TACAIDS (PM's Office); at the same time, why NACP* (Ofisi ya Wizara ya Afya office)? Maana wote wanashughulikia masuala ya UKIMWI; huu ni mwingiliano/mgongano wa majukumu na kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Abuja la asilimia 15 limeshakamilishwa kwa hapa nchini kwetu? *MDG's/SDG's limefanikiwaje kuhusu yale malengo yake hapa nchini kwetu?* Mpango wa Afya ya Msingi (MAM) tunahitaji tupewe *data*; Serikali imefikia wapi? Kwani hii iko katika llani yetu ya Uchaguzi wa CCM na huduma bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JULIANA D. SHOZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Serikali kwa kukubali ombi la kupandisha hadhi Hospitali ya Wilaya ya Mbozi na hatimaye kuwa na hadhi ya Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri machache. Hospitali hii inapandishwa hadhi ikiwa na changamoto nydingi. Idadi ya Manesi na Madaktari ni ndogo mno ukilinganisha na mahitaji yaliyopo, ukizingatia kuwa Hospitali ya Wilaya ya Mbozi inahudumia Wilaya ya Mombasa, pia kutokana na kwamba Wilaya ya Mombasa mpaka sasa hakuna Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo ya kuwepo kwa uhaba wa Madaktari inapelekea Madaktari kufanya kazi kwa muda wa ziada huku ulipwaji wa *on call allowance* wakicheleweshewa kupatiwa hivyo kupunguza ufanisi. Naomba Serikali katika ajira mpya zinazotarajiwa kutolewa, basi na Hospitali ya Wilaya ya Mbozi iliopandishwa hadhi iongezewe Madaktari, kwani mpaka sasa kuna *MD* watano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, changamoto ya dawa bado ni kubwa pamoja na jitihada za Serikali ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 fedha za dawa zilizokuwa zimetengewa ni Sh. 143,937,133/= na zilizopelekwa mpaka Aprili, 2017 ni sh. 165,144,778/=. Hivyo Serikali ilivuka malengo, tunaishukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya dawa katika mwaka huu 2017/2018 ambapo tayari hospitali hii imepandishwa hadhi ni Sh. 173,938,158/=. Ongezeko hili ni dogo ukizingatia kuwa tayari hospitali hii imepandishwa hadhi na kuwa ya Mkoa. Hivyo, naomba bajeti ya dawa iongezwe pia *MSD* wahakikishe wanaleta dawa kulingana na bajeti ya fedha waliyopewa ili kupunguza tatizo la uhaba wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Hospitali ya Wilaya ya Mbozi imepewa hadhi ya Mkoa, lakini katika Bajeti ya mwaka huu sijaona mahali popote kuhusu mchakato wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Songwe. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha Bajeti yake, aniambie ni lini mchakato wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Songwe utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu kuwa ni lini Wilaya ya Momba ambayo iko mpakani mwa Tanzania na Zambia itapatiwa Hospitali ya Wilaya, ukizingatia kuwa Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni yake Mjini Tunduma, 2015 aliahidi kutupatia majengo yaliyoachwa na Wakandarasi kuwa Hospitali ya Wilaya? Ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ili wanawake na wananchi wa Wilaya ya Momba wapate haki yao ya kupata huduma hiyo muhimu ya kiafya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kufahamu, ni lini Serikali itafikiria kuwa wagonjwa wa kisukari nao wapatiwe kadi bure kama ilivyo katika wagonjwa wa UKIMWI? Pia Serikali ijitahidi dawa za wagonjwa wa kisukari ziwe zinapatikana kwa wingi katika hospitali zetu ili kuwapunguzia mizigo wagonjwa wa kisukari kwa kununua katika maduka binafsi ambapo zinauzwa ghali.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi kubwa anayofanya katika kuiongoza Wizara hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa jinsi ambavyo anamsaidia Waziri wake na kujibu maswali kwa ufasaha kabisa Bungeni. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza timu yote ya Wizara ya Afya chini ya Katibu Mkuu kwa jitihada zinazoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wilaya yangu kuwa katika Mpango wa Kuboresha Vituo vya Afya, hususani Kituo cha Afya cha Mkili. Hata hivyo, kuna Kituo cha Afya cha Kihagara ambacho kinaendelea na ujenzi. Nitaomba tupewe jengo moja tu kwa mwaka huu kwa ajili ya wodi ya wanawake kwa kuanzia na upande mwingine wanaweza wakakaa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyasa, *with a very beautiful land* kwa sasa tuna mpango mkubwa wa Nyasa Maridadi, Nyasa iwe safi, Nyasa ipendeze na hivyo kuwa ni mahali pazuri pa kuishi na kutalii. Idadi ya watu wanaotembelea Nyasa imeongezeka sana. Kitu cha kusikitisha ni kuwa hakuna uhakika wa usalama wa wananchi hao na watalii kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya hii haina Hospitali ya Wilaya, tunategemea Kituo cha Afya cha Mbamba Bay ambacho hakina *Ultra-sound* wala *X-ray* na kadhalika. Tukipata majeruhi lazima wapelekwe Wilaya ya Mbinga au Peramiko na pengine Hospitali ya Rufaa Songea. Hao wananchi wengi wao ni maskini lakini ili kupata vipimo hivi vikubwa lazima walipe gharama ya nauji na baadaye walipe gharama nyingine zaidi kwa ajili ya kujikumu na dawa. Kwa *summary* naomba mtusaidie *Ultra-sound machine*, *X-ray machine* na *ambulance*, tafadhali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu kuna malalamiko makubwa juu ya mikopo ya pipipi ili yotolewa na Benki ya Wanawake wakati Mbunge wa Jimbo akiwa ni Mheshimiwa Marehemu John Komba. Wanadai kuwa

wamekuwa wakichangia lakini kila wakati wanatajiwa deni kubwa zaidi. Vile vile ni kuwa ukusanyaji wa madeni hayo hauleweki na wanapokea simu kutoka kwa watu ambao wanakuwa hawana uhakika nao na kuwatishia kuuza mali zao. Ni vema ufanyike mkutano wa wadeni na ikiwezekana nikaribishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maslahi ya Watanzania na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kusikitika juu ya kipaumbele kidogo kinachopewa kwa Wizara hii muhimu sana. Mfano bajeti ya Wizara hii imetekelozwa kama asilimia 25.8 tu kwa bajeti za maendeleo kwenye Sekta ya Afya. Pia kwenye Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni asilimia 5.65 tu ya bajeti ya maendeleo. Hii ni aibu sana kwa kweli kwa nchi. Hivi kwa mwendo huu tutafika kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 5.8 tu, lakini Serikali inashindwa kutimiza hili. Kwa mwendo huu tutafikia Abuja *Declaration* ya kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti kuu? Imekuwa ni kinyume kabisa! Kwanza katika kutenga; pili, katika kutekeleza hata kile kidogo kilichotengwa. Tanzania ya Viwanda itafikia wapi kama hatuwekezi kwenye afya ambapo tutakuwa tumewekeza kwenye rasilimali watu (*Human Capital Investment*) na tukifanya hivi tutakuwa na *skilled labour*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litawezekana tu kwa kuwekeza kwenye lishe (*nutrition*). Nchi yetu kwa sasa ina tatizo kubwa la *malnutrition, stunting, wasting*, hivi vinapelekea udumavu wa mwili (*physical development*) na udumavu wa akili (*cognitive development*). Tukiwa na Taifa la wadumavu daima hatutaweza kufika popote kama Taifa la Tanzania ya viwanda. Ni ndoto!

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia nzima kwa sasa wameamua kuwekeza kwenye lishe ili kuweza kuzalisha rasilimali watu na kukuza uchumi. Tuklwekeza kwenye lishe, tutapunguza vifo nya mama na mtoto, maana mtoto mwenye *malnutrition* huweza kupata maambukizi ya magonjwa kama vile *pneumonia*, kuhara, Malaria, utapiamlo na hata kupelekea kifo na ukiangalia idadi ya vifo nya watoto chini ya miaka mitano, bado ni tatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni jukumu letu sisi kuwekeza kwenye lishe kwa kufanya yafuatayo:-

(1) Kuhakikisha tuna Maafisa wa Lishe kuanzia ngazi ya Kijiji, Mtaa, Kata na Wilaya ili waweze kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi. Maana zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, cha kushangaza, mikoa yenye idadi kubwa ya watu wenye udumavu ni ile inayolima mazao mbalimbali ila hawana elimu ya lishe bora kwa afya bora;

(2) Kuhakikisha tunakuwa na vipeperushi vinavyotoa elimu juu ya umuhimu wa lishe na ni nini lishe bora ili wananchi wa vijijini na kaya maskini wajue ni jinsi gani wanapata mlo kamili wenye lishe bora?;

(3) Kuweza kutoa ruzuku kwenye viwanda vinavyozalisha chakula ili waweke virutubishi kwenye *packages* zao;

(4) Kuwekeza, kutoa *Supplement Bills* hasa kwa akinamama wajawazito wasiokuwa na uwezo wa kupata hivi vidonge vyenye madini ya chuma na *vitamins*;

(5) Kuweza kuwa na miundombinu imara ya maji, hospitali, zahanati na vituo nya afya; na

(6) Kuepusha mimba za utotonii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njikite kwenye utatuzi wa huduma ya afya kwenye Jimbo la Tarime Mjini. Kwanza kabisa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilituahidi tutapata

vituo vinne vyaa afya, maana kwa sasa hatuna kituo cha afya hata kimoja. Hivyo naomba sana mtupati hivi vituo vyaa afya ili kutatua tatizo la huduma za afya Jimboni kwangu, maana sasa ni tegemeo la Hospitali ya Mji ambayo nayo inahudumia Wilaya nzima na hata Wilaya jirani kama Serengeti na Rarya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu mzigo mkubwa wa Hospitali ya Mji wa Tarime ambayo bado inasomeka kama Hospitali ya Wilaya, lakini *basket fund* na *OC* zinakuja kwa kuzingatia idadi ya watu na Mji wa Tarime na siyo Wilaya nzima. Hii inapelekea upungufu wa Watumishi, mfano hili la vyeti feki limeondoka na Madaktari wawili, hivyo tumebakii hoi na inaweza kupelekea vifo vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tumeepata Madaktari watatu; wale wa Kenya lakini tumeondokewa na wawili, hivyo tatizo la uhaba lipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hatua za haraka zichukuliwe ili tupate hao Madaktari, Manesi na Wahudumu wengine wa Afya. Pili, Hospitali yetu itambulike kwa idadi ya watu wa Wilaya ya Tarime na siyo Mji wa Tarime ili kuwe na uhalisia wa huduma ya afya inayotolewa, maana kule Halmashauri ya Wilaya haina Hospitali. Tunaomba sana.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mpango wa uzazi. Rejea hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ibara ya 43, ukurasa wa 16, nitanukuu mwisho wa Ibara hiyo: "Wizara kwa kushirikiana na wadau, imetoa mafunzo kwa watoa huduma 3,233 ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma za aina mbalimbali za uzazi wa mpango. Hadi sasa kiwango cha kutumia uzazi wa mpango kimepanda kutoka asilimia 27 mwaka 2010 hadi asilimia 32 mwaka 2015/2016. Lengo ni kufikia asilimia 45 mwaka 2020."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kasi ni ndogo sana. Ajenda ya mpango wa uzazi inahitaji kupewa kipaumbele kama mkakati sahihi wa kukabiliana na changamoto zetu za maendeleo. Tanzania ina kasi ya asilimia 2.9 ya ongezeko la watu, kasi ambayo ni kubwa. Akinamama wengi huzaa

wastani wa watoto watano. Idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 65 ifikapo mwaka 2025, miaka nane kutoka sasa. Idadi kubwa ya watu ina matokeo hasi kwa maendeleo, ukuaji wa Miji na maisha ya watu (*socio-economic growth*); inagusa malengo yetu ya maendeleo endelevu katika sekta karibu zote; elimu, afya, uchumi, kilimo, mazingira na Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya kuzaliana ikipungua tutakuwa na rasilimali za kutosha kuboresha elimu na kilimo chetu. Elimu na kilimo ni sekta muhimu kwa nchi yetu, idadi ikipungua, Serikali itaweza kuweka akiba na kuongeza uwekezaji kukuza uchumi wetu, ujenzi wa reli, barabara, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika, zikiwemo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ipatiwe bajeti ya kutosha kuwezesha Halmashauri kutekeleza mipango ya uzazi (*family planning*) yenye matokeo. *Programme* za afya ya mama na mtoto zipewe uzito stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha afya ya Watanzania. Pia nawapongeza Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utoaji huduma ya afya katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ni changamoto kubwa. Hospitali hii ni ya zamani sana tangu uhuru, miundombinu ya hospitali ni chakavu sana na haitoshi. Hospitali inahitaji wodi za wanawake, wodi za wanaume, chumba cha kujifungulia, wodi ya wazazi, *OPD* na miundombinu mingine. *OPD* kwa mfano, ni chakavu sana, inahitaji ujenzi mpya. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo haina uwezo wa kugharamia ujenzi na ukarabati mkubwa unaohitajika. Namwomba Mheshimiwa Waziri aiwezeshe Halmashauri kwa bajeti maalum ili kuiboresha hospitali hii iweze kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha upungufu wa miundombinu, hospitali ya Wilaya pia ina upungufu wa vifaa tiba na madawa. Nashauri Wizara itusimamie katika matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti tangu iinglie madarakani na Mawaziri kufanya kazi kwa bidii na umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Msanginya kikiwa chini ya Wizara ya Afya killilingia mkataba na Mkandarasi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Chuo hicho, lakini mpaka sasa ujenzi umesimama na Mkandarasi hajalipwa kwa kazi za awali. Pia miundombinu mingi bado ni chakavu sana. Hivyo Serikali inaombwa kuangalia na kutatua kero hizo kwa kuongeza bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa wito kwa Serikali kulipa deni hili na kazi ikamilike ili huduma ziboreshwé na vijana wapate elimu bora na kuwasaidia katika maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za Bima ya Afya kwa hospitali binafsi nyingi hazijaingia mkataba, hivyo kutowapa fursa wanachama wa *NHIF* kufaidika na huduma hiyo. Hivyo basi, Serikali itoe mwongozo kwa hospitali zote binafsi kupokea Bima za *NHIF*. Vilevile namna ya kuhudumia wateja wa *NHIF* iwe bora zaidi kwa kuwa wateja wa *NHIF* hupewa Wauguzi wachache na kuathiri muda wa kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuathiri mila, desturi na imani zetu, Serikali haina budi sasa kuleta Sheria ya Ndoa ya 1971 iboreshwé ili kurekebisha umri wa mtoto kuolewa na kuo a iwe miaka 18. Kwa kuwa miaka ya sasa, elimu kwa watoto angalau idadi kubwa wanafika kidato cha nne, kwa nini tuondoe haki ya watoto kupata elimu ya sekondari ukizingatia kuwa sekondari takriban kila kata zipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, nchi haina dini, hivyo imani za watu wachache zisizuiwe haki za watoto kupata elimu na kuondokana na mimba zenye kuhatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa katika nchi zipo kikanda ili kusaidia mikoa yote, lakini Kanda ya Magharibi hatujaona katika hotuba ya bajeti. Hivyo, tunashauri Mkoa wa Katavi uwe na Hospitali ya Rufaa kwa Kanda ya Magharibi kukidhi Mikoa ya Katavi, Kigoma, Tabora na Rukwa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Wizara ya Afya haiwajibiki moja kwa moja, lakini kwa kupitia wafadhili mbalimbali na kutimiza sera mbalimbali hususan kupunguza vifo vya mama na mtoto, Halmashauri ya Nsimbo bado tunahitaji gari la wagonjwa kutokana na moja lillipo kuwa halikidhi mahitaji, sababu ya eneo liliyvo la Jimbo la Nsimbo na pia miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Saratani ya *Ocean road* inahitaji kutanua huduma zake kwenye Hospitali za Rufaa kila kanda na kuwa na watumishi wanaowajibika moja kwa moja ili kusogezza huduma karibu kwa wananchi kwa kuwa ugonjwa wa Saratani umekuwa tatizo kubwa hasa kwa akina mama (*cancer ya uzazi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaji wa Benki ya Wanawake bado kuongezwa kwa kiasi cha kukidhi haja za wanawake, nchi nzima, hivyo tunashauri Serikali iongeze mtaji kama tulivyotoa tangu mwaka jana bajeti ya 2016/2017. Vile vile Halmashauri nyingi hazijatumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, hivyo basi Wizara itoe taarifa kwa Wakurugenzi ili fedha zitoke na wanawake watumie fursa ya kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu na huduma za lishe ni muhimu sana ili kuondoa udumavu kwa watoto. Hivyo Wizara isimamie Halmashauri zote kuhakikisha zinatoa elimu

na kusimamia lishe kwa watoto kwa kuhakikisha wazazi wanachangia gharama za lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitoa taarifa nyakati tofauti kuwa mikoa tisa itapata Madaktari bingwa na Mkoa wa Katavi ukiwemo. Sasa zoezi hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri akubaliane nami kuwa afya ya kiumbe hai yejote inapotetereka na maisha yake pia yanakuwa hatarini wakati wowote. Kwa hiyo basi, afya ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu, kiumbe hai chochote ikiwemo mimea na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Hospitali ya Kaloleni iliyopo Mkoa wa Arusha ambayo imekuwa ikitumika sana sehemu ya kusaidia magonjwa ya mlipuko mfano, kipindupindu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hii haina vifaa kama dawa na hata dawa za kawaida tu za kutuliza maumivu zinashindwa kupatikana katika hospitali hii na hata karatasi za kuandikia (*description*) hakuna. Ukienda *Nurse* anakwambia kanunue daftari kwa ajili ya kuandikia. Hata dawa ya kufungia kidonda tu, hakuna. Mashuka ya kulalia na kujifunika hatuna na idadi ya mashuka hayo ni 15 tu, lakini Serikali imeshindwa kupeleka hata hii idadi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya *Mount Meru* inafanya kazi kama siyo Hospitali ya Rufaa kwa kukosa madawa na vifaa vingi vya matibabu na naona hata Serikali ilikosea kuipa hadhi ya Hospitali ya Rufaa, kama ilikuwa hajijajiandaa kupeleka vifaa hata vile muhimu tu. Achia mbali *MRI*, lakini *ultrasound, X-Ray*, hazifanyi kazi. Kuna

mashine mbili za *X-Ray*, moja ambayo ni nzuri inaweza kufanya au kupima vipimo vingi, haifanyi kazi kwa muda mrefu sasa na inayofanya kazi ni moja tu, ambayo haipimi vitu vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iangalie hospitali hii na kuitendea haki kama Hospitali ya Rufaa.

**MHE. BALOZI ADADI RAJABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga hoja mkono na kuwapongeza wote; Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya *NIMR* ni muhimu sana na ina sifa kubwa kwa tafiti mbalimbali za magonjwa ya binadamu Afrika na dunia kwa ujumla. Taasisi hii tawi lake lipo Muheza na lina mpango mahususi kabisa wa kuanzisha Chuo Kikuu kwa msisitizo wa masomo haya ya Tafiti za Binadamu, masomo ambayo hayapo hapa Afrika. Majengo yapo ila yanahitaji ukarabati kidogo huko Amani, Muheza. Sasa ni kwa nini Wizara haikutoa umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muheza. Tunaomba Wizara iangalie uwezekano wa kusaidia ujenzi wa hospitali ili isaidiane na Hospitali Teule ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kupeleka *CT-Scan* na utengenezaji wa *lift* katika Hospitali yake ya Bombo, Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ambayo yametolewa Kanda ya Ziwa, uwezekano wa magari hayo kutolewa kwenye Vituo vya Afya vya Muheza uangaliwe, maana kuna matatizo makubwa ya usafiri wa kuapeleka wagonjwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Chuo cha Mafunzo mbalimbali ambacho kipo maeneo ya Kiwanda, Muheza. Chuo hiki kipo chini ya Mheshimiwa Waziri lakini kimedharaulika kabisa, ni kama hakipo. Idara ya Ustawi wa Jamii imekisahau kabisa. Kina matatizo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam wake ili tushirikiane tuweze kukubaliana tutakisaidia vipi Chuo hiki kisife?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa juhudi zao wote Wizarani.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia uzima hatimaye nami nimepata fursa ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu katika Wizara hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, napenda nianze kuchangia kwenye Wizara hii kwa kuzungumzia Hospitali ya Mwananyamala. Hospitali yetu ya Mwananyamala imepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya rufaa, lakini kwa masikitiko makubwa bado Serikali haitoi ruzuku ya kuiendesha hospitali hii, badala yake, mzigo wote wa uendeshaji umeachiwa Manispaa ya Kinondoni peke yake. Kwa ukubwa wa hospitali, Manispaa inatumia kiasi cha Shilingi milioni 69 kwa wiki jambo ambalo ni mzigo mzito kwa Manispaa ya Kinondoni yenye changamoto lukuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, namwombwa Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini basi Serikali itaanza kutoa ruzuku ya uendeshaji wa Hospitali ya Mwananyamala kwa sababu sasa siyo Hospitali ya Manispaa ya Kinondoni tena? Aidha, kwa kuwa Hospitali ya Mwananyamala imepandishwa hadhi: Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mabwepande hasa ukizingatia kuwa Hospitali ya Mwananyamala imezidiwa na mlundikano na

wagonjwa, bila kusahau wakazi wa maeneo ya pembezoni, itakuwa ni mkombozi wao hasa kutokana na umbali na msongamano wa foleni za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Mwananyamala ina changamoto na matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Hospitali ya Mwananyamala inahudumia wagonjwa 2,500 kwa siku, wagonjwa wa kawaida na wagonjwa 1,500 vijana walioathirika na madawa ya kulevyta. Hivyo kufikisha jumla ya wagonjwa 4,000 kwa siku, jambo ambalo limepelekea upungufu wa Madaktari na Wauguzi, vifaa tiba na hata uhaba wa vitanda. Hivyo tunaiomba Serikali ituongezee Madaktari Bingwa 10 ili tuwe na 26; Madaktari wa kawaida (*General Medical Officer*) 20 ili tufikie 100 na Wauguzi 100 ili tuwe na Wauguzi 350.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba haya kwa kuwa hospitali hii inatuhudumia watu wote wa kutoka mikoa yote kwa sababu Kinondoni ndiyo Dar es Salaam na Dar es Salaam ndiyo Tanzania. Hivyo basi, Kinondoni ndiyo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa zinazotumika kwenye hospitali zetu, zinatoka katika maghala ya *MSD*. Wakati mwingine *MSD* inakuwa haina dawa inayotakiwa kwa wakati muafaka, hata kipelekeea maduka yetu na hospitali (za Serikali) kukosa dawa. Kwa bahati mbaya, hakuna ushindani katika jambo hili kwa maana ukikosa dawa *MSD*, basi unaweza kuzinunua kwa wengine kama Wakala wa Serikali, badala yake unatakiwa ufuate utaratibu wa kawaida wa Manunuzi ya Umma, jambo ambalo lina mlolongo mrefu wa kuchukua muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba, kwa nini isiweke ushindani katika biashara hii ya dawa ili kurahisisha upatikanaji wa dawa kwa wakati? Mfano *MSD* iweipo na Wakala mwingine kama *MSD*. Aidha, kwa nini Serikali isiweke masharti nafuu ya kununua dawa bila ya

kufuata mfumo wa manunuzi wa kawaida endapo *MSD* haina dawa inayotakiwa kwenye hospitali zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mwananyamala haina mashine ya *CT-Scan* na nyingine kwa ajili ya kupima baadhi ya wagonjwa. Wote tunajua hali za hospitali zetu na Serikali kwa ujumla. Aidha, hospitali ya Mwananyamala wanataka kumaliza jengo la Bima ya Afya na kununua mashine ya *CT-Scan* kwa mkopo kutoka Shirika la Afya kwa makubaliano ya kulipa kidogo kidogo kutokana na kukusanya malipo ya kuchangia gharama za matibabu hospitalini hapo: Je, Serikali iko tayari kuidhamini Hospitali ya Mwananyamala ili iweze kukopesheka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vifaa vyta vipimo ni għali sana; na vinahitajika sana hasa katika Hospitali yetu ya Kinondoni: Je, Serikali iko tayari sasa kutumia mfumo wa *PPP* (*Public Private Partnership*) ili wafanyabiashara na wanaotaka kushirikiana na Taasisi zetu za Umma waruhusiwe kwa makubaliano ya kugawana faida inayopatikana kutokana na uchangiaji wa gharama za vipimo?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali ya Awamu ya Tano ifanye ujasiri kama ilivyofanya kwa uchangiaji wa gharama za elimu, yaani kufuta uchangiaji wa gharama ya matibabu ya msingi iwe bure. Naomba hayo kwa sababu zifuatazo:-

(1) Idadi kubwa ya wagonjwa wetu katika afya ya msingi ni kutoka katika makundi maalum, yaani watoto wa chini ya miaka mitano, wazee wa zaidi ya miaka 60 na akinamama wajawazito. Hawa wote wametibiwa bure.

(2) Wagonjwa wa Ukimwi, Kifua Kikuu na Kisukari wote wanatibiwa bure. Hili nalo lina idadi kubwa.

(3) Vijana walioathirika na madawa ya kulevya, nao wanatibiwa bure.

(4) Maskini wanapaswa kutibiwa bure kwani asilimia 70 ya Watanzania ni maskini, wanaishi chini ya dola moja na hasa Watanzania wa Vijijini, wanastahili kupata huduma ya afya bila malipo.

(5) Serikali inatoa dawa (fedha za dawa) kwa Vituo vya Afya nchi nzima, dawa ambazo zinaweza kuwatibia wagonjwa bure.

(6) Utaratibu wa Bima, wananchi wengi wakijiunga na Bima inatosha kugharamia wachache wallobaki kuweza kupata huduma bure.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mbunge na Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana. Jambo la kwanza, naipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ya kuwatumikia wanyonge; pili, nyongeza ya Wizara, hii Bajeti itaweza kuwasaidia Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie Jimbo langu la Rufiji. Kwa bajeti mbili sasa za Wizara hii, Serikali imesahau Wilaya ya Rufiji. Mwaka 2016 haikutengwa fedha yoyote kwa ajili ya Hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji ni moja ya maeneo ambayo Serikali inapaswa kutoa kipaumbele sana. Hii ni kutokana na kwamba, kwa muda mrefu Jimbo la Rufiji limesahaulika. Kwa sasa tuna changamoto kubwa sana za kiusalama; kumewepo na ujambazi mkubwa na mauaji yanayoendelea; na kunahitajika mahitaji makubwa ya huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ilijengwa mwaka 1960, lakini mpaka sasa haijawahi kukarabatiwa na

majengo mengi ni mabovu yanayohitaji kubomolewa. Hakuna hata vitanda vya upasuaji; kilichopo kimoja ni cha miaka ya 1960; hali ya hospitali ni mbaya sana. Wakati wote yanapotokea matatizo makubwa kwa watu kudhuriwa kwa risasi, tunalazimika kusafirisha majeruhi kwenda Wilaya ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji ilizaliwa kabla ya uhuru, lakini ndiyo Wilaya yenye matatizo makubwa. Umuhimu wa kuiboresha Hospitali ya Wilaya hauepukiki, kwa kuwa umbali uliopo kutoka Rufiji kwenda Hospitali ya Mkoa wa Pwani ni wa masaa zaidi ya sita kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Utete. Wagonjwa wengi hufia njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naipongeza Serikali kwa kutuletea Mganga Mkuu Mchapakazi. Naomba huruma ya Mheshimiwa Waziri, akisaldie Kituo cha Afya Ikwiriri kuongeza vifaa na ununuzi wa jenereta; Kituo cha Afya Moholo, kutuongezea fedha za ununuzi wa vifaa; na ujenzi katika Kituo cha Afya Mwaseni Mloka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akifika hapa azungumze kauli ya Wizara yake ili kuweza kusaidia Watanzania wanyonge walioko Rufiji ambao hukosa msaada wa matibabu kutokana na hali ya Hospitali yetu ya Wilaya iliyojengwa mwaka 1960; akinamama wanakufa kutokana na uhaba wa Watumishi, kuwashudumia majeruhi wanaoshambuliwa na majambazi, matatizo yanayoendelea kila wiki sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. QULWI W. QAMBALO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ina umri wa zaidi ya miaka 20 na bado haina Hospitali ya Wilaya. Wananchi wengi na hasa wazee, akinamama na watoto wanapata shida sana kufuata matibabu mbali. Tunacho Kituo cha Afya Karatu ambacho kina miundombinu ya kutosha na kama Wilaya na Mkoa tumekubaliana kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya.

Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Afya aone umuhimu wa kupandisha hadhi kituo hicho ili kichukue nafasi ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sera katika Wizara hii inayosema kuwa na *dispensary* kila kijiji na Kituo cha Afya kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ina Kata 14 na ni Kata tatu tu zenye Vituo vya Afya. Huu ni upungufu mkubwa sana. Hata hivyo, vitatu vina upungufu mkubwa wa vifaa tiba na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko *dispensary* zimefungwa kwa kukosa watumishi mfano Zahanati ya Makhomba Endashangwet na kadhalika. Suala la afya ya wananchi wetu ni suala muhilmu sana. Nchi yetu ni ya wakulima na illi mtu alime anahitaji afya timamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la maendeleo ya Jamii limesahaulika kabisa. Kitengo hiki kinapaswa kuwa injini katika Halmashauri zetu maana hawa ndio wanapaswa kufanya maandalizi ya jamii ili mradi iweze kufanikiwa. Huko nyuma tulikuwa na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, mfano Tengeru, Monduli na kadhalika. Vyuo hivi vimetoa wataalam wazuri sana wa kuwahamasisha wananchi kupokea miradi na kuwaandaa ili mradi iwe endelevu. Hali ilivyo sasa, kitengo hiki kimemezwa na Idara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwawezeshe watumishi wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii ili wawafunze wananchi kwa utekelezaji wa miradi.

**MHE. KANYASU J. CONSTATINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia *Ambulance* na pia mgawo na Madaktari wanne ambao tayari wamefika Geita. Kwa bahati mbaya mmoja bado yupo masomoni China mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yafuatayo:-

(i) Hospitali yetu ya Wilaya imekuwa ya Rufaa ya Mkoa, kwa sasa imezidiwa sana na wagonjwa, gharama za dawa na huduma ziko juu kwa *level* ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Naomba sana juhudhi za kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mheshimiwa Waziri aipe kipaumbele ili kupunguza gharama kwa wananchi.

(ii) Bado tuna uhaba mkubwa sana wa Madaktari Bingwa, Madaktari wa katni na wahudumu wa Afya, kama *Nurses* na watu wa Maabara. Naomba sana mwaka huu wakati wa mgao wa Watumishi wa Afya, Wizara isaidie kuitazama Hospitali ya Geita kwa jicho la huruma. Pamoja na suala hili kuwa la TAMISEMI bado Wizara ndiyo yenye jukumu.

(iii) Bado hospitali ya Rufaa ya Geita tunahitaji Duka la Dawa la *MSD*. Kosa kubwa limefanyika Geita ni kupeleka Duka la *MSD* Hospitali ya Wilaya Chato ambapo hakuna wagonjwa wengi, matokeo yake mahitaji ya msingi yamesahaulika au kupuuzwa. Ombi langu, Duka hili la Makao Makuu ya Mkoa lifunguliwe.

(iv) Ufanisi duni wa *MSD*, Halmashauri zetu zimekosa dawa muhimu kwenye bohari ya dawa, mafunzo yake, pesa hiyo inatumika kununua vifaa ambavyo siyo vya lazima na kuacha uhaba wa dawa ukiwa pale pale, matokeo yake *MSD* wanatoa *O/S release* kwenda kwa *Private Vendor's* ambaao huuza dawa na vifaa tiba kwa gharama kubwa, mara kumi zaidi ya bei ya soko ambalo watu wa kawaida wanunu. Hii maana yake ni kwamba pesa ya kutosha kutoa huduma mwezi mmoja kwa gharama za *Private Vendor's* inatumika siku 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuhakikisha *MSD* wanazo dawa wakati wote kuepuka kupoteza fedha za umma.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha kuwa ugharamiaji mdogo umedhoofisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za *BRN* mwaka 2014 zinaonesha kuwa matumizi ya Serikali katika Afya ni asilimia 11.1 ya matumizi yote ya Serikali. Sekta hii ni muhimu kwa ustawii wa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati nyingi katika Halmashauri zote za Katavi, Nsimbo, Mlele na Mpanda; asilimia 90 ya zahanati hizi za Katavi ziko nje ya mji. Kwa jiografia, ni ngumu kidogo. Wananchi wanateseka, wanasafiri kutoka Kata ya Kabage Jimbo la Tanganyika, umbali wa kilometra zaidi ya 40 kufuata zahanati katika Kata ya Isengule au Kapala, Msenga, anafika Zahanati ambayo haina dawa wala Wauguzi. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kila kata inapata huduma za afya bila kusafiri umbali mrefu kiasi hiki? Huu ni unyanyasaji kwa watu wa vijiji hususan Katani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa Fedha Serikali ilitenga shilingi 1.99 sawa na asilimia 9.2% ya bajeti yote ya Serikali. Bajeti ni ndogo sekta hii ni kubwa mno na Wizara ni pana, naomba iongezewe bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na jamii yenye uwezo kwa kuchangia katika ujenzi wa uchumi, hatuwezi kukwepa kuwekeza ipasavyo kwenye Sekta ya Afya. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Mkao Katavi? Hospitali iliyopo ni ndogo na mahitaji ni makubwa mno. *Oxygen Machine* ni moja tu haikidhi mahitaji ya Wanakatavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 alifariki Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda. Inawezekana tungekuwa na mashine za *oxygen* mbili au tatu, Mkurugenzi angepona kwa sababu siku hiyo Mkurugenzi huyu anapata shida ya kupumua, mashine ilikuwa inatumiwa na mama mjamzito aliyekuwa hoi *threate*. Je, hamwonni kwamba kwa uchache huu Serikali itaendelea kupoteza watu na viongozi bila sababu zisizo na msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara iangalie Mkao wa Katavi, iongeze bajeti, vifaa tiba, dawa na *BP machine*.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa kipaumbele kwa Wizara ya Afya. Hivyo basi, pongezi pia ziende kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Samia Sulu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pongezi nyingi kwa Waziri husika Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake Dkt. Hamis Kigwangalla na Watendaji wote, kwa kusimamia vyema Wizara hii na matunda tunayaona, pamoja na ufinyu wa bajeti. Waswahili husema, ng'ombe haelemewi na nunduye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ipandishe hadhi baadhi ya Vituo vya Afya vilivyopo Mkoa wa Pwani. Hii ni kutokana na umuhimu wa kuongeza/kupanua huduma kwa jamii. Vituo hivyo ni Kibiti, Muhoro (Rufiji), Mlandizi (Kibaha Vijijini), Ubena (Chalinze), Mzenga (Kisarawe) na Kibaha Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa kutaimarisha huduma hizo, pia vituo hivi viko barabara kuu za mkoa ambapo usafiri wa aina mbalimbali hupita hivyo, endapo kukitokea ajali kunakuwa hakuna uwezo wa kutoa huduma na hivyo kulazimika kusafiri kwenye Hospitali za Wilaya au kupelekwa Hospitali za Mkoa jirani, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde, pamoja na matatizo ya kiufundi (kama yapo) tusaidiwe X-Ray ya Mafia ipate ufumbuzi wa kufungiwa, ukizingatia Mafia ni kisiwa na hawana pa kukimbilia endapo imetokea dharura. Nimalizie kwa kuomba suala la maji kwa zahanati na vituo vya afya. Ni muhimu, kuwe na elimu ya uvunaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na Serikali kwa kujitahidi kutatua changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna mahali popote amezungumzia Hospitali ya Mkoa mpya wa Songwe. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga au kuimarisha Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, yaani Vwawa kwa kuongeza wataalam, vifaa tiba na bajeti ya hospitali ili itoe huduma kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu mahitaji ya Madaktari na Wahudumu wa Afya katika zahanati, vituo vya afya na Hospitali ya Vwawa. Hivi sasa Mhudumu wa Afya yaani (*Nurse*) anahudumia *ward* zaidi ya moja. Zahanati nydingi zimekamilika lakini zimekosa wafanyakazi, bado kufunguliwa. Suala hili linawakatisha tamaa sana wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu umaliziaji wa majengo ya Vituo vya Afya katika sehemu mballmballi. Madai ya muda mrefu ya stahili za Madaktari wa Wilaya ya Mbozi hususan Hospitali ya Vwawa kama vile *Night Call Allowance, allowance* za majukumu na kadhalika, tafadhali naomba yashughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu; naomba maelezo ya kina, nini kinaendelea juu ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Songwe? Hii ningependa majibu ya kina.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri. Pamoja na pongezi hizo, kwa kifupi, lazima niwaombe mambo mawili, matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Ambulance* mbili kwa Halmashauri ya Arusha *DC* kwa ajili ya Kata zangu mbili za Oldonyowas na Kata ya Bwawani. Hali za wanawake na watoto kwa maeneo haya ni mbaya. Panapotokea dharura, wanataabika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Mkoa haina mashine za *X-Ray*, *CT-Scan* na *MRI* na hata huduma ya *Ultra sound* haitolewi hospitalini hapo. Umuhimu wa vifaa hivi katika

hospitali kama *Mount Meru*, wote tunaujua. Mheshimiwa Waziri atusaidie wakazi wa Arusha na viunga vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huduma za Bima za *NHIF*na *CHF*ziboreshe ili wananchi wawe na imani nayo, ili waweze kujunga kwa wingi na mifuko hii iweze kuwa na tija na iweze kupata uwezo zaidi. Kwa sasa hata sisi wanasiwa tunaogopa kuwahimiza wananchi kujunga na mifuko hii, kwani changamoto za matibabu ni nyinyi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haya tu kwa sasa. Shukrani.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mtwara ya Mkoa haina *X-Ray* na iliyopo ni mbovu. Naomba kuuliza, kwa nini hospitali hii ya Mkoa wa Mtwara haipelekewi *X-Ray* ya uhakika wakati kila mwaka tunaongea hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali inayotumika kama ya Wilaya inaitwa Hospitali ya Likombe iliyopo Mtwara Mjini, kwa nini haina *X-Ray* mpaka leo? Bajeti ya mwaka 2016/2017 Mheshimiwa Waziri alisema hospital hizi za Mtwara Mjini zitapelekewa *X-Ray*, mpaka leo bado. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge wamepewa *Ambulance*: kwa nini Mtwara Mjini Wizara hajatuletea *Ambulance* hizo? Naomba Wizara itueleze Wanamtwara Mjini, juu ya *Ambulance* kwa ajili ya Tarafa ya Mikindani na Tarafa ya Mjini ili kuondoa kero na adha kubwa wanayopata wagonjwa wa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wodi ni chache katika Hospitali ya Likombe ambayo ndio Hospitali ya Wilaya, Mtwara Mjini. Naomba kujua, ni lini wodi zitaongezwa, nyumba za Madaktari na Wauguzi wa Hospitali ya Likombe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira ya Wodi za Hospitali ya Mkao (Ligula) siyo nzuri kabisa, naomba hospitali ipakwe rangi, vyoo vitengenezwe na huduma ya maji katika Hospitali ya Ligula yarekebishwe haraka iwezekanavyo, maana hali ya vyoo ni mbaya sana katika hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Waziri katika kitabu chake kinaonesha Mtwara Mjini dawa zinapatikana kwa asilimia 92% kitu ambacho ukienda Hospitali ya Ligula ya Mkao na Wilaya hali ni tofauti kabisa. Wagonjwa wanaambiwa baada ya siku mbili tu dawa zimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi, kwa nini tunaambiwa dawa zinapatikana kwa asilimia kubwa, lakini hospitali dawa hakuna na zikiwepo zinakwisha kwa siku mbili tu?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kusikiliza kilio cha Wanaliwale na hatimaye kutupatia Madaktari wawili hivi karibuni. Namwomba Mungu awaongezee umri mrefu. Hata hivyo, naendelea kusisitiza kuwa tatizo la ikama ya watumishi katika Wilaya ya Liwale bado ni tatizo kubwa. Wilaya ya Liwale yenye Kata 20 na Vijiji 79 ina Zahanati 31 tu na Kituo Kimoja cha Afya. Jambo hili linaifanya Hospitali ya Wilaya kuwa na mzigo mkubwa kuliko uwezo wa hospitali hiyo. Zahanati zote zinaendeshwa na *enrolled nurses (EN)*. Wilaya nzima ina *Clinical Officer* wanne tu. Vile vile kuna mashine ya *X-Ray* ambayo haina mtaalam wa kupiga picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Halmashauri kuwa na mapato kidogo na hivyo kushindwa kujenga hospitali mpya ili kukidhi mahitaji ya sasa kwa hospitali iliyokuwepo, ni ile iliyokuwa Kituo cha Afya cha Liwale Mjini kwani miundombinu ya hospitali hiyo siyo rafiki kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa madawa kwenye Halmashauri ya Liwale ni mdogo sana hasa ukilinganisha na Halmashauri za jirani. Ni bora sasa Serikali ikatumia takwimu

za Hospitali hiyo badala ya kutumia takwimu za mwaka 2012 (sensa). Kwa maneno mengine, kuna wakazi zaidi ya 10,000 wa Wilaya ya Liwale ambao hawana dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inatambua kuwepo kwa wazee nchini, kwa nini Serikali haitaki kuleta Sheria ya Wazee nchini ili kuwatambua huko, kuwepo kisheria. Wazee wengi nchini wanaishi kama wakiwa, kienyeji, kwani hawajui hatima yao katika nchi hii. Hawazijui haki zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri alete hiyo sheria hapa kwa kuzingatia kuwa wote ni wazee watarajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na ukiritimba mkubwa sana juu ya matengenezo na service za mashine za *X-Ray* nchini. Hadi sasa kampuni pekee iliyopewa kazi hiyo nchi nzima ni Kampuni ya *Phillips*. Je, Serikali haioni imefika wakati sasa wa kutafuta kampuni nyingine, kwani kampuni hiyo imeshindwa kazi? Ubovu wa mashine za *X-Ray* ni wa nchi mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Mama na Mtoto pamoja na kupewa kipaumbele katika Wizara hii, bado utekelezaji wake siyo wa kuridhisha kwani huduma hii bado hajjawafikia akinamama wa vijiji mahali ambapo zahanati au vituo vya afya vikiwa mbali na vijiji hivyo. Hata hivyo ni vyema basi Serikali ikawekeza zaidi kwenye miundombinu ya usafiri vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa fedha ni jambo linalofanya Halmashauri nyingi kukosa dawa licha ya kuwa wanalipa dawa hizo, *MSD* haina uwezo kuleta dawa kwenye Halmashauri zetu kwa mujibu wa mahitaji ya Halmashauri husika. Vile vile wakati mwingine huleta dawa nje ya wakati na pengine nje ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Posho ya Mazingira Magumu (*On Call Allowance*) kuziacha chini ya Halmashauri ni kutokuwatendea haki watumishi wa kada ya Madaktari kwani vipaumbele vya Halmashauri hutofautiana toka Halmashauri moja hadi nyingine, hivyo kukosa uwiano wa

vipato vya watumishi hawa. Hivyo ni bora posho hizi na *allowance* zake zikachukuliwa na Wizara husika ili zitolewe kwa mazingira yalivyo sasa kwa watumishi wa ngazi husika kutokana na mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna ubaguzi mkubwa sana wa watumishi kupandishwa madaraja. Kuna watumishi wa muda mrefu hawajapandishwa wakati wapo wa muda mfupi wamepandishwa japo wana vigezo vinavyolingana, jambo linalopunguza morali ya kazi na ufanisi kazini. Vile vile viko vitendo kwa kuadhibu watumishi kwa kuwashusha vyeo na mishahara yao bila kuzingatia sheria za kazi. Jambo hili hupunguza ufanisi wa mhusika na matokeo yake hasira zote huishia kwa wagonjwa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa vitengo mbalimbali vya Wizara ya Afya. Pamoja na juhudhi za Serikali za kuisaidia sana Hospitali ya Muhimbili, lakini bado kuna changamoto nydingi ikiwemo ya upungufu wa Wauguzi na Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na wagonjwa wengi katika Hospitali ya Muhimbili kunatokana na kutoimarka kwa Hospitali za Mikoa na Wilaya, kunasababisha Hospitali ya Muhimbili kuzidiwa na wingi wa wagonjwa. Naomba Serikali iangalie upya na kuzidi kuziimarisha hospitali zetu za Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuongeza teknolojia ya kupunguza muda wa kupata mionzi. Sambamba na hilo, naomba Serikali wafanye tafiti mbalimbali kutafuta kila kinachosababisha ugonjwa na kuongezeka kwa haraka sana. Kansa inaua watu wengi sana. Kwa sasa inaonekana hakuna dawa kutokana na watu kukosa elimu ya kutosha kutokana na viashiria vya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa *MOI*. Wagonjwa wa mifupa wamekuwa wengi wanakaa kwenye *waiting list* ya kusubiri *operation* kwa

muda mrefu sana kutokana na kitengo hiki kuzidiwa na wagonjwa, lakini pia upungufu wa Madaktari. Pamoja na kwamba natambua kinachosababisha hayo ni wenye bodaboda, ndio walio wengi na wanababisha ajali kuwa nyingi sana, majeruhi wamezidi *MOI* kutokana na ajali za barabarani: Je, Serikali inaisaidiaje *MOI* kudhibiti ongezeko la ajali za barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali isaidie *MOI* kwa kuongeza kujengea uwezo Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala. Serikali ikizijengea uwezo Hospitali hizo za Mkao wa Dar es Salaam zinaweza kusaidia sana katika kuipunguzia *MOI* msongamano. Naomba pia hospitali hizo ziweke vitengo vya mazoezi ya viungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Kitengo cha *Emergency* cha Muhimbili. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kiasi cha kufanya wananchi wajenge imani ya kupona hapo. Kwa kweli wagonjwa walio wengi wanaokuja mahututi wanaamka hapo; kama kufa, wanaenda kufia kwenye wodi kama hawatapata huduma stahiki. Naomba vitengo vya *emergency* vya Hospitali ya Temeke, Amana na Mwananyamala nazo ziwe na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi za Mkuu wa Mkao kuamua kusaidia katika kujenga majengo ya huduma za dharura katika Hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala, lakini naomba Serikali iongeze nguvu kwa kuleta vifaa kwa hizo *emergency Unit* zilizopo, tupate angalau huduma kwa kipindi hiki cha mpito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa uamu wake wa kujenga vyumba vya upasuaji kwa kila hospitali au zahanati kwa lengo la kuokoa afya ya mama na mtoto. Changamoto kubwa iliyopo Muhimbili imezidiwa na wingi na akinamama; wazazi ni wengi lakini watoa huduma ni wachache na hasa Wauguzi. Kwenye wodi moja unakuta wauguzi ni wawili. Naomba Serikali ituongezee Wauguzi na

Madaktari katika Hospitali ya Temeke, Amana, Mwananyamala na Vituo vya Afya vilivyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ina ongezeko kubwa la wageni wanaokuja takriban mabasi 300 yanaingia kila siku kutoka mikoani. Hivyo tunahitaji ongezeko la bajeti katika huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya akili yameongezeka sana, kwa mfano Hospitali ya Temeke imetoka kwenye wagonjwa watano hadi saba mpaka wagonjwa 105 mpaka 120, lakini hakuna wodi za wagonjwa wa akili katika Hospitali za Mikoa ili kupunguza msongamano wa wagonjwa wa akili Muhimbili. Naomba Madaktari wapewe posho Maalum ya Mazingira Hatarishi ya maisha yao kwani wagonjwa wanaowahudumia ni wa hatari sana. Sambamba na Madaktari na Wauguzi wa Wagonjwa wa Akili, Serikali ifanye utafiti, ni tatizo gani linafanya ongezeko la maradhi ya akili kuongezeka kwa kasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa watoto kudondoka ni tatizo kubwa sana. Walianza wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari na sasa wanaanguka hata watoto wadogo ambao hawajaanza shule. Naiomba Serikali iangalie kwa kina, ni nini kimekosekana au ni madini gani yamekosekana mpaka watoto wanaanguka ovyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Madawa ya Kulevyia vimezidiwa sana. Kulingana na juhudzi za Serikali kupiga vita madawa ya kulevyia, ambazo naunga mkono, ongezeko la wagonjwa hao ni kubwa sana na huduma inahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iongeze vituo vya *Methadone* katika Hospitali ya Kigamboni kuwasaidia vijana kuepukana na tatizo la nauli ya kufika Temeke. Pia Kituo cha Muhimbili, Mbagala na Chamazi kinachohudumia wagonjwa wa akili, naomba kiwekwe kituo cha *Methadone* kusaidia vijana wa Mbagala, Chamazi,

Tuangoma, Kijichi na Mbagala Kuu wapate huduma hiyo kwa urahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kutengea hii Hospitali ya Chanika ambayo itatusaidia sana katika kupunguza idadi ya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Muhimbili, wodi ya wazazi mpya, kwa sisi Dar es Salaam tunaita Jengo la Rais Magufuli. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwasaidia akinamama wajawazito. Kwa kweli jengo lile ni mkombozi wa wanawake. Limesaidia sana kiasi cha kujuliza, wale akinamama kama kungekuwa hakuna jengo lile tungewaweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wanaruhusiwa saa 8.00 mchana lakini wanatoka hospitali saa 2.00 usiku kusubiri bili za kawaida na Bima ya Afya. Kitengo cha *accounts* kiongezewe nguvu, kero hii ni kubwa. Usiku una mambo mengi, wazazi wanaweza kuibiana watoto ikawa tatizo kwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, asilimia mia kwa mia.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Fungu 52 inaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea sh. 314,673,230.000.95 sawa na asilimia 43 ya bajeti ya Wizara, zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu fedha za maendeleo, randama zinaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 ni asilimia 34 tu ya fedha za ndani ndizo zilitolewa na Hazina na kwa fedha za nje ni asilimia sita tu ya fedha hizo zilitokuwa zimetolewa na Hazina kwa kipindi hicho. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani haijatekelezwa kwa asilimia 63 na kwa fedha za nje haijatekelezwa kwa asilimia 94. Kwa utekelezwaji huu duni

wa bajeti ya maendeleo katika fungu hili, maoni yangu ni kwamba Serikali iwe makini kabisa na afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu 53, kwa mwaka wa fedha 2016 - 2017 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 49.9. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 41 na shilingi bilioni 8.848 zikiwa ni fedha za maendeleo. Hata hivyo, fedha za maendeleo hadi kufikia Machi, 2017 ni sh. 497,718,250/= sawa na asilimia 5.62 tu ya shilingi bilioni 8.8 zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni kwamba bajeti ya maendeleo katika fungu hili la Maendeleo ya Jamii haikutekelezwa takriban kwa asilimia 95. Fungu hili ndilo linalohusika na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; na kwa maana hiyo, utekelezaji duni wa bajeti wa vyuo hivyo haviwezi kuwa na uwezo wa kujindesha na kuzalisha wataalam wa kusaidia jamii zetu kujiletea maendeleo kwa kuweza kuibua fursa zilizo katika jamii zao.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kutekeleza majukumu yao vizuri pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara na Serikali kwa ujumla. Hakika mimi binafsi nardhika sana na utendaji wao na nawaomba waendeleze ubunifu, uadilifu na kujituma katika kuwashudumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza zaidi kwenye changamoto ya uhaba wa vituo vya tiba katika Wilaya ya Malinyi (Morogoro). Wilaya ya Malinyi ina Kituo kimoja tu cha Afya cha Mtimbira na haina Hospitali ya Wilaya. Halmashauri imependekeza kukipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Mtimbira ili kiwe na hadhi kama ya hospitali ili kiweza kuhudumia wananchi wengi wanaohudumiwa na kituo hicho lakini majibu ya Serikali bado hayakubaliani na ombi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na changamoto za Kituo hicho cha Afya cha Mtimbira, tunaiomba Wizara kuona namna mbadala au kutoa upendeleo wa kipekee kwa kuongeza mgao wa dawa, watumishi, vitendanishi na kadhalika ili kukidhi mahitaji halisi ya wagonjwa wanaohudumiwa na kituo hicho cha afya. Halmashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI, tutajitahidi kujenga vituo vingine vyta afya katika Halmashauri ya Malinyi lakini katika kipindi hiki cha mpito, tunaiomba Wizara ya Afya kuliangalia ombi letu la Kituo cha Mtimbira kupata hadhi ya hospitali. Ahsante.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuwa nilipata dakika chache za kuchangia kwa kuzungumza, hivyo, maelezo haya ni nyongeza ya mchango wangu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ndiyo Taifa lenyewe. Bila ya afya, bila mazingira mazuri ya wazee wetu na watoto wetu, bila mfumo nzuri wa jinsia - mahusiano ya wanawake na wanaume maendeleo ya jamii hayatapatikana. Kwa masikitiko makubwa Wizara hii imekumbwa na tatizo sugu la utendaji wa Serikali ya CCM tatizo la kutopeleka fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa Wizara na Taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inasema katika ukurasa wa 19 kuwa, bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017 hajatekelezeka kwa asilimia 60%. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za mwaka 30 Machi, 2017. Hii ni kucheza na uhai na maisha ya Watanzania/wananchi wetu. Katika mjadala wa bajeti kwa mwaka 2016/2017, nilishauri kuhusu kubadili mfumo/utaratibu/mchakato wa bajeti nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa bajeti unafanyika kama ni jambo la kawaida tu kufanyika miaka nenda rudi matatizo na kasoro zile zile zinaendelea kujitekeza lakini Serikali haioneshi dalili za kubadilika ili kuwa na mchakato wa bajeti inayoteklezeka na unaoweza kuleta tija katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kulifanya kazi kwa umuhimu wa kipekee ni takwimu kuhusiana na upungufu wa wataalam wa afya zilizotolewa na hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye ukurasa wa saba. Picha hii inatisha sana na si jambo la kupuuzia hata kidogo. Tukibadili mchakato wa bajeti na kuufanya kuwa '*integrated*' itasaidia kuwa na vipaumbele vichache vyta Taifa badala ya huu utaratibu wa sasa unaokuwa na vipaumbele vingi kwa kila Wizara, matokeo yake ndiyo hili tatizo sugu la bajeti zisizotekelzeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *intergrated budget process* itasaidia kuondoa tofauti kubwa za kimaendeleo na utoaji huduma za msingi za jamii. Kujenga barabara za kisasa, *flyovers* na usafiri wa mwendo kasi katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kigezo cha mchango wake katika pato la Taifa ni sawa lakini muhimu vilevile kuangalia *spill-over effects* zake kwa maeneo mengine na haki ya Taifa. Maeneo mengi ya vijijini likiwemo Jimbo langu la Mafia yanaendelea kubaki nyuma katika maendeleo na upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mafia ina matatizo lukuki kuanzia wafanyakazi mpaka vifaa, inafikia wakati Nesi mmoja anapangiwa wodi mbili. Uwepo wa hospitali ilio kamili/inayojitosheleza ni muhimu sana kwa Wilaya ya Mafia kutokana na jiografia yake kuwa kisiwani. Wilaya ya Mafia haina usafiri wa kuvuka kwenda Dar es Salaam au Mkuranga ili kupata huduma kama za *X-ray* au rufaa husika. Namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie Hospitali ya Wilaya ya Mafia kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge. Hata hivyo, nawapongeza sana Waziri na Naibu wake kwa uwajibikaji wao mahiri. Ni matumaini yangu Serikali itawapa mazingira mazuri ya kufanya kazi hii adhimu. Nashukuru sana.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Waziri, Naibu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri wa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ambalo nalirudia mara kwa mara katika Wizara hii ni upungufu wa Madaktari na Wauguzi katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Handeni. Hili ni tatizo kubwa sana na mara kwa mara hutokea vifo wagonjwa wakiwa wanasubiri huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaliongelea kwenye kipindi cha maswali na majibu, Hospitali ya Wilaya ya Handeni inahudumia takribani majimbo manne na ukiangalia hakuna bajeti yoyote ya kujenga hospitali nyiningine hivi karibuni. Kutokana na hilo, hospitali inaelemewa na uhitaji wa vifaa tiba. Namwomba Mheshimiwa Waziri na kwa vile ameshatutembelea na anajua hali yetu, basi atuangalle kwa jicho la tatu kwenye vifaa tiba na madaktari. Namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho aizungumzie na Hospitali yetu ya Handeni ili hata wananchi wetu wapate imani kwamba matatizo yetu yatafanyiwa kazi.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu kwa maandishi kuhusiana na hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja Watendaji wake kwa kuandika hotuba hii kwa ufundi na utaalam mkubwa, namwombea kila la kheri katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu rasilimali watu katika sekta ya afya. Rasilimali watu ni miongoni mwa jambo muhimu katika nchi hasa katika Wizara kama hii ambayo inahitaji utendaji wa kitaaluma zaidi. Ushauri wangu

katika Wizara hii ni kuongeza juhudini ya kuwasomesha Watanzania katika fani zote hasa ya udaktari ili kupunguza pengo kubwa liliopo kati ya Madaktari na wanaohudumiwa. Takwimu zinaonesha kuwa uwiano (*ratio*) kati ya Madaktari na wagojwa ni mkubwa sana. Hivyo juhudini za makusudi zinahitajika ili kuondoa kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuongelea kuhusu uboreshaji wa huduma za uchunguzi. Uchunguzi wa maradhi ni hatua muhimu sana katika matibabu. Mgonjwa anapochunguzwa na kuonekana kinachomsumbuu ni mwanzo mzuri wa matibabu. Ushauri wangu katika jambo hili ni kwa Serikali kuongeza fedha za kutafutia vifaa vya kisasa zaidi vinavyoweza kuchunguza maradhi kwa ubora zaidi. Kuna matukio mengi ambapo wagonjwa wanachunguzwa na kupewa majibu ambayo ni tofauti na maradhi yanayowasumbua. Hii ni kutokana na kutumia vifaa ambavyo havina ubora. Hivyo juhudini za makusudi zinahitajika ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu udhibiti wa UKIMWI. Naipongeza Wizara kwa juhudini kubwa inayochukua kudhibiti na kuwashudumia waathirika wa maradhi ya UKIMWI. Napenda kuishauri Wizara kuongeza juhudini ya kutoa elimu kwa wananchi hasa wa vijijini ili kuelewa zaidi sababu zitakazowafanya wapate maradhi hayo. Inaonekana kuwa elimu ya UKIMWI inatolewa zaidi katika miji na kidogo sana katika vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu fedha za *Busket Fund- Mafinga Town Council*. Suala hili nimelizungumzia mara kadhaa katika jitihada za kutafuta ufumbuzi. Tulitembelea TAMISEMI tukaonana na viongozi wa Wizara akiwemo NKM na Mkurugenzi wa Huduma za Afya. Ombi letu, Serikali itoe maelekezo mahsusini kwa Halmashauri Wilaya ya Mufindi sehemu ya fedha wanayopokea iende kwenye Hospitali ya

Mafinga ambayo inahudumia Wilaya nzima (*Mafinga TC* na *Mufindi DC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, mwaka 2016/2017, *Mafinga TC* tulipangiwa shilingi milioni 101, *Mufindi DC* walipangiwa *around* shilingi milioni 700. Kwa mwongozo, inatakiwa 30% ya fedha hiyo iende ikahudumie hospitali. Kabla hatujawa Halmashauri mbili tulipokea *around* shilingi milioni 800 ambapo 30% yake sawa na shilingi milioni 240 ilienda kuhudumia Hospitali ya Wilaya lakini ilivyo sasa *Mafinga TC* tunapokea *around* shilingi milioni 100 ambapo 30% yake ni *around* shilingi milioni 30 ndiyo inayoenda kuhudumia hospitali. Kwa hiyo, utaona upungufu kutoka shilingi milioni 240 mpaka shilingi milioni 30, ni punguzo kubwa, tunapokea 12.5% tu ya kuhudumia hospitali suala ambalo linaathiri mno utendaji wa kazi na kuhatarisha maisha ya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu, kwa kuwa Hospitali ya Mafinga inahudumiwa na *Mafinga TC* lakini *function wise* hospitali inahudumia Halmashauri zetu mbili, Serikali kwa maana ya Wizara ya Afya na TAMISEMI, itoe maelekezo kwa Halmashauri ya Mufindi ili sehemu ya fedha za *Busket Fund* zipelekwe *Mafinga TC* kwa nia ya kuhudumia hospitali ya Mafinga inayohudumia Wilaya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni fedha za Mfuko wa Wanawake (5%). Nimepitia kitabu na *Mafinga TC* ni katika ya Halmashauri chache sana ambazo hajizawapa vikundi vya wanawake fedha zao. Hii ni kutokana na *conflicting interests*. Nashauri na naomba Wizara izitake Halmashauri hizo zitoe maelezo kwa nini mpaka sasa tupo robo ya mwisho ya mwaka fedha hizo hajizatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ukiangalia katika Jedwali hata Halmashauri ambazo zimetoa fedha, *percentage wise* ni kasi kidogo sana. Hali hii inatokana na ukweli kwamba Halmashauri zinachukulia suala la 5% ya fedha ya Mfuko wa Wanawake kimzaha. Nitatoa mfano, kwa mujibu wa mwongozo wa matumizi ya fedha za makusanyo

ya ndani 5% + 5% = 10% ni ya wanawake na vijana, 50% ya kuendeshea ofisi na 40% kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, haijawahi kutokea ile 50% ya kuendeshea ofisi ikakosekana. Halmashauri zinatumia kila kinachokusanya kwa ajili ya kuendeshea ofisi na kupuuza kutenga fedha za Mfuko wa Wanawake. Je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha kuwa suala hili haliendelei kujirudia kwa sababu hata Kamati ya *LAAC* suala hili limekuwa likirudia kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu kutoa ruzuku/mkopo kwa wanafunzi wa kozi za uuguzi. Nimekuwa nikipendekeza kuwa kwa kuwa mahitaji ya kada hizi kuanzia *AMO, Laboratory Technician* na kadhalika ni makubwa na wazazi wengi wanashindwa kumudu gharama za kuwalipia, je, kwa nini Serikali isifikie hatua ikaunda utaratibu wa kutoa ruzuku/mkopo kwa wanafunzi wenye nia na sifa za kusomea fani hizo? Ahsante.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jinsi anavyotuongozza katika nchi yetu. Pia nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuwezesha zahanati na vituo vya afya vya Jimbo la Njombe kupata dawa. Jimbo la Njombe lina changamoto nyingi za kiafya ikiwemo miundombinu, vifaa tiba, dawa na watumishi. Watumishi na wahudumu wa afya ni wachache sana. Katika Hospitali ya Kibeda Nesi moja anahudumia wagonjwa na kufanya usafi, ni kazi kubwa sana inayosababisha kushusha tija na kuleta manung'uniko kwa watumishi. Niiombe Serikali ilione suala hilo. Pia katika zahanati vijijini mhudumu akienda likizo huduma inasimama na wananchi wanakosa huduma.

Nitoe rai kwa Serikali iisaidie Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa kuiongezea watumishi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Afya, lipo tatizo la tezi dume ambalo sasa linazidi kusababisha vifo vingi nchini. Niiombe Serikali iongeze nguvu katika kutoa elimu za utambuzi wa tatizo hili katika hatua za awali na tiba. Vilevile Serikali itoe elimu kwa waganga wengi ili waweze kufanya upasuaji mapema na kuepusha vifo visivyo vya lazima.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwa hai, mzima na kunipatia nguvu ya kuweza kuchangia mada ambayo ipo hewani sasa. Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo analiongoza Bunge hili kwa upendo na umahiri pia na uvumilivu mkubwa anaouonyesha ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia mambo sita yafuatayo:-

Moja, UKIMWI; Taifa letu sasa linahujumika kwa maradhi haya na wengi wao ni vijana ambao ndio *manpowers* ya Taifa. Naomba hapa Wizara husika iendelee kutoa elimu ndani ya nchi yetu namna unavyoambukizwa bila ya kuona haya, hali inatisha. Kwa upande mwingine ni vyema hizo dawa za ARV zikawekwa maeneo mengi zaidi tena kwa waziwazi pasi na kuficha.

Pili, malaria; nikienda kwenye malaria, haya ni maradhi bado yapo ijapokuwa yamepunguka. Jitihada za makusudi za kuyamaliza maradhi haya zinahitajika. Malaria ni maradhi ambayo huenezwa zaidi na mbu, mbu hawa kama tukiweka mikakati ya kusafisha maeneo, kupiga dawa za kuulia wadudu (*insecticides*) nchi nzima hasa kwenye mitaro ya maji machafu utapungua ama kwisha kabisa. Pia malaria ina kina, ni vyema tukaangalia zaidi kuwapatia watu wetu chanjo ya malaria.

Tatu, Madaktari na Wahudumu wengine wa Afya; ni vyema wakaongezewa mishahara kwani kazi ambazo wanafanya ni kubwa sana na maslahi bado ni duni kwa watumishi hawa. Nikiendelea kuchangia mada hii ni kwamba kwenye hospitali zetu na vituo vya afya bado watumishi ni haba, hawatoshi. Niombi Serikali kwa heshima zote iongeze watumishi katika sekta hii.

Nne, vituo vya afya; naomba Serikali iangalie tena upya namna ya kuboresha vituo vya afya hasa vilivyoko vijijini kwani havitoshi kulingana na mahitaji.

Tano, vifaa vya kisasa; hapa ndipo penye matatizo makubwa. Hospitali zetu hasa za Serikali hazina vifaa vya kisasa vya kutosha. Niiombe Serikali kwa heshima zote iliangular suala hili kwa huruma sana, tunahitaji *X-ray*, *Ultrasound*, *CT Scan* na vifaa vingine maana ni vichache sana.

Sita, maradhi yasiyo ya kuambukiza. Maradhi haya kama *pressure*, sukari yanazidi kuendelea kuwaumiza watu wetu. Kwa heshima zote niiombe Serikali/Wizara husika itoe elimu ya kutosha juu ya kujilinda na maradhi haya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ili kuwasaidia Watanzania walio wengi wanaosumbuliwa na magonjwa makubwa, mfano magonjwa ya moyo, ni vema Serikali iwekeze sana kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete inayoshughulika na magonjwa ya moyo. Vifaa vyote vinyavyotakiwa kwa ajili ya matibabu ya moyo vinunuliwe kwani kuwa na Madaktari Bingwa peke yake bila vitenda kazi haitasaidia. Kwa kuboresha Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Serikali itaokoa fedha nyingi sana ambazo zingetumika kuwatibu wagonjwa wetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Afya ndiyo Wizara Mama kwa maisha ya Watanzania. Hivyo, ipo haja bajeti inayotengwa kutolewa yote ili kuiwezesha na kuipa wepesi Wizara hii kutekeleza majukumu yake. Bila afya nzuri hakuna viwanda wala shughuli zingine zinazoweza kuinua uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi, nashauri bajeti inayotengwa itolewe yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Korogwe haina hospitali. Asilimia 60 ya wananchi wanapata matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe Vijiji lakini jitihada za makusudi zinafanyika kujenga kituo cha afya chenye majengo ya ghorofa matatu. Nimshukuru kwa ziara alioifanya Korogwe, alishiriki shughuli za maendeleo (*Msalagambo*) na kuahidi kuchangia shilingi milioni 300 katika ujenzi unaoendelea. Aidha, nimshukuru ametuahidi kutupatia *ambulance*. Mwenyezi Mungu ampe wepesi kukamilisha ahadi ambazo wananchi wa Korogwe wamejenga matumaini makubwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Chuo cha Wauguzi Magunga lililopo Korogwe Mjini la ghorofa ambalo lilianza 2010 kwa ajili ya madarasa na Ofisi za utawala limetelekezwa kwa kutotengewa fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Mwaka wa fedha 2016/2017 lilitengewa shilingi milioni 400 lakini hazikupelekwa hadi sasa. Niombwe Serikali kulitengea fedha jengo hili kwani linachakaa na litasababisha hasara kwa Serikali kutenga fedha zingine kwa ajili ya ukarabati, huko kutakuwa ni kufuja fedha za wananchi walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali iangalie upya kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwanusuru akinamama wajawazito. Kutofanya hivyo kutaendelea kusababisha vifo vyta wanawake hawa na kupunguza nguvu kazi ya Taifa ambayo kwa namna moja

au nyingine wanawake ndiyo watenda kazi wazuri katika Taifa hili.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naipongeza Wizara kuititia Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa juhudini kubwa wanazofanya kushughulika na afya za Watanzania na kuboresha maendeleo ya jamii. Sambamba na hilo ni weledi wao ulioifanya Wizara hii kusonga mbele na kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji na kuwashudumia Watanzania popote walipo mjini na vijijini. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wanawake kiuchumi. Naipongeza Wizara kwa mipango mizuri ya kuwainua wanawake kiuchumi. Hata hivyo, bado juhudini zaidi zinatakiwa kuchukuliwa kwani bado wapo wanawake wengi wajasiriamali hawajawezeshwa kiuchumi, wanajitahidi wenyewe lakini kutokana na mtaji kuwa mdogo wanashindwa kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya wanawake, iko mbali na wanawake walioko vijijini. Je, ni lini Wizara itaielekeza benki hiyo kufungua angalau dirisha katika maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hisa katika Benki ya Wanawake, wapo baadhi ya Wabunge tumeshiriki kununua hisa kwa ajili ya uanzishwaji wa benki hii. Je, ni lini tutaarifiwa juu ya kinachoendelea na hatma yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu unyanyasaji wa wanawake na watoto. Naipongeza Serikali kwa juhudini mbalimbali inazochukua katika kukabiliana na tatizo hili lakini bado juhudini zaidi zinahitajika kwa kuungana pamoja kupiga vita hali hii isiendelee. Wazee/wazazi waache tabia ya kuwatumia watoto wadogo kama kitega uchumi kwa kuwaingiza katika ajira za watoto hasa kuwatumikisha majumbani na kuwakosesha haki zao za elimu na matunzo ya karibu ya wazazi. Kwa nini Wizara isielekeze ajira za

majumbani zifanywe na watu wazima badala ya kuwatumia watoto wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Monduli katika Kata ya Makuyuni na Esilalei wameunga mkono sera ya kuwa na kituo cha afya kwa kila kata na wamefika mahali pazuri kwa nguvu na michango yao, tunaomba Wizara itazame namna ya kuwa-*support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuna tatizo la chumba cha upasuaji katika wilaya yetu, tunaomba Wizara itoe namna ya kusaidia ujenzi wa chumba cha upasuaji.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa wema wake kwa Taifa letu na kwa Bunge letu. Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko Mezani. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii muhimu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu; Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya kuhudumia wananchi kwa weledi mkuu na umahiri wa kiasi cha kuridhisha. Pongezi nydingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita kwenye wasilisho la Mheshimiwa Waziri kwenye eneo la maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto. Ni kweli, kuwa, kwa ujumla wake bajeti ya Wizara imeongezeka mara dufu, lakini Fungu 53 bado halijatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara hii ndiyo inayofanya kazi ya kuhamasisha wananchi tangu ngazi ya kaya, shina, kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi Taifa. Hii idara ikiwezeshwa kikamilifu itasaidia sana kuweka mazingira mazuri

kiasi kwamba, hata huduma za afya uhitaji wake utapungua. Idara hii inapaswa kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii kila kata, ili wawe wahamasishaji na waraghibishi wa mafunzo yanayohusu usafi wa mazingira (*sanitation*), masuala ya lishe bora kwa ujumla, lakini pia kwa watoto wanawake na wazee, masuala ya chanjo mbalimbali, masuala ya ujasiriamali, biashara, masoko na kadhalika. Hata Mawaziri wa Sekta nyingine huwatumia hawa Maafisa Maendeleo kuhamasisha masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii ni muhimu sana kuhakikisha kuwa Idara hii ina vitendea kazi vya muhimu kwa majukumu yake kwa maana ya magari, pikipiki, ofisi zinazokidhi, *computer* na watumishi wa kutosha na wenyewe weledi wa kutosha kwenye masuala haya. Hali iliyopo hairidhishi na maafisa hawa wengi wamekata tamaa. Idara hii ni muhimu sana kwa kuhakikisha kuwa mikakati ya kinga dhidi ya magonjwa, elimu kwa vijana juu ya mabadiliko ya maumbile na jinsi ya kupambana na mihemuko kwa njia sahihi na salama, idara iwezeshwe kutimiza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udumavu; napenda kuishauri Serikali kuendeleza mkakati ulioanzishwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete wa *Scaling Up Nutrition (SUN)* kitaifa. Serikali ilete Bungeni mkakati wa uwekezaji katika lishe ili kupambana na tatizo kubwa la udumavu nchini. Katika hili, pamoja na juhudini zinazofanywa za kuhamasisha lishe bora kwa mama mjamzito na mtoto, Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza, katika mikopo inayotolewa kwa Serikali basi Serikali *i-negotiate* fungu la kuwekeza kwenye siku 1,000 za kwanza za mtoto. Kwa sababu, bado hatujaona kuwa hili ni kipaumbele katika Taifa. Kwa sababu kuwekeza katika siku za kwanza 1,000 za mtoto kutahakikisha vizazi salama kwa mama na mtoto, lakini pia, itapunguza vifo vya mama na mtoto na kuleta ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa.

Pili, Serikali iweke mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuingia katika uwekezaji kwenye masuala/huduma/mazao ya lishe. Serikali haiwezi kulifanya hili peke yake.

Tatu, Serikali ianzishe Jamii ya Vijana wa Kujitolea (*Volunteer Community Workers*) ambao watafundishwa masuala ya uraghibishi wa afya vijiji na watakuwa wa msaada mkubwa kwa karibu sana na kuongeza tija kwenye shughuli za Wizara katika ngazi ya kaya, tawi, hata na wilaya. Hawa kwa kuwa, watatokana na maeneo hayo watakuwa na gharama ndogo.

Nne, Serikali katika kujenga maadili mema kwa jamii zetu iangalie uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa wanawake watu wazima kutoa ushauri nasaha kwa vijana wanawake wakati wa balehe, ujauzito na wanapokuwa katika ndoa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wazee bado halijakaa vizuri kwa maana ya mkakati mahsusini wa kuwahudumia wazee kiafya, kiuchumi na kisaikolojia. Iko haja ya kuwa na njia inayotambulika ya kuwawezesha wazee kujisajili kwenye kata zao ili huduma kwao ziwe rahisi katika kila nyanja. Wazee mahitaji yao mengi ni ya kisaikolojia jinsi ya kuukabili uzee, lakini pia kiafya na mwisho lishe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watoto Njiti; idadi ya watoto hawa inaongezeka katika watoto 10 wanaozaliwa mmoja ni njiti na wanapona kwa 40% tu. Hii ina maana vifo vyta watoto wachanga vinachangia kwa 40% ya vifo vyta watoto chini ya miaka mitano. Kila siku watoto 100 wanakuwa kwa sababu ya *complications* kama kushindwa kupumua na kuzaliwa kabla ya wakati. Kila mwaka watoto 213,000 wanazaliwa njiti, watoto zaidi ya 9,000 wanazaliwa kwa matatizo hayo. Vifo vyta watoto njiti ni sababu ya pili kwa ukubwa wa vifo vyta watoto wachanga Tanzania. Kumekuwa na ongezeko kubwa na hatua madhubuti zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe suala la watoto njiti linafahamika na jamii kwa ujumla kuwa sio mkosi, wala kosa lolote la mzazi, ukoo wala jamii na kuwa watoto njiti wanaweza kukua vizuri na kuwa raia wema na wenye akili timamu na afya njema, ilimradi wapate matunzo yanayofaa kwa kuwarudisha katika afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe vituo vya afya na hospitali zinapata vifaa muhimu vya kuwatunzia watoto njiti kama *oxygen concentrator* ya kumsaidia mtoto kupata *oxygen*; *neonatal jaundice and phototherapy* ya kugundua *jaundice*(manjano) mapema; *resuscitation machine* ya kumstua mtoto ili apumue mara tu akizaliwa maana mapafu yake yanaweza kuwa hayana nguvu ya kutosha; *electric and manual suction machine* ya kutoa uchafu kooni na puanı kusafisha njia ya kupitisha hewa; *digital thermometer* ya kupima na kudhibiti joto la mwili wa motto; *diaspect machine* ya ku-check damu ya mtoto kama inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wafundishwe jinsi ya kutunza watoto njiti kwa kuhakikisha wanawabeba kama kangaroo na hawawaachi wazi.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara hii na napongeza sana jitihada ambazo Waziri na timu yake wanafanya katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Busega ni Wilaya changa sana haina Hospitali ya Wilaya na watendaji wa kada ya afya wenye sifa na kwa mujibu wa mahitaji. Naomba Wizara isaidie kupatikana fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya zikiwemo wodi, maabara, *theatre* na miundombinu stahiki ili wananchi waweze kupata huduma ya tiba. Pia tupewe kipaumbele katika suala la upatikanaji wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa baadhi ya watumishi yaani kada ya *Clinical Officers (AMOs et cetera)* wana wajibu wa kuwa wasimamizi wakuu wa vituo na zahanati, lakini unakuta kuna Wauguzi kwa ngazi ya shahada (*degree*) wanafanya kazi chini yao na pia mshahara hulipwa chini ya hao *COS*. Je, Wizara ina mpango gani wa *ku-rationalize* hizi kada kuondoa mkanganyiko wa maslahi kwa watumishi hawa? Naomba Wizara ichanganue kada hizi na maslahi stahiki yatolewe kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa kuwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na hasa Busega unaweza kuchukua muda mrefu kukamilika; na kwa kuwa uwepo wa *DDH* husaidia sana kutoa huduma kwa wananchi ndani ya mkataba, Busega tulishaomba *Mkula Hospital* iwe *DDH* na Mheshimiwa Waziri alitembelea na kuahidi kutekeleza kauli hiyo ndani ya miezi mitatu ambayo ilishapita muda mrefu. Hivi sasa imesababisha wananchi walioahidiwa na Mheshimiwa Waziri kwenye m kutano wa hadhara kuona ahadi ya Waziri ilikuwa ni uongo. Je, Serikali kwa nini isiharakishe au kusaidia mchakato wa kukamilisha suala hili? Naomba Wizara kuititia kwa Waziri itimize ahadi ambayo imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi hata kama kuna upungufu basi Wizara isaidie mchakato huo ili kuwezesha wananchi wa Busega na wa jirani wapate huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa kuwa *Mhula Hospital* kuna Chuo cha *Nursing*, je, Serikali haioni umuhimu wa kukisaidia ili kiweze kupanuliwa na kutoa mafunzo kwa kada hii muhimu na hasa Mkoa wa Simiyu? Naomba Serikali isaidie upatikanaji wa fedha na watumishi watakaoweza kusaidia chuo hiki muhimu na pia Wizara isaidie namna ya kuboresha badala ya kubeza na kutokutoa ushirikiano unaotakiwa. Ikiwa hoja hizi hazipati majibu stahiki nitashawishika kuomba maelezo zaidi yatakayopelekea nikalale na mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa nafasi ya pekee namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwa karibu na wananchi wa Busega na hasa katika ziara yake wakati wa uzinduzi wa nyumba za watumishi zilizojengwa kwa hisani na Taasisi ya Mheshimiwa *Benjamini Mkapa Foundation*. Ahadi yake ya kufanya ziara rasmi bado tunaisubiri kwa hamu. Nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara. Tunashukuru pia kwa msaada wa *ambulance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALMA J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kuniwezesha kusimama ili niweze kutoa mchango wangu kwa Taifa langu. Pili, nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji wake mahiri wenye nia thabiti ya kuwaaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia sekta ya afya hapa nchini. Nina faraja kubwa kwamba juhudhi wanazofanya katika kusimamia sekta ya afya zinaonesha matunda chanya. Nina imani kubwa na utendaji wao na sina shaka kwamba sekta ya afya chini yao itaendelea kuimarika siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea jitihada katika kupambana na vifo vyatyanayi na watoto. Tafiti mbalimbali zilizofanywa na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zimeonesha kuwa Tanzania imejitahidi kwa kiasi kikubwa katika kupambana na tatizo la vifo vyatyanayi na watoto walio chini ya miaka mitano. Jitihada hizi ni matokeo ya hatua za dhati zilizochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa inaimarisha huduma mbalimbali katika sekta ya afya kama vile upatikanaji wa vifaa tiba, chanjo za watoto na huduma za kinga pamoja na tiba za magonjwa kama vile kuharisha, utapiamlo, surua, malaria na maambukizi katika mfumo wa upumuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada zilizofanyika katika kupambana na vifo vyatyanayi na watoto walio na umri chini ya miaka mitano bado kumekuwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi zimebabishwa na matatizo kama vile upatikanaji wa huduma bora za dharura za uzazi kwa akinamama hasa maeneo ya vijijini ambapo akinamama wajawazito wengi hufariki kwa kukosa huduma za upasuaji wa dharura wakati wa kujifungua; upatikanaji wa damu salama kwa akinamama ambao hupoteza damu nydingi wakati wa kujifungua; hali duni ya akinamama wajawazito hasa maeneo ya vijijini ambapo huhitajika kwenda na vifaa kama vile *gloves*, pamba, sabuni

na vifaa vingine vya kujifungulia jambo ambalo huwafanya akinamama wengi kuamua kujifungulia kwa wakunga wa jadi ambao baadhi yao hawakupata mafunzo ya kutoa huduma za uzazi; utoaji wa mimba usio salama na kifafa cha mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza jitihada katika kukabiliana na vifo vya akinamama na watoto vinavyotokana na changamoto zinazojitokeza katika sekta hii ya afya ya mama na mtoto, ni vyema Serikali ikachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha jamii itoe taarifa kuhusu ubora wa huduma za afya kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kueleza hali ya upatikanaji wa wataalam wa afya na hali ya matibabu;

(ii) Kusaidia katika kujenga uwezo wa mfumo wa afya wa wilaya ili kuwezesha katika utoaji na usimamiaji wa huduma bora za afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na uzuiaji wa maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto;

(iii) Wizara ihakikishe kunakuwa na dawa za kutosha kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya VVU kwa akinamama wajawazito ili kusaidia katika kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa watoto kwa lengo la kuwezesha watoto wengi zaidi kuzaliwa wakiwa salama;

(iv) Kuhamasisha jamii na familia kuunga mkono wanawake na kuwawezesha kuwa na kauli katika masuala yanayohusu huduma zao za afya; na

(v) Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya habari itetee kwa nguvu ongezeko la uwekezaji katika huduma za afya ya wanawake katika ngazi ya Taifa na ya Serikali za Mitaa kwa kutumia vielelezo vinavyoonesha maafa na athari ya vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kampeni ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI toka kwa akinamama

kwenda kwa watoto. Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imekuwa katika vita dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI hasa upande wa maambukizi ya UKIMWI toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ambao wanakufa kutokana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama zao ni kubwa. Serikali inapaswa kufanya jitihada kubwa za kuhakikisha inaokoa maisha ya watoto hawa ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha jitihada hizi zinafanikiwa, ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa:-

(i) Inatoa programu nyngi za uzuaji wa maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (na kinga nyngine) zlikwemo programu za kuwasaldia wanawake kuwa na afya kwa muda mrefu kwa msaada wa lishe na matibabu;

(ii) Kutoa mafunzo kwa wanaishi wengi, wafanyakazi wa jamii wa kujitolea na wakunga wa jadi ili kuwafikia wanawake wengi na taarifa za kuaminika na ushauri kuhusu mambo ya kufanya wanapokuwa na maambukizi ya VVU. Wanawake wanaoishi na VVU wanahitaji kujua nini cha kufanya, kwa mfano, kuepuka mimba zisizotakiwa na hatari zinazoweza kutokea kwa watoto wachanga kutokana na lishe duni na maambukizi yanayohusiana na ulishaji mbadala; na

(iii) Kuboresha hali ya huduma za afya ili kuhakikisha kuwa watoto wachanga hawaambukizwi wakati wa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto. Nianze

kwa kuunga mkono hoja na sababu zangu za kuunga mkono hoja ni kama ifuatavyo:-

(i) Randama na hotuba ya Waziri imeandaliwa vizuri na kitaalam; na

(ii) Serikali ya CCM chini ya uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii wanafanya kazi nzuri ya kuhakikisha wanaboresha huduma za afya hapa nchini. Ni ukweli usiopingika kuwa katika kipindi hiki kifupi, wameendelea kuonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya CCM ya kuboresha huduma za afya kwa wananchi, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, kwanza napenda kushauri Serikali:-

(a) Itoe fedha za kutosha za utekelezaji wa majukumu ya sekta hii muhimu;

(b) Iboreshe maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya afya na maendeleo ya jamii na kuongeza idadi ya wafanyakazi;

(c) Iendelee kununua vifaa tiba katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mkoa;

(d) Ipeleke wataalam kama vile Madaktari na Wauguzi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zote;

(e) Ilandae mpango maalum utakaoleta matokeo ya haraka ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na ukamilishaji wa mpango wa hospitali za rufaa za kila mkoa, lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Muhimbili, KCMC na Bugando. Hapa naishauri Serikali kujenga vituo vya afya viwili viwili katika kila halmashauri, kwa halmashauri tulizonazo  $183 \times 2 \times 3 = 1,098$ ;

(f) Ikamilishe vituo vya afya vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi ili visaidie kutoa huduma badala ya kubaki kuwa magofu;

(g) longeze fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara (*Mwalimu Nyerere Memory Center*);

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuongelea huduma ya afya ya uzazi na mtoto. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuboresha huduma inayotakiwa kwa wanawake kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na wiki sita baada ya kujifungua, naomba niungane na Serikali katika ukurasa wa 16 kuwa kweli bado ipo changamoto kubwa ya wanawake wanaofariki wakati wa uzazi. Kwa mujibu wa tafiti zilizopo hapa nchini ya mwaka 2015 zinaonesha kwamba vifo vinavyotokana na uzazi havijapungua, idadi ya vifo ni 556 kwa kila vizazi 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mpango wa Wizara ulioandaliwa na unaotekelizwa kuanzia 2016 hadi 2020. Hapa napenda nipate muhtasari juu ya mpango huo, tangu mpango huo umeanza kutekelezwa tumeweza kuokoa vifo vingapi vya wanawake? Ni kwa nini vifo vimeongezeka badala ya kupungua? Takwimu za 2016/2017 zinaonesha hali ikoje juu ya vifo vya wanawake ikilinganishwa na ya mwaka 2015?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti). Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Mamaye 2017 kwa kushirikiana *DFID*, watoto 2,013 wanazaliwa kabla ya wakati na watoto 3,900 waliozaliwa bila kufikisha umri, wanaofariki dunia. Watoto wanaozaliwa kabla ya wakati pia ni sababu ya watoto wanaofariki kabla ya kufikisha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kunusuru maisha ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati naishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

- (i) Tuwe na wodi/chumba maalum kwa ajili ya watoto hawa kwa sababu hali ilivyo sasa hakuna vyumba maalum katika baadhi ya vituo vya afya na hospitali zetu;
- (ii) Kuwe na vitanda vya kutosha kwa ajili ya kuwalaza watoto hao;
- (iii) Kuwe na mashine ya kusaidia watoto kupata joto ili kuwafanya waishi;
- (iv) Kuwe na mashine za kuondolea ugonjwa wa manjano; na
- (v) Elimu kwa jamii itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ugonjwa wa saratani – shingo ya kizazi, matiti na tezi dume. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za kupambana na ugonjwa wa saratani kwa kuboresha Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* na hospitali za kanda ili ziweze kutoa huduma kwa wagonjwa wa saratani, bado ugonjwa wa saratani umekuwa ndio ugonjwa tishio kwa wanawake na wananchi wengine kwa ujumla. Kwa kuwa ugonjwa huu ni hatari na dawa za saratani ni ghali sana, naiomba Serikali itenye na kutoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya ugonjwa wa saratani. Pia naomba Serikali itoe msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa saratani kama ilivyo kwa wagonjwa wa UKIMWI kwa sababu wanawake na wananchi wanaouagua ugonjwa huu wa saratani hawana uwezo wa kumudu kununua dawa za ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, dirisha la wazee, wanawake na wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Pamoja na kupongeza Serikali kwa kuweka na kuanzisha dirisha la wazee na wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, bado ipo changamoto kubwa ya utoaji huduma hii kwa wazee, wanawake wajawazito na watoto. Changamoto kubwa sana ya kundi hili ni dawa/fedha zinazopelekwa hazitoshelezi. Nashauri, Serikali iwapatie huduma za bima ya afya wazee, wanawake na watoto. Pia

iongeze fedha kwa ajili ya kuhudumia kundi hili na kuondoa adha wanayoipata kwa kukosa huduma ya afya kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Wanawake ndiyo nguvu kazi, wanawake ndiyo walezi wa familia, unapomkomboea mwanamke kiuchumi unakomboea familia kwa ujumla. Taarifa inaonesha jitihada zilizofanywa na Serikali katika kuwezesha wanawake kupitia mipango na program mbalimbali kwa kuwekeza nguvu zaidi kwa wanawake na watu wenye ulemavu. Pamoja na kupongeza Serikali, nina ushauri katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kutoka Serikali Kuu. Mfuko huu umekuwa ni mkombozi. Kwa vipindi vyta miaka ya hivi karibuni na hata bajeti ya mwaka 2017/2018, mfuko huu haukutengewa fedha. Naomba Serikali itenge na kutoa fedha kwa aili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kama ilivyofanyika kwa vijana. Kutotenga fedha kwa ajili ya wanawake ni kurudisha nyuma jitihada za wanawake katika kujikomboa kiuchumi kwa sababu mfuko huu unaotolewa na Wizara ulikuwa ni ukombozi kwa vikundi vyta wanawake badala ya kutengewa 10% ya Mfuko wa Wanawake na Halmashauri tu ambao pia hakuna uhakika kwa sababu Halmashauri nydingi hazitengi na kutoa fedha hizo.

(ii) Tatizo la kutolipa 10% ya wanawake na vijana. Lipo tatizo katika Halmashauri kutotenga 10% kwa ajili ya mfuko wa vikundi vyta maendeleo ya wanawake na vijana katika Halmashauri zetu. Naomba kutoa ushauri kwamba kwa kuwa utaratibu wa kutoa fedha hizo 10% ya vikundi vyta wanawake na vijana ni maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu miaka zaidi ya 20 iliyopita, Serikali ilete Muswada ili Bunge litunge sheria itakayoweka utaratibu wa kutenga, kutoa na kurudisha fedha hizo kwa vikundi vyta maendeleo ya wanawake na vijana kuliko ilivyo sasa, kwani jambo la kutoa fedha hizo limebaki kama ni jambo la hisani na si jambo la lazima kwa sababu hakuna sheria inayotekelawa.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kila unapofanyika ukaguzi linatokea tatizo la kutotoa fedha kwa vikundi vya wanawake na vijana, Halmashauri zilizo nyingi zimeonesha yapo madeni makubwa. Hapa ningependa kusikia kauli ya Serikali juu ya ulipaji wa madeni haya ili fedha hizi zielekezwe katika kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana.

(iii) Riba katika taasisi zinazotoa mikopo kwa vikundi vya wanawake. Pamoja na kuzipongeza taasisi za fedha kwa kutoa mikopo midogo na mikubwa kwa vikundi vya wanawake na vijana, lipo tatizo kwa baadhi ya taasisi za fedha viwango vyao vya riba ni vikubwa sana mpaka kufikia 35%. Jambo hili husababisha wanawake na vijana kushindwa kujikomboa kiuchumi badala yake wameambulia kufanya kazi za uzalishaji na kuwanufalsha wallowapa mikopo na wao kuambulia kutaifishiwa mali zao kwa mfano vifaa vya nyumbani kama vitanda, magodoro, vyombo na kuuziwa mashamba. Nashauri Serikali itoe riba elekezi kwa taasisi zote zinazotoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana lengo likiwa ni wanawake na vijana wanufaikie na mikopo hiyo kuliko ilivyo sasa.

(iv) Benki ya Wanawake ilianzishwa kuwakomboa wanawake waishio vijijini na mijini ambao hawana fursa za kufika taasisi nyingine za fedha. Nashauri Serikali itoe fedha kwa benki hii ili ipate mtaji wa kufungua matawi katika mikoa yote hapa nchini. Vilevile masharti ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake yaangaliwe upya kwa sababu hayatofautiani na masharti ya benki zingine, hivyo wanawake walio wengi hasa waliolengwa na kuanzishwa kwa benki ni wanawake wanyonge ambao hawana mali za kuweka kama dhamana wanashindwa kukopa katika benki hii. Hivyo, malengo ya kuanzishwa kwa benki hii bado hayajafikiwa. Pia Serikali irejee upya masharti ya kutoa na kurudisha mikopo ili Benki hii ya Wanawake iwe mkombozi kwa wanawake na Watanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu athari za upungufu mkubwa wa dawa na chanjo kwa akinamama na watoto. Itakumbukwa kuwa mwishoni mwaka jana hadi mwanzoni mwa mwaka huu na sina uhakika kama tatizo hilo limekwisha hadi tunapozungumza hapa ndani sasa kwenye Mkutano wa Bajeti, nchi yetu ilikumbwa na ukosefu au upungufu mkubwa wa dawa pamoja na chanjo za magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilikuwa mbaya kiasi cha Serikali kujichanganya katika kauli zake za kujitetea na kutaka kuonesha kuwa ilikuwa suala dogo lakini ukweli ni kwamba halikuwa suala dogo ndiyo maana Makamu wa Rais alisema kauli nyiningine Wizara wakasema kauli nyiningine. Wakati Waziri mhusika, Mheshimiwa Ummy Mwalimu akisema kuwa hakuna tatizo la ukosefu wa dawa na kwamba hizo ni habari za kwenye mitandao tu, kesho yake bosi wake, Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu akiwa pale Mwananyamala Hospitali akakiri kuwa nchi ina tatizo la upungufu mkubwa wa dawa na chanjo lakini eti halitakuwa la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukiri kule, kauli ile ya Serikali ilikuwa ni ya ajabu na ilikuwa na ukakasi mkubwa sana masikioni mwa Watanzania ni kama vile walikuwa wanaambiwa wavumilie hali hiyo kwa sababu haitakuwa ya muda mrefu. Hivi kuna mahali mnawenza kucheza na maisha ya Watanzania kama kwenye afya na matibabu (uhai)? Hivi mnawezaje kusema ukosefu wa dawa halitakuwa tatizo la muda mrefu bali mfupi tu huku mnajua kuwa wakati huo kuna wagonjwa hospitalini wanahitaji dawa na wanakufa kwa kukosa dawa? Mnawezaje kusema kuwa tatizo hilo halitakuwa la muda mrefu wakati kuna akinamama wajawazito hospitalini wanasubiri matibabu na wengine wamejifungua wanahitaji matibabu na watoto wao wanahitaji chanjo? Huku ni kucheza na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata taarifa ya Serikali na wananchi wangu wa Mwanza wanataka kusikia Serikali ikisema hapa Bungeni, je, akina mama wangapi

hususan wajawazito na wale waliojifungua na watoto waliozaliwa wameathirika na ukosefu huo wa dawa na chanjo hospitalini? Tumefikia hatua nchi inakosa dawa na vifaa tiba na chanjo za kifua kikuu, polio, surua, lubele, kichaa cha mbwa, manjano na magonjwa mengine hatari kwa afya ya mama na mtoto. Kwa hiyo, Watanzania na kipekee wananchi wa Mwanza wangependa kusikia Serikali ikiliambia Bunge hili athari ambazo Taifa hili limepata na litazipata miaka mingi ijayo kwa kitendo cha akinamama wajawazito kukosa dawa na chanjo, akinamama waliojifungua na watoto wao kukosa dawa na chanjo, nini athari zake kwa jamii yetu ambayo bado inapambana na utapiamlo, udumavu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujenzi wa vituo vitatu kila Halmashauri kuboresha huduma na uchunguzi na matibabu ya mapema ya saratani ya matiti na mlango wa kizazi kwa kina mama. Hivi karibuni wakati akizindua kampeni ya bure ya uchunguzi wa saratani ya matiti na mlango wa kizazi kwa akinamama iliyofanyika mjini Mwanza, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu alisema kuwa Serikali ina mpango wa kujenga vituo vitatu kwa kila Halmashauri nchini kwa ajili ya kuboresha huduma na uchunguzi na matibabu ya mapema ya magonjwa hayo ili kuwanusuru akinamama. Ilisemwa kuwa zimetengwa shilingi bilioni saba na Serikali hii na Benki ya Dunia itasaidia shilingi bilioni tano katika kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimepitia taarifa ya bajeti ya Wizara hii kuangalia utekelezaji wa kauli hiyo ya Serikali sijaona mahali ambapo fedha hizo zimetengwa. Wananchi wa Halmashauri za Mwanza wanasubiri kwa hamu kuona utekelezaji huo ambao utaweza kuokoa karibu wanawake asilimia 60 walioko katika hatari ya vifo vinavyosababishwa na magonjwa hayo huku wakiacha nyuma watoto wanaohitaji malezi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali ituambie hapa imefikia wapi katika kusogea huduma za magonjwa hayo katika hospitali za Bugando na *KCMC*kama

alivyosema Makamu wa Rais ili kupunguza mahitaji ambayo hospitali ya *Ocean Road* inakabiliana nayo kwa sasa. Pia naomba kujuu maendeleo ya kampeni hiyo ya bure hususan kwa Mkoa wa Mwanza ambayo ingepaswa kwenda sambamba na utoaji wa elimu au kujikinga au kuzuia magonjwa hayo kwa akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kampeni ya malaria na ugawaji wa taulo za usafi wa mwili kwa mabinti kwenye shule zetu. Hivi karibuni taarifa kutokana na tafiti zilizofanyika zilionesha kuwa wasichana walioko shule au walio na umri mdogo wanapata athari kubwa sana kutokana na ugumu wa kupata mahitaji ya taulo za usafi wanapokuwa katika mzunguko wao wa kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari hizo ni mimba za utotoni kwa sababu ya kudanganywa ili wapate fedha za kununua taulo; wanashindwa kuhudhuria shulen na kukosa masomo kwa siku tano hadi saba kila mwezi; kupunguza uwezo wao wa kufaulu kwa kukosa masomo na kuwa katika uwezekano wa kupatwa na magonjwa mbalimbali kutokana na kutumia vifaa visivyo sahihi na visivyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kumekuwepo na kampeni kubwa dhidi ya malaria ambayo nasikia imefika hadi kwetu Buchosa kwa ajili ya kupulizia dawa ndani na kwenye kuta za nyumba, ni wakati muafaka sasa Serikali ikalivalia njuga na kulipatia uzito mkubwa suala la kuwasaidia hawa watoto na mabinti zetu walioko shulen wapate taulo hizo ili wabakie shulen wasome, waepuke mimba za utotoni na magonjwa hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara walione hili na walichukue kwa uzito mkubwa sana. Inaweza hata kwa kuanzia kushirikiana na watu au mashirika ambayo tayari yameanza kampeni hii kama walivyokuwa wakifanya watu wa *East Africa Television* na *East Africa Radio* ambao walifanya kampeni kubwa kuhamasisha watu kusaidia mabinti hawa walioko shulen wanaoteseka kwa sababu ya kukosa taulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, matibabu ya bure kwa wazee, kambi ya wazee wa Bukumbi na kambi ya walemavu Misungwi. Wazee wangu wa Mwanza, maeneo ya Buchosa, Sengerema, Illemela, Nyamagana, Magu, Sumve, Ukerewe, Ksimba na Misungwi bado wanasubiri lini Serikali itatekeleza kwa dhati huu mpango badala ya kuwa kwenye makaratasi na maneno ya hapa Bungeni na kwenye mikutano au semina au warsha na makongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati lilifanyika zoezi la kutoa vitambulisho kwa wazee wanaotakiwa kutibiwa bure, naomba Serikali kupitia Bunge lako iwaambie Watanzania zoezi hili limefikia wapi na wazee wangapi wamepata hivyo vitambulisho hususan kwa Mkoa wetu wa Mwanza ambako wazee wetu waliotumikia Taifa letu wakiwa wakulima, wafugaji, wafanyakazi Serikalini sasa wamestaafu wanahangaika sana kupata matibabu. Tunaomba mtuambie kama mtawenza kuitekeleza kwa vitendo sera hiyo ambayo tunajua haikuwa ya kwenu. Kama imewashinda tuwaambie wazee wetu na watu wengine ambao tu wazee watarajiwa kuwa hilo litawezekana tu pale ambapo Serikali ya UKAWA itaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mwanza wanapata shaka sana iwapo Serikali itaweza kutekeleza kwa vitendo sera hiyo wanapoangalia kambi ya wazee wasiojiweza ya Kigongo, pale Misungwi namna ambavyo wazee wale wametelekezwa na Serikali, hawana dawa, wanapumbuliwa na magonjwa na hawawezi kutibiwa, wanapangiwa bajeti isiyotosheleza kwa chakula wala matibabu. Hali hiyo mbaya ya kituo cha wazee cha Misungwi ambayo hata Mama Janeth Magufuli aliishuhudia mwenyewe haijaishia hapo pekee, kuna kilio kikubwa pale shule maalum ya walemavu wa ngozi ya Mitindo iliyoko Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii ambayo inashirikiana na Wizara zingine kuhakikisha watoto wale wanapata stahili za kulinda afya zao. Vinginevyo iko siku tutaona machozi mengine humu Bungeni kuwalilia watoto

wale kama ambavyo Waziri Mkuu aliyejita alitoa machozi kwa ajili ya *albino*.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii muhimu na adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima. Nikushukuru wewe kwa kuniruhusu na mimi nichangie ingawa kwa ufupi mapambano ya UKIMWI pamoja na kuendelea ndani ya nchi yetu lakini inaonekana bado UKIMWI unaongezeka pamoja na maambukizi mapya na kama juhudzi za makusudi hazitachukuliwa basi Taifa letu litafika pabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa UKIMWI umekuwa uko sirini sana kiasi ambacho watu wengi wamekuwa na matumaini makubwa kwamba UKIMWI umepungua kwa *style* za watu zilivyo. Watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI si rahisi kuwatambua kama hajajieleza mwenyewe. Hii inatokana na kuitikia wito wa kujunga na vituo vya dawa za *ARV*, kwa hiyo, watu wengi kwa kupungua athari za kuonekana moja kwa moja wanadhani UKIMWI umepungua. Kwa hiyo, ushauri wangu, mikakati na juhudi ziendelee kuelimisha Watanzania kwamba UKIMWI upo na bado unaua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa UKIMWI wametoa taarifa kwamba Mkoa wa Njombe unaongoza kwa UKIMWI ambao una 14.8% hii ni asilimia kubwa na ya kutisha. Naomba Serikali ifanye utafiti ni jambo gani linalosababisha maambukizi makubwa kiasi hiki katika Mkoa huu, tatizo lijulikane, itolewe elimu ya uhakika kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu wazee. Tunafahamu fika kwamba wazee wa sasa ndio vijana wa juzi na jana ambao walijituma kwa utumishi uliotukuka na mafanikio ya utumishi wao mwema ndiyo uliolifikisha Taifa letu hapa lilipo. Hivyo, naishauri Serikali kutokuwasahau na kuwadharau wazee ambao ndiyo waliokuwa dira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba, wazee hawapati huduma inavyopasa na badala yake wazee wanaonekana kama hawakuwa na mchango wowote katika Taifa hili. Mfano, katika huduma za matibabu, wazee wamekuwa wakisumbuka kana kwamba hawastahili kupatiwa huduma hii. Wamekuwa wakitozwa malipo makubwa ambayo hawayamudu lakini ni haki ambayo imeidhinishwa na Serikali kupatiwa. Naishauri Serikali kuweka kipaumbele juu ya kuwajali wazee kwa kuwapatia huduma wanazostahili. Serikali ina nia na dhamira thabitijuu ya wazee ila inaonekana changamoto hii inayowakumba ni utendaji mbovu usiojali mchango wa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia hoja yangu, napenda kugusia angalau kidogo suala la mazoezi ya viungo kwa jamii. Mazoezi ni jambo muhimu sana kwa afya ya mwanadamu na michezo ni sehemu ya mazoezi. Kwa hivyo, michezo ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi na hasa katika kuimarisha miili yetu kiafya na kuwa wakakamavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekumbwa na magonjwa mengi sana ambayo kama tungekuwa makini na mazoezi tusingeathiriwa sana na magonjwa haya. Mfano wa magonjwa hayo ni kama vile kisukari, moyo na kadhalika. Magonjwa haya kwa ujumla wake yanaitwa magonjwa sugu yasiyoambukiza na yanayogharimu pesa nyingi za wananchi na Serikali. Naishauri Serikali na Wizara ya Afya kuhamasisha jamii kuhusu suala zima la kufanya mazoezi na kutoa misaada pale inapobidi ili kuendeleza mazoezi.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha vizuri hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya ni moja kati ya sekta nyeti Tanzania inayosimamiwa na Wizara ya Afya pamoja na hospitali zote za rufaa, hospitali za wilaya pamoja na vituo vya afya na zahanati zilizopo chini ya Serikali za Mitaa

(Manispaa na Mitaa). Hizi zipo chini ya Wizara ya TAMISEMI pamoja na kwamba zote zinapata miongozo ya kiutendaji kutoka Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa Idara hii ya Afya, Mkoa wetu wa Iringa unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kukosekana kwa chumba cha uangalizi wa wagonjwa wa nje wa dharura *OPD (Casuality/Emergence)* hivyo kusababisha msongamano mkubwa wodini kwa zile huduma zinazohitaji uangalizi wa muda mfupi;

(ii) Uwiano mdogo wa daktari kwa mgonjwa, hivyo kufanya kuwa na msongamano mkubwa katika vyumba vya Madaktari wachache wanaokuwa zamu na kuongeza *workload* kwa Madaktari;

(iii) Kuna wodi nzuri za watoto zilizojengwa kwa ufadhilli wa Hospitali ya Vicensa ya Italia na mzalendo mmoja, familia ya ASAS, lakini hakuna Daktari Bingwa wa watoto (*pediatrician*) pamoja na idadi kubwa ya watoto wanaolazwa hospitalini hapo;

(iv) Hakuna Kitengo cha *ENT* (sikio, pua na koo) wala Daktari wa *ENT* hivyo, case zote za *ENT* lazima zipewe rufaa au kusubiri *visiting doctor* ambapo ni kero kwa wagonjwa wenye matatizo hayo;

(v) Vitendea kazi muhimu wodini ni vichache kama vile *oxygen cylinder* na *oxygen concentrators*, *pulsometor* za kupimia kiwango cha *oxygen* kwa wagonjwa, *BP machines* hazina uwiano unaostahili kwa ugonjwa (wodi nzima inaweza kuwa na mashine moja tu) na vipimo vya sukari kwa wagonjwa wa sukari waliopo wodini wanaohitaji uangalizi wa kina;

(vi) Kitengo cha Afya ya Akili hakikidhi haja na mahitaji ya wagonjwa wa afya ya akili kwa sababu kina vyumba vinne yaani viwili kwa wanaume na viwili kwa

wanawake vyenye uwezo wa kukaa na wagonjwa wawili kila chumba. Hivyo, uwezo wa hospitali kuhudumia wagonjwa wa akili ni wagonjwa nane tu ambayo ni hatari kwa hospitali yenye kiwango cha Hospitali ya Mkoa ya Rufaa;

(vii) Wagonjwa wanaohitaji msamaha hawapati huduma za dawa kama inavyostahili kutokana na dawa nyingi kutokuwepo hospitalini. Hali hii husababisha shida zaidi kwa wagonjwa wasio na uwezo, wazee na wenye magonjwa ya kudumu (sukari, akili, *TB* na *HIV*);

(viii) Nyumba za Madaktari, zaidi ya 85% ya Madaktari na wahudumu wengine wa afya wanakaa maeneo ya mbali na hospitali kutokana na kukosekana nyumba. Hii ni changamoto hasa inapohitajika huduma ya dharura kwa mgonjwa hasa nyakati za usiku;

(ix) Kukosekana kwa huduma nyingine za msingi kama *CT Scan*, *MRI*, *ECG*, *ECHO* katika Hospitali ya Mkoa na kusababisha rufaa nyingine zisizokuwa na lazima ambapo ni kero kwa wananchi wanaohitaji huduma hizo;

(x) Kukosekana kwa mifumo ya kielektroniki inayowezesha daktari kupata majibu ya mgonjwa kutoka maabara na taarifa nyingine za mgonjwa kwa haraka kama ilivyo hospitali nyingine za *private*;

(xi) Kila wakati kukosekana kwa dawa muhimu hospitalini na kusababisha wagonjwa kuhangaika kwenda kutafuta dawa kwenye maduka ya watu binafsi na kero zaidi inakuwa wakati wa usiku ambapo na hayo maduka binafsi yanapokuwa yamefungwa, inaweza kuhatarisha maisha ya mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Benki ya Wanawake. Niipongeze Serikali kwa kuweka dirisha la kuweza kuhudumia wananchi wa Mkoa wa Iringa. Hata hivyo, niiombe Serikali itoe mtaji wa kutosha ili ile dhamira ya kusaidia benki hii kwa ajili ya wanawake ipate kutimia. Pia nashauri

kuwepo na *mobile agency* kwa ajili ya huduma hii kufikishwa mpaka vijiji ni kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu vituo vinavyolelea watoto yatima. Pamoja na wamiliki wa vituo hivi vyta watoto yatima kuisaidia Serikali katika wimbi hili la watoto yatima na watoto wa mtaani lakini kuna changamoto nydingi zilizopo katika vituo hivi, kuna vituo havina hata uwezo wa kuwatibu watoto hawa wanapouguu au kupata ajali. Hivyo, ni vema Serikali ikaweka utaratibu wa kusaidia vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kugawanywa kwa Manispaa ya Kinondoni na kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Ubungo, Hospitali ya Mwananyamala kwa sasa inahudumia zaidi Manispaa ya Kinondoni. Hospitali ya Sinza Palestina ili yobaki katika Wilaya ya Ubungo haina hadhi na uwezo wa kutoa huduma kwa Manispaa nzima. Hivyo, Wizara ichukue hatua za haraka za kuboresha huduma katika hospitali hiyo ya Palestina ilingane na wajibu wa kutoa huduma kwa Manispaa mpya ya Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hospitali hiyo iko mbali na Jimbo la Kibamba lenye Kata za Goba, Saranga, Msigani, Mbezi, Kwembe na Kibamba; na pia kimuundo Wilaya ya Ubungo inapanuka kuelekea Kata hizo za pembezoni makao makuu ya muda ya wilaya yakiwa kwenye Kata ya Kibamba na ya kudumu yakitarajiwa kujengwa kwenye Kata ya Kwembe. Kadhalika kuna ujenzi wa Mji Mpya wa Viungani (*Satelite town*) katika eneo la Luguruni hivyo, ni muhimu kukawa na mkakati wa kupandishwa hadhi kituo cha afya kuwa hospitali ya wilaya na zahanati kuwa, kituo cha afya katika kila mojawapo ya kata hizo za pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, kuna hospitali kubwa katika Chuo Kikuu cha Afya (*MUHAS*), *Campus* ya Mloganzila. Hata hivyo, hospitali hii hadhi yake

itakuwa sawa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili hivyo, haitakuwa rahisi kwa wananchi wa Jimbo la Kibamba kupata huduma za kawaida zinazotolewa na vituo vya afya na hospitali za wilaya. Hivyo, ni vyema Wizara ikafanya kazi mchango huu na kunipatia majibu yanayostahili.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nami nichangie katika Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa afya na uzima wa Watanzania. Naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, hususan Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu ya Wizara hii kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ari na kasi kubwa hasa katika ongezeko kubwa la kibajeti na upelekaji fedha hususan za dawa katika Halmashauri zetu. Vilevile naishukuru Serikali kwa kuonesha nia na kutuweka katika mpango wa kuboresha huduma ya afya na upanuzi wa miundombinu katika Kituo chetu cha Afya Mkuyuni ili kiweze kutoa huduma za upasuaji na wodi za akinamama ili kuwa na uzazi salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi na shukrani hizo, naomba kutoa maombi yangu kwa niaba ya watu wa Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Vijiji kwa ujumla, kama ifuatavyo:-

(i) Ahadi ya Rais kuhusu gari la wagonjwa. Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alituahidi kutupatia gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya Mkuyuni tangu mwaka 2010 na mwaka 2014 katika Kituo cha Afya, Kinole, mbele ya aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli baada ya kupokea ombi hilo toka kwa watu wa Kinole kupita kwa Chifu Kingalu Mwana Banzi wa 14 lakinis mpaka sasa magari hayo hayajapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu kuititia kwa Mheshimiwa Waziri kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais na kutupatia magari hayo mawili ili kuokoa

maisha ya watu wetu hasa akinamama wakati wa kujifungua ukizingatia hatuna hospitali ya wilaya na hali ngumu ya kijiografia katika eneo letu kutokana na milima iliyoko kule Kinole. Pia, tunategemea Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ambayo iko mbali na jimbo na halmashauri yetu.

(ii) Ombi la Hospitali ya Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ni ya muda mrefu lakini mpaka sasa hatuna hospitali ya wilaya na kutegemea hospitali ya mkoa. Ombi langu ni kuomba Serikali kutujengea hospitali ya wilaya ili kutoa huduma karibu na wananchi na kupunguza msongamano katika hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri wangu, wakati tunasubiri ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao utachukua muda, naomba Serikali iteue kituo kimoja cha afya kati ya Tawa, Dutumi, Mkuyuni ama Ngerengere kuwa hospitali ya wilaya ili kutoa huduma kwa wananchi kutokana na halmashauri kwa sasa kuhamia kijijini Mvuha ambapo ni mbali na hospitali ya mkoa.

(iii) Kutokana na hali ya kijiografia ya Jimbo letu, naomba Serikali kutujengea na kuzipandisha hadhi zahanati za *Mikese Station*, Mkulazi, Tununguo, Seregete, Kinole, Kibuko na Kiroka kuwa vituo vya afya ili kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale yote niliyochangia hapo awali, naomba kutumia fursa hii kuchangia yale niliyoshindwa kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ukerewe Mkoani Mwanza ina changamoto kubwa ya mimba za utotoni na uzazi usio na mpangilio. Jambo hili limezua uwepo wa wategemezi wengi kuliko wanaotegemewa. Hivyo basi, nipende kuiomba Serikali kuliangalia suala hili kwa ukaribu

zaidi na kuweza kuweka mkakati wa *campaign* ya masuala ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana AMREFkwa kudhamini *theatre* za vituo vya afya vya Kata za Muriti na Kagunguli ndani ya Wilaya ya Ukerewe. Tayari miundombinu imekamilika bado tu ukamilihaji wa vifaa husika. Wasiwasi wangu upo kwenye Kituo cha Afya cha Kagunguli ambacho bado hakijapata huduma ya maji salama na katika ziara ya Makamu wa Rais Wilayani Ukerewe, Waziri wa Maji aliagizwa kusimamia suala hilo. Kweli mradi uliana kwa kasi kubwa na cha kushangaza mradi huo umesimama sasa kwa takribani miezi miwili. Naomba Waziri mwenye dhamana ya maji asikie kilio hiki na atuondoe katika hali ya sintofahamu tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nillyochangia hapo awali ya ukosefu wa hospitali ya Wilaya ya Illemela, lipo tatizo lingine la Wilaya ya Illemela kukosa vituo vya afya vya kutosha. Jimbo la Illemela lina kata 19 ila cha ajabu ni kwamba lina zahanati tatu tu ambazo hata miundombinu yake hajakamilika. Kwa mfano, Kituo cha Afya cha Buzuruga hakina wodi ya wanaume wakati kinahudumia maelfu ya wananchi kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Illemela. Napenda kuiomba Serikali kukiangalia Kituo hiki cha Afya cha Buzuruga kwa jicho la pekee na kama nilivyosema kuwa hakuna hospitali ya wilaya na vituo vya afya ni vitatu tu wilaya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ksimba, Jimbo la Ksimba, kipo Kituo cha Afya cha Mwamashimba ambacho hakina *theatre* na kusababisha wananchi kukosa upasuaji na wengine wamekuwa kwa kukosa huduma ya upasuaji pale kunapotokea dharura. Naiomba Serikali kufanya maarifa ili kituo hicho cha afya kiweze kupata *theatre* ili kunusuru maisha hasa ya akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ksimba ipo Zahanati ya Buyogo ambayo kwa kweli ni ya mfano. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Waganga na Wauguzi wa zahanati hii kwa kazi nzuri. Wamekuwa wakihudumia wananchi wengi

kuliko hata hospitali ya wilaya na huduma zao ni nzuri. Mimi leo naungana na Mbunge wa Kwimba kuomba Serikali kuiwandisha hadhi zahanati hii ya Buyogo kuwa Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, naomba Wizara itutatulie matatizo ya ukosefu wa maduka ya *MSD* katika hospitali za wilaya za Mkoa wa Mwanza na tatizo la ukosefu wa Waganga na Wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nina hawa wachangiaji wawili, dakika kumi kila mmoja, halafu atafuata Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na baadaye mtoe hoja. Mheshimiwa Angella Kairuki dakika kumi, halafu Mheshimiwa George Simbachawene dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Afya. Kipekee nipende kumpongeza sana pacha wangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika kuboresha utoaji wa huduma ya afya, masuala ya maendeleo ya jamii, ulinzi kwa mtoto pamoja na masuala mengine ambayo yako chini ya usimamizi wa Wizara yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuongelea suala kubwa kuhusiana na ajira. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kwa hisia kubwa, lakini lengo kubwa ikiwa ni kupaza sauti kwenye suala zima la umuhimu wa kuwa na watumishi katika sekta ya afya wanaotosheleza kwa ajili ya kutoa huduma ya afya iliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010 mpaka mwaka 2015, Ofisi yangu imetoe vibali vya ajira 52,947 kwa ajili ya kada mbalimbali

katika sekta ya afya. Ukiangalia katika mwaka huo huo miaka hiyo mitano takribani watumishi 14,860 hawakuripoti katika vituo walivyopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa, mahitaji ni makubwa lakini udahili katika vyuo vyetu pia haujajitosheleza na tumeshaanza kuchukua hatua ya kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na vyuo vikuu vinavyotoa taaluma hizo ili kuona ni kwa namna gani wanaweza kuongeza udahili ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalam wa kutosha watakaotosheleza soko letu la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kuchukua hatua, kama ambavyo mmeshasikia tumeshaanza kuajiri watumishi wa sekta ya afya, Madaktari 258 na tayari wameshapangiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma, Kibong'oto pamoja na Mirembe. Vile vile kwa upande wa TAMISEMI wamewapangia pia katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya pamoja na Halmashauri nyingine za miji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza jana na leo pia nilieleza; kwa kutambua zoezi letu lilitokuwa likiendelea, baada ya matokeo ya uhakiki wa vyeti; tunatambua ni kweli katika hospitali nyingi, katika vituo vingi vya afya na zahanati kumekuwa na upungufu mkubwa baada ya baadhi ya watumishi nao kuwa wamekumbwa na kadhia hiyo. Tumechukua hatua za haraka na za makusudi, tumeshatoa kibali cha ajira kwa ajili ya watumishi 15,000 na tutaweza kuwapangia. Tumeanza mashauriano na TAMISEMI ili kuweza kujua ikama ikae vipi, eneo gani lina upungufu mkubwa; na tunaamini kwa wiki ijayo zoezi hili litaweza kufika katika sehemu nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, hii ni kati ya sasa na mwezi Juni, lakini kwa kiasi kikubwa watumishi wengi pia watakuwa katika sekta ya afya. Kwa hiyo, niwatoe hofu sana Waheshimiwa Wabunge, tutajitahidi kucheza na

namba hizo 15,000 na tunaamini zitawenza kwa kiasi kikubwa kupunguza upungufu mkubwa wa wataalam wetu uliopo katika sekta hii ya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika mwaka ujao wa fedha kuanzia mwezi Julai tutatoa pia tena ajira nyingine 52,436 na kwa kiasi kikubwa ajira nyingi zitakwenda katika sekta ya afya, elimu pamoja na Sekta nyingine. Kwa hiyo niwatoe tu hofu Waheshimiwa Wabunge, nimewasikiliza vizuri na tutaangalia kwa kweli ikama imekaa vipi kuhakikisha kwamba yale maeneo ya pembezoni, maeneo yenye upungufu mkubwa na kada zile za kipaumbele basi zitawenza kutendewa haki kama ambavyo inahitajika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda nizungumzie suala zima la *telemedicine*. Nilimsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja wa Mbeya akielezea umuhimu wa kuweza kutoa matibabu au rufani kwa njia ya *telemedicine*. Bahati nzuri kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ofisi yangu Wakala wa Serikali Mtandao tunahimiza masuala ya matumizi ya TEHAMA katika huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kupitia mradi wa *RCAP* ambao tunafadhiliwa na Benki ya Dunia na kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tumeshaweza kujenga mfumo huu wa *telemedicine* na mfumo umekamilika, lakini vile vile tumeshafunga vifaa mbalimbali na tunesimika mfumo katika vituo vyote isipokuwa Mafia ambako kulikuwa kuna changamoto kidogo ya mawasiliano lakini tunaendelea kuifanya kazi na naamini suluhisho litawenza kupatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo huu wa *telemedicine*, lakini vile vile tutaanza majoribio kuanzia tarehe 15 Mei mwaka huu hadi tarehe 15 Juni na tunaamini majoribio haya tutayafanya katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi, Hospitali ya Wilaya ya Nyangao Lindi Vijijini, Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, Hospitali ya Rufaa Morogoro, Hospitali ya Wilaya Turiani,

Hospitali ya Wilaya Kilosa pamoja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Baada ya majaribio hayo tunaamini sasa tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwenda katika hospitali zote kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala zima la maslahi kwa watumishi wa sekta ya afya. Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwa hisia kubwa na ni kweli tunatambua *risk* mbalimbali ambazo wataalam hawa wanakutana nazo wanapokuwa wanatenda kazi zao. Vile vile tumejitahidi kuweka aina mbalimbali za maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kubwa na rai kwa waajiri, wanapopanga bajeti zao wahakikishe wanazingatia stahiki mbalimbali za watumishi wakiwemo watumishi wa sekta ya afya. Waangalle masuala mazima ya *on-call allowances*. Wameeleza Waheshimiwa Wabunge masuala ya upungufu wa *uniforms* na wamefanya mpaka *comparison* kwa nini sekta nyininge wanununuliwa na sekta nyininge hazinunuliwi. Tuombe sana kwa masuala ya muhimu kama haya ni vema mwajiri katika *first charge* ya vipaumbele vyake akaweka masuala haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa George Simbachawene, una dakika kumi zako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake kwa bajeti nzuri ambayo kwa kiasi kikubwa imejikita kutatua matatizo ya afya kwa Watanzania. Pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri tumeisikia na kwa kuwa tuna shida ya muda pengine si rahisi sana kujibu kila hoja na hivyo nitajikita kwenye maeneo manne ambayo yamezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza liliwa ni mpango gani upo kwa ajili ya kumalizia maboma ya vituo vya afya na zahanati katika maeneo yetu. Napenda tu nichukue nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa ni wawakilishi lakini pia wanaishi katika maeneo hayo, kwamba vyanzo vikuu vya mapato kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na hasa katika sekta zote ikiwemo sekta ya afya kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ni hivi vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa ni nguvu kazi, nguvu ya wananchi. Lazima tutambue kwamba wananchi hawa nguvu yao ni rasilimali ya Taifa, kwa hiyo lazima itumike katika kutatua matatizo yanayogusa maisha yao. Tukumbuke tu kwamba nchi yetu ni nchi inayofuata misingi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na ndivyo Katiba yetu inavyosema. Bado tunaamini kwamba kwa nchi masikini kama yetu tunapaswa kutumia nguvu za wananchi wetu katika kutatua kero za wananchi na kujiletea maendeleo. Vile vile tabia hiyo inajenga umoja lakini pia inajenga *ownership* kwa wananchi juu ya miradi inayowahusu ya huduma za jamii kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini chanzo kingine cha pili ni vyanzo vya ndani vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambavyo, nilipowasilisha bajeti ya TAMISEMI, nilisema, asilimia 40 ya fedha za ndani zitakwenda kwenye maendeleo na maendeleo yenye ni pamoja na kuchangia ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya huduma za kijamii ikiwemo huduma za afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti eneo la tatu ni Mfuko wa Maendeleo (*Local Government Development Grant*) ambayo kwa miaka mitatu nyuma ilikuwa haitoki lakini bajeti ya mwaka 2016/2017 tulitenga kiasi cha billioni 158 na hadi mwezi Desemba tumepeleka kiasi cha billioni 56 kwenye Halmashauri mbalimbali na wamezitumia katika kuhakikisha kwamba wanamalizia maboma yaliyojengwa ya kutolea

huduma za afya pamoja na elimu. Zimetolewa fedha hizi na kwa hivyo ni mipango na vipaumbele tu vya halmashauri ndivyo vinavyotakiwa ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tumetenga kiasi cha shilingi billioni 251.184. Fedha hizi zikigawanywa vizuri kwenye Halmashauri zetu na zikatumika kwa mujibu wa mwongozo tuliooutoa wa asilimia karibu themanini kwenda kwenye miradi ya Maendeleo nina hakika zitawezu kupunguza matatizo ya umalizaji wa maboma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ni mamlaka ya Serikali za Mitaa kuweka Mipango yake kwa kutambua vyanzo hivi; ndiyo itatupeleka kumaliza matatizo haya ya upungufu wa miundombinu ya utoaji wa huduma za afya. Wananchi watakaojitoa na kujituma Serikali itapeleka fedha za kutosha kuititia mfuko huu ili waweze kumalizia kuezeka na kufanya *finishing* ili huduma ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoelezwa juu ya kuwepo kwa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata. Tunazo kata karibu 4,200 kwa nchi nzima na tathmini tulizozifanya kwa ramani iliyotolewa na Wizara ya Afya ni takribani shilingi billioni 2.4 zinahitajika katika kukamilisha kituo kimoja cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, pamoja na mipango mingine ambayo Serikali inayo lakini ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwanza kuweka kwenye mipango yao lakini pia kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo ingawa tunayo mipango mingine ambayo tunaendelea nayo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba tunakwenda kidogo kidogo kwa vituo vichache vichache na hatimaye tuweze kumaliza kwa nchi nzima angalau kwa kila Halmashauri kuwa na kituo kimoja kipywa ukiondoa vile vya zamani. Kwa kufanya hivi tutakuwa

na vituo vingi sana kuliko vituo tulivyovijenga toka tulivyopata uhuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu hapa kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, tujitahidi basi kuwahamasisha wananchi, kutenga yale maeneo kama tulivyosema na wale waliokwishatenga yale maeneo si kwamba tumewaacha, hapana, tunafahamu na tuko kwenye michakato mbalimbali wa kuhakikisha kwamba tunatafuta *funds* ili tuweze kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Lakini mipango iwepo kwanza kwa wananchi wenyewe wa mamlaka husika na hicho kidogo kilichoko ikiwa ni *ku-clear* na kuanza hata kidogo kwa kutumia ramani iliyopo waanze halafu Serikali inakwenda ina-*respond* na *ku-support* pale ambapo wameanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lilirozungumzwa ni asilimia tano ya wanawake, zile ndizo tunazosemaga asilimia 10 kwa wanawake na vijana, lakini hapa nizungumzie tano ambayo ndiyo inayohusika na Sekta ya Wizara ya Afya. Kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia mwezi Desemba tumepeleka kiasi cha shilingi billioni 15.6 kwenye Halmashauri ikiwa ni kiasi cha asilimia hizo zilizotengwa kutokana na mapato ya ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti nilisema kwamba mapato ya ndani ni pamoja na *OC* inayotoka Hazina ukijumlisha na *Own Source* na makusanyo ya ndani ya Halmashauri, ukijumlisha ndipo unapata *the total*, ile *total* yake ndiyo unachukua asilimia 10 unapata ile inayotakiwa kupelekwa kwa wanawake na vijana. Kwa hivyo, naamini kabisa hadi sasa wanufaika 18,000 kwa nchi nzima 233 wakiwemo wanawake wamenufaika na fedha hizi billioni zaidi ya 15 zilizopelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si jambo ambalo halifanyiki linafanyika, lakini nitoe rai kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba wanapeleka kiwango hiki cha fedha kadri wanavyokusanya ili wasiwe na *audit query* kwa sababu jambo hili sasa Waheshimiwa Wabunge

tunalisimamia kwa karibu. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kusaidia kuzishauri Halmashauri lakini pia huko kwenye Halmashauri miliko ndiko zinakotolewa hizo fedha na ndiko zinakopatikana. Kwa hiyo, washauri wazuri na tuwaelekeze ili waweze kutekeleza agizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti dhana ya ugatuaji wa madaraka katika sekta ya afya. Wakati mwingine kunazungumzwa kwamba kuna mkanganyiko. Niseme tu kwamba hakuna mkanganyiko wowote katika utoaji wa huduma ya afya kwa maana ya ugatuaji madaraka. Wizara ya Afya kazi yake ni kusimamia Sera ya Afya ya Taifa na katika kusimamia Sera ya Afya ya Taifa jukumu lake kubwa ni kuseti miongozo na *standards* ya utoaji wa huduma ya afya nchini; ambapo kwa kufanya hivyo tunazingatia viwango vya kimataifa, mahitaji ya kimataifa lakini pia na mahitaji ya ndani; wao ndio wanaosimamia sisi TAMISEMI ni watekelezaji wa maelekezo hayo. Kwa hiyo, wala hakuna mkanganyiko na Serikali ni moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugatuaji huu duniani kote maeneo ambako utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya watu yamekuwa *realized* imetokana na dhana ya upelekaji madaraka kwa umma. Unapopeleka madaraka kwa umma unawapa the *ownership* na kwa kusema hivi hata mara moja haiwi mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kwamba unaposema TAMISEMI imepewa jukumu unamaanisha nini? Waheshimiwa Wabunge unaposema TAMISEMI impelekewa jukumu hili, unamaanisha uwepo wa Mkuu wa Mkoa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Mkoa akisimamia rasilimali zote zinazokwenda kwenye Mkoa wake. Unazungumzia na wataalam wote tulio wapeleka kwenye Mkoa, unazungumzia uwepo wa Mkuu wa Wilaya na watalaam alionao, lakini pia unazungumzia uwepo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mkurugenzi na wataalam waliopo na Madiwani wanaosimamia kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *ownership* hii ndiyo iliyofanywa kwa nchi zilizoendelea kama Uchina, ndiyo inayofanywa na Japan. Sisi hatuwezi kuanzisha mfumo wa peke yetu, tukaanzisha jambo ambalo hatuwezi kuwa na *ownership* ya wananchi, maendeleo lazima yawe yanaguswa kwa *ownership* ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu TAMISEMI tuna uwezo wa kufanya kazi hii na tunapata *support* nzuri sana kutoka Wizara za Kisekta ikiwemo Wizara ya Afya katika Sekta ya Afya na tunakwenda vizuri na tunashirikiana vizuri sana, tuendelee na utaratibu huu utatusaidia kuivusha nchi yetu kwenye matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla una dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwangi wa rehemma na mwenye kurehemu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili nami niweze kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufikishe kwa Mheshimiwa Spika salamu zangu za masikitiko makubwa lakini pia nikuunganishe na wewe kwenye salamu hizo za pole pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote kwa misiba mbalimbali iliyotukuta. Tukianza na msiba wa aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samuel John Sitta, lakini pia Wabunge wenzetu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha. Kwa wote hawa naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwa namna ya kipekee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kunipa ushirikiano na kunishirikisha kwa ukaribu katika utekelezaji wa jukumu hili la kusimamia na kuiongoza Wizara hii. Pia naomba nimshukuru mke wangu mpenzi Dkt. Bayum Kigwangalla na watoto wetu Sheila, Hawa na H.K Junior kwa kunitia moyo na kunivumilia wakati wote ninapokuwa mbali na familia yangu nikitekeleza majukumu mbalimbali ya kila siku ya ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia kwa kipekee nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyevit wote wa Bunge kwa uongozi thabiti mnaotoa kila siku na ushirikiano mnaotupa katika kutekeleza majukumu yetu tuliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia siku hata siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza watumishi wote wa Wizara yetu ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakiongozwa na Katibu Mkuu Idara Kuu ya Afya, kaka yangu Dkt. Mpoki Ulisubisy na Katibu Mkuu Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii ndugu yangu mama Sihaba Nkinga pamoja na wafanyakazi wote wa sekta za afya na maendeleo ya jamii nchini kwa kazi yao nzuri na iliyotukuka ambayo wamekuwa wakiifanya kila siku katika kuboresha maisha ya Watanzania wenzetu. Nawaomba sana tuendelee kufanya kazi kwa ushirikiano huu, lakini pia kwa uadilifu mkubwa ili kufikia malengo yetu tuliyopewa na kufikia malengo ya Taifa kadri tunavyotarajiwa na Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kusema hapa Bungeni. Michango yenu kwa hakika inalenga kuboresha huduma za afya na maendeleo ya jamii

zinazotolewa na kusimamiwa na Wizara yetu. Kama mlivyoona ndugu zangu, hoja zilizotolewa ni nyingi lakini muda tuliopewa hautoshi kujibu hoja zote, hivyo majibu ya kina ya hoja moja baada ya nyingine tutayawasilisha kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge wote mtapatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa nijibu hoja chache ambazo nimepewa nizzungumzie katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba kuzungumzia kuhusu mfumo wa afya (*health system*). Kwa hakika mfumo wa afya tangu tumepewa majukumu haya na Watanzania mwaka 2015 umeendelea kuimarika kwa kasi ya ajabu. Mafanikio haya ya kuimarika kwa mfumo wa afya yaani (*health system*) hayawesi kuzungumziwa bila kuutambua na kuuthamini mchango mkubwa wa viongozi wetu wakuu wanaoongozwa na Rais wetu mpwendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye hata kabla hajatuteua sisi kwenye nafasi hizi alionesha nia yake ya dhati ya kutaka kuleta mabadiliko kwenye Sekta ya Afya kwa kuanza kusimamia sekta hii yeye mwenyewe kwa ziara zake maarufu za kushtukiza alizozifanya Hospitali ya Taifa Muhimbili na matokeo yake sote tunayaafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kiongozi wetu Mkuu mwingine Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa *champion* wa mambo yote yanayohusu akinamama lakini pia afya ya uzazi salama ambapo pia amekuwa karibu sana na Wizara hii akitupa mwongozo, maelekezo na ulezzi wa kila siku katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye amekuwa mstari wa mbele kwenye utekelezaji wa majukumu ya sekta hii na tumemwona kila alipofika kwenye mkoa wowote ule kwenye nchi yetu amekuwa akitusaidia kufanya usimamizi wa moja kwa moja yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa sababu linatokana na utafiti ambao umefanywa na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya TWaweza, ambapo katika utafiti huo matokeo waliyatoa mwaka jana katikati, wameonesha kwamba mfumo wa afya umeimarika kutokana na takwimu za sauti za wananchi ambao waliwahoji. Kwa msingi huo mafanikio haya kazi yetu sasa ni kuendelea kuyalinda lakini pia kuendelea kusonga mbele siku hata siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ninayopenda kuzungumzia inahusu rasilimali watu. Mfumo wa afya una vitu vikubwa vitatu; cha kwanza ni rasilimali watu; cha pili ni vifaa, vifaa tiba, dawa, vitendanishi; lakini cha tatu ni miundombinu ya kutolea huduma za afya. Eneo la muhimu kuliko yote katika muktadha wa kutoa huduma bora za afya ni eneo la rasilimali watu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala hili kwa uchungu kuanzia kwenye mambo ya udahili, ajira kwa watumishi kwenye sekta hii pamoja na motisha, yote haya yanahu su eneo la rasilimali watu. Kwa kuwa ni wengi waliochangia, nawatambua wachache tu, wengine naomba mjue kwamba katika majibu ya hoja kwa ujumla wake mtapata majibu ya kina na majina yenu yatakuwa yamewekwa humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ambayo napenda kuifafanua kwa ujumla wake kwa sababu muda hautoshi ni mchango wa Mheshimiwa Devotha Minja, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mussa Sima, Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa mama Anna Makilagi. Kwa pamoja wamezungumzia mambo ya motisha na mambo mbalimbali, lakini pia kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia mambo ya fukuza fukuza ambayo imekuwa ikifanyika na naomba nizungumzie hili la mwisho nililolisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi kama Wizara ya Afya hatupendezwi sana na fukuza fukuza isiyofuata utaratibu kwa sababu sisi tuna jukumu la kusimamia sekta hii na katika kusimamia sekta hii tunafahamu hatuwezi kutimiza malengo

yaliyopo kwenye Sera ya Afya ya Taifa bila kuwa na rasilimali watu ambayo ina motisha ya kutosha. Ni kwa msingi huo, mara kwa mara tumeshuhudia Waziri wa Afya akitolea msimamo thabiti suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu kwenye sekta ya afya ni ina gharama kubwa sana, kuanzia kwenye *training* kuja kwenye ajira, gharama za kuwalipa mishahara, gharama za kuwapa motisha, gharama ya kumhudumia daktari mmoja ni kubwa sana ukilinganisha na wataalam kwenye sekta nyingine. Wataalam hawa wanatoa huduma kwa kiwango cha hali ya juu sana na mara nyingi, nje ya muda wao wa kawaida wa kufanya kazi. Kwa namna yoyote ile, watumishi wa Sekta ya Afya wanapaswa kutiwa moyo na sio kudhalilishwa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kwenye sekta hii tunasema tutaendelea kulinda maslahi ya watumishi wa Sekta ya Afya kama hawatofukuzwa au kusimamishwa kazi kwa taratibu za kimaadili ambazo sisi Wizara ya Afya tunazisimamia. Kuna taratibu za kiutawala hayo hatutayaingilia, lakini kwa mambo yote yanayohusu uadilifu wa watumishi kwenye sekta ya afya, mabaraza yote ya kitaaluma yako chini ya Wizara yetu na hivyo mtu yoyote yule awe kiongozi anayesimamia eneo lake la utawala ni lazima afuate utaratibu wa kisheria ambao unasimamiwa na Wizara yetu. Tunahitaji staha kwa wataalam hawa ili waendelee kupata moyo wa kuwashudumia Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la rasilimaliwatu tumepata mafanikio makubwa sana katika miaka ya hivi karibuni. Miaka iliyopita takriban 15, (miaka hiyo na mimi nilikuwa nasoma udaktari Chuo Kikuu) tulikuwa tunahitimu si zaidi ya 100 kwa nchi nzima; lakini leo hii kwa mwaka tuna uwezo wa kuzalisha Madaktari takriban 1,100 kila mwaka unaopita. Pia Wauguzi tu kwa mfano miaka hiyo ya 2000 mpaka 2005, tulikuwa tuna uwezo wa kuzalisha Wauguzi wasiozidi 3,500; leo hii ninavyozungumza hapa tuna

uwezo wa kuzalisha Wauguzi wapatao 13,562, hii ni idadi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokuja, kwa bahati mbaya hatuisimamii sisi kwenye sekta yetu na tunaendelea na mazungumzo na wenzetu ili tuweze kuipatia ufumbuzi, ni changamoto ya kuwa-*absorb* kwenye mfumo wa afya wataalam wote ambao tunawazalisha. Hii changamoto si yetu peke yetu, ni changamoto sana sana unaweza ukasema ya kitaifa kwa sababu inahusiana na ukomo wa bajeti, jambo ambalo linahusiana na ukuaji wa uchumi wetu. Kwa hivyo hatuwezi kumnyooshea kidole mtu yejote yule kati yetu kwa sababu ni jambo ambalo wakati mwingine liko nje na uwezo wetu wa kibinadamu, kwa sababu kama hakuna pesa za kuwalipa mishahara, unafanya nini hata kama unatamani kuwaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, pamoja na mafanikio makubwa tuliyoyapata kwenye eneo la *production* ya *health care workers* lakini tuna changamoto kubwa sana ya *absorption* ya *health care workers* kwenye *health system* ya nchi yetu. Changamoto hii tutaendelea kuitatua taratibu kama ambavyo Waziri anayehusika na Manejimenti ya Utumishi wa Umma amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wanapotaka kupata watumishi kwenye maeneo yao wanazungumzia kupata watumishi kutoka Wizara ya Afya; lakini wanashahau kwamba bajeti ya watumishi hawa iko kwenye dhamana ya watumishi ambao ni *Accounting Officers* kwenye maeneo yao; Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakurugenzi wa Hospitali mbalimbali, wote hawa wanapaswa kupanga bajeti kwa ajili ya kuajiri rasilimali watu kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kazi yetu ni kuzalisha, kuwasajili, kuangalia wanafanyaje kazi, kuangalia uadilifu wao na takwimu za rasilimali watu kwenye sekta ya afya nchini lakini si kuajiri. Kibali cha kuajiri kipo kwa wenzetu wa Menejimenti ya Utumishi wa umma lakini pia mishahara ipo

kwa wenzetu wa Hazina. Bajeti ya kuwaajiri ipo kwa Wakurugenzi wetu wa Halmashauri. Kwa hivyo, napenda kutumia jukwaa hili kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waanze kwanza wao wenye kwenye Halmashauri zao kupanga bajeti ya kuajiri rasilimaliwater ya kutosha kwenye maeneo yao kabla ya kuja kuomba sisi tuwasaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kwenye eneo hili la rasilimali watu ni changamoto ya *retention* ya *health care workers*. Changamoto ya kuhakikisha rasilimali watu kwenye sekta hii inabaki kwenye eneo husika, haiondoki kwa sababu tunaona sasa hivi Madaktari hao wachache tulionao kwa zaidi ya asilimia 70 wapo kwenye maeneo ya mijini tu, maeneo ya vijijini hakuna. Wakati wanapangwa na Wizara ya Afya pale mwanzoni ukifuatilia kuna *tracer studies* mbalimbali zinazofanyika ambazo zinafuatilla wafanyakazi walihitimu wapi, walihitimu lini na walipelekwa wapi na sasa wako wapi imeonekana kwamba wengi wanaopelekwa kwenye maeneo ya pembezoni wanahama kutoka huko, wanahamia kwenye maeneo ya *centre*; wanahamia kwenye Wilaya za Mjini ama kwenye miji mikubwa ama kwenye hospitali kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto ambayo inasababishwa na kuwepo kwa *imbalances* za kijiografia ambazo zinajitokeza kwenye mfumo wa afya, ambapo kuna baadhi ya maeneo ni *lucrative*, ni ya kijani zaidi kuliko maeneo mengine. Sasa kwa msingi huo ni lazima waajiri, kwa maana ya Wakurugenzi ama Wakurugenzi wa Hospitali ama wa Halmashauri ama Makatibu Tawala, wanapowaajiri ni lazima watengeneze *package* ya kutoa motisha kwa rasilimali watu kwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo nataka kulizungumzia limeshazungumziwa na Mheshimiwa George Simbachawene, linahusu ugatuaji wa madaraka (*decentralization by devolution*) na hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, Mheshimiwa Lwota, Mheshimiwa Restituta Mbogo, Mheshimiwa Jasmine Tiisekwa,

Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Makilagi na Mheshimiwa Shally Raymond, naomba niliache hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maendeleo ya jamii. Kwenye suala la maendeleo ya jamii mambo makubwa yaliyozungumziwa hapa jambo la kwanza ni la *training*. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati wamechangia kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Jamii tuvihamishe kutoka kwetu tuvipeleke Wizara ya Elimu. Jibu la hoja hii ni fupi tu, kwamba vyuo hivi sio vyuo vikuu ni vyuo vya kada za kati ambazo zinahitajika kwa ajili ya kuendeleza Sekta yetu ya Maendeleo ya Jamii na hivyo si lazima vikae kule kwenye Wizara ya Elimu, japokuwa mitihani yote ambayo inatolewa na vyuo hivi inatolewa na Taasisi ya *NACTE* lakini pia vinasimamiwa na *NACTE* ambayo ni Taasisi iko chini ya wenzetu wa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyonayo kwenye eneo hili ni namna ya kuwaajiri – *absorption* kama nilivyosema pale mwanzoni. Tunao watumishi wengi ambao tunawazlisha kila siku wataalam kwenye eneo hili lakini namna ya kuwaajiri ni changamoto. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote wanaosimamia maendeleo kwenye mikoa na wilaya kuweka bajeti ya kuajiri wataalam hawa, lakini pia kuweka bajeti kwa ajili ya kuwapa vitendea kazi na kuwapa maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaeleza kwamba Sera yetu ya Maendeleo ya Jamii inataka kwa uchache wawepo wawili kwenye kila Kata, wasikae kwenye ofisi kuu pale Wilayani, wakae kwenye kata, wapewe vyombo vya kufanyia kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne linahusu huduma za tiba kwenye Hospitali za Muhimbili, *MOI, Ocean Road*, Kitengo cha *Psychiatric* kimezungumziwa pamoja na kitengo cha moyo *JKC* pamoja na *KCMC* na Bugando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitazungumzia moja tu la tiba ya saratani. Tiba ya saratani wakati tunaingia

kwenye majukumu haya zilikuwa haziridhishi kwa kiasi kikubwa sana, lakini mikakati ambayo imewekwa imeanza kuboresha huduma kwenye eneo hili kwa kasi ya ajabu. Kwa sababu kwa mfano, tiba ya *chemotherapy* ilikuwa mtu anapaswa kusubiri kwa miezi zaidi ya mitatu, leo hii tumeweza kupunguza *waiting time* kutoka hiyo zaidi ya miezi mitatu mpaka kufikia wiki tano hadi sita tu na tunakusudia kufikia mwisho wa mwaka huu tuweze kushusha *waiting time* mpaka kufikia kati ya wiki mbili mpaka wiki nne mgonjwa awe ameshapata tiba anayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hakukuwa na baadhi ya vifaa vya kutolea tiba ya mionzi. Vile vilivyokuwepo vimekuwa ni vya zamani sana na sasa tayari tumepewa bajeti na tuko katika mchakato wa kununua mashine mpya ya *linear accelerator* pamoja na *CT simulator* kwa ajili ya kutoa tiba ya mionzi, ambao tuna uhakika mwisho wa mwezi huu utakamilika. Tuna malengo ya mbali zaidi ya kununua mashine nyininge ya kisasa ambayo katika ukanda huu wa maziwa makuu hakuna hata nchi moja imefunga mtambo huo unaoitwa *Pet CT* ambao nao lengo lake ni kufanya uchunguzi na kubaini kwa uhakika zaidi yaani kufanya *dermacation* ya eneo ambalo limeathiriwa na *cells* ambazo ni *malignant* ambazo zina *cancer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuna mambo makubwa mawili yanafanyika pale ambayo ni *state of the art*, ni ya kisasa sana, na hii ni upandikizaji wa kifaa cha usikivu kinachojulikana kama *cochlea implant*. Hizi ni *operations* mpya ambazo zitaanza kufanyika pale na zitatusaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaanza kufanya *operation* za kupandikiza mafigo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na hii pia itatusaidia kupunguza wagonjwa kwenda nje ya nchi. Hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais alilizungumza wakati anazindua Bunge hapa hapa Bungeni

la kupunguza idadi ya wagonjwa wanaoenda kutibiwa nje ya nchi kwa kuboresha huduma za rufaa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kuzungumzia ni hospitali za rufaa za mikoa. Hili lingeweza kwenda sambamba na lile la *decentralization by devolution* ambalo nimeliruka kwa sababu limeelezewa.

Waheshimiwa Wabunge wengi na hususan Wajumbe Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wamekuwa wakitamani sana, huduma za afya zisimamiwe moja kwa moja na Wizara ya Afya Makao Makuu, yaani kama *Sectorial Ministry*. Sisi tunadhani na tunaamini kwa dhati kabisa kwamba mfumo uliopo sasa ndio mfumo mzuri zaidi wa kuhudumia wananchi kwenye sekta hii ya afya hapa nchini, kwa sababu wananchi kwa kuititia mfumo huu wanakuwa na sauti ya moja kwa moja kwenye huduma zinazotolewa kwenye vituo vya afya kule chini mpaka kufikia ngazi ya hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoki-*plan* na kufikiria ndani ya Serikali kwa sasa ni angalau kama tutaweza tutenganishe mifumo miwili ya kutoa huduma za afya. Bado ipo katika fikra, kwamba mfumo wa afya ya msingi yaani kutoka zahanati, kituo cha afya mpaka ngazi ya hospitali ya wilaya usimamiwe na wenzetu wa TAMISEMI kuititia mamlaka zao za Serikali za Mitaa, lakini hospitali za mkoa kwa sababu ni hospitali za rufaa uje kwenye fungu 52, yaani Wizara ya Afya usimamiwe huku pamoja na huduma nydingine za rufaa. Ni wazo ambalo tunalifikiria ili ku-*accommodate* mapendekezo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Muda wako Mheshimiwa ndio huo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii na naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Afya. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mtoa Hoja Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ahitimishe hoja yake. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia hoja yangu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye amewasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti yetu. Pia niishukuru sana Kamati kwa sababu wamechambua mapendekezo yetu na tunawashukuru Kambi ya Upinzani kwa hotuba yao ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, tunapokea pia maoni na ushauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni na ushauri wao na niseme tu kwamba tumepokea hoja nyingi na kwa sababu ya muda sitaweza kupitia *book* lote hili kumjibu Mbunge mmoja mmoja, lakini katika hatua hii niseme tumepokea maoni na ushauri wenu. Kubwa ambalo ilimetupa faraja wote Bunge hili tumeungana tunakubaliana kwamba afya ni maendeleo, afya ni elimu, afya ni kilimo, afya ni viwanda, afya ni ulinzi, afya ni uchumi, kwa hiyo, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu ni 164. Waliochangia kwa kuzungumza ni 61 na kwa maandishi ni 99

na wakati wa mjadala wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Waheshimiwa Wabunge wanne pia wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitawataja, lakini nitaomba sasa nitoe maeneo makubwa ambayo yameelezwa na Kamati na vile vile yameelezwa na Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Kabla ya kuondoka katika Bunge hili la bajeti, tutawasilisha majibu ya hoja zote. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufanuzi alioutoa katika baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitajikita katika mambo makubwa matano. Jambo la kwanza nitazungumzia rasilimali fedha kwa ajili ya sekta ya afya; pili, nitazungumzia upatikanaji wa dawa; tatu, nitazungumzia afya ya uzazi na motto; na nne nitazungumzia suala la kuthibiti vifo vya watoto wadogo na pia nitazungumzia kuwawezesha wanawake kiuchumi na masuala ya Sheria ya Ndoa ikiwemo sheria zinazolinda haki ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limetolewa maoni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ni kuhusu rasilimali fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya, kwamba ni ndogo ni chache na haziakisi hali halisi ya changamoto zilizopo katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hali halisi ya ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu. Pili, ningetaka kuwatahadharisha Waheshimiwa Wabunge watofautishe Bajeti ya Wizara ya Afya na Bajeti ya Sekta ya Afya. Kuna mambo mawili niyaweke wazi. Kwa mfumo wa Nchi yetu ambao Mheshimiwa Simbachawene ameuongelea, hela kwa ajili ya kutatua changamoto za sekta ya afya zipo chini ya Fungu 52, lakini pia tutazikuta chini ya Fungu 56 kwa ajili ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa pamoja na halmashauri. Kwa hiyo, kuna Mheshimiwa amesema bajeti ya sekta ya afya, ni asilimia tatu, si sahihi. Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya

Sekta ya Afya ni trillioni 2.2. Nikichukua fedha za TAMISEMI na fedha zilizotengwa chini ya Wizara yangu ni trillioni 2.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwapitisha Waheshimiwa Wabunge wakaangalia. Mwaka 2015/2016, Sekta ya Afya ilitengewa shilingi trillioni 1.8; mwaka 2016/2017, Sekta ya Afya imetengewa trillioni 1.9, mwaka 2017/2018 Sekta ya Afya imetengewa shilingi trillioni 2.2. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kati ya vipaumbele vitatu vya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, sekta ya afya ni ya tatu baada ya miundombinu inafuatia elimu halafu inakuja sekta ya afya. Sisemi kwamba fedha hizi zinatosha, lakini Serikali inajitahidi kwa dhahiri kuonesha kwamba afya za Watanzania ni kipaumbele na ni jambo ambalo tumeliahidi katika llani ya Uchaguzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija sasa nikiangalia Bajeti ya Wizara ya Afya, Fungu 52, unaiona kabisa dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendelea kuwekeza katika afya za Watanzania. 2014/2015, bajeti ya Wizara ya Afya ilikuwa ni bilioni 713; mwaka 2015/2016 bilioni 780; na sasa hivi kwa ajili tu ya Fungu 52 na nimechukua tu, nimeondoa maeneo mengine sasa hivi (2016/2017) inaenda kwenye bilioni 796 na jana nimeomba trillioni 1.1 kwa ajili ya *Vote 52*. Kwa hiyo, jambo ambalo nataka kuwasilitiza Waheshimiwa Wabunge, ni kweli tumeridhia Azimio la Abuja la kutenga asilimia 15 kwa ajili ya Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile ni azimio lazima tuangalie pia vipaumbele vingine vinavyoikabili nchi yetu. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wanatoa kipaumbele kwa ajili ya sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limeongelewa pia na Kamati ya Kudumu ya Bunge pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge Lucy Owenya, Suzan Lyimo na rafiki yangu mpenzi Azza Hilary kwamba tunategemea sana fedha za wafadhili kwa ajili ya kuendesha kutatua changamoto za sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge tumeanza kuwekeza, tumeanza kutumia rasilimali zetu za ndani kwa ajili ya kutatua changamoto za sekta ya afya. Natoa kutoa mfano, mwaka 2014/2015 fedha za ndani kwa ajili ya bajeti ya sekta ya afya zilikuwa bilioni 54; mwaka 2015/2016 bilioni 66; mwaka 2016/2017 na hizi ni fedha za maendeleo sizungumzii OC; zimeenda mpaka bilioni 320 na mkiangalia fedha za ndani ambazo sasa tunaomba kwa ajili ya kuetkeleza miradi ya maendeleo ni takribani bilioni 336.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ongezeko hili linaonesha ni jinsi gani Serikali inatekeleza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwamba ni lazima tutumie rasilimali za ndani kwa ajili ya kutatua changamoto za sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali katika miradi kwa mfano ya UKIMWI, ukoma, malaria na kifua kikuu asilimia kubwa ya fedha zinatoka kwa wafadhilli, lakini kwa mfano dawa za UKIMWI, tumeanza kutenga rasilimali zetu za ndani kwa ajili ya masuala ya UKIMWI. Pia katika masuala ya uzazi wa mpango kwa mara ya kwanza, tumetenga bilioni 14, fedha za ndani kwa ajili ya masuala ya uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe hoja hii kwa kusema kwamba zipo chngamoto za rasilimali fedha, kwa sababu pia zipo changamoto nyingi za kimaendeleo katika nchi yetu. Nataka kwathibitishia dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kuwekeza katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni faraja kwetu, kwa mara ya kwanza tumekuwa tukipata fedha za kutekeleza miradi, nitatoa mfano wa fedha za dawa. Mwaka 2015/2016 fedha za dawa zilizotolewa ilikuwa ni bilioni 24 tu, nchi nzima iliendeshwa kwa fedha za dawa kwa bilioni 24 tu. Leo ninapoongea jana nilisema ni bilioni 112 lakini tumepata bilioni 20. Kwa hiyo sasa hivi tunaongea bilioni 132 ambazo zimetolewa na Hazina kwa ajili ya fedha za dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi pamoja na Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu upatikanaji wa dawa. Tunapokea pongezi za Waheshimiwa Wabunge, kwamba tumeboresha upatikanaji wa fedha za dawa, lakini pia tumepokea changamoto kwamba kupatikana kwa fedha za dawa sio kupatikana kwa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi hapa. Katika Hotuba yangu, nimezungumzia upatikanaji wa dawa katika Bohari ya Dawa ni asilimi 81 nimetumia vigezo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi haiwezi kuwa na dawa zaidi ya; tukasema bohari ya dawa ina dawa 3000, 4000 tunaangalia tunaita dawa muhimu zaidi (*Essential Medicine*) ziko 135. Kwa hiyo, tunaposema upatikanaji wa dawa ni asilimia 81 maana yake katika kila zile dawa 135 asilimia 81 ya dawa hizo zinapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hizi takwimu sio za dawa 2,000, dawa 3,000, ni dawa 135 ambazo ndizo za kuokoa maisha. Hata hivyo, sasa tumeenda mbali zaidi, kutohana na maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, mlitushauri tusiishie tu katika Bohari ya Dawa, ndiyo maana katika bajeti yangu kwa mara ya kwanza tumeenda mpaka katika mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ambazo nimeziweka katika jedwali la pili, tumeleteewa na Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya. Katika hotuba yangu tumeleeza tunaendelea kuboresha mfumo ili tujiridhishe kwamba, takwimu hizi tulizoleteewa ni sahihi. Kwa hiyo, nakubali zipo changamoto za dawa kuwepo katika vituo vya afya na katika zahanati. Changamoto ya kwanza, maoteo ya mahitaji yanaletwa kwa kuchelewa. Nitumie fursa hii kuzitaka halmashauri zote kuleta maoteo ya mahitaji ya dawa kama Kanuni ya Sheria ya Manunuzi inavyotaka. Wanatakiwa watuletee by terehe 30 Januari ya mwaka huo

kusudi tuweze kuisaidia *MSD* kununua dawa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Bobali aliniambia kama haya majedwali yanatofautiana; nadhani hajanielewa. Tutofautishe fedha za dawa na upatikanaji wa dawa. Mheshimiwa Mwenyekiti ni Mwanasheria, moja ya sifa kubwa ya Wanasheria ni kusoma kila kitu na kukitafakari. Kwa hiyo, nimeisoma hotuba zaidi ya mara 10 siletewi. Kati ya jambo ambalo labda Watumishi wa Wizara ya Afya wananchukia ni kwa sababu, nasoma kila kitu, niko tayari hata nirudishe mara 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimejifunza kwako wakati nafanya *internship* yeye alikuwa ndio Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia, nimejifunza kwake wakati ni Mwenyekiti wa Kamati Namba Moja, Kamati ya Kuandika Katiba inayopendekezwa. Kwa hiyo, wanasheria tunasoma, hatuletewi tu ukapitisha. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana Mheshimiwa Sannda, shemeji yangu, amezungumzia tatizo la *prescription*. Kwamba, dawa zipo, lakini saa nydingine wataalam wetu badala ya kuandika dawa zilizopo katika kituo anaamua kuandika dawa pengine zilizo katika duka lake nje ya hospitali, kwa hiyo, hili tutalisimamia. Kwenye kuandika dawa wanatakiwa watu waandikiwe dawa zile ambazo ni dawa muhimu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, dawa zitapatikana kwa sababu tayari tumeingia mikataba mitano na wazalishaji wa dawa. Kwa hiyo, dawa zitatoka moja kwa moja kwa wazalishaji, maana yake zitapatikana kwa urahisi. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge na mimi siogopi kuwajibika, nilisema nataka kupimwa kwa mambo ikiwemo upatikanaji wa dawa na hili nataka kuwathibitishia, dawa 135 zitapatikana kwa angalau asilimia 95, hizo nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge, lakini kama kuna

mtu atataka dawa ambayo ni *brand*, si dawa zile 135, hilo siwezi kumthibitishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidi kuboresha upatikanaji wa dawa *Ocean Road*. Sasa hivi *Ocean Road* ina dawa kutoka asilimia tatu mpaka asilimia 60. Dawa za Saratani ya mlango wa kizazi ni mpaka asilimia 60. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulitolea ufanuzi ni; Mheshimiwa Zedi, tumepokea ushauri wako, lakini taarifa zetu kidogo zinakinzana. Nataka kukuahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi. Nitoe ufanuzi kwa Waheshimiwa Wabunge, tumeshtoa maelekezo kwa *MSD* suala la *OS (Out of Stock)*, tumemwelekeza *MSD* kama umeombwa upeleke dawa ndani ya saa 24 kama hiyo dawa huna, umwambie halmashauri hiyo dawa sina kwa hiyo, nakupa kibali ukununue kwa mshitiri mwengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, halmashauri zetu zianze kuwatambua washitiri (*Suppliers*) kwamba, kama *MSD* hana na una hela yako, akupe *OS* ndani ya *24 hours* kusudi mkanunue dawa maeneo mengine. Nawathibitishia dawa zitapatikana na niko tayari kuwashibitishia Waheshimiwa Wabunge hili suala linawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bulembo, Mheshimiwa Umbulla na Kambi ya Upinzani mmezungumzia kuboresha Bohari ya Dawa. Kama nilivyosema hayo mabadiliko ndiyo tumeanza na kubwa kwa kweli sasa hivi, nashukuru Waheshimiwa Wabunge mmekubali, si fedha ni mifumo. Hii mifumo ndio tunahangaika nayo ikiwemo mifumo ya ugavi na usambazaji wa dawa. Kwa hiyo, Mungu akijalia, nikija kwenye bajeti nyingine tutakuja na takwimu mpaka za zahanati. Tutakuja na takwimu za dawa mpaka katika ngazi ya vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa kwa hisia kubwa suala la kuhusu kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Walioongea hili ni Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kambi Raskmi ya Upinzani, Mheshimiwa Risala, Mheshimiwa Moshi, Mheshimiwa Mgeni, Mheshimiwa dada yangu Amina Makilagi, Mdogo wangu Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Bukwimba, Mama yetu Mheshimiwa Mama Salma Kikwete na Mheshimiwa Kemilembe. Tunapokea maoni yote kuhusu kuboresha jitihada ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe uafanuzi mmoja; nakubali kwamba vifo vitokanavyo na uzazi bado ni tatizo katika nchi yetu. Naomba niseme, siyo kwamba tumejikwaa wapi? Wala siko hapa kubisha kuhusu takwimu; kwa sababu, ukiangalia sensa limekuwa ni jambo ambalo kidogo limeshtua watu kwa sababu, sensa ya mwaka 2012 ilikuwa inaonesha vifo vya akinamama wajawazito ni 430 katika kila vizazi hai laki moja, lakini takwimu za 2015/2016 ndiyo zinatupa 556.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Waziri mwenye dhamana, mama, mwanamke, nikisema takwimu hizi sizikubali nitakuwa siwatendei haki Waheshimiwa Wabunge, siwatendei haki wanawake wenzangu wa Tanzania. Nataka kuwathibitishia, ndiyo maana jana nilisema ukiniuliza Waziri wa Afya, Bajeti hii inajibu kero gani? Kama llani ya Uchaguzi ya CCM inavyotuelekeza tupunguze vifo; bajeti hii inajibu kupunguza vifo vya akinamama wajawazito. Tumeonesha, kwanza tumewekeza katika huduma za uzazi wa mpango. Kwa sababu wataalam wanasema, uzazi wa mpango unaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 30.

Waheshimiwa Wabunge, niwape changamoto, tunapofanya mikutano katika Majimbo yetu, tuhimize masuala ya uzazi wa mpango. Mheshimiwa Shally Raymond umeongea vizuri kwamba, sasa hivi bado kiwango cha uzazi Tanzania ni asilimia 2.7, *I mean population growth*; na mwanamke wa Tanzania sasa hivi anazaa watoto kati ya watano mpaka sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena nyie watani wangu Wasukuma tena, ndiyo kidogo kule Kanda ya Ziwa matumizi ya uzazi wa mpango hayako vizuri. Nataka kuwaambia, zama... (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaona Wasukuma watani zangu. Nataka kuwaambia kwamba zama zimebadilika. Sasa hivi ukizaa hata watoto wawili, wataatu na tumeboresha huduma za chanjo, watoto wale wanaishi. Kwa hiyo, zile zama za kwamba lazima mtu azae watoto 10, 12, lakini tuangalie pia, hao watoto utaweza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kukuthibitishia jambo la pili ambalo tutalifanya sambamba na kuimarisha huduma za uzazi wa mpango, tutaimarisha huduma za akinamama wakati wa ujauzito. Ni kweli, unaweza ukaenda katika Kituo cha Afya ukakuta mama mjamzito hapimwi hata wingi wa damu, hapimwi protini, hapimwi hata kama *pressure* iko juu au haiko juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene hayupo, lakini nitoe maelekezo kwa Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa, hufai kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya na Mkoa kama zahanati yako inakosa hata mashine ya kupimia *BP* kwa mwanamke mjamzito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu wataalam wanaita *albu stick* kwa ajili ya kupima mkojo kwa akinamama wajawazito kama protini ni nyingi. *Stick 50* zinazuwa sh. 9,000/= tu, *DMO* unasubiri Mheshimiwa Waziri Simbachawene akuletee sh. 9,000/= kwa ajili ya kununua vipimo vyta kupima protini kwa akinamama wajawazito! Kwa hiyo, kati ya eneo ambalo nitakuwa mkali ni suala la huduma za wajawazito wakati wanapohitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; ye ye amekuwa ndio nguzo yangu, ndio chachu yangu na amekuwa akinipa moyo wa kuendelea kupambana, kwa sababu mimi na ye ye na bahati nzuri tulipita wote kuomba

kura, eneo ambalo tunataka kukumbukwa na wanawake wa Tanzania ni katika afya ya uzazi na mtoto na hili tutaweza kulifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii tumeonesha kwamba tutajenga Benki za Damu tano. Haijawahi kutokea katika bajeti ya Wizara ya Afya. Benki za Damu katika mikoa mitano. Tumeonesha Manyara, tutajenga Katavi, tutajenga Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika bajeti hii, jana nimeeleza kwa uchungu mkubwa, kwa mara ya kwanza tunatenga fedha zetu za ndani kwa ajili ya huduma za msingi za uzazi za dharura (*BIMOC*). Kwa hiyo, sasa hivi na ninarudia tena, Waheshimiwa Wabunge nataka muwe mashahidi, hakuna mwanamke mjamzito atafariki kwa kukosa sindano ya *oxytocin* kwa sababu tu amevuja damu. Hakuna mwanamke mjamzito wa Tanzania atafariki kwa kukosa dawa inaitwa *Magnesium Sulphate* kwa ajili ya kifafa cha mimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka bajeti hii tunaanza na hizo dawa mbili, lakini mipango yetu baadaye; sababu nyingine ya vifo vitokanavyo na uzazi ni uambukizo. Kwa nini wanawake wajawazito wanakuwa? Kwanza wanavuja damu; pili, wanapata kifafa cha mimba; tatu, wanapata maambukizi na nne, wanapata uzazi pingamizi. Kwa hiyo, kwenye kifafa cha mimba na kwenye masuala ya kuvuja damu, tumekuja na hiyo *intervention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzazi pingamizi, ndio maana tumesema tutaboresha Vituo vya Afya 150 ili viweze kufanya upasuaji, huduma za uzazi za dharura, ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni. Mheshimiwa Bobali kwa kweli, unajua kuna jambo ulilisema, Mheshimiwa Waziri, unajua tumekupigia makofi kwa sababu ni mtu wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu watu wa Tanga tumeumbwa wanyenyekemu, watu wema, hatujui kujikweza; lakini licha ya kwamba natoka Tanga na unyenyekevu wangu na kutojikweza, lakini haya ninayoyaongea siyo ya kwenye makaratasi, nimetafuta hela kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha Vituo vya Afya 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pesa shilingi bilioni 67 ipo tayari kwenye akaunti za Wizara. Tumeshawaelekeza TAMISEMI watuletee mapendekezo ya Vituo vya Afya vya kuboresha. Katika hivyo vituo 100 tutajenga *theatre*, tutajenga wodi ya wazazi, tutajenga Maabara ya Damu na tutajenga nyumba ya watumishi.

Kwa hiyo, kaka yangu Mheshimiwa Bobali siyo maneno ya kwenye makaratasi, ni maneno ya vitendo na Waheshimiwa Wabunge wanawake nawashukuru sana kwa kuniunga mkono na naamini wote Waheshimiwa Wabunge... (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, imetosha. Ahsante kwa heshima mliyompa Mheshimiwa Waziri. Tuendelee.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe kuitishwa bajeti, maana naona Waheshimiwa Wabunge wameridhika.

**MWENYEKITI:** Tuendelee.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kushughulikia tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme suala la vifo vya watoto wenye umri wa chini ya siku 30, Mheshimiwa Kemilembe, Mheshimiwa Mama Salma Kikwete

wameliongea sana. Tumetoa maelekezo; tumetoa mchoro mpya kwa ajili ya hospitali. Hatutapitisha mchoro wowote wa hospitali ambao hautakuwa na chumba kwa ajili ya watoto wachanga (*neonatal ward*). Kwa hiyo, suala la pili, tumeshazielekeza Hospitali za Rufaa za Mikoa zote kuanzisha wodi kwa ajili ya watoto wachanga na sisi Wizara ya Afya tutaendelea kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Fedha kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea mambo mengi kwa ajili ya Sekta ya Afya, lakini naomba kabla sijazungumza maendeleo ya jamii, nizungumzie kidogo kuhusu lishe. Lishe ni muhimu sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmetoa maoni, ushauri, jinsi ya kuboresha huduma za lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo tumelfanya kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe, tumetengeneza mkoba kuonesha umuhimu wa siku 1,000 za kwanza za mtoto. Maana yake toka mimba ilipotungwa hadi mtoto anapofikia umri wa miaka miwili. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia *community health workers*, wahudumu wa afya wa jamii, tutatumia pia redio na *TV* ili kuwahamasisha wananchi pamoja na wanawake kuwekeza katika afya zao na watoto wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la chanjo. Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imesema kuna uhaba wa chanjo. Kuna mambo mengine mnachukua yamepitwa na wakati, mambo ya kwenye mitandao. Hatuna tatizo la uhaba wa chanjo za watoto nchini. Kwa hiyo, hayo yalikuwa ni mambo ya kwenye mitandao yanaletwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo chanjo za kutosha na ndiyo maana nimesema, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa chanjo, tumetenga fedha za chanjo tumezitofautisha na fedha za dawa. Kwa sababu mtu akikosa dawa ataenda kununua kwenye *pharmacy*, lakini chanjo hazinunuliwi sehemu yoyote, zinatolewa na Serikali tu. Kwa

hiyo, tunakiri kuanzia mwaka 2016 kidogo tulikuwa na changamoto, lakini sasa hivi hayo mambo yamepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la maendeleo ya jamii. Kubwa ambalo limeongeleva na Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Faida, kuhusu Benki ya Wanawake Zanzibar, Mheshimiwa Dada yangu Mheshimiwa Faida ameongea kwa uchungu sana, wifi yangu Mheshimiwa Munde, lakini pia Mheshimiwa Neema Mgaya, mdogo wangu amezungumzia suala la Benki ya Wanawake kwa nini haiko Njombe? Kamati ya Kudumu ya Bunge pia, imezungumzia suala la Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri kwamba, sasa hivi kidogo kuna changamoto katika Benki ya Wanawake, kwa hiyo, tayari tumeshamwomba Mkaguzi Mkuu wa Serikali afanye ukaguzi maalum ili kubaini changamoto zinazokwamisha na kuweka mikakati ya kuboresha. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie kidogo, kabla hatujaenda kufungua matawi mikoani, tusubiri taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali tuone ni mapendekezo gani atayatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, suala la riba ya Benki ya Wanawake, naomba nijibu kwamba, tusubiri pia hiyo taarifa ya ukaguzi maalum wa CAG ili tuweze kuboresha utendaji kazi wa Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ya Kudumu ya Bunge imezungumzia suala la sheria kandamizi dhidi ya wasichana na watoto, ikiwemo Sheria ya Ndoa. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alitueleza changamoto tunazopipata katika kufanyia marekebisho Sheria ya Ndoa. Ninachowezwa kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge ambaao mmeongea kwa hisia kubwa, wakiwemo Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Richard

Mbogo na Mheshimiwa dada yangu Sophia Mwakagenda, ni kwamba, nitaendelea kushirikiana na wenzangu Serikalini kuangalia ni jinsi gani tunaweza kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nami ni Muislamu, ziko changamoto zinazohusiana na masuala ya dini. Nimekutana na Mashehe na wameniambia ukisoma vizuri Kitabu cha Mwenyezi Mungu unaweza ukasema wala hakuna tatizo katika kufanya marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe changamoto ambayo nimeshampelekea Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bangladesh asilimia takribani zaidi ya 90 ya Bangladesh ni Waislamu, lakini wamepitisha Sheria ya Ndoa mwezi Januri mwaka huu, 2017 ambapo wao sasa wamefanya hivi, wameongeza umri wa ndoa, wamesema umri wa ndoa kwa mwanamke utakuwa miaka 18 na kuendelea, lakini wakasema *under special circumstances* ndoa chini ya umri wa miaka 18 inaruhusiwa.

Kwa hiyo, nitaenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali angalau kutoa pendekezo hili, angalau *na-raise minimum age of marriage* kutoka *14 years to 18 years*, lakini unatoa *exceptions* kidogo. Kwa hiyo, nimeangalia Malawi wenzetu wamepitisha Sheria ya Ndoa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** (Hakusikika)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Hapana Mheshimiwa Mnyika. Kuna watoto saa nyingine, Bangladesh wamesema kama ni mtoto *under 18 years* na *under a special circumstances such as pregnancy, wameandika kama amepata mimba*. Kwa hiyo, hiyo kidogo naweza nikawashawishi wenzangu ndani ya Baraza la Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba tunaweza tukabadilisha. Kwa sababu kilio kikubwa ni *minimum age of marriage* (umri wa kuolewa). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Njombe, amezungumzia sana

kwamba tumesema watoto ni asilimia 51, kwa hiyo, mnafanya jitihada gani za kuwekeza kwa watoto wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rose Tweve nataka kukuthibitishia, kati ya jambo kubwa katika kulinda haki za watoto wanaonyonya; na Mheshimiwa Jenista nakushukuru sana; tulipeleka kwa Mheshimiwa Jenista mapendekezo ya kufanya marekebisho ya Kanuni za Sheria za Kazi na Ajira; kwa sababu ile sheria ukiiangalia inasema mwanamke akimaliza *maternity leave* anaruhusiwa kunyonyesha, lakini sheria haisemi ananyonyesha kwa muda gani.

Mheshimiwa Jenista nakushukuru sana, tumepeleka mapendekezo, sheria inasema hivi, kwamba mwanamke mjamzito anaruhusiwa kunyonyesha baada ya *maternity leave* kwa muda wa miezi sita ndani ya masaa mawili na muda wowote ndani ya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tutaendelea kuwataka waajiri kuzingatia mabadiliko ya sheria ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyapitisha kuhakikisha watoto wananyonyeshwa na mama zao. Kwa hiyo, sasa hivi ni miezi sita baada ya *maternity leave* na masaa mawili, muda mwanamke mwenyewe mfanyakazi atakaosema. Akisema anaingia kazini saa 4.00 badala ya saa 2.00 sheria inamruhusu, akisema atatoka masaa mawili kabla ya muda wa kazi kwisha, sheria inamruhusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipozungumzia suala la ukatili dhidi ya watoto, sitawatendea haki watoto wa Tanzania. Nataka kuwathibitishia, licha ya kwamba tumetunga sheria kali dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, lakini bado vinajitokeza kama nilivyoonesha katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kubwa ni kuendelea kuhamasisha jamii, walezi na wazazi. Mheshimiwa Mbunge aliongea jambo zuri sana, sasa hivi hata kama ni

mila zetu mgeni kulala na mtoto mdogo; nataka niwaambie siyo salama kwa mgeni; awe ni mjomba, awe ni baba mdogo, kulala na mtoto wa kiume. Kwa sababu, kwa mujibu wa taarifa zetu, ubakaji dhidi ya watoto na ulawiti unafanywa na watu wa karibu ndani ya familia zetu. Kwa hiyo, tuchukue tahadhari ya kuwalinda watoto wetu dhidi ya vitendo vyatukilili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi kama nilivyo sema, lakini tunawashukuru sana kwa michango yenu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia na kwa ushirikiano mzuri mnaotupatia, lakini kipekee nirudie kuwashukuru sana wafadhili wetu ambao wanatuwezesha kutekeleza miradi yetu ya Sekta ya Afya, ikiwemo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya, nillwataja jana; Denmark, *CDC*, Ireland, Canada pamoja na Korea ya Kusini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee jana sikuweza kuwashukuru Shirika la Afya Duniani ambao kwa kweli wanatupa msaada mkubwa katika kutekeleza masuala ya afya, hasa masuala ya kitaalam. Vile vile tunawashukuru sana *UNICEF* kwa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, sitaki kupigiwa kengele, niseme kwamba tumepokea changamoto. Nimalize moja, la Sheria ya Wazee, ni kweli, tuliahidi Sheria ya Wazee tutailetta Bungeni. Tumekwama kwa sababu, zipo taratibu ndani ya Serikali za kutengeneza sheria. Kwa hiyo, litakapomalizika tutakuja katika Bunge lenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema jana, sote ni wazee watarajiwu. Ni jukumu la kila mtu ikiwemo Serikali kuhakikisha tunaweka mazingira mazuri na salama kwa ajili ya kuwalinda na kuwatunza wazee wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsanteni sana. (*Makof*)

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hoja yako.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 - Afya**

Kif. 1001 – Admin & HR Mgnt... .... .... .... Sh. 5,558,700,000/=

**MWENYEKITI:** Hapa Waheshimiwa Wabunge, ndiyo mnaelewa mambo. Sawa, niokoe muda; tunao Mheshimiwa Upendo Peneza, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Sannda, Mheshimiwa Lupembe, Mheshimiwa Koshuma, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Balozi Adadi, Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Mmasi, Mheshimiwa Ndaki na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. Hayo ndiyo niliyonayo.

Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Kandege. Dakika tatu tu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika kifungu

cha mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ni ukweli usiopingika kwamba sisi wote humu ndani tunaguswa kwa namna moja au nyininge juu ya uwepo na ulazima wa kumalizia zahanati pamoja na vituo vya afya. Pia ni *commitment* ambayo ilitolewa na Serikali hii ambayo bado na sisi hatujasahau na hili jambo halijajitokeza wazi wazi na bahati nzuri walikuja na kwenye Kamati ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nisipopata maelezo ya kuridhisha, nakusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba namheshimu sana, naye analijua hilo.

**MWENYEKITI:** Hili linahusu nini Mheshimiwa?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Kutenga pesa kwa ajili ya kumalizia zahanati ambazo wananchi wamejitolea pamoja na vituo vyake.

**MWENYEKITI:** Sawasawa. Hili linafahamika kabisa. Serikali! Ili lingependeza sana tukaelewana vizuri. Nakumbuka kwenye Kamati ya Bajeti yaliyosemwa na ahadi ya Serikali kwa nia njema kabisa na TAMISEMI ningependa mwongee lugha moja, maana Serikali ni moja. Mheshimiwa Simbachawene simwonni, ingependeza, nimemwelewa sana Mheshimiwa Kandege kwa nini amekuja na sura hiyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Kandege. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba nitoe ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi imeliweka wazi kabisa suala hili kwamba tutajenga zahanati kwenye kila kijiji na kituo cha afya kwenye kila Kata. Sasa utaratibu wa namna ya kujenga hauwekwi na llani unawekwa na taratibu mbalimbali za Serikali. Utaratibu ambao tunao mpaka sasa ni kwamba zahanati hizi na vituo vya afya

vingepaswa kuanza kujengwa na wananchi wenyewe mpaka kufikia hatua ya kukamilisha boma. Halafu Serikali ikaja kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema Serikali, pamoja na kwamba kuna Serikali za Mitaa lakini pia kuna Serikali Kuu. Sasa ukamilishaji ungepaswa kumalizwa na Serikali za Mitaa zenyewe. Sisi kama Wizara ya Afya tulichokifanya kwa sababu tunasimamia sera kutokea juu mpaka kule chini, tumefanya tathmini ya kina ya kubaini mahitaji angalau ya kukamilisha majengo ya vituo vya afya angalau kimoja kwenye kila Wilaya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ambayo tumeipata kwa tathmini yetu ni kwamba kituo kimoja cha afya kitahitaji shilingi bilioni 2.4 ili kukamilika. Sasa kwa vituo hivyo ili kukamilisha angalau kimoja kwenye kila Wilaya, maana yake tutahitahi shilingi bilioni 440. Kwa hiyo, tunaendelea na mazungumzo na tafakari mbalimbali ndani ya Serikali, ni namna gani tutazipata fedha hizi ili tuweze kukamilisha azima yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hii ambayo inaletwa na Serikali haina tofauti ya ile ambayo ililetwa mwaka 2016. Serikali illahidi kwamba inakwenda kutuletea gharama halisi ili tuhakikishe kwamba tunaenda kujenga vituo vya afya kuanzia mwaka huu wa fedha. Sasa naomba niendelee na kusudio langu la kutoa shilingi ili Waheshimiwa Wabunge wenzangu wapate fursa ya kuweza kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofii*)

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya, naona imeitungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, najua mnapenda sana uwiano, lakini tukienda kwa uwiano saa hizi, tutapata shida. Tunaanza na Mheshimiwa Musa Ntimizi, Mheshimiwa Mbene; wenye Serikali, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Serukamba; hawa jamani hawajatosha! Haya naendelea.

Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Ngombale...

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Ngwali!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali, wewe si upo kwenye hoja yako; na hili unataka uchangie?

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Hoja yangu imeingia hapa.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Ngwali. Jamani wametosha hawa. Mnaonaje? Mheshimiwa Ngonyani, *Tanga line*.

Haya Waheshimiwa Wabunge, mnaona shida niliyonayo! Hoja ya msingi, tunaanza na Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami naungana na Mheshimiwa Kandege katika kuiomba Serikali kwa kweli kuja na majibu ambayo yatatusaidia kuondoa changamoto za afya katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa zahanati na vituo vyta afya limekuwa linazungumzwa muda mrefu. Wananchi wetu wamejitolea kwa kiasi kikubwa kujenga maboma katika maeneo mbalimbali ambayo mengine yana

zaidi ya miaka mitano hayakamilika, lakini hakuna mkakati maalum ambao tunaupata kila mwaka kuona zile zahanati zinakwisha katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji kuna shida kubwa ya afya, wananchi wetu wanahangaika sana, lakini wananchi wetu ni wasikivu, unapowaambia wachange, wanachanga kuhakikisha kwamba wanajenga maboma ya zahanati kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wajibu wetu sisi ni kujenga maboma ili Serikali imalizie; kwa kweli halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kujenga vituo vya afya ni muhimu kwa sababu sasa hivi watu wakitoka kwenye zahanati zetu wanakwenda kutibiwa katika Hospitali za Mikoa na kusababisha wananchi wengi kujazana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji vituo vya afya vijengwe katika maeneo yetu. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, dakika mbili tu. Unaunga mkono hoja yako fupi, sababu yako fupi au siungi mkono. Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hii hoja kwa sababu hili suala nzima la kujenga vituo vya afya wala siyo hayo maboma peke yake, ni suala lilanzishwa na Serikali wenyewe. Haiwezekani leo waanze kulirudisha tena kwa Halmashauri eti wakamalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zimeachiwa mzigo mkubwa sana, hawataweza kulimudu hili. Serikali lazima itie mkono wake. Wananchi wanajitolea kwa kusikiliza Serikali inaomba kuwa anzeni sisi tutakuja kumalizia. Leo wamefika mahali, mnawaambia tena aaah, malizieni huko huko! Siyo sawa. Naomba hili jibu lipatikane. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** ahsante sana. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE.PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Naomba nijaribu kutoa wazo ambalo labda Serikali walifanyle kazi. Nadhani umefika wakati; tulifanya hivyo huko nyuma kwenye shule za kata; kwa nini sasa zisiambiwe ma-*DED* wote nchini kwenye bajeti kila mwaka za Halmashauri angalau tuwekewe vigezo kwamba ili Mkurugenzi uendelee kuwa Mkurugenzi, lazima mwaka kesho ujenge vituo viwili vya kata, ujenge zahanati nne. Ukipanya hivyo, tuna hakika baada ya miaka mitano tutakuwa tumeefika mbali kama nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninaloliona hapa Mwenyekiti ni kwa sababu hatuweki vigezo, hatuweki malengo, tunasubiri tumeepata shilingi tano; lakini nadhani ili tuweze ku-solve tuijwekee malengo kwenye Halmashauri zetu pamoja na Serikali hii ya kujenga hivyo vituo kila mwaka.

**MWENYEKITI:** ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini napenda tu kushauri kwamba hili suala la kujenga maboma kwa wananchi, imekuwa mara nydingi sana wananchi wanajitolea sana. Nadhani Serikali ikiweka mkakati mzuri wa kuwawezesha; kwamba nguvu ya wananchi isiwe inapotea bure, kwa sababu vinginevyo tunawakatisha tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kupitia bajeti yetu, hasa ningependa kusema kwamba Wizara ya TAMISEMI, maana ukiingia kwenye Wizara ya Afya, wao ni kisera zaidi. TAMISEMI kupitia Mheshimiwa Simbachawene, wekeni mkakati wa kibajeti kwa kila mwaka. Hii itatusaidia sana kuwa na mwelekeo unaoonekana. Hadithi na ngonjera za kila mwaka tutafanya hivi, tutafanya hivi, haitusaidii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba tu Serikali izingatie haya matakwa ya wananchi. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbunge wa Sikonge.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa, Mwenyekiti, vipaumbele vya Mpango wa Miaka Kumi wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (*MMAM*) ambao ni wa mwaka 2007/2017, vipaumbele vyake vikuu vilikuwa ni kujenga zahanati kila kijji na kujenga kituo cha afya kila kata. Sasa *performance* ya utekelezaji wa mpango huo mpaka sasa hivi iko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali kama iliviyotuahidi miaka ilipita, watoe *commitment* hapa kwamba kila Wilaya itajenga vituo vya afya labda vitatu na zahahati labda sita kila mwaka ili kusudi haya malengo yaweze kutimia katika vipaumbele hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo kwa kweli naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege, aendelee kushikilia shilingi mpaka maelezo ya kutosha yatolewe. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Kandege. Naomba Serikali iiongezee fedha Wizara hii kwa sababu moja maalum. Kuna sehemu nyingi sana tumeanzisha miradi lakini mpaka leo hii haiendi. Leo ukisema Halmashauri itenye pesa, pesa hiyo itaipata wapi? Kuna Halmashauri nyingi Tanzania ambazo ni hoi hoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwamba Serikali iangalie ni namna gani Wizara hii iongezewe fedha ili tujengewe Vituo vya Afya na yale magofu ya mikano ambayo yalikuwa yamejengwa hajakwisha, kwa mfano Hospitali za Mikoa, pia hawana hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kabisa hoja ya Mheshimiwa Kandege kwamba Serikali...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege kwamba miradi ya wananchi iheshimiwe. Serikali imewahadaa wananchi, imewadanganya wananchi na ilisema, pale ambapo wananchi wakiweka nguvu zao Serikali itatia mkono wake. Serikali Kuu ni vema wakati huu iangalie namna bora ya kuongeza fedha ili nguvu za wananchi ziweze kuthaminiwa, majengo haya yamalizwe na migogoro hii ya wananchi iweze kumalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Mheshimiwa Kandege kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, katika bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) hakuna fedha zozote zilizotengwa za kujenga vituo ama kuboresha hivyo vituo. Katika Wizara ya Afya yenyewe hakuna fedha zozote zilizotengwa. Kwa maana hivo, dhana ya kusema kwamba Serikali kuja kwa wananchi sijui wajenge ni dhana ya kubabaisha tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ya msingi hasa papa, hakuna fedha; au Serikali ituambie fedha hizo zimetengwa mahali gani? Mheshimiwa Ummy anasema, fedha zimo

kwenye akaunti. Fedha zimo kwenye akaunti, Mheshimiwa Ummy namna gani? Tunataka tuzione pesa kwenye bajeti siyo kwenye Akaunti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu. Akaunti inakuwaje sasa!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngombale.

**MH. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege kwa sababu hali ya kuchangia maendeleo kwa wananchi wetu inazidi kushuka chini kwa sababu wanatekeleza hii miradi ya maendeleo lakini Serikali inashindwa kuwaunga mkono. Kwa mfano, kuna zahanati nyingi ambazo tayari zimeshakamilika kujengwa, lakini Serikali inashindwa kuzifungua. Isitoshe, kuna urasimu mkubwa, hata pale mtakapofuata taratibu za kwamba zahanati imekamilika, wenzetu wa Wizara ya Afya kutoka Mganga Mkuu wa Mkoa mpaka huku chini; namna gani sasa hiyo zahanati inafunguliwa? Kuna urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niunge mkono hoja ili basi Serikali ije na hoja mahususi ni namna gani itashughulikia suala hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege. Sisi watu wa Wilaya ya Kinondoni na hasa hospitali yetu ya Mwananyamala imekuwa ni Hospitali ya Rufaa lakini tunabeba gharama kubwa ya kuiendesha na wakati huo huo tunatakiwa tujenge Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima Serikali itujengee Hospitali ya Wilaya ambayo tumeshaanza kujenga baadhi ya maeneo, wamalizie ile hospitali. Wenzetu wanamalizia maboma, nasi wamalizie hospitali yetu ile au

ikiwezekana basi wachukue gharama zote za uendeshaji wa Hospitali yao ile ya Rufaa, sisi tuendelee na Hospitali yetu ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege. Ni kweli kwamba wananchi wanajitolea, tena wananchi maskini, wanajenga maboma ya zahanati; yale maboma Serikali haimalizii, yanabomoka tena. Kwa hiyo, ni muda muafaka Serikali ituambie ni lini itakamilisha yale maboma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukashangaa Serikali haina hata takwimu ya maboma yote ambayo yamejengwa na wananchi mpaka sasa hivi ambayo yana uhitaji wa kukamilika ili tuweze ku-save vifo vyta akinamama na watoto ambao wanatembea muda mrefu kwenda kufuata huduma ya hospitali kwenye Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu sana, utakuta Majimbo mengine hayana hata vituo vyta afya kama kwangu Tarime. Wakamilishe yale maboma ya zahanati ambayo tumejenga ili angalau wananchi wapate hizo huduma ambazo ni za msingi sana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege. Wananchi wamekuwa wakijitolea, lakini Wabunge kupitia mifuko yetu ya Majimbo, tumekuwa tukiungana na wananchi kuhakikisha tunajenga hizi zahanati, lakini Halmashauri zetu nyingine bado changa, mkisema tuziachie Halmashauri zikamilike wakati kuna vyanzo vyta mapato Serikali imechukua na mwisho wa siku mnashindwa kurudisha zile fedha ili zahanati na vituo vyta afya vikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunarudisha jitihada za wananchi kujitolea. Wananchi wanajitolea, Waheshimiwa Wabunge wanaunga mkono kupitia Mifuko ya Jimbo pamoja na Wabunge wa Viti Maalum ili kuondoa vifo vya akinamama na watoto lakini bado Serikali mbali ya kuchukua vyanzo vya mapato, vimeshindwa kupeleka fedha ili basi hizizzahanati na vituo vya afya vikamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kandege.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuwarudisha nyuma kidogo Waheshimiwa Wabunge, kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yake yote alivyotueleza na jitihada alizozichukua mpaka sasa za kuweza kupata mpaka pesa ya kuandaa vituo 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani na Mheshimiwa Waziri kwamba safari ameianza na ana dhamira ya dharti. Mimi mwenyewe ni Mbunge, ninayo maboma ya namna hiyo, naomba tumpe fursa; hapa alipokuwa anazungumza, amejiapiza mno na tumempigia makofi sisi wenyewe. Muda haujapita, tumpe fursa, huyu mama atapambana na ataweza kututengenezea mazingira mazuri ya vituo hivyo na kufunika majengo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mapendekezo yangu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuonesha concern kubwa kwenye eneo hili la huduma za afya ya

msingi. Wizara yangu ndiyo inayosimamia utekelezaji wa utoaji wa huduma hizo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dai la Waheshimiwa Wabunge hapa ni kwamba nguvu za wananchi zimefanya kazi na Wabunge wenyewe wakihusika, wamejenga maboma na kwamba sasa Serikali ina fedha gani au ina mpango gani au ina *commitment* gani katika kuhakikisha kwamba maboma yale yanaezekwa na kumaliziwa ili huduma itolewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu changu cha majedwali wakati wa bajeti yangu nilieleza kwamba fedha ya maendeleo (*LGDG*) ambayo ni fedha ya maendeleo isiyo na masharti hupangwa kule kule kwenye Halmashauri. Tumepanga fedha ya kutosha na imeanza kutolewa kwa mwaka huu wa fedha. Kwa mwaka wa fedha tunaoumaliza, mpaka sasa tumeshapeleka zaidi ya shilingi bilioni 60, lakini iliyokuwa imepangwa ni shilingi bilioni 158.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkumbuke kwamba fedha hii ya maendeleo ilikuwa hajatolewa kwa miaka mitatu nyuma na ndiyo maana maboma hayo yakabaki yako hayajamaliziwa. Sasa hivi inatoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nisome kwa Mkoa wa Rukwa, Kalambo yenyewe itapata sh. 1,254,313,000/=, hiyo ni Halmashauri; Nkasi itapata sh. 1,520,000,000/=; Sumbawanga itapata shilingi bilioni 1.6; *Sumbawanga Municipal Council* itapata shilingi bilioni 1.2 na Halmashauri zote nchi nzima zitapata hiyo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachowea kuelekeza...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hapana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Hujaniruhusu bado?

**MWENYEKITI:** Kwenye Kamati unajua hakuna hayo mambo ya Taarifa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa muhimu sana naitoa kwa Bunge.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa. Kwa heshima zote, kaa tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu fedha hii ya ruzuku isiyokuwa na masharti, isiyokuwa na maelekezo, yaani wanaamua wenye kwenye Halmashauri ndiyo iliyokuwa inatumika kuezeka maboma haya ya huduma ya afya na elimu; sasa ilikuwa imesimama kwa miaka mitatu. Sasa imeanza kutoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba kwa bajeti hii na namba hizi, tukisimamia bajeti hii ikatekelezwa na fedha hizi zitakuja. Nataka niwahakikishie kwamba tutayaezeka haya maboma yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo langu tu kwa mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini, sasa hivi masharti ya mgawanyo ya zile fedha, ni asilimia 10 kwa sababu ya *capacity building* na mambo mengine, asilimia 10 kwa ajili ya shughuli nyingine, lakini asilimia 80 kwa ajili ya maendeleo *perse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo langu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwamba asilimia 40 ya hiyo asilimia 80 ambayo ni kwa ajili ya maendeleo, ikamalizie maboma ya vituo vya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa Kalambo, samahani naomba nimalizie, kwa Kalambo ukigawanya kwa fedha watakayopata, asilimia 40 ni shilingi milioni 460. Wanaweza kabisa kama boma lipo, kwa shilingi milioni mbili na kitu, wakamalizia vituo vya afya viwili, kwa hiyo tukawa tuna vituo vya afya viwili katika halmashauri moja kwa mwaka mmoja wa bajeti. Je, mwaka unaokuja, tukimalizia viwili; tutakuwa tumefika mbali sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege, mwenye hoja hii, baada ya maelezo hayo!

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao kimsingi wameunga mkono hoja na naamini hata Mheshimiwa Simbachawene kwa namna moja ameunga mkono hoja, kwa sababu tatizo nililonalo mimi hakuna Mbunge awaye yejote ambaye tatizo hili halipo kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niikumbushe Serikali kwamba kunako uhai, ukitoa ahadi mwaka mmoja siyo mrefu. Walikuja wakaahidi kwenye Kamati ya Bajeti, nami ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati wa Bajeti, kwa hiyo, haya ninayoyasema, nina uhakika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana na Serikali mwaka 2016 kwamba wakapige hesabu walete ili tuwe na mpango mahususi wa namna ambavyo tunakwenda kumaliza tatizo la umalizaji wa Vituo vya Afya pamoja na Zahanati, sasa ukitafuta kwenye vitabu vyote, hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ule mlango walioingilia, bado uko wazi. Namna pekee ambayo naweza nikaachia shilingi hii ni pale ambapo Kiti kitaelekeza. Mlango bado uko wazi na ndiyo maana upo utaratibu wa bajeti hii; tuna nafasi ya kujadiliana na Serikali. Kabla hatujahitimisha

bajeti kuu, lazima tukubaliane kwamba pesa inapatikanaje kwenda kumalizia zahanati pamoja na vituo vya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana. Serikali! Ukishaona *mood* hii na mwenye hoja amekupatia njia ya kutokea, chomoka. (*Makofi*)

Naagiza sasa suala hili kwa mujibu wa Kanuni ya 105, lirezee tena kwenye Kamati ya Bajeti mkatoe maelezo kwa *commitment* ambayo mlikuwa mmeitoa wakati ule na nini ambacho kitafuata. Hiyo Kamati ya Bajeti watakapokuja kutoa taarifa yao Bungeni na hili litakuwa sehemu ya taarifa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kandege, baada ya maelekezo haya, nakuomba useme tu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naamini Serikali watasema na wewe usikie ili iwe kwenye *record* kwamba hilo ambalo kimsingi umeagiza, Serikali watekeleze tukutane halafu tuje tulete ripoti kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo narudisha shilingi kwa sababu umetupa mlango wa kutokea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kufanikisha suala sugu la upatikanaji wa madawa hospitalini, lakini vilevile kugawa vitanda katika Halmashauri mbalimbali nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika suala zima la afya ya mama na mtoto. Mheshimiwa Waziri ambaye pia ni mwanaharakati mwenzangu na vilevile ni mwanamama mwenzetu, amejibu na ameeleza kwa mapana sana katika suala zima la afya ya mama na mtoto na wanawake wote Waheshimiwa Wabunge humu ndani ni mashahidi, tumempigia makofi kwa kiwango cha juu sana, nakupongeza sana mwanaharakati mwenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujuua, mwaka 2000 *among* kila vizazi hai 100,000 kulikuwa na vifo 529. Leo hii miaka 15 baadaye ni vifo 556 kwa vizazi hai 100,000. Nataka kujuua, Mheshimiwa Waziri atueleze, ni kwa nini mpaka sasa hivi Serikali hajawenza kupunguza? Vinginevyo nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwalize, katika pande zote; wa CCM, upande wa CHADEMA kuna Mbunge ambaye hoja yake inafanana na hiyo ili tuwaondoe ili nisiwe naitaita kwa hoja ambayo imesemwa! Kuna *similarities* (usare)?

Hakuna! Haya. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa hoja yake. Nimejaribu kueleza, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwa nini vifo havijapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa, takwimu ambazo tulikuwa tunatumia zamani katika kuainisha vifo vitokanavyo na uzazi, tulikuwa tunatumia sensa. Kwa hiyo, ukiangalia Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ambayo ilifanyika mwaka 2012, ilibainika kwamba vifo vitokanavyo na uzazi vimeduwa ni 432 katika kila vizazi hai 100,000. Kwa hiyo, takwimu ambazo tumezitoa, kwa sababu nami ndiye

nilizindua, tumezitoa Desemba, 2016 ni *TDHS*, Takwimu ya Hali ya Afya ya Uzazi na Viashiria vya Malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, takwimu zile ambazo walifanya taasisi ya Serikali (*National Bureau of Statistics*), kwa hiyo, pia tunaheshimu na ndiyo maana hoja yangu wakati na-*wind up* hapa nimesema *whether* ni takwimu za sensa au ni takwimu za *TDHS* ya 2015, hatuko hapa kwa ajili ya kubishana, kwa sababu mwisho wa siku wawe ni wanawake 432 au wanawake 556, bado ni Watanzania wenzetu wanaofariki. Lengo letu ni kwamba ifikapo mwaka 2020 tupunguze mpaka 292.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa na Waheshimiwa Wabunge, tumejitahidi na nataka kwa kweli kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Hali imekuwa nzuri. Hata ukiangalia takwimu ambazo tunazipata kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya, anakwambia Mheshimiwa Waziri nimepunguza vifo; mwaka 2016 nilikuwa na vifo 50, mwaka huu nina vifo 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumaamisha, hatutaki kupingana na takwimu, muhimu mwangalie tumejipangaje katika kutatua changamoto hiyo na ndiyo mambo nimeyaeleza hapa na nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge; nami ni mama tena wa binti warembo wawili. Kwa hiyo, kila mwanamke anayebeba ujauzito, tunataka kumthibitishia usalama wake na kichanga chake, ndiyo maana ya Bajeti hii ya 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, nawaahidi kwamba tuendelee kushirikiana kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, umeridhika naona, twende mbele. (*Kicheko*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri, lakini nilichokuwa nazungumza ni tamko la Serikali katika kupunguza vifo badala ya kuongezeka. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayekuheshimu sana, vilevile ushauri wangu wa bure pia, kwa nini Serikali isifanye kozi ya ukunga ikawa ni ukunga tu badala ya kujumlisha pamoja na uuguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, katika hatua hiyo *option* ni moja tu.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi, sijaridhika.

**MWENYEKITI:** Unaelewa maana yake? Hujaungwa mkono, basi.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja, sijaridhika bado.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Mukasa. Tunaanza nawe Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama alivyosema mtoa hoja na kama nilivyosema kwanza, Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kweli wanafanya kazi vizuri, lakini yapo mambo yanayogusa kule chini ambayo tusipoyafanya vizuri hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema mwenyewe hapa, mama mjamzito hapimwi mkojo, hapimwi *BP*, hapimwi chochote anachotakiwa kufanya pale; sasa kuna mwanafalsafa anasema, katika

mchanganyiko wa *factors* za *success* na *factors* za *failure* matokeo huwa ni *failure*. Ndiyo maana anafanya vizuri sana at *policy level* na unamwona anaunganisha vizuri sana wadau, lakini kwa sababu hashuki chini kuhakikisha mama anapimwa mkojo, kuhakikisha mama anapimwa *BP*, lakini pia kutenganisha hii habari ya Manesi wa jumla na *midwives*; ukichanganya *failure* na *success* majibu yatakuwa *failure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mkakati wa kushuka chini; na ameonesha ana uwezo, hatuna mashaka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda usiozidi nusu saa kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1). Tunaendelea na Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najua dada yangu, Mheshimiwa Ummy, nawe ni mwanaharakati kwenye masuala ya akinamama na watoto, lakini naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. Kwa kweli vifo vyta akinamama na watoto vimekuwa ni tatizo kubwa katika Taifa letu na bado hatujaona jitihada za makusudi katika kuhakikisha tunakabiliana navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani tumesema kumekuwa na programu nydingi sana, lakini hata bajeti yenye ni finyu katika kukabiliana na tatizo hili. Kwa hiyo, tunaona bado kunahitajika jitihada za makusudi katika kuhakikisha tunamkomboa mama pamoja na mtoto katika masuala mazima ya afya na uzazi ili kukabiliana na vifo vyta mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul. Kama huna mchango, tunaendelea.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu nilimpoteza Mheshimiwa Diwani katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu, alifariki wakati anajifungua na mtoto akafa, kisa tu damu imekosekana. Wakati anajifungua damu ilipungua lakini kwenye Hospitali ile ya Hydom hapakuwa na akiba ya damu tukapoteza mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu visto. Nilitaka kutoa mfano huo tu wa juzi, wiki chache zilizopita ili Mheshimiwa Waziri ajue kwamba tunayoyaongea siyo kwamba ni *story*, ni vitu visto. Sasa kwa ngazi ya Serikali ni vizuri mkashuka chini mkaona ni mahitaji gani ya akinamama wajawazito yanatakiwa yawepo muda wote na siyo ya kutafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema kwamba hili ni kundi maalum na hili kundi linapofika katika hospitali zetu wamekuwa ni mzigo, kwa sababu Serikali fungu mnalopeleka halitoshelezi; tuna wazee, tuna watoto na akinamama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atoe kauli ambayo itatuhakikishia kwamba hili tatizo sasa linaweza likapungua. Vinginevyo tukinyamaza hali...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. Mheshimiwa Waziri nafikiri anakumbuka miaka ya nyuma kulikuwa na mkakati kwa ajili ya kutafuta namna gani ya kuweza kuwasafirisha akina mama kutoka mahali walipo kwenda kwenye huduma zilizo sahihi. Mpaka sasa hivi bado juhudu hizo hazijafanyika. Ukiangalia hata magari ya wagonjwa wenywewe ni mpaka yalipiwe kodi; huko vijijini watu wanapata matatizo. Vituo hivi tunavyosema vyaya afya na zahanati zetu ndiyo maboma yenywewe haya hayamaliziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba *commitment* ya Serikali ni namna gani kweli mnaweza mkamkomboa mwanamke? Mtu anaambiwa aende na *kit* hospitali ajiandae, hivi kweli jamani! Naomba sana kuwe na *commitment* ya namna gani mnaweza mkawahudumia hawa wanawake wawe *comfortable*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, maelezo baada ya michango hiyo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa anataka tamko la Serikali kuhusu vifo vitokanavyo na uzazi. Tamko letu, Serikali ya Awamu ya Tano itapunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Tunapunguza? Ndiyo nimeeleza katika bajeti hii; kuna *interventions* ambazo zimethibitishwa Kimataifa ni jinsi gani ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi? Ni maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ni kuwekeza kabla ya mwanamke kuwa mjamzito huduma za uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba tumetenga shilingi bilioni 14 kwenye bajeti yangu kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni suala la huduma wakati wa ujauzito. Tena kuna mengine wala siyo ya Serikali. Kwa mujibu wa takwimu ambazo tumezindua mwaka 2016, wanawake ambao wanahuduria *clinic* angalau mara nne wakati wa ujazito ni asilimia 51. Hili sisi Waheshimiwa Wabunge tukawahamasishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kusubiri, wewe mwanamke mjamzito unao wajibu wa kuhudhuria *clinic* angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito wako na hili Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tutaendelea kuwahamasisha wanawake wajawazito wahudhurie *clinic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nimelisema, anapohudhuria *clinic* huyu mama mjamzito, apate huduma zote muhimu. Ndiyo maana labda wanawake wengine wajawazito hawaendi, kwa sababu akienda pale hapewi huduma. Ndiyo nikatoa angalizo kwa Waganga Wakuu wa Wilaya. Hufai kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya kama unakosa hata vifaa vidogo tu katika zahanati zako kwa ajili ya kuhakikisha huduma za uzazi kwa wanawake wajawazito zinapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaenda mbali; sehemu ya tatu, huduma wakati wa kujifungua na wiki sita baada ya mwanamke kujifungua. Nimeonesha kwamba, kuna kitu tunasema ahudumiwe na Mkunga mwenye ujuzi. Tumeonesha kwenye bajeti yetu, kuwa tumeongeza kiwango cha wanawake wanaojifungua na kuhudumiwa na mtumishi mwenye ujuzi kutoka asilimia 51 hadi asilimia 64. Kwa hiyo, wanawake 64 kati ya 100 ya Watanzania wanaojifungua wanahudumiwa na mtoa huduma mwenye ujuzi. Sasa hiyo ndiyo mikakati ambayo tumeweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaenda mbali nikasema sasa inapotokea huduma za uzazi za dharura, mmejipangaje? Ndiyo nikasema kwenye bajeti yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa tumezungumzia sababu, kwa mara ya kwanza tutajenga Benki za Damu za Mikoa mitano ndani ya bajeti yangu. Nikasema tutahakikisha pia upatikanaji wa dawa za kuzuia mwanamke kuvuja damu na dawa za kudhibiti kifafa cha mimba. Yako humu na haya siyo maneno yangu, ni maneno ya bajeti. Tunawashukuru sana wenzenzu wa Hazina kwa sababu angalau wamesikia hoja zetu; haikuwa rahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho Mheshimiwa Dkt. Mary, ndio nimesema pale tumepata fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kuboresha Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto. Kati ya fedha hizo, nirudie kwa Mheshimiwa Ngwali, katika fedha hizo kuna vyanzo vya ndani ambavyo nimevionyesha, lakini tumepata hela kutoka Benki ya Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela hizi zipo. Nimeshaomba wenzangu wa TAMISEMI waniletee mapendelekezo na wakishaniletea sisi tutafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombwa sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa anirudishie shilingi kusudi nikapambane katika kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Anirudishie shilingi nishirikiane na Wabunge Wanawake, wanawake wote Tanzania na wanaume tuwahakikishie usalama akinamama wajawazito na vichanga vyao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, upepo unauona.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameunga mkono hoja hii. Hii ni kuonyesha umuhimu wa afya ya mama na mtoto katika nchi yetu hususan kwa sisi ambao pia ni wanawake humu ndani na Mheshimiwa Waziri akiwa ni mwanaharakati mwenzangu na mwanamama kama mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakaa, Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa umuhimu wa ukunga, akinamama wanavyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unajua kanuni!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimrudishie rafiki yangu shilingi. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Sawa sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kupata maelezo ya Serikali. Ukiangalia vitabu vya bajeti, *demands* za afya ni kubwa sana na moja ya eneo ambalo linahitaji fedha nyngi sana ni kwenye vifaa vya mahospitali. Sisi tulikuwa tunaomba, umefika wakati kama nchi ndiyo maana nimesimama ili Serikali itoe msimamo kwamba kwa nini tusiende wanakokwenda wenzetu duniani kwamba vifaa unaweza uka-*outsource*, mtu akaja kwenye hospitali vifaa vyote ameweka yeye. Kwa hiyo, tunavyo-*charge* ndiyo kazi yake. *Maintenance* na kununua vifaa siyo shughuli yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Tutapata fedha nyngi sana ambazo zitakwenda sasa kwenye madawa, vifaa tiba vingine na zitakwenda kusaidia huko kwenye zahanati zetu ili jukumu hili tuliache kwa wafanyabiashara, wafanye hiyo kazi badala ya kuiachia Wizara. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Unakumbuka malalamiko ya Mheshimiwa Bashe kuhusiana na kampuni fulani inayofanya *maintenance*? Msaidie hapo, enhe Mheshimiwa. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii kwa kweli kama inavyoletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imekuwa ikijirudia sana kwenye Kamati yake wakipendelea Serikali itumie hiyo *innovation* ya *systems* za kisasa za kukodi mitambo kwa ajili ya kutoa huduma kwa watu wetu hususan

huduma za uchunguzi ama *system* ya kufunga mikataba na watoa huduma binafsi kwa ajili ya kuja kuza huduma kwenye Vituo vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatupingani na hii *innovation* ambayo imekuja kwenye miaka hii ya karibuni; hususan kama ukituangalia sura zetu hatujafika miaka 50. Nasi wenyeewe tumezaliwa kwenye zama hizi hizi za *innovations* hizi ambazo zipo kwa sasa ambazo msingi wake ni kwenye teknolojia ya habari na mawasiliano (*ICT*), ndiko ilikoanza, baadaye ikaingia kwenye Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kwa sasa, tunapenda kuwa *cautious* sana kabla ya kuingia kwenye mikataba hii, kwa sababu unaweza ukadhani unasaidia kupunguza matatizo ya mabadiliko ya haraka ya teknolojia kama utamweka *supplier* kama kampuni labda ya *Phillips*, *General Electric* ama *Toshiba* akaweka *ultra sound*, *CT-Scan* ama *MRI* kwenye hospitali yako, halafu aanze kuwachaji wananchi. Baada ya kufunga mkataba tu, anaweza akawazunguka akaanza kuleta vikwazo na matokeo yake gharama badala ya kushuka, zikapanda, zikawa kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaangalia *moda/nzuri* ya kutumia ili kulifua suala hili, lakini mpaka sasa hatujafikia kuwa na msimamo thabiti ndani ya Serikali kwamba tufanye nini. Kwa hiyo, pindi tutakapokamilisha tathmini yetu na kufanya tafiti kwenye nchi mbalimbali zilizojaribu, kwa mfano jirani yetu, kuna nchi ya Kenya wamejaribu kwenye baadhi ya vifaa tiba, lakini pia kuna nchi ya Ethiopia na Ghana wamejaribu. Sisi tunajifunza kutoka kwao ili tuone kama inaweza ikawa ni suluhu ya changamoto za utoaji wa huduma za uchunguzi kwenye Sekta ya Afya hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Serukamba, maelezo mazuri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua suala la *PPP* ni gumu sana na watu wa Serikali hili jambo hawalipendi sana, lakini...

**MWENYEKITI:** Katika hatua hii, unaendelea kutoa shilingi?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Naam, nataka kutoa hoja tujadili suala la *PPP*, natoa hoja mniunge mkono.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Oscar; wewe unarudia sana; Mheshimiwa Devotha Minja, Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Mtulia.

Hoja ya Mheshimiwa Serukamba imeelewaka, hatutaki kuirudia. Mwalimu, ulisimama? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya kaka yangu pale, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Serukamba; nami kwenye michango yangu nililisema hili kwamba Serikali imefika mahali sasa, mfano kama sisi watu wa mjini Hospitali zetu za Rufaa watu wetu wanakuja pale wanataka huduma na wapo tayari kulipia, lakini hatuna uwezo wa kumiliki vile vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isione ukakasi; tujaribu. Kama watashindwa kufanya kwa nchi nzima, basi wateue baadhi ya hospitali iwe kama ni *sample, pilot study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Kinondoni, watu wa mjini, tuko tayari. Waturuhusu tuingie kwenye hiyo *program* ya *PPP* na kama watashindwa, basi wawe

wadhamini wetu tunapokwenda kukopa katika taasisi nyingine ambazo zitakuwa zipo tayari kutusaidia kupata hizi mashine, ni jambo muhimu sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Massare, zamu yako.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja hii, kwa sababu dunia inavyokwenda, hatuwezi kwenda kinyume nyume. Serikali kuwa inanunua vitu ambavyo vinaendana na teknolojia, itakuwa ni vigumu kwenda na wakati. Ni bora sasa Serikali ikakubali; tunao wataalam wengi wamebobe, wapo wanasheria na mikataba yoyote lazima kuwe na mkataba namna ya kuvunja mkataba kama huyu ambaye tumeingia naye mkataba atakwenda kinyume. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kuelewa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa kaka yangu, Mheshimiwa Peter Serukamba, napenda kuunga mkono hoja ya Serikali kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP Act* ambayo tunayo, ukiangalia maudhui yake yalijikita sana kwenye mambo ya *infrastructure* kwa maana ya miundombinu kama barabara na reli. Ina changamoto nyingi ambazo inabidi zirekebishwe ili iweze kuwa na tija hata katika hayo maeneo ya *infrastructure*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *PPP* ni *long term by nature*, kwa hiyo, mikataba yake inakuwa ya miaka mingi, yaani 30 au zaidi. Kwa hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kingwangalla, kwa

sababu kwa upande wa afya bado hatujajikita vizuri, hata kwa upande wa *infrastructure* bado tuna changamoto, tukikimbia kwenda *PPP* kwenye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Umeeleweka. Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Serikali ikubali tu kwamba haiwezi kununua vifaa vyote yenye. Serikali ikubali kushauriwa kwamba ni wakati sasa wa kuingia mikataba na hayo makampuni yawasaidie. Tumejifunza kutoka sehemu mbalimbali; hata mabenki yanafanya hivyo; hata wamilliki wa vyombo vyta habari ambao wanawatumia mitambo kutoka nje wanawatumia wa-Israel. Kwa hiyo, ikifika kwenye suala la *maintenance*, wataalam wanakuja wanafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe tu mfano mdogo, pale Morogoro *X-Ray machine* ambayo kuitengeneza ni shilingi milioni 20, lakini kununua mpya ni shilingi milioni 70; unaweza ukaona ni namna gani? Kama Serikali ingekuwa imeingia mkataba na hawa *suppliers*, kwa vyovoyote vile wangebeba jukumu la kufanya *maintenance* na kupunguza mizigo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wakati ambapo Serikali lazima ikubali kushauriwa ili iwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Hoja yake inabidi itazamwe kwa upana;

anaongelea *PPP* kama namna ya kutafuta fedha za vifaa, lakini namna zipo nyingi. Tukiokoa pesa upande mwingine tutanunua vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa inasema, asilimia nne tu ya Watanzania wana vyoo. Kwa hiyo, watu wengi waliofoleni kule hospitali wanaenda kwa sababu wanaharisha. Ukizua ukaweka vyoo, kitu ambacho wanaweza, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naye zikawekwa nguvu chini kule watu wasipate magonjwa ya kuhara *uta-save* pesa ya dawa na utapeleka kwenye vifaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani hapa, yaani asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge waliko hapa, kule kwao watu hawana vyoo, wanaharisha na familia zao zinaharisha wakati tunaweza tuka-*save* pesa za madawa za kuharisha na tukanunua vifaa. Hili tunaweza TAMISEMI na Afya, watu wapate vyoo, tusimamie na *tu-save* pesa kwenye madawa ya kuharisha. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa ushauri mzuri. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Peter na nialewa hofu ya Serikali. Nimeiona hofu hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Innocent kwamba kwenye mikono yetu tuna *inefficient system* tuliyonayo sasa. Nataka nitoe mfano mdogo kwamba, tuna mkataba na *Phillips* wa *ku-service x-rays* mpaka leo *x-ray* ya Nzega na niweke kwenye kumbukumbu, *Biomedical Engineerwa Hospitali* ya Bugando kapigwa simu na *Engineer anaitwa Mvanga* kutoka Wizarani akitishwa kwa nini kaenda kuigusa *x-ray* ya Nzega?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *inefficient system* ili yopo leo. *Should we go on with a status quo?* Kama Sheria ya *PPP* ina matatizo, kwa sababu *bottom line* ni *service delivery*, kwa nini isije iweze kupitiwa upya ijibu mahitaji yetu? Ni lazima tutoke kwenye *traditional way* tuangalie dunia inapokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushuru sana. Pia Waheshimiwa Wabunge misisahau kwamba tuna jukumu sisi kama Wabunge kwa mujibu wa kanuni kwamba unaweza ukaleta mapendekezo yako ya *Private Bill*, ukajenga hoja kama eneo hili la Sheria yetu ya *PPPhaijaka* vizuri, inanyooshwa ili iweze kukaa vizuri.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wakuruhusu iingie humu ndani ni kazi.

**MWENYEKITI:** Hapana. Haya, Mheshimiwa Waziri nimekuona, ulikuwa unataka kuchangia Mheshimiwa Mhagama?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Wizara ya Afya wataliweka jambo hili vizuri.

Mheshimi Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, baada ya kusikia mchango wenyewe wa Waheshimiwa Wabunge na hasa jinsi ambavyo Mheshimiwa Bashe hapa ametoa mifano ambayo ukiisikiliza unajifunza kwamba lipo jambo la kimsingi kabisa, pia ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge katika jambo hili unaona kabisa lipo jambo la kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Bashe tukuombe tuelewe hicho ulichokisema lakini na Waheshimiwa Wabunge waliochangia jambo hili pamoja na Mheshimiwa Serukamba ambaye amejenga hoja hii; kwetu sisi kama Serikali nadhani tuna umuhimu wa kurudi ndani kwenda kulitazama kwa umakini na undani wa kutosha. Tulifanyie kazi kabisa *with serious note* ya kuona ni namna gani tunaweza kujitoa mahali hapo na kufanya vifaa tiba hivi katika hospitali zetu viweze kupatikana na viweze kuwa vinakarabatiwa kwa wakati kadiri inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Serukamba atuachie jambo hili turudi nalo ndani ya Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya na timu yao, yale ambayo tutakuwa tumeyaona kwamba sasa ni mambo yanayofaa, Bunge lako bado lipo, tutaendelea kuja kutoa taarifa ili tuweze kuhangaika kuona namna gani kwa pamoja wote tunaweza sasa kuwa tumetatua tatizo hili la msingi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Peter Serukamba atuelewe katika msimamo huo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno mazuri yaliyotolewa na *Chief Whip*, tunamshukuru Mheshimiwa Serukamba kwa hoja. Kama alivyosema Naibu Waziri, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wenzetu Kenya waliweza kujenga uwezo wa huduma za uchunguzi wa magonjwa *diagnostic services* kwa kutumia hiyo *PPP*. Kwa hiyo, tunaichukua hiyo hoja kama alivyosema, tutaifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama niongeze jambo moja, wakati tunaangalia mazingira ya kuingia katika mfumo huo wa *PPP*, tumeanza pia kutumia mifuko *especially Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, NHIF* kwa ajili ya kuzikopesha hospitali zetu kununua vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulianza siyo lazima *PPP*, lakini pia kuna mdau *NHIF* ambaye amefanya kazi nzuri ya kuzikopesha Halmashauri kununua *X-Ray* na *Ultra Sound* lakini bado hajafika hata Hospitali ya Benjamin Mkapa (*UDOM*). Ni kwa sababu ya mkopo ambao Serikali tumeupata kwa *NHIF*. Kwa hiyo, tunalipokea na tutaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme suala la *Phillips*, tunakubali ni tatizo na tutalifanya kazi. Mheshimiwa Bashe kwa niaba ya mtendaji wangu wa Wizara, nakuomba radhi na ninamwomba radhi *Engineer* wa Bugando ambaye

amepigiwa simu na Mtendaji wangu na kupewa vitisho. Siyo utaratibu na tutachukua hatua za kinidhamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, labda *time line* maana sikusikia, wanataka walichukue tu, labda tuelekee katika kuliboresha hili.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Mheshimiwa Waziri Jenista. Nami nilichukua shilingi ili hili jambo tuanze tulifiki kizuri kama Taifa. Kwa sababu hivi tutaweka *MRI* Bariadi lini? Tutapata *MRI* Kigoma lini? Vipo vyombo ambavyo kibajeti tutatumia muda mrefu sana. Sasa ipo njia ya mkato na njia ya mkato ni hela za watu ambazo ni *PPP*. Suala la bei siyo la kweli, kwa sababu tutali-*control*/kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka ni Serikali tulifiki hili jambo. Tukaangalie linakotokea kwingine duniani ili tukiona ni jambo la maana linatufaa, litatusaidia katika kutatua matatizo ya afya ya watu wetu kwa haraka zaidi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimerudisha shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa uungwana wako.

Waheshimiwa Wabunge, tutende haki pia; Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani na hata katika mchango wangu, tumezungumzia suala la Serikali kukubali

kubadili mfumo wa kibajeti ambapo pesa za dawa na vifaa tiba zihame kutoka katika fungu la bajeti ya maendeleo na kuhamia katika matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa ya kufanya hivyo ni kwamba , pesa za maendeleo kupatikana inakuwa ni kazi na unavyoangalia ni kwamba hela za bajeti ya maendeleo lengo lake liko kwa ajili ya kutengeneza miradi ambayo ni ya kutumia kwa muda mrefu, lakini suala la dawa ni suala ambalo linahitajika kila siku, Watanzania wanahitaji dawa kila siku ya Mungu. Kwa maana hiyo basi, pia Serikali haitoi pesa kwa maana ya kila mwisho wa mwezi au katika utaratibu mzuri ili zile pesa za maendeleo ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia ambalo lilzungumzwa hata na Kamati ya Afya, imeweza kuzungumzia kwamba hata masuala ya UKIMWI na *TByamekuwa hayapati* pesa kwa sababu pesa za maendeleo zinategemea zaidi pia wahisani. Suala hili la kuhamisha pesa za dawa; nikisema pesa za dawa, namaanisha dawa na vifaa tiba ambavyo vinasaidia kwa ajili ya kutoa hiyo huduma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama sitaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mwongozo wa Spika. Mwongozo wa Mwenyekiti! (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nani?

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Suleiman.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Suleiman, haya.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Hapana, sijakuruhusu. Nakusihi ukae. Haya, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru mdogo wangu, Mheshimiwa Upendo Peneza kwa hoja yake, lakini bado ningetaka kumshauri, kwetu sisi Serikali hatuoni shida tena tunaona kwa upande wa Wizara imetusaidia sana kwa fedha za dawa kuingizwa katika bajeti ya *development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumeziingiza kwenye bajeti ya *development*? Waziri wa Fedha hayupo, lakini tulipitia *international classification* ya *expenditures* kwa sababu dawa, vifaa tiba unawekeza katika *human capital development*, katika maendeleo ya watu. Ni sawa sawa na *training* kwa watumishi kwamba *whether uiweke kwenye recurrent au uiweke kwenye development*, lakini mwisho tumeona *international standard* kwamba dawa unawekeza katika maendeleo ya watu, kwa hiyo, ndiyo maana tumeiweka kwenye *development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumeanza kuiweka kwa *development*. Tangu tumeanza kuiweka katika *development* hatujapata tatizo la kupata fedha za dawa. Nimesema mwaka 2016 hela ya dawa iliyotoka *it was only 24 billion*, mwaka huu tumeshapata shilingi billioni 132.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ikiwekwa kwenye *development* imekuwa pia *protected*. Kwa hiyo, haiwezi tu ikawa inatumika hovyo hovyo. Bado sisi hatuioni kama ni hoja nzuri, tumeamua kuendelea na hela ya dawa. Kwa mfano, kama alivyosema Mheshimiwa Serukamba, tumetoka kuzungumzia *investment* ya *MRI, CT-Scan*, ambayo *ina-cost six billion, four billion, you cannot put it under recurrent cost* kwa sababu itaendelea kufanya kazi kwa miaka minne mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Upendo, hiyo siyo hoja.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Hata miaka 20.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Eeh, hata miaka 20 Naibu Waziri ananiambia. Sisi tunadhani hiyo siyo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro dawa za UKIMWI, *TB* na Malaria ndio tunapata kutoka kwa wafadhilli, lakini hela ya dawa ya sasa hivi ni uwekezaji wa fedha za ndani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba dawa zetu tunanunua kwa kodi zetu na siyo kwa msaada. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, umeridhika?

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siridhiki na majibu ya Mheshimiwa Waziri; na anavyosema kama ni *international classification* ni suala ambalo sisi Tanzania hatufanyi, lakini nchi za Afrika Kusini, Zambia...

**MWENYEKITI:** Toa shilingi *straight*.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waweze kuniunga mkono katika hoja hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Toa hoja, hakuna kuomba.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt Kijaji, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware. *Doctor*, tunaanza na wewe.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa MwenyeKITI, nashukuru. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Upendo Peneza kwa kuangalia tu *trend* ya bajeti yetu inavyotoka kwenye Wizara mbalimbali. Wizara ya Afya ukiangalia, bajeti zetu zinatoa mishahara, *recurrent* ipo asilimia zaidi ya 40, 50 na kuendelea mpaka 70; lakini ukiangalia hela za *development* mpaka asilimia mbili kwa mfano kwenye Wizara yetu kama ya Kilimo; au namwuona hapa Mheshimiwa Ummy kwenye Wizara yake ya Afya katika vifungu vyake viwili iko chini ya asilimia 40 kwenye fedha za *development*. Sasa masuala ya afya kama chanjo za watoto au chanjo hata za *tetanus* ime-*improve* hata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kanuni sasa zinanifunga mikono, sina uwezo tena. Tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu.

### Fungu 52 – Afya

Kif. 1001 – <i>Admin. &amp; HR Mgmt</i> . . . . .	Sh. 5,558,700,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> . . . . .	Sh. 1,272,639,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> . . . . .	Sh. 1,062,625,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> . . . . .	Sh. 182,756,000/=
Kif. 1005 – <i>Government Comm.</i> . . . . .	Sh. 220,680,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Manag. Unit</i> . . . . .	Sh. 176,535,000/=
Kif. 1007 – <i>Legal Services Unit</i> . . . . .	Sh. 39,800,000/=
Kif. 1008 – <i>Information Comm. &amp; Techn.</i> . . . . .	Sh. 140,508,000/=
Kif. 2001 – <i>Curative Services</i> . . . . .	Sh. 205,396,435,000/=
Kif. 2003 – <i>Chief Medical Officer</i> . . . . .	Sh. 43,555,336,000/=
Kif. 2004 – <i>Nursing &amp; Midwifery Serv. Div.</i> . . . . .	Sh. 321,316,000/=
Kif. 2005 – <i>Pharmaceutical Services Unit</i> . . . . .	Sh. 167,363,000/=
Kif. 3001 – <i>Preventive Services</i> . . . . .	Sh. 22,010,343,000/=
Kif. 3002 – <i>Health Quality Assurance Div.</i> . . . . .	Sh. 323,129,000/=

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kif. 4002 – *Social Welfare* .... .... .... .... .... .... .... .... Sh. 0/=  
Kif. 5001 – *Human Resource Dev.* .... .... .... Sh. 11,503,887,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia,  
Wazee na Watoto**

Kif. 1001 – *Administration & HR Mgmt.* .... ..Sh. 3,440,406,000/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts*.... .... ....Sh. 369,029,000/=  
Kif. 1003 – *Policy and Planning* .... .... ....Sh. 582,538,012/=  
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* .... .... .... Sh. 452,639,000/=  
Kif. 1005 – *Government Comm. Unit* .... .... Sh. 206,550,331/=  
Kif. 1006 – *Procurement Manag. Unit*.... .... Sh. 390,015,000/=  
Kif. 1007 – *Information Comm. & Techn*.... .... Sh. 315,074,188/=  
Kif. 1008 – *Legal Service Unit*.... .... .... Sh. 191,723,000/=  
Kif. 2001 – *Training & Folk Dev. Colleges*...Sh. 12,773,064,012/=  
Kif. 2002 – *Community Development* ..... Sh. 9,094,418,457/=  
Kif. 3001 – *Gender Development* .... .... .... Sh. 688,018,000/=  
Kif. 3002 – *Children Development* .... .... Sh. 686,887,000/=  
Kif. 4001 – *Non-Government Org* .... .... .... Sh. 506,708,000/=  
Kif. 5001 – *Social Welfare Division* .... .... .... Sh. 5,603,532,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 52 – Afya**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* .... .... .... .Sh. 115,235,311,000/=  
Kif. 2001 – *Curative Services* .... .... .... Sh. 62,852,890,000/=  
Kif. 2005 – *Pharmaceutical Serv. Unit*.... Sh. 236,409,940,000/=  
Kif. 3001 – *Preventive Services*. .... .... .... Sh. 368,307,811,000/=  
Kif. 4002 – *Social Welfare* .... .... .... .... .... .... .... Sh. 0/=  
Kif. 5001 – *Human Resource Dev.* .... .... .... Sh. 3,000,000,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia,  
Wazee na Watoto**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* .... .... .... .... .... .... Sh. 0/=  
Kif. 2001 – *Training and Folk Devpt Colleges* .... .... ..Sh. 0/=  
Kif. 2002 – *Community Development*.... .... ..Sh. 832,000,000/=  
Kif. 3001 – *Gender Development* .... .... .... Sh. 344,604,109/=  
Kif. 3002 – *Children Development* .... .... .... Sh. 208,900,000/=  
Kif. 5001 – *Social Welfare Division* .... .... .... Sh. 1,220,773,891/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi  
yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa  
Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio  
ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara ya Afya,  
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Fungu 52 na  
Fungu 53 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kifungu kwa  
kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naomba sasa  
Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kutamka kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na *team* yako, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara hii, napenda kuwapongeza sana kwa kazi nzuri mliyofanya. Pia wakati unahitimisha hoja yako, ulivyoungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge, inadhihirisha imani kubwa ambayo wanayo kwako na kwa Wizara. Kwa hiyo, maadam uamuzi umetolewa kupata fedha hizi, tutegemee mtiririko mzuri wa mafungu yote mawili, Fungu la 52 na 53 muweze kufanya kazi yenye tija kwa faida ya Watanzania. *(Makofi)*

Vile vile niungane nawe uliposema kwenye upande wa Sheria ya Bangladesh; Waheshimiwa Wabunge, nilitumwa na Mheshimiwa Spika wetu kuongoza ujumbe wa Waheshimiwa Wabunge kwenda kwenye Mikutano wa IPU, ni kweli katika kufuatilia; maana unapokwenda kwenye mikutano hii, unauliza na mambo mengine kujifunza.

Katika eneo hili ni kweli wenzetu hawa ambao wamekuwa wakihangaika na suala hili na wenyewe wamepitisha hiyo sheria. Kwa hiyo, tunajifunza. Maana katika mazingira maalum, sasa tutakuja tuangalie maana yake ni nini, lakini njia ipo. Kwa hiyo, nadhani Waheshimiwa

Wabunge, kazi hii ipo, tukiamua kwa Taifa hili kulinda watoto wetu, tunaweza tukafanikiwa pamoja na *cautions* zote ambazo zipo. (*Makof*)

Sina matangazo mengine, kwa hiyo, nawashukuru sana pia nanyi Waheshimiwa Wabunge kwa kazi mliyofanya. Nimetenda haki sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, huwa nawaeleza, Kanuni hizi ni zetu, kwa hiyo, *discretion* ya Kiti, ndiyo utambue kwamba hawa ni wengi ndiyo maana baadaye nikasema sasa nashuka niende huku, lakini ndiyo hivyo, uamuzi ndiyo huo, tunavumiliana hivyo. (*Makof*)

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, siku ya Ijumaa, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.12 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 5 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*